# Ufafanuzi Wa Agano Jipya

# Mathayo





**Na Dorothy Almond**
mwisho na Askofu Francis Ntiruka

www.africanpastors.org

Ufafanuzi Wa
Agano Jipya

# Mathayo

## Dorothy Almond

© African Pastors Fellowship 2010

Kimetolewa na:
**AFRICAN PASTORS FELLOWSHIP**
Station House, Station Approach, Adisham
Canterbury, Kent CT3 3JE
United Kingdom

www.africanpastors.org


# DIBAJI

Aliyeandika kitabu hiki cha ufafanuzi ni Sista Dorothy Almond aliyeishi Tanzania kwa miaka 31, na sasa yu Uingereza hali amestaafu. Alikuwa mwalimu katika Chuo cha Theologia, Kongwa kwa miaka 16 na katika Shule ya Biblia, Morogoro kwa miaka 6 na katika Shule ya Biblia, Msalato kwa miaka 4.

Mchoraji ni Peter Kasamba. Yeye ni Mwuganda anayeishi huko Kampala. Kwa muda mrefu amechora picha zote kwa vitabu vya APF. Anaongoza pia Kwaya ya AYF.

Kitabu hiki chatolewa kwa msaada wa African Pastors Fellowship. Lengo ni kuwasaidia watumishi wa Kanisa wanaosoma katika Shule za Biblia na Masomo ya Nyumbani

# RAMANI YA PALASTINA WAKATI WA KRISTO



# UTANGULIZI

Injili ya Mathayo imewekwa kuwa ya kwanza katika orodha zote zilizopo za Injili nne na za Agano Jipya lote. Ila si wataalamu wote wanaokubali kwamba ni ya kwanza kuandikwa. Injili hiyo ilipendwa sana na kuhesabiwa kuwa ya muhimu sana katika Kanisa, waandishi wa kwanza wa kikristo waliitumia zaidi ya zile zingine katika maandishi yao.

### (a) Utungaji

Mawazo yatofautiana jinsi Injili hiyo ilivyotungwa. Hatutaangalia habari hiyo kwa kirefu sana, ila twatoa mawazo mbalimbali ya wataalamu. Vema tukumbuke ya kuwa hao hubadili mawazo kufuatana na maendeleo ya uchunguzi *wao.* Kusudi la kitabu hiki ni kutazama yaliyomo.

Baadhi ya wataalamu hufikiri kwamba Injili hiyo ni tafsiri kwa Kiyunani ya Andiko la Kiebrania lililotangulia na hilo la Kiebrania liliandikwa kabla ya Injili zingine tatu. Papia, mwandishi mmoja wa Kikristo katika karne ya pili alisema hivi, na Eusebio, mwandishi wa historia ya Kikristo alitaja kwamba Papia alisema hivyo. Ireneo aliyejulikana sana kwa maandishi yake ya Kikristo alisema kwamba Mathayo aliandika hiyo Injili wakati Petro na Paulo walipokuwapo Rumi wakiihubiri Injili na kabla ya Injili ya Marko kuandikwa. Jerome aliyeishi baadaye ameshuhudia vivyo hivyo, ila aliongeza kusema kwamba haijulikani ni nani aliyefanya tafsiri ya Kiyunani.

Ila wako wasioweza kukubali hayo kwa sababu ya hali ya Kiyunani cha Injili tuliyo nayo sasa, ambayo haiwaruhusu kufikiri ni tafsiri bali ni andiko ambalo kwa asili liliandikwa kwa Kiyunani. Injili ya Mathayo ina sehemu kubwa ya Marko ndani yake, karibu yote isipokuwa vifungu kama 55 tu. Mathayo amefupisha mengine kutoka Marko na kutengeneza kidogo kidogo kulingana na lengo lake.

Kwa hiyo wataalamu wengine hufikiri kwamba Injili ya Marko ilitangulia kuandikwa. Kama ni hivyo kwa nini Mathayo aliye Mtume aliitumia sana na Marko hakuwa Mtume? Pengine Mathayo alitafsiri Andiko lake la Kiebrania baada ya B.K.70 (Mt. 22:7).

Wazo lingine ni kwamba Mathayo aliandika "Misemo ya Yesu" (Sayings of Jesus) na ndiyo hiyo iliyoingizwa katika Tafsiri ya Kiyunani na kusababisha iitwe Injili ya Mathayo. Wanaoelekea kufikiri mwandishi ni Mathayo huona amejitaja katika Mt. 9:9 na pengine ni nyumba yake ambayo imetajwa katika Mt. 9:10; 10:3; 13:1; 17:25. Yawezekana amejieleza katika Mt.13:52. Twajua aliweza kuandika kutokana na kazi yake ya hapo nyuma. Alizoea mambo ya fedha na ameweka mifano miwili kuhusu fedha, isiyopatikana katika Injili zingine. Alitaja walinzi kupewa fedha, pia alitoa habari ya Yuda kutupa vipande vya fedha hekaluni.

### (b) Tarehe ya Kuandikwa

Katika neno hili la tarehe, tena wataalamu hutofautiana katika mawazo yao. Baadhi yao wamependa kuipa tarehe ya baadaye, wakifikiri Injili ya Marko iliandikwa kama B.K. 65 na kama Mathayo aliitumia, basi Mathayo aliandika baada ya B.K.65. Wapendao tarehe kabla ya hiyo hufikiri kwamba ni vigumu kuona kwa nini Mathayo ataja mambo ya hekalu, kama Yerusalemu umeisha kuanguka (B.K. 70).

### (c) Mtindo wake

Kama ambavyo tumekwishasema, Mababa wa kwanza waliipenda na kuitumia sana hata ikajulikana kama “Injili ya Kanisa". Kwa nini ikawa hivyo? Ni kwa sababu ilisaidia Kanisa kwa njia tatu. Katika kuitetea Imani ya Kikristo iliposhambuliwa na Wayahudi waliokataa kuamini. Katika kuwafundisha waongofu maadili ya Kikristo. Katika kuwasaidia Wakristo kuishi maisha ya pamoja kama jamii mpya ya watu wa Mungu, wakijenga maisha yao juu ya maneno na matendo ya Bwana Yesu. Bila shaka walipokutana juma kwa juma kwa ibada walisomewa kutoka Injili hiyo, mpango na utaratibu wake ukiwasaidia kufanya hivyo.

Injili hiyo imekuwa msaada kwa Kanisa sikuzote kutokana na mtindo wake wa kupanga pamoja mambo yanayofanana hasa kwa kukusanya mafundisho na maadili pamoja. Ni vema tukumbuke ya kuwa watu hawakuwa na nakala zao wenyewe, njia ya kujifunza ilikuwa kwa kusomewa na kukariri. Twaona kwamba mwandishi alipanga mambo yaliyopatana kwa hesabu ya tatu, au tano, au saba, ili watu wasaidiwe kukumbuka vizuri. Kwa mfano Petro alimkana Yesu mara 3; Yusufu alipata ujumbe mara tatu. Katika sura ya 13 mifano 7; Sura 23 ole 7. Alikusanya miujiza kadha pamoja bila kujali mfuatano wa kutokea kwao. Aliyaweka mafungu makubwa matano ya Mafundisho: Sura 5-7; 10; 13; 18; 24-25. Kila baada ya kumaliza fungu fulani alitumia maneno yaliyofanana (7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1).

### (d) Ujumbe wake

Injili hiyo ina mwelekeo wa Kiyahudi, lengo la mwandishi lilikuwa kuwathibitishia Wayahudi kwamba Yesu ni Masihi wao wa kweli. Katika Yesu unabii wa Agano la Kale umetimizwa, hivyo imani ya Kikristo si mpya bali ni utimizo wa kweli wa imani iliyotangulia ya Kiyahudi. Katika Agano la Kale Mungu aliyafunua mapenzi yake na makusudi yake ya kumleta Masihi, aliye Kristo.

Mwandishi ameonyesha kwamba Torati ya Kale imetiliwa maana mpya na Kristo, viini vyake vimedhihirishwa wazi. Watu wa Mungu, Israeli wa zamani wanaendelea katika jamii mpya ya Wakristo. Mara nyingi alitilia mkazo hayo yote kwa kuweka vifungu vya Agano la Kale kuwa thibitisho lake. Mwandishi anataka tumwone Yesu kuwa Masihi na Mfalme aletaye ufalme wa Mungu

karibu nasi. Iwapo ameweka mafundisho mengi ya Yesu, yaliyo mazuri mno, zaidi anataka tumwangalie Yeye aliyetoa mafundisho hayo na kufahamu Yesu Mwenyewe ndiye Fundisho Kubwa ili tumzingatie Yeye ni nani na anadai nini.

Mara katika sura ya kwanza Yesu amewekwa wazi kuwa Masihi, Mwana wa Daudi (1:6). Mama yake aliposwa na Yusufu wa uzao halisi wa Daudi (1:20) kwa hiyo, kisheria Yesu ni mzao halali wa nyumba ya kifalme. Mara nyingi ameitwa 'Mwana wa Daudi' (9:27; 12:23; 15:22; 20:30; 21:9, 15). Mamajusi walipofika waliuliza "yuko wapi aliyezaliwa Mfalme". Pamoja na hayo Mathayo alipambanua utofauti wa Mfalme huyo, atakuwa na tabia za kiuchungaji, na hasa atajitoa kama Mtumishi; (12:19-20; 9:13; 12:7). Atakuwa mnyenyekevu na mpole, atawashughulikia wanyonge, na walionewa, walioachwa kando na wenzao, wajane na wageni, na wasiopendwa. Alipoujia Yerusalemu na kudai kutawazwa kuwa Mfalme aliingia hali amepanda punda, dalili ya unyenyekevu na upole wake. Wote watakao kumfuata na kuuingia ufalme wake budi wazishiriki tabia zake (5:1-10 na 18:1ku). Ufalme wake haulindwi na upanga na upanga hautaushinda. Mbele ya Kuhani Mkuu alikubali kabisa kuwa Masihi, Mwana wa Mungu, ndipo akakubali kufa, kwa sababu ufalme wake sio wa hapa duniani, utatimizwa baadaye atakaporudi mara ya pili.

Mwandishi hakueleza desturi za Kiyahudi, dalili ya wasomaji wengi watakuwa Wayahudi waliozifahamu. Tena husema 'ufalme wa mbinguni' si ufalme wa Mungu; Wayahudi hawakupenda kutaja jina la Mungu. Katika nasaba mwandishi ameanzia kwa Abramu, baba wa taifa lao. Katika mazungumzo na majadiliano mambo ya sabato, kufunga, hekalu, sadaka, kodi ya hekalu, n.k. yalizungumzwa; mambo yaliyo kawaida ya Wayahudi. Yesu alipowatuma wanafunzi aliwatuma "kwa waliopotea wa nyumba ya Israeli" na aliwakataza Mitume wasiwaendee Wasamaria. Ni hapo tu Wasamaria wametajwa (10:5,6).

Katika majadiliano na viongozi na Mafarisayo aliwakemea vikali hata kiasi cha kuonekana ni kinyume chao. Kwa hiyo iwapo amewalenga Wayahudi ili awavute kumpokea Kristo ni dhahiri ni Mkristo halisi ambaye ameelewa kabisa kwamba katika Injili mataifa yote wamekaribishwa kwenye ufalme wa Mungu na ya kuwa Wayahudi waweza kupoteza nafasi yao wasipomkubali Kristo (8:10-12; 21:43; 23:29-39; 27:24-25). Mwisho wa Injili amemaliza na agizo kuu la Yesu kwa wafuasi wake kwenda ulimwenguni mwote na kufanya watu kuwa wanafunzi. Injili hii iliwasaidia viongozi wa Kanisa kuelimisha waumini juu ya uhusiano kati ya imani ya Kiyahudi na ya Kikristo, hasa kuhusu mahali pa Torati, Sabato, Mapokeo, n.k. Myahudi aliyeongoka kuwa Mkristo atapaswa kutazama hayo kwa macho yaliyotiwa nuru ya Injili. Neno "kanisa" latokea mara mbili katika Injili hiyo, halipo katika Injili tatu zingine.

Kwa kujumlisha twaona kwamba iwapo inaonekana kuwa mwandishi kama ni Mathayo au mwingine ni Myahudi na lengo la kwanza ni kuwasaidia Wayahudi wenzake, hata hivyo ni mtu aliyekolewa kabisa Injili. Ameonyesha mizizi ya Ukristo kuwa katika dini ya Kiyahudi, hata hivyo ametambua ya kwamba Injili yapaswa kuwa badala yake sawa na matimizo kuwa badala ya matayarisho.



## KUZALIWA KWA YESU NA UTOTO WAKE 1:1 - 2:23

**1 :1-17 Nasaba ya ukoo wa Yesu Kristo**

Yesu yu nani? Yesu ametoka wapi? Kwa kuandika nasaba hiyo Mathayo amelenga kujibu maswali hayo. Kwa Wayahudi nasaba ilikuwa jambo muhimu sana (Mwanzo 2:4; 5:1; 10:1; 11:10, 27). Kwa nasaba hiyo Mathayo ametoboa wazi kwamba Yesu ni Masihi aliyeahidiwa katika Agano la Kale. Kif.1 na k.17 vinaunganisha Yesu na Abramu, baba wa taifa la Israeli, aliyeahidiwa "katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa" (Mwa.12:3); hivyo Yesu ni Myahudi halisi. Tena vifungu hivyo vimeunganisha Yesu na Daudi, Mfalme, ambaye "mwana wake" atakuwa Masihi; (2 Sam. 7:12). Kwa hiyo mwandishi amemweka Yesu katika historia ya Israeli ya Agano la Kale. Jina lafuata jina la watu maarufu katika historia yao, historia iliyoendeleza makusudi ya Mungu ya kuokoa kwa kumleta Mwana wake, Yesu Kristo. Ndiyo sababu katika sura ya kwanza na ya pili mara tano mwandishi ameweka vifungu vya Agano la ·Kale.

Katika orodha Yesu ameonyeshwa kuwa ametoka katika ukoo wa Kifalme wa Yuda, na kwa sheria ni mrithi halali wa ukoo wa Kifalme, ana haki ya kuitwa Mfalme wa Wayahudi, na Mwana wa Daudi. Kwa hiyo lengo la mwandishi kuonyesha Yesu ni TIMIZO la ahadi za Mungu katika Agano la Kale limeonekana wazi. Yesu si mtu aliyesimama peke yake, bali ni mtu asiyeelezwa nje ya historia iliyomtangulia. (Luka katika nasaba yake amerudi mpaka Adamu na kumweka Yesu katika ukoo wa taifa zima la wanadamu - Lk. 3:23 ku.)

Mpango wa nasaba

Katika mpango wa nasaba twaona tabia ya mwandishi kuweka mambo pamoja kusudi watu wakariri bila shida. Amegawa historia tangu Abramu mpaka Kristo kwa mafungu makubwa matatu. Kuanzia kwa Abramu, chanzo cha taifa hadi Daudi, mfalme maarufu. (taz. iwapo orodha ni ya wafalme ni Daudi tu ambaye ametajwa hasa kuwa mfalme k.6). Halafu tangu Daudi mpaka uhamisho wa Babeli, wakati ambapo ufalme ulipotea. Ndipo tangu uhamisho hadi Kristo kuzaliwa. Katika Kristo huo 'ufalme' hufikia upeo wake katika kutimiza shabaha ya kweli ya Mungu.

k.17. Mpango ni wa mafungu matatu, kila fungu kuwa na vizazi kumi na vinne, hata hivyo tukitazama tungu la kwanza na la tatu lina vizazi kumi na vitatu tu. Inaonekana wafalme watatu wamerukwa k.8 na ametaja vizazi kumi na vitatu katika muda wa miaka mia sita!. Viko vizazi 27 tangu Daudi na Luka katika nasaba yake anavyo 42. Bila shaka alikusudia kufanya hivyo kupatana na lengo lake la kusaidia watu kukumbuka na kukariri. Alipenda hesabu ya 3 na 7, tazama k.17 ni 3 mara (7 x 2 =14). Pia herufi za Kiebrania zilikuwa takwimu pia na Jina la Daudi hufikia 14 - D = 4; W = 6; D = 4; Jumla 14 .

Wanawake wanne wametajwa katika ukoo wa kifalme - Tamari (Mwa.38) Rahabu (Yos.2:1-7) Ruthu (Kum.23:3) Bathsheba (2 Sam.12:24). Kuna mawili juu yao; i. wengine si Wayahudi na wote isipokuwa Ruthu hawakuwa na sita nzuri. Kwa nini watajwe? Pengine ni kupunguza nguvu ya wale waliosikia mashaka juu ya Yesu na kuzaliwa kwake. Watu waliona ni vigumu kupokea kwamba alizaliwa na bikira, jambo lisilowezekana kibinadamu. Tena alizaliwa na mwanamke aliyetoka mji usiojulikana.

Habari hiyo iliwakumbusha kwamba Mungu katika historia yao ametumia watu wasiokuwa na maisha mazuri ya ndoa kuendeleza makusudi yake ya kuleta Masihi. Pia watu wasio Wayahudi. Mathayo ameingiza hayo ili ajenge picha ya Yesu kuwa Masihi, Myahudi halisi, ambaye pia ni yule wa kuruka mipaka ya Wayahudi na kuufungua ufalme wake kwa jamaa zote za dunia, ufalme wa wenye dhambi walio tayari kutubu.

Mungu ndiye KIONGOZI wa HISTORIA yote ya wanadamu, iwapo vipingamizi na uasi vyajaribu kuyazuia mapenzi yake, hata hivyo mapenzi yake yatimizwe - alifaulu kumleta Kristo iwapo Israeli walimwasi kila wakati. YESU NI UFUNGUO WA HISTORIA, amesimama kati ya yaliyotangulia, ya yaliyopo, na ya yatakayokuwepo.

1: 16 linganа Lk. 3:23. Mathayo asema baba wa Yusufu alikuwa Yakobo na Luka asema ni Eli. Eli ni baba yake kimwili ila Yusufu ni mwana wa Yakobo kwa kufanyiwa, kama Yakobo hakuzaa mwana Yusufu alifanyiwa kuwa mwana na mrithi wake. Tukumbuke amefuata ukoo wa Kifalme kwa kuonyesha Yesu kuwa mrithi halisi kisheria wa ufalme. Luka alikuwa na kusudi tofauti, amefuata ukoo

upande wa mwili, hivyo tofauti zipo k.16.Mathayo aliandika kifungu hicho kwa uangalifu sana. Yesu si mwana wa Yusufu kimwili, ila kisheria ni mwana kwa sababu amemposa Mariamu na v.18-25 vyaeleza hayo.

## 1 :18-25 Yesu Kristo kuzaliwa

Mathayo hatoi habari nyingi za Yesu kuzaliwa. Mkazo wake ni kuonyesha asili yake kwa njia ya kuchukuliwa mimba na bikira, ametoka kwa Mungu, na jina lake lasababishwa na unabii wa Agano la Kale. Ameeleza jinsi tukio hilo lilivyomgusa Yusufu, kwa sababu tumekwisha kufahamishwa kwa njia ya nasaba uhalali wa Yesu kisheria hutokana na Yusufu,ndipo uhusiano wake na Mariamu umeelezwa. Yusufu alishtushwa na hali iliyoonekana kwa Mariamu na malaika alimsaidia kufahamu kwamba Yesu ametoka kwa Mungu. Ni "malaika wa Bwana" aliyemtokea, |tena katika ndoto.

k.18 Mariamu alichukua mimba wakati alipoposwa na Yusufu. Kwa mila ya Kiyahudi uchumba ulifanyika kwa muda wa kama mwaka mmoja. Uchumba ulihesabiwa kuwa patano lenye nguvu, patano lisilovunjwa ila kwa kifo, mwanamke akifiwa aliitwa mjane. Hakuweza kuachwa bila kupewa talaka sawa na kwa wale wenye ndoa. Mwanamume alihesabiwa ni "mume" k.19. Katika muda huo mwanamke aliishi katika nyumba ya baba yake. Ndoa ilikamilika wakati mwanamume alipomchukua mpaka nyumbani mwake kwa sherehe maalum k.24. (25:1-13); ndipo walikaribiana na maisha ya ndoa yakaanza.

k.18,20 Roho Mtakatifu ndiye njia ambayo kwayo Mariamu alichukua mimba.(Lk. 1:35) Twaona katika Agano la Kale ni Roho Mtakatifu aliyehusika katika uumbaji na katika kutoa uzima. (Mwa.1:2; Eze.;7:1-14). Ni Mungu aliyetangulia katika Yesu kuzaliwa. Pia katika Agano la Kale Roho Mtakatifu alihusika na habari za Kuja kwa Masihi na dahari mpya. (Isa.11:2; 42:1; 61:1; Yoe 2:28).

k.19 Adhabu kwa makosa kabla ya kufunga ndoa ilikuwa kumpiga mkosaji kwa mawe (Kum. 22:13-21; 24:1). Yusufu alitaka kushika torati kama Myahudi mzuri, ila hakutoka kumwaibisha Mariamu kwa kumfikisha mbele ya hakimu. Iliyobaki amkatie talaka kwa siri mbele za mashahidi wawili.


k.20 Wakati huo wa mashaka ya kujua la kufanya, alipata msaada wa uongozi kwa njia ya ndoto. Malaika alimwita Yusufu "Mwana wa Daudi" akamwambia amchukue Mariamu nyumbani kwake ili akamilishe ndoa naye ili Yesu athibitishwe kuwa wa ukoo wa Daudi mbele ya sheria.

k.21, 25 Kwa kumpa Jina Yusufu alimkiri kuwa mwana wake na hivyo kumfanya kuwa "Mwana wa Daudi" pia. Katika habari hizo za Yesu kuzaliwa na kuhusu utoto wake Mungu alimwongoza Yusufu kwa njia ya ndoto (2:12, 13, 19,22;) ila baada ya hapo Mungu hakutumia njia hiyo tena ila kwa mke wa Pilato (27:19).

Katika ndoto tatu "malaika wa Bwana" ametajwa, na tena 28:2. Mathayo alitaka kukaza kwamba ni Mungu aliyemwongoza Yusufu ili Maandiko yatimizwe.

k.21,23,25 Jina la Yesu na Jina la Imanueli. Katika Agano la Kale majina yalikuwa na maana kubwa. Yesu ni kama Yoshua, jina la watu wengi, maana yake 'Yahweh ni wokovu' au 'Mungu okoa' "maana Yeye ndiye atakayewaokoa watu na dhambi zao". Kwa hiyo Yesu ametumwa kuokoa na dhambi - neno hilo ni rekebisho kwa mawazo ya wale waliofikiri Masihi atawaokoa na utawala wa Kirumi. Yesu hakutumia jina la Imanueli hasa linaonyesha kazi yake ya Kumleta Mungu kwa wanadamu. Dhambi hutenga wanadamu na Mungu, kwa hiyo, Yesu atakapowaokoa na dhambi, Mungu atapatanishwa na wanadamu. Yesu Mwenyewe ni Mungu pamoja nasi. Mathayo alifunga Injili na ahadi ya Yesu kuwa pamoja na wafuasi wake (Mt. 28:20).

k:24, 25 Yusufu hakumkaribia Mariamu mpaka Yesu alipozaliwa. Yawezekana baadaye walizaa watoto kama kawaida ya wanadamu.



*Kuzaliwa kwa Yesu*

## 2: 1-12 Kuja kwa mamajusi

Hao ni watu wa wapi na wa hali gani? Neno 'mamajusi' ni la Kiuajemi. Yasemekana kwamba lilikuwepo kundi la watu ambao walikuwa makuhani huko Uajemi. Baadaye neno lilitumika kwa watu walioshughulikia mambo ya nyota - baadhi yao walikuwa wataalamu, watu wazuri; ila baadhi hawakuwa wazuri, walitumia uchawi (Mdo.13:6). Walitoka mashariki, Arabuni au Babeli. Siku zile wengi wa mahali pengi walivutwa na mambo hayo, wakifikiri nyota zinahusika na matukio makuu ya historia. Nyakati zile wazo au uvumi ulikamata usikivu wa

wengi kwamba Mfalme mkuu atatokea kwa Wayahudi, naye atatawala ulimwengu na kuleta amani. Huenda tumaini la kupata Masihi lililisha wazo hilo na kulisaidia kuenea.

2: 1-2 Wataalamu hufikiri tafsiri "tumeona nyota yake mashariki" si tafsiri nzuri, bali badala ya 'mashariki' tusome 'ikizuka'. Kutokana na nyota hiyo na kuzuka kwake mamajusi waliamini kwamba Mfalme amezaliwa kwa Wayahudi. Wakaamua kufunga safari kwenda kumwabudu. Pengine nyota haikuwaongoza wakati wote wa safari, yatosha waliiona ikizuka, nayo ni ya pekee. Baada ya kumfikia Herode na kuondoka Yerusalemu ndipo ilionekana tena, nayo ikawaongoza mpaka ikakaa juu ya nyumba alimokuwamo Yesu. Twasoma walifurahi sana kuiona tena.

k.2 Ni dhahiri kwamba kitu kilichowaongoza kuja Yerusalemu ni imani yao kuwa Mfalme amezaliwa kutokana na kuzuka kwa nyota 'yake'. Hawakuwa na shabaha yoyote ila kumwona na kumsujudia. Bila shaka Mathayo mwandishi alitaka kutilia mkazo lengo lake la kumwonyesha Yesu kuwa Mfalme ambaye hata Wamataifa watampokea. Maneno ya swali lao “yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" laonyesha uhakika wao.

k.3-4 Habari za Herode Mkuu. Swali la hao wageni pamoja na kufika kwao kutoka mbali kungemtia mfalme yeyote wasiwasi nyingi, ila zaidi sana Herode. Kwanza hakuwa Myahudi kamili, alikuwa nusu Mwedomu. Alikuwa amewekwa na Warumi kuwa liwali K.K.47 ndipo kwa kuwasaidia katika vita vya nje na vya ndani walimweka kuwa 'mfalme' wa Wayahudi K.K.40. Kwa hiyo Wayahudi hawakumkubali moja kwa moja kuwa Mfalme wao halisi. Alipozaliwa Yesu Herode amekuwa Mfalme kwa muda mrefu. Aliitwa Herode Mkuu, na katika mengine alistahili kuitwa hivyo. Alifaulu kuleta amani, pia alikuwa mjenzi hodari, na jengo moja lililowafurahisha Wayahudi ni hekalu lao. Alipotaka aliweza kuwa mkarimu na wakati wa shida alitoa msaada kwa watu.

Kwa upande wa pili alikuwa na tabia ya wivu, alitawaliwa na mawazo ya kuonea mashaka watu, akiogopa kupinduliwa. Alimwua mkewe, mwana wake mkubwa, na wana wawili wengine; hata mmoja alisema kwamba “ni afadhali kuwa nguruwe wake kuliko kuwa mwana wake"!!! Kwa hiyo si vigumu kutambua wasiwasi wake alipojiwa na mamajusi na kuulizwa habari za mfalme ambaye tayari amezaliwa. Ni yeye na Yerusalemu yote iliyofadhaika - yawezekana watu waliogopa itikio la Herode au pengine maana yake hata wakuu hawakutoka kumpokea Huyo aliyezaliwa pasipo wao kujulishwa.

k.4 Ili apate jibu kwa mamajusi kuhusu mahali alipozaliwa, Herode aliwakusanya viongozi wa dini akiwauliza “Kristo azaliwa wapi"?, kumbe mara moja mawazo yamekwenda kwa Masihi; wakuu waliweza kumpa jibu sahihi kutoka Maandiko - ni Bethlehemu, mji wa Daudi, alipozaliwa Daudi; (1 Sam.16:1. Ling. na Lk. 2:4).

Mambo mawili ya kushangaza ni itikio la Herode na itikio la wakuu wa dini: Herode hakujihoji itakuwaje nikimwua Masihi aliyetumwa na Mungu; na wakuu hawakuonyesha nia yoyote kwenda kumwona Masihi wao, bila shaka kwa sababu Mungu amepitia kando yao na kuwajulisha wachungaji na kwa njia ya nyota hao wageni.

k.5-6 Mathayo amepambanisha 'ufalme wa hapa duniani' na 'ufalme wa Mbinguni'. Yesu atakuwa Mfalme Mchungaji atakayelisha na kutunza watu; mpole, mnyenyekevu, wa amani.

k.7 Herode alitumia hilo ili apange njia ya kumwua Kristo. Aliwapeleleza juu ya muda tangu nyota ilipozuka. Alitumia uongo akiwaomba wampitie ili apate habari kamili juu ya mahali alipo. Alificha mpango wa kumwua Kristo kwa kuwaambia anataka kumwendea na kumsujudia.

k.9-11 Walipofika Bethlehemu muda umepita, Yesu ni mtoto, si mchanga, yu katika nyumba si kibanda cha wanyama. Walimtolea vipawa vya thamani vilivyolingana na umaarufu wake - dhahabu kwa Mfalme, uvumba kwa Kuhani, na manemane kwa Mwokozi atakayekufa. (Zab. 45:8 72:15; Isa. 60:6; Mk. 15:23;- na Yn. 19:39), Walikuwa wangapi? Biblia haisemi, ila watu wamezoea kuwaza walikuwa watatu kwa sababu ya vipawa vitatu.

Baadaye walidhaniwa kuwa wafalme na kupewa majina ila hamna msingi kwa mawazo hayo. Kuja kwa Mamajusi ni ukumbusho wa Malkia wa Sheba aliyemjia Mfalme Sulemani, mwana wa Daudi.

**Tarehe Ya Kuzaliwa Kwa Yesu**

Wataalamu wa historia wameweka Kufa kwa Herode Mkuu K.K.4. Yesu alizaliwa kabla ya Herode kufa kwa hiyo tarehe itakuwa K.K.4 au kabla yake K.K.5 au 6. Kweli ni shida kusema Kristo alizaliwa kabla ya Kristo K.K.4-6. Sababu ni kwamba mpango wa kugawa historia kwa Kabla ya Kristo (K.K.) na Baada ya Kristo (B.K.) ulifanyika miaka mamia baada ya Kristo kuzaliwa. Ushuhuda mbalimbali ulitokea uliowapasa kurudisha miaka nyuma kidogo, wala si ajabu kwa sababu zamani zile hamna maandishi mengi ya kuwasaidia kama vitabu, mawe, n.k., na tofauti ni kidogo sana.

**2:13-15 Kukimbilia Misri**

Tangu alipozaliwa Yesu alipingwa na kukataliwa, ila mipango ya wanadamu haimzuii Mungu na makusudi yake ya milele.

k.13-14 Twaona Yesu amewekwa kabla ya mama yake kwa mfuatano wa maneno.

k.15 Kama desturi yake Mathayo ametia kifungu cha Maandiko kutoka Hosea 11: 1. Masihi ni Israeli ya kweli, naye ataonja mambo kama Israeli ya zamani.

Iwapo mwandishi hasemi wazi inaonekana anamkumbuka Musa na kumwona Yesu kama Musa wa pili, mkuu kuliko wa kwanza, atakayefanya wokovu ulio mkubwa kuliko ule wa Musa. Katika mambo mbalimbali Yesu na Musa hufanana - wote waliokolewa kwa ajabu wakati wa utoto wao; wote walikimbia makwao; wote walirudi makwao ili wafanye ukombozi. Musa alipatwa na hasira ya Farao na Yesu ya Herode. Katika historia ya watu wa Mungu nchi ya Misri imekuwa msaada wakati wa njaa pia nchi ya mateso na utumwa.
Neno kuu la kujifunza ni kuona jinsi awezavyo Mungu kwa upendo mkubwa kuuendeleza mpango wake wa wokovu bila kukata tamaa na bila kuudhika kati ya chuki na upinzani wa wanadamu.

Yusufu aliushiriki mpango wa Mungu kumsalimisha Yesu kwa kuongozwa naye kwa ndoto; naye akamtii. Mpango wa Herode, na nyuma yake wa Shetani, ulishindwa. Ilikuwa lazima wakati huo Kristo aishi ili baadaye, wakati ulioamriwa na Mungu, Kristo afe ili awakomboe wanadamu. Kwa Mathayo Maandiko yalitimizwa.

### 2:16-18 Kuuawa kwa watoto wa Bethlehemu

Herode alipotambua mamajusi wamerudi makwao bila kumpitia aliutekeleza mpango wa kuwaua watoto wa kiume wa Bethlehemu kulingana na muda ambao ndani yake alikuwa na uhakika Yesu atapatikana. Watoto waliouawa ni kama 'wafia dini' 'mashahidi' walitoa maisha yao iwapo hawakunia wala kufahamu wenyewe. Waligharimiwa maisha yao katika vita ambayo daima ipo kati ya Kristo na Shetani, kati ya nuru na giza, na kati ya utu wema na uovu. Mathayo alitumia Maandiko kuonyesha kutimizwa kwake (Yer.31:15-16). Maneno ya Yeremia yalihusu wakati watu wazuri walipopelekwa utumwani huko Babeli - nafsini mwake alisikia kama Raheli wa zamani bado alikuwa akilia-lia walipopitia karibu na kaburi lake huko Rama. Mungu alimshauri Yeremia asilie kwa sababu Raheli hakufa bure - katika kufa kwake Raheli alimzaa Benyamini. Mateso ya Babeli hayatakuwa bure - watarudi kutoka utumwani. Mateso ya hao watoto hayatakuwa bure, Kristo ataishi ili baadaye afe kwa wote. Hata mateso ya Kristo hayatakuwa bure, ulimwengu utakombolewa. Bila kutoka na bila kufahamu watoto wameingizwa katika vita, ambayo lengo la Shetani ni Kristo afe mapema ili asifanye kazi ya ukombozi.

### 2:19-23 Kurudi kutoka Misri na kuishi Nazareti

Yusufu aliongozwa na Mungu kwa njia ya ndoto kuondoka Misri. Sababu ni kwamba Herode Mkuu amekwisha fariki dunia. Walirudi Nazareti badala ya Bethlehemu kwa sababu Arkelau, mkali kuliko babaye ameshika utawala sehemu ya kusini; hakupewa yote aliyetawala babaye. Pia Nazareti ni mahali pao (Lk. 2:4). Mathayo aliona Maandiko yametimizwa katika habari hiyo ya Nazareti, shida ni kwamba hamna kifungu cha Agano la Kale kinachosema hivi, ila amesema "manabii" kama amejumlisha wazo lililowaelekeza watu kujua Masihi atakuwa mnyenyekevu, asiyetaka makubwa. Nazareti haukutajwa katika

Agano la Kale, haukuwa na sifa yoyote, ndani yake Wamataifa waliishi pamoja na Wayahudi.

*MASWALI: KUZALIWA KWA YESU*

1. *Mt.1:18-25. Utawafundisha Wakristo nini kuhusu uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke kabla ya ndoa kufuatana na kielelezo cha Mariamu na Yusufu?*
2. *Je! wafikiri ni jambo muhimu kukaza usafi wa maisha hasa kwa sababu siku hizi mambo yamelegea sana?*
3. *Utawasaidiaje vijana wa siku hizi?*
4. *Mungu aliwaleta wachungaji wa karibu kuja kumwabudu Yesu alipokuwa angali mdogo, vilevile aliwaleta mamajusi wa mbali kuja kumwabudu Yesu. Neno hilo lakusaidia kufahamu nini juu ya shabaha ya Mungu kuhusu wokovu wa watu? Neno hilo lagusaje huduma yako kwa watu mbalimbali?*

## MATAYARISHO KWA HUDUMA YAKE 3:1 -4:16

### 3: 1-12 Huduma ya Yohana Mbatizaji

Kabla ya Yesu kujidhihirisha kwa watu alipokuwa na umri wa miaka 30 (Lk. 3:23); aliishi Nazareti na wazazi wake. Kwa muda huo wote tunayo habari moja tu juu yake (Lk. 2:41-45). Yesu alipokuwa angali Nazareti Yohana Mbatizaji alitokea katika jangwa la Yudea. Watu walishtuka sana kwa sababu kwa miaka mia nne walikuwa hawajapata kuona nabii. Nabii Amosi aliyeishi miaka mia minane kabla ya Yesu na miaka mia nne kabla ya Malaki alitabiri kwamba Israeli itakosa nabii (Amo. 8: 11); na kweli neno hilo lilitimia. Malaki alitabiri kwamba 'Eliya' atakuja kabla ya Masihi (Mal.4:5).

Yohana aliitwa na kutumwa na Mungu, hata kuzaliwa kwake kwaonyesha kazi ya Mungu (Lk. 1: 15-25; 57-80). Alitokea jangwani katika mpango wa Mungu na ujumbe wake ulilenga mapenzi ya Mungu katika kuwatayarisha watu kwa Masihi.

Alitangaza kwa nguvu "tubuni, ufalme wa mbinguni umekaribia" maana yake yule mwenye ufalme yu mlangoni. Mathayo aliona Maandiko yametimia (Isa.40:3). Maisha yake magumu na maneno yake ya mamlaka na nguvu yalifanana na manabii wa kale (2 Waf. 1:8). Shabaha ya Yohana ilikuwa kuamsha taifa zima na kugusa watu maishani mwao ili watubu kwa kweli na kuonyesha toba lao kwa kubatizwa hadharani hali wakiziungama dhambi zao. Aliihukumu dhambi popote alipoikuta, kwa mfalme, kwa wakuu, na kwa watu. Ila hayo yote yalikuwa matayarisho tu. Atakapotokea Kristo Yeye atabatiza kwa Roho, Roho atawagusa watu kwa ndani na kwa uwezo tofauti na maji. Huduma ya Yohana na baadaye huduma ya Yesu zitasababisha utengano katika Israeli, Myahudi wa kweli atadhihirika na asiye wa kweli pia. Kudai kuwa "wa Abramu" haitoshi (Rum. 2:28-29).

Watu wengi walimwendea Yohana na kubatizwa naye. Hata Mafarisayo walimwendea, ila Yohana hakudanganywa na kuja kwao, aliwafananisha na nyoka wanaokimbia moto unaowaka vichakani. Aliwaonya kwa ukali sana. Wengine walimdhani Yohana kuwa Masihi, ila yeye alikataa kwa nguvu (Yn.1: 19ku). Wakati wote aliwaelekeza watu kwa "yule ajaye". Kweli Yohana alifanya kazi kubwa ya maana sana na kazi iliyo ngumu. Kuamsha watu si kazi rahisi na kuwakabidhi kwa mwingine baadaye si rahisi, lakini hayo yote alifanya kwa moyo, kwa furaha, na kwa kuvumilia magumu mengi.

27 -30 Alifaulu na Yesu alipotokea aliwakuta wengi waliokuwa na hamu sana kumsikia na kumfuata. Yohana aliamsha taifa zima na kulileta kwenye njia panda, kutokea kwa Masihi, na itikio lao kwa Masihi litasababisha matokeo makubwa, ama wataendelea kuwa taifa na kuwa watu wa Mungu, au watawekwa kando na Mungu na Wamataifa watapandikizwa mahali pao, (Mt. 8:10-13; Rum.1:11-24). Shoka limewekwa kwenye shina la mti, hukumu kuu itafanyika. Huduma ya Yohana ilianza kupungua na ya Yesu kuzidi. (Mengine kuhusu Yohana na huduma yake yapatikana katika Yn. 1:6-8; 19-37; 3:22-36. Kuzaliwa kwake Lk. 1:5-25, 57-80 na Kifo chake Mt. 14:3-12)

### 3:13-17 Yesu kubatizwa

Tumeona kwamba taifa zima waliuitika wito wa Yohana, walimwendea na kubatizwa naye katika Mto Yordani - ubatizo wa maji, wa toba.

Baadaye Yesu naye alimwendea ili abatizwe naye. Yesu hakuwa na dhambi za kutubia, kwa hiyo, Yesu binafsi hakuwa na haja ya ubatizo huo. Kama ni hivyo, kwa nini amwendee Yohana? Kwanza kwa sababu ya uhusiano mkubwa kati yao, huduma ya Yohana ilikuwa ya maana sana katika kutayarisha njia ya Masihi. Yesu amekuja ili awaokoe watu na dhambi zao, kwa hiyo tangu mwanzo wa huduma yake alijiweka mahali pao, na njia mojawapo ya kufanya hivyo ni kuupokea ubatizo wa toba, ili baadaye afe mahali pao, akiwa fidia ya dhambi zao. Mapema sana amekubali kutwisha dhambi zao na humo kwa ubatizo huo wa toba amezikataa, akijitoa kuwa mpatanishi wa dhambi. Pia ni wakati wa kumpokea Yohana kikazi na kuchukua hatua maalumu katika kukubali mapenzi ya Mungu kuwa Mwokozi wa ulimwengu. Miaka ya kimya huko Nazareti imekwisha, tangu sasa atajidhihirisha kwa watu.

k.14 Yesu alipofika mbele ya Yohana, Yohana hakupenda kumbatiza. Si wazi sababu yake. Huenda alimtambua kuwa na mamlaka na tofauti na wengine na alijua Masihi atamzidi (k.11). Tukisoma Yn. 1:32-34 inaonekana hakujua Yesu ni Masihi mpaka Roho alipomshukia. Yesu alimjibu kwa kumwambia kwamba walihitaji kufanya alivyotaka Mungu, ni hatua iliyopo katika kutekeleza mpango wa Mungu, "kutimiza haki" yawezekana maana yake ni kutunza uhusiano wao mwema na Mungu.

k.16 "mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua juu yake" (Isa. 64:1). Tukijumlisha twaweza kusema kwamba Yesu alijiweka

mahali pa wenye dhambi; Yesu alimpokea Yohana kikazi; Yesu alijiweka wakfu kwa huduma iliyo mbele yake; na Yesu aliwekwa rasmi kwa kazi yake kwa Roho kushuka juu yake na Baba kumtangaza kuwa Mwana wake, mpendwa wake. Si kwamba hakuwa na Roho kabla ya hapa, alikuwa naye, ila alipewa Roho ili awezeshwe kutimiza wito wa kuwa Masihi, na kusimikwa kuwa Mfalme wa Israeli (zamani Wafalme walipakwa mafuta). Si kwamba Yesu hakuwa Mwana wa Mungu, ila tangu sasa atadhihirika kuwa hivyo na Roho ni thibitisho la Umasihi wake Isa. 41:2; 42:1; 61:1 - hayo Maandiko yalikubalika kuwa yamhusu Masihi.

Sauti ya Baba yake: Bila shaka katika hatua kubwa, nzito, ya kujitwika *wito/utume* wa kuwa Masihi alifarijika sana na kutiwa moyo kwa sauti hiyo ya Babaye. Ndani ya maneno aliyosema Baba upo ufunuo wa aina ya Umasihi wake. Maneno yenyewe yalitoka Zab. 2:7 na Isa. 42:1. Katika Zab. 2:7 Bwana wa Israeli ameonekana kama anamvika taji Mwana wa Daudi kuwa Masihi. Katika Isa. 42: 1 kuna picha ya Mtumishi Mzuri atakayefanya mapenzi ya Mungu kwa njia ya kutumika na kutii. Atakuwa Mtumishi atakayeteswa kwa ajili ya watu wake (Isa. 53). Kwa hiyo, kwa maneno hayo aina ya Umasihi wake ilifunuliwa. Kwa hiyo Yesu ni Masihi - ni Mwana wa Daudi, ni Mwana wa Mungu, na ni Mtumishi atakayeteswa.

Sasa Yesu yu tayari kuanza Huduma yake, ila bado liko jambo moja mbele yake la kujaribiwa, yaani wito wake upimwe, Shetani apewe nafasi ya kumshambulia, na Yeye asimame imara tofauti na Adamu wa kwanza aliyeanguka.

Yawezekana Mathayo amewaza Wayahudi ambao, baada ya kutoka Misri, walipitia Bahari ya Shamu, mfano wa ubatizo, ndipo walipitia jangwani, mahali pa majaribu, mahali pa kupimwa. Yesu amebatizwa, sasa atakwenda jangwani ili ajaribiwe.

*MASWALI: YOHANA MBATIZAJI*
*Kuhusu huduma ya Yohana Mbatizaji bila shaka kuna mengi ya kujifunza. Kielelezo chake cha kumwachia Yesu uwanja wa kazi baada ya kufanya shughuli nyingi zilizo ngumu chakusaidiaje? Ikiwa utaitwa kumwachia mwingine kazi fulani baada ya wewe kuwa umejitoa kwelikweli katika ile kazi - kiutendaji utamkabidhi kwa hali gani? Pia utasema nini kwa watu?*

### 4: 1-11 Yesu kujaribiwa
Habari hii ilitoka kwa Yesu Mwenyewe, maana alikuwa peke yake jangwani. Kabla ya kuchunguza habari hiyo ni vema tuchunguze mazingira yake. Neno 'jaribu' lina maana ya 'kupimwa'. Yesu ametoka kwa ubatizo - katika ubatizo huo Roho amemshukia na Baba amemshuhudia. Amehakikishiwa kabisa kuwa Mwana wa Mungu, Mpendwa wake, ambaye juu yake mpango wa kuokoa wanadamu utatimizwa. Yu katika hali ya kujua ni Mwana wa Mungu, pia ni Masihi, na Mtumishi wa kuteswa.

Hivyo yampasa apimwe ili aonekane kuwa Mwana Mtiifu wa Baba, ndiyo maana ya k.1 "alipandishwa na Roho ili ajaribiwe na Shetani". Ni mapenzi ya

Mungu apimwe kuhusu Uana wake na Umasihi wake. Shetani ni chombo ambacho Mungu alikitumia akimruhusu kumpima Mwana wake - nia ya Shetani ni kumpinga. Twaona unyenyekevu mkuu wa Mungu katika kumruhusu Shetani ampime Mwana wake mpendwa.

Alipandishwa nyikani, mahali pagumu, pa ukimya, pa upweke, pa shida kwa mahitaji ya kimwili, ila pazuri kwa kutafakari juu ya ubatizo wake, Uana wake, na umasihi wake. Sehemu hiyo inatukumbusha sana Israeli ya zamani na 'kupimwa kwao' jangwani (Kum. 8:2-3). Ni msaada sana kusoma Kum. 6-8 majibu yote ya Yesu yalitoka humo. Yesu ni Israeli wa kweli (Mt. 2:15). Yesu amekuja kumshambulia Shetani juu ya mamlaka yake na vita kali itatokea kati yao Yesu anapouleta Ufalme wake kati ya wanadamu (Mt. 12:24ku. 13:19, 39; 16:23). k.2 Yesu alifunga siku 40: Yawezekana alikula kile kilichopatikana jangwani, hivyo, baada ya siku 40 alisikia njaa kali. (Musa - Kut.34:28; Kum. 9:9,18; Eliya-1 Waf.19:8, na Israeli miaka 40 jangwani wakilishwa na mana Kum.8:2-3). Yesu hakuepa shida za kimwili, alikuwa na ubinadamu kama wetu, alisikia njaa.

4:3-4 Jaribu la kwanza
Shetani alimjia Yesu aliposikia njaa, na kumshambulia katika "Uana wake", Je! ana haja ya kusikia njaa kama ni Mwana mwenye uwezo wa kutosheleza mahitaji yake? (Mt. 14:15-21; 15:32-38) Yesu alikumbuka funzo la Mungu kwa Israeli jangwani (Kum. 8:3), njaa ni kitu cha kumfundisha mtu kumtegemea Baba. Katika huduma yake ya Neno la Mungu atapatikana na magumu mengi ya kimwili (Mt. 8:20). Akiepa magumu hayo atashindwa kuutimiza wito wake. Hana budi kumtii Baba kikamilifu. Pengine Shetani alitaka kumtilia mashaka kuhusu Uana wake ila zaidi alitaka na kumshawishi asionyeshe utayari wa kumtii Babaye, utii ulio halali kwa Mwana wa kweli.

Pamoja na hayo apaswa kuishi kama wanadamu wasio na uwezo wa kubadili mawe kuwa mkate. Baadaye aliwafundisha wanafunzi kuomba "Baba yetu .... utupe leo riziki zetu". Kwa njia hiyo astahili kuwa Mwokozi na Bwana wetu. Mungu alitunza Israeli jangwani. Shetani alitaka kuutikisa uhusiano wake na Baba kwa kutumia maneno ‘ukiwa ndiye' na kwa shauri lake.

"Si kwa mkate tu" Yesu hakusema "si kwa mkate" aliongeza neno la maana "tu" maisha yetu ni ya kimwili, twahitaji chakula ila pia ni ya kiroho, ya kushirikiana na Mungu. Twahitaji kulitii Neno la Mungu "tafuteni kwanza" (Mt. 6:33).

4:5-7 Jaribu la pili
"Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu ..... " kama alimchukua kwa kweli au ni katika maono au mawazo, hatujui, (Eze.8:1-3; 11:24). Yesu kama Mwana wa

Mungu aweza kuudai ulinzi ulioahidiwa katika Zab.91. Shetani alidaka k.11 na 12 katika ahadi za Zab.91. Shetani alitaka Yesu amlazimishe Baba kuuonyesha ulinzi si katika mambo yatakayomjia siku kwa siku bali kwa njia ya pekee; akiwa juu ya kinara cha hekalu ajitupe chini. Kwa njia ya kujitupa chini na Baba kumsalimisha hatakuwa na mashaka tena juu ya Uana wake.

Lakini Yesu alikumbuka jinsi Israeli zamani walivyomjaribu Mungu huko Massa (Kut.17:2-7 hasa k.7). Yesu kama Mwana budi aishi kwa kumwamini Babaye bila kujitia mahali pagumu halafu amlazimishe amwokoe. Katika kuyatumia Maandiko Shetani aliachia maneno machache ya maana "atakulinda katika njia zako zote", kwa kweli Yesu atahitaji kulindwa na Baba mara nyingi kutokana na upinzani na ukali wa adui zake, na kwa sababu ya ugumu wa watu kumwamini, watu waliodai ishara daima. Kwa hiyo twaona shabaha kuu ya Shetani ilikuwa kuutikisa uhusiano wake na Baba, na kwa ujanja alilitumia Neno la Mungu isivyo halali. Kuna ukumbusho wa Mal. 3:1-2 wengi walifikiri kwamba Masihi atatokea hekaluni na ishara kubwa zitafanyika, (Isa.35). Kweli Yesu atafanya ishara, ila hazitalenga faida yake wala hazitapinga mapenzi ya Baba yake

4:8-10 Jaribu la tatu
Yesu alikuja kufanya vita na Shetani juu ya "mamlaka yake ulimwenguni" (Lk. 4:6; Yn. 12:31; 1Yoh. 3:8; 5:19). Vita hiyo itakuwa kali mno. Shetani alitaka kumpa Yesu milki yake bila vita, mradi Yesu aridhiane naye. Amwasi Baba yake, asipitie njia ya msalaba, aiache njia ngumu, afuate njia ya mkato isiyo na maumivu na machozi. Yesu alikuwa amekuja ili atawale yote mbinguni na duniani (Dan. 7:14; Mt. 28:18). Zaburi 2 iliyomhusu Masihi ilitoa ahadi ya kurithi mataifa yote (Zab. 2:8) (tukumbuke kwamba Baba yake alitumia maneno ya Zaburi hiyo alipobatizwa) Israeli ya zamani hawakuwa tayari kujitenga na watu na miungu ya Kanaani (Kum. 6:10-15 hasa k13 Kut.32:1-6). Daima Shetani hutafuta kujiweka mahali pa Mungu pa kusujudiwa, na kuuondoa utiifu wetu kwa Mungu na kujichukulia kwake. Hapo Yesu alichoka na hilo na udanganyifu wa Shetani, alitambua hilo yake ya kutenganisha Uana wake na Umasihi wake wa kuwa Mtumishi atakayeteswa, akamfukuza kwa nguvu.
k.11 Kipindi hicho cha kuwa jangwani kilimgharimia Yesu nguvu, na malaika walikuja kumhudumia, hatujui kama walimletea chakula na kumtia nguvu au vipi. Neno la kuona ni kwamba Mungu alituma msaada, kweli Mungu atamlinda katika njia zake zote, hata za njaa na magumu yote.

Iwapo tumeangalia majaribu hayo kwa kulinganisha na Israeli jangwani, vilevile twaweza kuyalinganisha na ya Adamu na Hawa bustanini (Mwa. 3). Yesu kama mwanadamu alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote (Ebr. 2: 14ku. 4: 15-16). Adamu na Hawa walijaribiwa kuhusu chakula Mwa. 3:6 na kwa kujifurahisha Mwa. 3:6 na kwa kutoka kuwa kama Mungu: Mwa. 3:5. (Ling.na 1 Yoh. 2:15-17).

Twajifunza kwamba sisi kama watoto wa Mungu twapaswa kumtii Baba na kumtegemea. Magumu na shida ni njia ya kuupima utii wetu, ahadi yake husimama, atatulinda katika njia zetu zote. Lazima tumfukuze Shetani kwa kutumia Neno la Mungu hali tumelikolewa sana na kulifahamu kwa ndani si kwa juujuu. Tufuate kielelezo cha Yesu, hakuingia majadiliano na Shetani, hakuonyesha 'hekima' au 'kiburi' cha kujitegemea.

Ilikuwa lazima Yesu ayashinde majaribu, ilikuwa kazi ya Roho kumshindia, na kwa kuyapitia salama alikuwa amepiga hatua kubwa katika kumtii Baba, ambao upeo utafika atakapoitwa kutoa maisha yake msalabani. (Flp. 2:8 na Ebr. 5:7-8). Tutashinda tukitaka na tukitafuta kufanya mapenzi ya Mungu.

**4:12-16 Yesu kwenda Galilaya**

Yohana Mbatizaji alifungwa gerezani ndipo Yesu akaondoka kwenda Galilaya. Alibadili mahali pa kufanyia kazi na kubadili kazi yenyewe. Kusini alikuwa akibatiza watu (Yn.3:22ku. 4:1-2). Alipofika kaskazini alianza kutembea huko na huko akihubiri na kuponya wagonjwa, kutoa pepo, na kufundisha (Mt. 4:23-25). Huduma ya Yohana itapungua na ya Kwake itazidi.

k.13 Yesu aliweka makao yake Kapernaumu (9:1 na 17:24-25). Si kwamba aliishi pale moja kwa moja (8:20) ila alirudi pale kila baada ya safari. Kapernaumu ulikuwa mji wa pwani, mji ulio hai, wa watu waliofuata shughuli mbalimbali. Hapa alikutana na watu wengi na habari zake zilienea kwa upesi, watu wa Nazareti walikuwa wamemkataa (Lk. 4: 28-30).

Kwa nini Yesu aliye Masihi wa Wayahudi aanze huduma yake Galilaya penye wengi wasio Wayahudi? kumbe kama desturi ya Mathayo ilivyo aliona jibu lapatikana katika unabii wa Isa. 8: 23-9:1. WaMataifa wataangaziwa mwanga mkuu, katika maeneo yaliyodharauliwa Masihi ataanza huduma yake.
Sehemu hii kubwa inahusu Huduma ya Yesu kati ya watu huko Galilaya, inafuatwa na Huduma katika Yudea. Ilianza Yesu alipotokea akihubiri na iliendelea mpaka wanafunzi walipomkiri kuwa Mwana wa Mungu na Masihi (16:21). Hatujui ilichukua muda gani. Mathayo hakupanga mambo katika mfuatano wa kutokea kwake, ila alikusanya mambo yaliyofanana pamoja, k.m. mafundisho 5-7; miujiza 8-9; mifano 13; n.k. Imani ya wanafunzi ilizidi kukua katika muda huo na upinzani wa wakuu wa dini ulizidi pia.

*MASWALI: MAJARIBU YA YESU:*

*Twajua majaribu ya Bwana Yesu yalikuwa ya pekee, yakihusu Wito na Utume wake.*

*Mapasta na wainjilisti n.k. wameitwa na Mungu na kupewa Utume wa Kuhubiri na Kufundisha n.k. Katika huduma yako Shetani hukuwekea mitego gani na kukushambulia kwa mambo gani hasa? Yesu alishinda kwa kumtii Baba na kwa*

*kuyafahamu Maandiko na kuyatii. Wewe utashindaje majaribu yako? Una mpango gani wa maombi na ya kufahamu Maandiko? Unabahatisha nafasi za kuomba na kutafakari Neno la Mungu? au una mpango maalumu? Eleza.*

## UTANGULIZI WA HUDUMA 4:17-25

**4:17 Yesu alianza kuhubiri**
"kutokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri .. tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia". Ni jambo jipya, Yesu alianza kuhubiri; na ujumbe ni uleule wa Yohana Mbatizaji (3:2); na wa wanafunzi waliotumwa naye baadaye (10:7).

Yesu aliita watu wakate shauri la kutubu, maana yake wamrudie Mungu na sababu ni kwamba hali mpya imetokea kutokana na Kuja Kwake - Ufalme wa Mbinguni umekaribia, upo katika Yeye, nao wataziona baraka zake katika kuponya watu, kufukuza pepo, kusamehe dhambi na kuweka watu huru. 'ufalme wa mbinguni' ni nini? - ni Mungu kumiliki, mapenzi yake kutendeka, na makusudi yake kutimizwa. Hayo yote yawezekana kwa njia ya Yesu Mfalme. Kwa hiyo wito ni "tubuni" watu wamtangulize Mungu maishani mwao. Hayo yote yalingana na Sala ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake "Ufalme wako uje, mapenzi yako yafanyike". Katika kumiliki, sehemu moja ni kuhukumu (13:41, 16:27, 19:28, 25:3Iku). Watu watahukumiwa kulingana na jinsi walivyouitika wito wa Yesu (7:21-23; 25:24ku), - kwa hiyo 'tubuni' ni jambo muhimu sana.

**4:18-22 Wanafunzi wanne kuitwa**
Simoni Petro na Andrea walikuwa ndugu, na Yakobo na Yohana vilevile, na wote wanne washirika kikazi, (Lk. 5:10). Simoni na Andrea walitoka Bethsaida (Yn. 1:44) halafu walikuja kuishi Kapernaumu (8:5,14). Petro, Yakobo, na Yohana walishirikiana na Yesu kwa ukaribu sana (Mk. 5:37; Mt. 17:1, 26:37). Mathayo hakutoa habari jinsi Mitume wengine walivyoitwa isipokuwa ya yeye mwenyewe (9:9); huenda shabaha yake ilikuwa kuonyesha kuwa wanafunzi walishirikiana na Yesu katika huduma yake. Bahari ya Galilaya ni kama maili 13 kwa 7 (kilometa 21 kwa 11). Biashara ya samaki ilisitawi, wavuvi wengine walikuwa na vyombo vyao wenyewe na uwezo wa kuajiri watumishi.

k.19 "nifuateni" yaani njooni nyuma yangu. Marabi walikuwa na wafuasi walioandamana nao na kusikiliza mafundisho yao, ila hawakuwaita watu, tofauti na Yesu aliyewaita watu, pia aliwashirikisha kazi "nitawafanya kuwa wavuvi wa watu".

k.20-22 "mara wakaziacha nyavu zao" na "mara wakakiacha chombo na baba yao". Neno 'mara' ni ishara ya mamlaka ya wito wa Yesu. Si mara ya kwanza wamekutana naye (taz. Yn. 1:35-42 Lk. 5:1 ku) ila ni mara ya kwanza kuitwa naye kuondoka nyumbani na kazini. Si wauze mali wala kuvunja uhusiano wao wa nyumbani (8:5,14 na Yn.21:3) ila tangu hapo maisha yao ya kila siku

yameingiliwa (Ling. Mt. 19:27-29).
4:23-25 Kujumlisha Huduma ya Yesu

Kila mara Mathayo alipenda kujumlisha mambo (8:16, 9:35, 12:15, 14:35-36, 15:30-31, 19:1-2) Hapo amejumlisha shughuli za Yesu kuwa:
i. Kufundisha katika masinagogi ya Wayahudi;
ii. Kutangaza habari njema ya Ufalme hadharani;
iii. Kuonyesha uwezo wa Ufalme kwa kuwaponya wagonjwa wa kila aina, kutoa pepo, n.k. dalili na uthibitisho wa Kufika kwa Ufalme katika Yeye.

Mathayo alionyesha upana wa kazi yake - k.23 Galilaya; k.24 sifa zake kufika mpaka Shamu; k.25 watu kumwendea kutoka kusini, mashariki, na WaMataifa kumjia. Wanafunzi walikuwa naye na baadaye atawatuma kufanya kama Yeye, sura ya kumi.

*MASWALI: YESU ALIWAITA WANAFUNZI WA KWANZA*

*Yesu aliwaita watu kadha kuwa Naye ili awatayarishe kwa kazi ya Kuhubiri Injili baada ya Yeye kuondoka.*

*"kuwa Naye" kweli hatuwezi kuwa Naye kama hao walivyokuwa. Utawezaje kuwa Naye? Utajengaje uhusiano wako na Bwana Yesu? Je! unafikiri ni hao walio na wito tu ambao wangeruhusiwa kuwa mapasta n.k? Kanisa Iifanye nini kuhakikishia kwamba watumishi wake wameitwa kweli? Vilevile Kanisa likaze nini kuhusu maandalio yao kikazi? Wa kwanza walijifunza kwa Yesu Mwenyewe, mara nyingi wa siku hizi wapelekwe masomoni ndipo wawekwa. Je! waonaje njia hii? ni nzuri? ina upungufu? Eleza.*

*Wewe una mawazo gani kuhusu matayarisho ya watumishi wa Kanisa?*

## MAFUNDISHO YA YESU KWA WANAFUNZI WAKE 5:1 - 7:29

Sura ya 5 hadi 7 ni mkusanyo wa mafundisho ya Yesu, mara nyingi imeitwa 'Hotuba ya Mlimani'. Katika sehemu hiyo twaona ufundi wa Mathayo katika kukusanya na kupanga mafundisho ya Yesu juu ya 'uanafunzi'. Yawezekana Yesu hakutoa yote yaliyomo mara moja katika hotuba moja. Karibu nusu yake yamo katika Luka 6:20-49 'Hotuba ya Bondeni' inaanza na 'heri' na kumalizika na Mfano wa wajenzi wawili ila haifanani sana, Luka ameingiza 'ole' kadha na kuweka mikazo tofauti. Katika Luka sehemu za hotuba zapatikana hapa na pale.

Kwa sababu Mathayo ametaja mlimani watu wamefikiri kwamba alitaka kumwonyesha Yesu kuwa Musa wa pili, mwenye mamlaka mpya na mwenye kuleta torati mpya. Ila kwa vyovyote tofauti ni kubwa kati ya torati ya Yesu na

ile ya Musa, hata ni vigumu kuiwaza kuwa torati. Kama si torati mpya ni nini basi? Ni mwongozo wa maisha kwa yule anayeitika wito wa Yesu wa kuingia Ufalme wake na kumfuata Yeye. Maisha hayo si katika kuzishika sheria kadha na kufanya matendo kadha za nje; La! hasa ni mwongozo kuhusu hali za ndani, tabia na mawazo mwa moyoni, ni kugusa nia na sababu za mtu.

Ni kwa 'wafuasi wake', ni itikio lao la upendo kwa Bwana wao kwa sababu ya 'neema' waliyotendewa walipopokelewa naye na kusamehewa mbali na 'sheria'. Ni sheria mpya ya Agano Jipya kama Yeremia alivyotabiri (Yer.31:33) "nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika".

Yesu alipotoa mwongozo huo alikuwa akipinga hali ya Mafarisayo na waandishi walioweka visheria vingi vya kushikiliwa jinsi zilivyoandikwa. Sheria mpya, yaani mwongozo alioutoa Yesu haina shabaha ya kushikiliwa kila neno kama lilivyoandikwa. Madai yake huzidi sheria yoyote iwezayo kutungwa, na huzidi uwezo wa mwanadamu awaye yote kutimiza, maana lengo ni 'ukamilifu' (5:48). Ni kutuongoza katika maisha ya kumpenda na kumtii Mungu kama Baba, na mengi yahusu uhusiano wetu kibinafsi na Mungu na watu. Yesu yu kati ya Hotuba hiyo, wanafunzi watateswa kwa ajili yake (5:11). Alionyesha mamlaka yake Mwenyewe aliposema "bali Mimi nawaambieni" (k.22, 28, 32, 34, 39, 44). Taz. 17-20 alipotoa maelezo juu ya sheria za zamani na juu ya mafunzo ya marabi, yaani mapokeo - alichimba chini kwenye viini vya sheria ili afunue mapenzi ya Mungu kuwa nini hasa. 'Mwisho' wa mtu utategemea itikio lake kwa Yesu na mafundisho yake (7:24-27).

## 5: 1-2 Utangulizi

k.1 Yesu aliketi kama marabi walivyofanya walipowafundisha watu wao. "wanafunzi walimjia" hasa hotuba ni kwao, ila si wanafunzi tu waliosikiliza, Mathayo ametaja 'makutano' (7:28-29).

### 5:3·10 Wanafunzi - baraka zao

Heri hizi zimepangwa kwa mfuatano ili zikumbukwe kwa urahisi. Ni katika mtindo wa shairi zikitaja aliye 'heri' ndipo thawabu yake. Neno 'heri' lina maana gani? ni kama pongezi, baraka, furaha.

Walio heri ni watu wa kupongezwa, watu wa furaha na baraka, watu wa kuonewa 'wivu mwema' kwa sababu ya uheri wao. Heri hizo zaonyesha njia bora ya kuishi, yenye sifa, yaliyo na baraka wakati huo na kuwa na thawabu

baadaye. Katika Agano la Kale heri zilitajwa (Zab. 1:1; Isa. 61:1, n.k) ila ni Yesu aliyeziweka pamoja akionyesha furaha na baraka za ufalme wake na za wale wajiwekao chini ya milki ya Mungu. Ila ni kinyume kabisa cha mawazo ya wanadamu, zinapindua kabisa jinsi wanadamu wanavyoziwaza baraka; wanadamu wa kawaida wasingalithubutu kumpongeza mtu kwa hali hizo.

5:3. "heri walio maskini wa roho" mtu maskini huwa na hali gani? ni mtu asiye na kitu, mtu aliyefilisika. Maskini wa roho ni akina nani? ni wale wanaojitambua kuwa 'hawana kitu kiroho' hawawezi kufanya lolote jema bila msaada wa Mungu; wenyewe hawawezi kufanya kama Mungu anavyowataka. Ni watu wanaojiona ni 'watupu' mbele za Mungu, na kwa sababu hiyo wako tayari kumtegemea Mungu kabisa, na katika uaminifu wao wako tayari kupata 'hasara' ya vitu vyao kwa ajili yake. "Ufalme wa mbinguni ni wao" hao ndio watu wa Mungu, milki yake, na raia wa urithi wake.

Heri hii ya kwanza ni msingi, kwa sababu bila hali hiyo mtu hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Sharti moja ya kuingia ni kutambua kwamba kwa vyovyote hakuna hata kitu kimoja, au hali yoyote, au jema lolote, litakalomfanya mtu akubalike mbele za Mungu (Yn.15:5) "sina cha mkononi, naja msalabani" ni njia ya kumwendea Yesu, tumeokolewa kwa neema (Lk 18:13; 1 Kor.1:28-29; Efe.2:8-9).

Heri hii ni kinyume kabisa cha mawazo ya wanadamu, ni nani apendaye kuwa maskini? Wenye kiburi, na wanaojiona na kujitegemea, hata katika mambo ya Mungu hawana sehemu katika ufalme wa Mungu. Ukoo, ukabila, elimu, kisomo, mali na vitu, na uzuri wowote si kitu mbele za Mungu.

5:4 "heri wenye huzuni" Ni nani apendaye huzuni? Kwa kawaida watu hawapendi kuwa na huzuni, maombolezo, kilio, n.k. afadhali kufurahi na kucheka. Yesu alisema "ole wenu wenye kucheka sasa" (Lk 7:25). Yesu Mwenyewe aliitwa "mtu wa huzuni" (Isa.52:2). Alilia kwa ajili ya Yerusalemu (Lk 19:1 na penye kaburi la Lazaro Yn.11:35). Ni huzuni kwa ajili ya nini? Ni aina gani ya huzuni ambayo Yesu amesema ni "heri"? Pengine ni kwa wale wasio na maisha ya raha, waliopatwa na shida, huenda kutokana na uaminifu wao kwa Mungu, wale wanaopingwa nyumbani, kazini. n.k. (Isa.61:2). Yawezekana ni wenye huzuni juu ya dhambi zao na za wengine, wakifahamu kwamba ni dhambi iliyosababisha Yesu afe, na mtu akiendelea katika dhambi Kristo asulibishwe tena (Ebr 6:6; 10:28-29). Pia walio na huzuni kwa ajili ya uovu usababishao shida nyingi zilizomo duniani. Uheri wao ni katika wokovu wa Bwana Yesu, raha yao yatoka kwa Yesu, nayo yapita raha zote za dunia hii (Mt.11:28-29). "watafarijika" Mungu atawafariji, atayafuta machozi yao, atawatia mafuta ya kulainisha majeraha na majonzi yao ya rohoni. Twaona kwamba hali hii ni kinyume cha mawazo ya wanadamu. Kwa kawaida ni vigumu kumpongeza mtu mwenye huzuni na kumwita heri, maana atawezaje kusikia baraka na furaha?

5:5 "heri wenye upole" Kwa kawaida watu huvutwa na uwezo, ushupavu, uhodari, ushujaa. Mara nyingi watu watumiao mabavu na kujisukuma mbele hufanikiwa. Wayahudi walitamani kupata Masihi atakayewafanya kuwa taifa la mbele, wa kufukuza Warumi, mtu wa fahari. Kumbe Yesu alikuja kwa upole, bila fahari, bila kutumia nguvu, bila kujitafutia makuu ya dunia hii, alidharauliwa (11:29,12:15-21,21:5). Upole ni hali ya watu wa Mungu tangu awali; Abramu,

Musa n.k. Upole ni nini hasa? Upole si udhaifu. Mpole aweza kuwa imara, si mtu wa kukubali mambo yote, si mtu wa kuridhiana na mabaya, la! Mpole ana nguvu ya ndani, anatawala mapenzi yake na hasira yake. Hasa mpole huushangaa upendo wa Mungu katika kumpokea, huwa tayari kujifunza kwa wengine, aweza kushauriwa, haoni kana kwamba anajua yote. Upole ni hali ya ndani ya kutokujiona na kutokujitanguliza (Zab. 37 hasa k11). "hao watairithi nchi" Mpole atapata haki yake kwa sababu Mungu yu upande wake wa kumpigania, atampatia lile ambalo mwenyewe hakuthubutu kulishindania. Mungu atakapowaondoa wenye kiburi waliompinga ndipo wapole watabaki na kurithi nchi.

5:6 "heri wenye njaa na kiu ya haki". Njaa na kiu ni vitu vikali vinavyomwuma mtu sana. Anayesikia hawezi kutulia mpaka amepata kula au kunywa, wala hatoshelezwi na kubembelezwa na kitu kingine. Mwenye njaa na kiu ya haki ni mtu wa aina gani? Ni mtu anayetamani sana kutunza uhusiano wake na Mungu kwa kumwamini na kumtii na kumpendeza. Anataka kuona ushindi wa Mungu juu ya uovu na ufalme wake kusimamishwa (Zab. 42:1-2) "atashibishwa". Atafurahi kuona makusudi ya Mungu yakitekelezwa na kusikia raha ya ndani anaposhirikiana na Mungu wake na kufanya mapenzi yake.

5:7 "heri mwenye rehema" Rehema hasa inahusu uhusiano wetu na wengine, jinsi tunavyowawaza na kuwafanyia. Mungu wetu ni wa 'rehema' na kwa rehema tumejaliwa kuwa watoto wake, ametuhurumia. Kurehemu ni kufanya nini? ni kuwafadhili wengine, kuwasaidia, kuwatakia heri na mafanikio. Mungu kwa rehema zake alitupenda sisi wenye dhambi kwa kumtuma Yesu ili atukomboe. Vilevile sisi nasi katika kurehemu watu twatambua ni dhambi iliyo shida ya mtu, wajibu wetu ni kumpenda na kumhurumia siyo kumlaumu. Sote tu wenye dhambi, tunahitaji rehema za Mungu, tunaporehemu mtu twamshirikisha kile tulichopata kwa Mungu (2Tim.1 : 16-18; 1 Tim.1 : 15-16). 'hao watapata rehema' kadiri tunavyowarehemu watu ndivyo na Mungu atakavyoendelea kuturehemu, wala hakuna wakati ambapo hatutahitaji rehema zake.

5:8 "heri wenye moyo safi" (Zab.24:3-4). Yesu alisema sana juu ya usafi wa ndani, kinyume cha Mafarisayo waliokaza usafi wa nje (15:2,8,18-20; 23:25-26). Yesu alifahamu kwamba shida kubwa ya wanadamu ni dhambi katika utu wa ndani na ni dhambi inayotupofusha tusimwone Mungu. Moyo ni kiini cha mtu. Adamu wa kwanza aliishi penye mazingara mazuri ya Bustani ya Adeni, lakini alianguka! Adamu wa mwisho, yaani Yesu aliishi katikati ya dunia mbovu, hakuanguka! kwa sababu alikuwa na moyo safi, hakuwa na dhambi. Moyo safi ni nini hasa? ni kuwa na nia moja na lengo moja la kumpendeza Mungu, ni kuwa mwaminifu Kwake. Ya ndani na ya nje kulingana, kuwa wa kweli. Mwenye moyo safi halengi mawili, hana unafiki wala maficho. Moyo umetakaswa na damu ya Kristo, na kwa Neno la Mungu anazidi kujitakasa (Ebr. 11:27).

"hao watamwona Mungu" Musa alimtii Mungu kama mtu amwonaye Yeye asiyeonekana. Bila utakatifu mtu hatamwona Bwana (Ebr. 12:14; Ufu. 21:27;

22:14). Kumwona Mungu na kutambua mapenzi yake na kushirikiana naye kiroho katika upendo usiogawanyika. Zaidi tutamwona Mungu mbinguni (1Yoh.3:2).

5:9 "heri wapatanishi" Mungu wetu ni 'wa amani' na Yesu aliondoka mahali pa juu, akaja duniani, kusudi afanye upatanisho iwapo uasi wote na makosa yalikuwa upande wetu. 'alifanya amani' Wayahudi walitaka Masihi wa kufanya vita ya kuwaondoa Warumi, lakini Yesu alikuja kwa upole ili afanye upatanisho kati ya Mungu na wanadamu, na kuleta uwezekano wa watu kuishi kwa amani wao kwa wao kwa kuondoa dhambi iliyo asili ya chuki, vita, wivu, kiburi, udhalimu na vitu vyote viletavyo uadui kati ya watu. Kuishi kwa amani si kuridhiana na mabaya wala kuhesabu mema na mabaya kuwa mamoja, La! Mpatanishi atajitahidi kutengeneza mabaya kwa upole na kwa haki, atajihadhari asilete vikwazo. Mtu wa amani ni mwepesi wa kusikia na kusikiliza; si mwepesi wa kusema wala kukasirika (Yak.1:19). Atatafuta ukweli kwa kuchunguza bila upendeleo. Kwa vyovyote atapenda amani na kuchukia na kuepukana na ugomvi na majadiliano yasiyo ya maana. Atawasaidia watu ili wapate kupatana.

"Wataitwa wana wa Mungu" kwa nini? kwa sababu kwa tabia wamefanana na Baba na Bwana Yesu, wakiishi kama wana wao.

5:10 "heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki"; Wakristo wa kweli wataudhiwa kama Bwana wao alivyoudhiwa. Yesu aliwaonya wanafunzi wake itakuwa hivyo, na Paulo vilevile aliwaonya waumini wapya (Mdo.14:22; 1The.33; Lk 6:26). Maisha ya tofauti ya Wakristo wa kweli ni hukumu kali juu ya maisha mabovu ya wengine. Hawana udhuru tena kwa maisha yao mabovu. Ila sharti maudhi yawe kwa ajili ya haki (1 Pet. 4:15) kwa kusimama upande wa ukweli, haki, na utakatifu unaodaiwa na Mungu na kwa kukataa kuridhiana na hali za dunia; (2Tim.3:12). "maana ufalme wa mbinguni ni wao" wanamiliki pamoja na Mungu kwa kuwa wamekubali kufuata kanuni za ufalme kiasi cha kukubali maudhi. Watazidi kumiliki pamoja na Mungu.

Heri ya kwanza ilikuwa na baraka 'ufalme wa mbinguni ni wao’ na hiyo ya 8 vivyo-hivyo

**5:11-16 Wanafunzi - upekee wao**
'heri ninyi' hapo Yesu asema moja kwa moja kwa wanafunzi wake walioketi na kumsikiliza. Yesu alijua kwamba wao watateswa sana kwa ajili yake, baadhi watauawa, wengine watafungwa, na kupigwa na kushutumiwa. Atakapoondoka Yeye ulimwengu utawageukia watu wake na kuwashambulia. Wanafunzi wameitwa kufurahi na kushangilia, siyo kuvumilia tu. Kwa nini? Kwanza, kwa sababu thawabu yao ni kubwa mbinguni; pili, kwa sababu wamo katika mfuatano mwema wa watu wa Mungu wa tangu zamani, ambaye Yesu ni kiongozi mkuu na kielelezo chema. Watahakikishiwa ukweli wa imani yao. Wakristo wameingizwa katika vita kuu iliyo kati ya Yesu na Shetani, na kati ya

utu wema na uovu, na nuru na giza. Katika vita haikosi watu kujeruhiwa na kuuawa. Mkristo hafurahi eti! ameteswa! La! ila afurahi kwa sababu amedhihirishwa kuwa mfuasi wa kweli wa Kristo (2Kor. 4: 17 -18).

Katika neno hilo twaona jinsi Yesu anavyopindua kawaida za watu kuwaza. Mtu hawezi kuona ni 'heri' anapopata shida na upinzani, kawaida atataka 'pole' si 'pongezi !!

5:13-15 "ninyi ni chumvi ya dunia" "ninyi ni nuru ya ulimwengu". Kwa mifano ya chumvi na nuru Yesu alitaka kufundisha wanafunzi wake juu ya uhusiano wao na dunia na kazi yao katika dunia. Wakristo wamo duniani, ila si wa dunia. Chumvi si chakula, ila inawekwa katika chakula kuleta 'ladha' zuri, kazi yake ni kukolea chakula. Tena kazi nyingine ya chumvi ni kuzuia maozo. Vivyo hivyo Wakristo kwa wito wao hufanya dunia kuwa mahali pazuri na safi. Waleta 'ladha' na tukichunguza historia twaona ya kuwa mengi mema yametokana na bidii zao. Pia maovu mengi yamezuiliwa kwa Wakristo kupigana ki-ushujaa na mabaya. Ila wapaswa kuwa tofauti na wengine ili waitimize shabaha ya kuwa 'chumvi', tofauti katika kanuni za kuishi kwao, katika mienendo yao ya kila siku, katika tabia zao, na kwa jinsi wanavyokabili matatizo mbalimbali. Wamo duniani ili 'wamdhihirishe Kristo'.

Hao walioambiwa "ninyi ni chumvi" ni watu gani? wa pekee? la! ni wa kawaida tu, wavuvi n.k. ambao wameitika wito wa Yesu na kumfuata. "nuru ya ulimwengu" ulimwengu umo gizani iwapo watu hujiona kuwa na ujuzi na elimu, hata hivyo, hawamjui Mungu wala kuelewa shabaha ya kweli ya kuumbwa kwao na kuishi kwao. Wakristo hufahamu kwamba wamo duniani kwa kusudi la kufanya mapenzi ya Mungu, wanayo shabaha ya kuishi. Yesu Mwenyewe alidai kuwa 'nuru ya ulimwengu' (Yoh. 8:12). Kazi ya nuru ni kuangaza, kutoa mwanga, kuonyesha njia. Mkristo huangaza kwa njia ipi? kwa matendo yake mema, kwa tabia njema zilizotajwa katika 'heri', anapoishi tofauti na kawaida za ulimwengu huu. Lengo lake ni Baba yake atukuzwe, si yeye. Kwa tofauti ya maisha yake watu watatambua amewezeshwa kuishi hivyo na Mungu. Mkristo asijifiche, asiwe mfuasi wa siri, apaswa kumshuhudia Kristo na kuwa nuru. Wengine watasaidiwa kuona vizuri, na kupata lengo la kuishi na shabaha ya kweli tutakapowaelekeza kwa Kristo mwenye msaada.

**5:17-20 Yesu: mawazo yake juu va Agano la Kale**

Sehemu hii inaanza na maneno "msidhani" kwa hiyo ni nini iliyofanya watu 'kudhani' kwamba Yesu anatangua torati na manabii? Alikuwa akiwaponya watu siku ya Sabato, alionekana mlegevu juu ya Sabato, ila hasa alikuwa akivunja sheria ndogondogo za mapokeo yao, si sheria ya Mungu. Ulegevu ulihusu jinsi alivyokubali "watoza ushuru na wenye dhambi" watu wasiojali mapokeo ya wazee. Alikula nao bila shida. Mara nyingi aliwapinga Mafarisayo na waandishi pamoja na mafundisho yao. Kwa hiyo swali lilizuka, Je! amekuja kutangua torati na manabii au vipi? "Nalikuja" mara nyingi ametajwa kuwa "yule ajaye"

kutokana na ahadi ya Masihi iliyomo katika Agano la Kale. Kwa maneno "nalikuja" ni kama anadai kuwa Masihi.

Neno "amina" ni sahihi ya Yesu, lafanana na usemi wa manabii waliopenda kusema "Bwana asema hivi". Hatuna habari kwamba marabi walitumia lugha ya aina hiyo. Katika Mathayo neno limetokea mara 31; na Yohana mara 25, pia "amina amina".
Swali kubwa linalotokana na maneno ya Yesu "sikuja kuitangua bali kuitimiliza" ni kuhusu Agano la Kale na kiasi cha mamlaka yake katika maisha ya Mkristo. Ni "Neno la Mungu" kwa njia gani? Je! Kila neno na sheria ni kwa muda wote? au lina mamlaka kwa jumla tu? Hivyo yatupasa kuwaza maana ya "kutimiliza". Yawezekana maana ni mpaka Yesu ameitimiza kwa kuitii kikamilifu, na ndivyo alivyofanya alipoishi bila kufanya dhambi na kwa kufanya mapenzi ya Mungu kwa moyo.
Maana nyingine yaweza kuwa ametimiza kwa kudhihirisha maana yake ya ndani kama afanyavyo katika mabeti yafuatayo. Tena maana nyingine yaweza kuwa kufikisha torati na manabii kwa 'mwisho' kwa njia ya Huduma yake na, kazi yake. Maana hiyo huenda ndiyo hasa maana yake, maana Yesu alitimiza Manabii pamoja na Torati na haki yake kwa Kuja Kwake. Ahadi za Agano la Kale zilitimizwa. Wayahudi walitazamia kwamba Masihi atatoa mafundisho kamili juu ya Torati. Kwa hiyo badala ya kuitanguaataileta kwenye upeo wake na kwa kufanya hivyo itafikia mwisho wa kuwa njia ya kupata haki (Rum. 3:19-31). Kwa hiyo Agano la Kale lina mamlaka kuwa Neno la Mungu, hata hivyo mafundisho ya Yesu yana mamlaka idumuyo. Mara sita katika vifungu vifuatayo maneno hayo yameandikwa "mmesikia watu wa kale walivyoambiwa" na "imenenwa" bali "Mimi nawaambieni". Yesu alionyesha kwamba Mungu hudai zaidi ya ilivyoandikwa na walivyoelezwa. Kwa kuwa Yesu ni Masihi anayo mamlaka ya kuchimba chini na kufunua wazi viini vya sheria za kale na kuonyesha mapenzi makamilifu ya Mungu.

k.18 'yodi' 'nukta' yodi ni herufi ndogo sana katika alfabeti ya Kiebrania, si lazima iwekwe kila mara; nukta ni kama 'mkia' iliyowekwa kutofautisha herufi zilizofanana.

Kujumlisha twaweza kufikiri kwamba maana ya sehemu hiyo ni kwamba Torati yadumu mpaka ifikie matimizo yake ambayo yatatokea hivi karibuni katika Huduma na Mafundisho ya Yesu. Iwapo Torati haibadiliki, siyo kusema iendelee baada ya kusudi lake kutimia. (Gal. 2:21; 3:19,21,24,25; Rum. 10:4).

k.19 Yesu aliwaonya wanafunzi juu ya kulegeza au kubadilisha sehemu yoyote ya Torati. Waiheshimu na kuitii, ila si katika hali ya kuifuata moja kwa moja kama ilivyoandikwa (legalistically) kama Mafarisayo walivyojaribu kufanya, maana hao hawakustahili Ufalme wa Mungu (2Kor. 3:6) bali kwa "haki izidiyo" ya kumpenda Mungu na kwa kutoka kwa moyo kufanya mapenzi yake. Kitu kikubwa ni uhusiano wao na Mungu.

**5:21-48 Mafundisho ya kina kuhusu maadili**

Hapo Yesu amechagua mambo sita kuhusu maadili na sheria za Agano la Kale na kutoa mafundisho makubwa juu yake. Kila mara amesema kwa mamlaka ya hali ya juu akitumia maneno "bali Mimi nawaambieni". Madai kimaisha ni makubwa, yagusa 'undani' wa mtu, nia na sababu zake, tena huweka tofauti kubwa na maadili ya watu wanaoishi bila Mungu. Ni tangazo la mapenzi ya Mungu, na mwishowe watu walishangaa mno (7:28-29). Bila

shaka Mathayo alitaka kuleta mbele ya watu Umasihi wa Yesu mwenye mamlaka ya kutoa mafundisho yapitayo ya Agano la Kale.

5:21-26 Uuaji na Hasira
Katika Amri 10 moja ilisema "usiue". Yesu alichukua amri hiyo na kuchimba chini yake na kuweka 'hasira' 'kufyolea' 'kuapiza' na bila shaka hali zote zinazosababisha uuaji kuwa sawa na tendo lenyewe la kuua. Si tendo la nje tu ambalo lapaswa hukumu, hata hali ya ndani ya chuki n.k itahukumiwa potelea mbali tendo lenyewe limetendeka au siyo. Mbegu za uuaji ndizo za hatari nazo haziletwi kwenye baraza duniani, ila kwa Mungu zitahukumiwa. Kwa hiyo licha ya kuondoa amri ya zamani, na licha ya kupunguza madai ya torati, Yesu aliisimamisha amri ya 'usiue', aliinoa vikali sana, mpaka shabaha ya ndani ilipata kudhihirika, na mapenzi ya Mungu kufunuliwa, ambayo ni wanadamu waishi kwa upendano na amani; badala ya 'usiue' katika Ufalme wa Yesu hewa yake ni "mpende jirani yako hata adui yako kama nafsi yako". Mawazo na nia na sababu viletwe mbele za Mungu.

k.23-24 Kwa sababu Mungu atahukumu hasira n.k. hatuwezi kumwabudu ikiwa tunavyo vitu vya namna hiyo moyoni. Likiwepo neno lolote kati ya mtu na mwenzake ni vema litengenezwe haraka iwezekanavyo, hata ikiwa ni kwa kuondoka katikati ya ibada na kulitengeneza. Kuutafuta upatanisho ni bora kuliko kuendelea na ibada.

k.25-26 Kwa nini haraka ni jambo muhimu katika upatanisho? Ni kwa sababu jambo laweza kuiva haraka, mtu asipojali aweza kujikuta yu barazani au kifungoni. Uhusiano wetu na watu ni wa maana sana machoni pa Mungu. Uhusiano huo umefumana na uhusiano wetu na Mungu. Vilevile tumo njiani kumwendea Mungu na hukumu, vema tuwe tayari. "senti ya mwisho" ni fedha ndogo katika fedha za Kirumi. Hukumu ya Mungu itakuwa kubwa isipozuiliwa na toba na kupatana. Yesu amekataa kufuata neno la andiko tu, kama limetosha. La! halitoshi kutimiza mapenzi ya Mungu. Jinsi tumwazavyo na kumtendea mtu Mungu huangalia.

5:27 -32 Kuzini na kutamani
Kama alivyofanya na amri ya "usiue" ndivyo Yesu alivyofanya kwa amri ya "usizini". Alifunua mapenzi ya Mungu kuwa usafi wa mawazo ya ndani na usafi wa maisha kimatendo. Mawazo ya ndani, nia ya mtu na tamaa zake zitaletwa

hukumuni hata ikiwa tendo la nje halikutendeka. Mbegu za dhambi ya uzinifu na uasherati zimo moyoni mwa mtu na chanzo cha tendo la nje ni ndani. Kwa macho yetu twasaidiwa tusijikwae na kuanguka, kumbe macho hayo yaweza kutuingiza katika majaribu. Jicho laweza kutumiwa kwa kulisha mawazo ya ndani, ndipo viungo vingine vyatekeleza tendo la nje. Mtu apaswa kujizuia kwa ukali anapojaribiwa - auvunje uhusiano na mwingine, au aache kuhudhuria mahali fulani, asisome vitabu au kutazama picha zinazoamsha mawazo mabaya - ndiyo maana ya kung'oa jicho na kukata mkono. Kwa nini? kwa sababu Yesu alifahamu kwamba tamaa hizo zina nguvu sana. Afadhali mtu aishi maisha "membamba" kuliko maisha "mapana" yatakayomfikisha kwenye jehanumu ambapo atapoteza maisha yote .

5:31-32 Talaka

Ling. na 19:3-9 Kum.24:1-4. Hapo tena Yesu alisema juu ya kusudi la Mungu alipowaumba wanadamu mwanzoni. Wayahudi walijadiliana sana juu ya 'sababu' za mtu kupata talaka, kwa kuwa maneno ya Kum. 24: 1 "ameona neno ovu kwake" si wazi, "neno ovu" ni neno gani? Walegevu waliona hata mke akiharibu chakula ni sababu ya kutosha apewe talaka. Wengine waliona neno ovu ni uzinifu tu. Yesu alikataa talaka kabisa isipokuwa kwa "uasherati", kwa kuzini mtu tayari ameivunja ndoa yake. Mafundisho ya Yesu ni magumu ila yafuata aliyoyasema juu ya "usafi wa ndani", yampasa mtu azizuie kwa ukali tamaa zake. Mungu alifunua wazi mapenzi yake alipowaumba wanadamu, mapenzi hayo ni kwa wanadamu wote, ila ni wafuasi wa Yesu ambao kwa neema yake wataweza kutunza ndoa zao.

5:33-37 Viapo na kusema kweli

Katika Agano la Kale viapo viliruhusiwa na mtu alifungwa na kiapo chake (Hes.30:2). Viapo vya uongo vilikatazwa pamoja na ahadi na viapo visivyotimizwa (Kum. 23:21; Law 19:12; Kut. 20:7; Zab. 15:4).

Tukilinganisha na Mt. 23:16ku. marabi wakati wa Yesu walitoa mafundisho yaliyolegeza nguvu ya viapo, wakiruhusu watu wasifungwe na viapo vyao kama wameapa kwa vitu fulani. Yesu alihesabu kwamba, potelea mbali wameapa kwa kitu gani, hata hivyo wamefungwa macho, maana kila kitu chatoka kwa Mungu. Ila Yesu hakuona kuna haja ya viapo, mapenzi ya Mungu ni mtu aseme kweli wakati wote bila nyongezo ya maneno. Ukweli ukisemwa hamna haja ya kutumia maneno kama 'haki ya Mungu'. Katika ufalme wake kweli itasemwa wakati wote, hivyo wafuasi wake wazoee kusema kweli (Yak. 5:12). Twaona mafundisho ya Yesu juu ya talaka na viapo yalipita mafundisho ya Agano la Kale. Aliziondoa ruhusa zilizotolewa na kuhesabu hazitakiwi kwa wafuasi wake. Viapo hushuhudia ukosefu wa watu kusema kweli na udhaifu wao katika matumizi ya maneno (Mt. 12:36).

5:38-42 Kisasi na kutokushindana

Agano la Kale lilitoa mwongozo katika kulipiza kisasi (Law 24: 19-20). Shabaha ilikuwa kuweka mpaka ili watu wasizidi, maana ni vigumu mtu ajitawale katika

kujitafutia haki. Kawaida, akipigwa atajibu kwa kutoa pigo lililozidi. Hivyo 'jicho kwa jicho' ilileta 'usawa' ni kama 'haki' na sheria hiyo ilileta nafuu. Inakubalika kwamba adhabu ilingane na kosa, na ndiyo msingi katika mambo ya hukumu. Ila Yesu alikataa kabisa - Yeye alisema "msishindane" yaani mtu asijitafutie haki, asipeleke kesi yake barazani, aiachilie kabisa. Akubali mashutumu, asijali mali yake, awe tayari kwenda maili ya pili. Siku zile Warumi walitawala nchi nao waliweza kumlazimisha mtu waliyemkuta njiani abebe kitu fulani kiasi cha maili moja. Watu waliichukia desturi hiyo na kuinung'unikia, ila Yesu alisema kwamba badala ya kunung'unikia maili moja, wajitoe kwa maili ya pili! (Mt.27:32).

Yesu alitaka kufundisha nini? Tusishikilie kila neno kama lilivyoandikwa, tukifanya hivyo tutafanana na Mafarisayo walioshika maneno yaliyoandikwa bila upendo wa ndani. Yesu apenda tuweke haja za wengine kabla ya matakwa yetu wenyewe, tuachilie kabisa kudai haki yetu, tusishikilie kwa nguvu mali yetu, kwa kufanya hivyo tutavunja mzunguko wa kutafutana. Tuwe na mzigo juu ya wengine. Hayo yahusu mambo ya 'binafsi'. Kuhusu 'haki za kibinadamu' na kuzipigania si neno linalozungumzwa hapo.

5:43-48 Kupenda jirani na kuchukia adui - kuwa wakamilifu
Yesu alikaza sana neno la 'kupenda' na katika sehemu hii ameonyesha upana wake. Katika Agano la Kale (Law 19:18) 'kupenda jirani' ni kupenda Mwisraeli mwenzake - maneno 'kuchukia adui' hayamo, ila ilikuwa rahisi kuwaza hivyo kwa sababu ya ubaguzi uliowekwa kati ya Waisraeli na wasio Waisraeli. Aliye adui wa binafsi afanyiwe vema (Kut 23: 4-5; 1Sam. 24:18-19; Mit. 25:21). Asiye Mwisraeli mmoja mmoja akaribishwe (Law 19:34; Kum. 10:19). Neno "kuchukia" halikuwa na maana ya kuchukia hasa, ni kama 'hakuna haja ya kumpenda' Yesu alikataa kufuata ubaguzi huo, hamna hata mmoja ambaye mwanafunzi asimpende, hata ikiwa huyo amemwudhi na kumtesa.

Kumpenda ni zaidi ya kutokumrudishia mabaya au kuachilia mambo. Ni upendo wa kumtafutia mema na kumwombea.

Upendo usio na ubaguzi utawathibitisha wanafunzi kuwa "wana wa Baba" wenye tabia moja naye. Tabia ya kuwashirikisha wote baraka zake bila ubaguzi, wakimpenda, wasimpende, awape mvua na jua na mahitaji ya lazima. Ni fadhili zake kwa wanadamu wote. Ila si baraka za kiroho, hizo ni kwa wale wanaotubu na kumwamini Kristo, wala hakuna maana kwamba wote wataokolewa, la!.

k.46-47. Kwa kawaida mtu huangalia mambo yake mwenyewe tu, ila mwanafunzi wa Yesu apaswa apite mipaka ya kawaida za watu, budi awaangalie haja za wasio ndugu wala rafiki.

k.48. Ling. na k.20 "haki yenu isipozidi" tangu k.21 hadi k.48 haki hiyo imeonyeshwa, lengo ni 'ukamilifu' ni kutimiza matakwa ya Mungu ambayo

huzidi sheria zilizoandikwa. Mkamilifu ni mtu aliyehitimu, aliyeweka maisha yake yote chini ya mapenzi ya Mungu, ili apate kufanana na Baba kwa tabia, na katika kuwa na moyo safi, nia na sababu zake kuwa safi, na maisha kiutendaji ni ya kumpendeza Mungu.

Hilo ndilo lengo ambalo Yesu aliliweka mbele za wafuasi wake katika hotuba hiyo. Ni lengo lisilowezekana nje ya neema yake.

**6:1-18 Mafundisho juu va kutoa, kufunga, na kusali**

Katika 5:21-48 Yesu alisema juu ya maadili, huenda alikuwa akiwaza waandishi na wazee walioyashughulikia mambo hayo. Katika 6:1-18 alisema juu ya kutoa, kufunga, na kusali, akiwaza Mafarisayo walioshughulikia eneo hilo. Katika dini ya Kiyahudi mambo hayo matatu yalikuwa muhimu na kwa kuyatimiza Myahudi alifikiri atakuwa amempendeza Mungu. Bila shaka shabaha ilikuwa kumleta mtu karibu na Mungu wake. Yesu amekwisha kuonyesha "haki izidiyo ile ya waandishi" (5:20) kwa mafundisho ya 5:21 ku. naye aliendelea kuionyesha katika

6:1 ku. Alisema kwa mamlaka "amin, nawaambia" (k2,5,16). Yesu hakuyakataa mambo hayo, wafuasi wake watafanya yayo hayo. Ila alihukumu jinsi watu walivyoyafanya kwa shabaha isiyo njema. Alitaja na thawabu yao. Ndipo alishauri jinsi ya kuyafanya, na kwa shabaha gani, na thawabu watakayoipata.

6:1 - 4 Kutoa
"Msifanye wema wenu machoni pa watu" Je! maneno hayo yanapinga "nuru yenu iangaze ... " 5:16? Ya 5:16 yahusu maadili, na 6:1 yahusu matendo ya dini. Twaweza kusema Mkristo aonekana kuwa anatenda matendo mema ila asitende ili aonekane. Shabaha itaongoza namna ya kutenda, kama shabaha ni kutazamwa na watu, basi mtu atafanya kwa kujionyesha; kama shabaha ni kumkaribia Mungu atafanya kwa siri.

k.2 'utoapo' si 'ukitoa' ilikuwa wajibu si hiari kwa Myahudi kutoa. Walikuwa na mipango mizuri ya kuwasaidia maskini kwa njia hiyo (Kum. 15:7-11; Zab. 11:2:9) "usipige panda" si kwamba watu walipiga panda ila ni msemo kuhusu kujionyesha. "wanafiki" Mathayo alitumia neno hilo mara nyingi k.5 na 16 na hasa katika sura ya 23. Neno lilitumika kwa mtu aliyemwiga mwingine katika viigizo na michezo, akijifanya kuwa yule mwingine.- kwa kiigizo ni sawa. Ila katika dini kufanya mbele za watu kama ni kiigizo si sawa. Siyo kusema kwamba hawakutoa, ila shabaha yao haikuwa njema.

"wamekwisha kupata thawabu yao" Neno "wamekwisha" lina maana ya kulipiwa mshahara walioustahili. Hawana chochote cha kufuata baadaye. Thawabu imelingana na shabaha. Aliyetaka watu wamwone na kumsifu, kumbe kweli wamemwona na kumsifu, na kumhesabu ni mtu mzuri wa dini, tayari amelipiwa mshahara.

k.3-4. Wafuasi wa Yesu watoe kwa siri "mkono wake wa kuume usijue" maana yake hakuna haja kwa watu kujua, wala kwa mtu mwenyewe kuendelea kukumbuka. Tutoe ndipo tusahau tumetoa, kusudi tusiingie hatari ya kuhesabu tumefanya vizuri. Ni wajibu wetu kutoa, kwa hiari, kwa ukarimu, kwa kumpenda Mungu na jirani, na kwa shukrani, wala si kwa kujistahilisha mbele zake. Ni itikio letu kwa neema ya Mungu maishani mwetu. Mungu huona nia na sababu za ndani (k 4, 6,18). Hakuna haja ya kuuvuta usikivu wake kwa matendo fulani. K 4 "atakujazi" "thawabu ya Baba yenu aliye mbinguni" atoaye kwa nia njema atapata thawabu, ni zaidi ya mshahara. Haitoki kwa watu bali yatoka mbinguni kwa Baba, yenye kujaa neema.

6:5-9 Kuomba
Yesu alisema juu ya kuomba kama alivyosema juu ya kutoa. Kwa kuomba mtu hushirikiana kwa ukaribu sana na Mungu na ni vigumu kufanya hivyo kwa shabaha ya kujionyesha ili atazamwe na watu, ila ajabu ni kwamba walikuwepo watu wa namna hiyo wakati wa Yesu na hata wakati wetu.
k6 Haina maana kwamba tusiwe na maombi ya pamoja na maombi hadharani, la: ila shabaha ya maombi yote iwe ya kumkaribia Mungu kwa kweli. Mfuasi wa Yesu atahitaji kusema na 'Baba' yake katika utulivu faraghani, pia Baba atapenda kusema na yeye.

k. 7-8 Yesu hakutoka wafuasi wake wafanane na WaMataifa jinsi walivyoomba kwa miungu yao: hao walifikiri ni lazima waseme-seme sana, na bila maana, wakitumia maneno mengi mengi ili miungu yao iwajali; kumbe, sivyo ilivyo kwa Mkristo na Mungu aliye Baba yake. Baba hana haja ya kuambiwa kwa kuwa anayafahamu mahitaji yetu, ila twaomba ili tumshirikishe.

Kuna maombi yaliyoandikwa tunayotumia katika ibada, tena kuna maombi ya moyo; si neno, mradi tunaomba katika hali ya kutambua tunafanya nini na kwa shabaha ya kumkaribia Mungu. Yeye huangalia ule moyo wa kumtegemea si maneno yetu. Ndipo Yesu alitoa 'mfano' wa sala kwa wafuasi wake kuitumia, tumezoea kuiita 'Sala ya Bwana'.

6:9-13 Sala ya Bwana
Ni sala ya kuombewa na wafuasi wa Yesu kwa sababu ni hao tu wawezao kumwita Mungu "Baba". Ni sala kwa watu wakiwa pamoja na sala kwa Kanisa kutumia. "Baba yetu uliye mbinguni" ni maneno yaletayo pamoja mawili tofauti - "Baba yetu" yaani Mungu wa karibu mwenye uhusiano wa ukaribu na wafuasi wa Yesu: twamwita "Baba" pia "yetu" "aliye mbinguni" kumbe aliye Baba yetu anao uwezo wote na madaraka yote hata mbinguni, ni wa juu kabisa.

Yafuata mambo yamhusuyo huyo Baba: "Jina lako litukuzwe" yaani Mungu aheshimiwe kwelikweli, apewe heshima zote zinazolingana na jinsi alivyojifunua

kwa wanadamu. Hasa zaidi ije ile siku ambapo wanadamu wote watamkiri kuwa Mungu na Bwana. "Ufalme wako uje" Mungu azidi kuusimamisha utawala wake juu ya uumbaji wake wote. Katika Yesu Ufalme umekwisha kuja, na ombi ni kwamba uendelee kuja mpaka ufike utimilifu wake. "Mapenzi yako yafanyike": watu huzidi kumtii Mungu katika ulimwengu wa sasa, na pia makusudi ya

Mungu yatekelezwe hadi mwisho. "hapa duniani kama huko mbinguni" upana wa mahali pa utekelezaji wa makusudi ya Mungu.

Hapo yafuata maombi matatu kuhusu mahitaji ya wafuasi wake: Ya kwanza "utupe leo riziki zetu" mahitaji ya lazima kwa kuishi kwetu. Ya pili "utusamehe deni zetu" neno deni lina maana ya dhambi. Haja ya msamaha kwa upande wa maisha yetu ya kiroho. Pia wajibu wetu wa kusamehe wengine. Ya tatu "usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu" haja yetu ya kulindwa ili tusianguke. Mungu kamwe haleti majaribu ya kutuingiza katika dhambi, ila pengine ataruhusu shida na magumu kwa kutupima. Kwa ombi hilo wafuasi wa Yesu hukiri udhaifu wao, wakiomba wasipimwe kuliko wawezavyo kustahimili. Wapaswa kumtegemea Mungu wakijua udhaifu wao.

"Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu hata milele" Pengine maneno hayo yaliongezwa baadaye wakati Kanisa lilipozoea kutumia Sala hiyo katika ibada (1 Nya. 29: 11-12).

k.14-15 Ni kama maelezo ya k.12 (Ling. 18:23-25). Si sharti tusamehe ndipo tusamehewe na Mungu, ila ni kuonyesha kwamba msamaha si wa upande mmoja. Ombi la kusamehewa limekosa "ukweli" kama limeombwa na mtu asiye tayari kusamehe. Kumbe! aomba kitu asicho tayari kutoa!

6: 16-18 Kufunga
Yesu alisema juu ya kufunga kama alivyosema juu ya kutoa na kuomba. Ni jambo kati ya mtu na Mungu wake, hakuna haja ya watu kujua.

### 6: **19-34 Wanafunzi na mali**
Katika mafunzo yaliyotangulia Yesu alitoa mafundisho yaliyopinga waandishi na Mafarisayo waliotafuta sifa za watu na kuwa na mzigo jinsi walivyoonekana machoni mwa watu. Katika sehemu hiyo Yesu alifundisha wafuasi wake juu ya uhusiano wao na mali na vitu vya dunia hii. "Haki inayozidi" itadhihirika kwa jinsi watakavyoishi maisha ya tofauti sana na wengine kuhusu mali.

Hasa mkazo wa Yesu ni kwamba mfuasi wake apaswa kumweka Mungu kuwa wa kwanza katika maisha yote. Yesu alionyesha kwamba mali ina nguvu ya kumvuta na kumkamata mtu ili asimweke Mungu kuwa wa kwanza. Mali huwa na nguvu ya kuuondoa utiifu wa mtu kwa Mungu wake, yaweza kuwa 'bwana' wa maisha yake na 'kumfunga'.

k.19-21. Katika k 4, 6, 18; Yesu alitaja thawabu ya mbinguni.

Hapo asema kwa nguvu "msijiwekee hazina duniani" neno "hazina" ni kuonyesha kwamba hatari moja kubwa ni kuhesabu mali kuwa 'hazina', na hatari ya pili ni kufikiri ni hazina idumuyo. Alitaja vitu vinavyoshambulia mali na kuifanya kuwa ya muda - nondo, kutu, wevi, na bila shaka panya, pesa za kushushwa thamani yake kwa haraka na kubadilishwa bila taarifa, hayo yote ni 'adui' wa mali. Kwa hiyo kuishi kwa kutegemea mali ni kuishi kwa mashaka. Kwa mfano, mtu aliye na mali nyingi nyumbani, huishije? mara nyingi ana hofu. Kama mtu atajisikia yu salama, siyo kusema kweli yu salama.

k.20. "jiwekeeni hazina mbinguni" hazina hii ni salama salamini, tena ni ya kudumu, na ni ile inayomshibisha mtu.

k.21. Hapo Yesu alitamka kweli ya maana sana, hali akitujua kabisa - moyo wa mtu hufuata 'hazina yake' - mtu huandama na kushughulikia ile ambayo kwake ameiona ni 'hazina'.

k.23-24. Jicho safi na jicho bovu: Jicho safi ni jicho lenye afya, linalomtia mtu nuru ili aione njia vizuri - njia ipi? ni ile ya kufuata kitu kimoja cha maana maishani mwake, ni kumpenda Mungu kuliko vitu vyake.

Mwenye jicho bovu akosa afya ya mwilini, haoni vizuri, hujikwaa kwa vile haoni vizuri. Wayahudi walitumia usemi huo kwa kueleza mtu mwenye wivu, mnyimivu, mwenye choyo. Ugonjwa alio nao ni kukosa utambuzi wa hazina ya kweli na kwa choyo na unyimivu afanya mali kuwa lengo na hazina yake. Sisi tuliumbwa kwa shabaha ya kuwa watumishi huru wa Mungu. Dhambi ilipoingia mapinduzi makubwa ya shabaha yalitokea. Tulitaka kuwa huru mbali na kumtumikia Mungu, ili tuwe 'mabwana' sisi wenyewe. Badala yake tumekuwa watumwa wa dhambi na Shetani. Hivyo ni rahisi 'mali' iinue kichwa chake itake kuwa 'bwana' na kututumikisha. Yesu alitumia lugha ya 'utumwa' alipolizungumzia habari hiyo ya mali na uhusiano wake na sisi.

k.24. "hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili" na "hamwezi kumtumikia Mungu na mali" Lugha ni wazi na maana ni wazi: kwanza 'hakuna mtu' sote tu pamoja katika habari hiyo; 'awezaye' yaani haiwezekani, neno hilo halina majadiliano. 'kutumikia mabwana wawili'. Mtumwa ni mtu aliye mali ya mtu mmoja tu, apaswa amtumikie wakati wote. Yesu alisema mabwana hao wawili ni 'mali' na 'Mungu'. Kumchukia haina maana kumchukia kwa 'chuki' bali ni kumweka nyuma si mbele, asiwe nambari ya kwanza.

Kwa hiyo Yesu alifundisha kwamba kuna upinzani mkubwa kati ya Mungu na mali. Kwa wakati mmoja hatuwezi kuweka hazina duniani na hazina mbinguni. Anapozungumzia mali Yesu asema juu ya mali yenyewe si juu ya njia iliyopatikana, kama ilipatikana kwa halali au siyo.
Alihesabu mali ni mshindani ikitaka kuwa kitu cha kwanza, kwa hiyo ipo vita kali kati yake na Mungu, kwa kuwa ni Mungu peke yake aliye na haki kuwa wa kwanza katika maisha yetu.

Yawezekana wengine wamefikiri kwamba wanamtumikia Mungu ila hawajatambua kwamba Mungu hakubali kuwa wa pili katika maisha, pia pengine hawajatambua hatari ya mali. Mara nyingi katika maisha yetu shughuli za mali zaanza polepole, ndipo zazidi, mpaka baadaye mtu hujikuta zinamtawala.

Yesu aliendelea kugusa sababu zimfanyazo mtu akusanye mali na kuishughulikia kupita kiasi. Sababu moja ni choyo iliyo mioyoni mwetu. Nyingine ni mashaka kama tutakuwa na mahitaji yetu kama chakula na nguo. Twakosa amani na hatumwamini Mungu kama Baba.

Yesu hukubali kwamba twahitaji kuangalia hayo mahitaji na kuyashughulikia. Ila alikataa hali ya kuyasumbukia. Yeye alitaka tufikiri sana – kama Mungu ni Baba aliyetupa mwili, Je! atakosa kutupa nguo za kuufunika? kama ni Baba aliyetupa kuishi, Je! atakosa kutupa chakula cha kuendelea kuishi? Ipi ni kubwa? mwili au nguo? maisha au chakula? Kama ametupa kikubwa na cha maana, kidogo, Je! kitamshinda?

k.26-29. Akiendelea kusema juu ya chakula na nguo, mahitaji yetu ya lazima, aliwafikirisha wasikilizaji wake juu ya viumbe kama ndege na maua, viumbe visivyo vya maana kama wanadamu. Ni wazi kwamba Mungu huwatunza. Yesu hakusema 'tuwaige' la! ila tuviangalie kwa shabaha ya kujifunza kwao. Ndege hufanya kazi nyingi za kujenga kiota na kulisha vifaranga, na kuwa na bidii nyingi, ila mengi hawawezi kufanya. Vivyo hivyo maua hujiweka mizizi chini kwa kupata maji na kuchanua maua mazuri. Ingefikiri hayafanyi lolote, na kweli mengi hayawezi kufanya kulingana na uwezo wa wanadamu kufanya. Hata hivyo, uzuri wao ni wa ajabu. Hayo yote ni msaada kwa wanadamu kuamini kwamba Baba yao wa upendo atazidi kuwatunza na kufanya kazi pamoja nao ili wapatiwe riziki. Hatuna Baba asiyejua mahitaji yetu (k.32) naye ametupa uwezo mwingi. Inayotakiwa tumtangulize Yeye katika maisha yetu yote (k.33).

k:27. Masumbufu ni bure, hata tukifanya nini tumebaki na mengine tusiyoweza. Kwa mfano twaweza kujipatia trakta, lakini hatuwezi kuleta mvua!!

Kusumbua ni dalili ya kutokuamini, ni kosa la kutokuweka "ya kwanza" kuwa 'kwanza' Neno la kwanza ni "ufalme wake na haki yake". Katika Sala ya Bwana tulifundishwa kuomba "Jina lako; ufalme wako, mapenzi yako:" ndipo "utupe leo riziki zetu" tusiweke gari kabla ya punda. Tafuteni kwanza, neno "kwanza" laonyesha yapo mengine ya kufuata, kama mahitaji.

**7: 1-6 Wanafunzi na uhusiano wao kwa wao**

Wafuasi wa Yesu huitwa kuishi kwa kusaidiana na kujengana. Watahadhari na hali ya "kuhukumu". Hapo neno 'hukumu' lina maana ya kuhukumu bila shabaha njema, ni kama kulaumu-laumu. Kuhukumu kama kumpima mtu kwa kazi fulani au cheo, au kwa kuamua jambo kati ya watu, au kufanya marudi

kanisani au shuleni n.k. si aina ya hukumu inayozungumziwa hapo. "msihukumu" kwa nini? kwa sababu hukumu hizo zitaleta hukumu ya Mungu. Tena hukumu yake italingana na ile tuliyotoa. Mtu anayelaumu-laumu mwenzake mara nyingi hafanyi kwa haki. Kutumia kipimo kimoja. Ni vigumu kumhukumu mtu sawa na tunavyojihukumu. Pia ni vigumu kujua yote kumhusu mwingine kama nia na sababu zake, malezi na historia yake, ili tufanye kwa haki.

k.3. Yesu alitoa mfano wa kujichekesha - wa useremala.

Tukumbuke Yeye Mwenyewe alikuwa seremala. Shida yetu ni hatuoni tunayo makosa au ikiwa tunayaona twayafikiri ni madogo kama "kibanzi". Kwa upande wa ndugu yetu tu wepesi wa kuona makosa yake kuwa makubwa kama "boriti". Kumbe kwa hali ya kuzoea kuhukumu-hukumu ni sisi tuliyo na "boriti" inayotufanya tusione vizuri na kutambua ya kwamba ndugu yetu ana "kibanzi" tu.

Si vibaya kutoa "kibanzi" cha ndugu yetu, yaani kumsaidia aelewe kosa lake, lakini kwanza vema tuone na kutengeneza makosa yetu. Tuwe wanyenyekevu na wepesi wa kujihukumu kuliko kuhukumu. Unafiki unatokana na kutokujihukumu kwa kipimo kimoja. Si kosa kutoa kibanzi, kama tumetoa boriti yetu kwanza. Tusipoangalia hali ya kulaumu-laumu tutafanya ndugu yetu akate tamaa. Pia kwa upande wetu tutajiona kuwa bora. Hali hiyo itaharibu uhusiano na ushuhuda wetu kwa watu

k.6. Hata hivyo hatuna budi kuyapima mambo. Wako wenye dharau kwa mambo ya Mungu. Tusiruhusu kweli za Mungu na mambo ya Mungu kuchezewa. "mbwa" na "nguruwe", ni lugha iliyotumiwa na Wayahudi juu ya WaMataifa, ila Yesu aliwaza wasiomcha Mungu wala kumjali. Busara inahitajika katika kumtumikia Mungu. Tumewekewa amana Injili iliyo hazina kuu.

**7:7-11 Wanafunzi na uhusiano wao na Mungu**

Wakristo huhitaji msaada mkubwa wakilenga kutimiza hotuba hiyo kimaisha. Ushindi wataupata kwa kuomba kwa nia ya kutoka ushindi, wakiwa na mzigo wa kuomba bila kukata tamaa na kwa kukazana. Baba yu tayari kabisa kujibu maombi, hakuna haja ya kumsukuma. Kuomba ni njia ya kumjulisha na kumwonyesha nia yetu ni ya kweli. Hatatoa kisichofaa, na msaada atakaoutoa utalenga haja zetu. Siri kuu ni kumtegemea Baba. Twakumbushwa tena Ubaba wa Mungu.

**7:12 Maadili ya Yesu kujumlishwa**

7:12 Amri ya Maana
Zamani watu walifundishwa wasimtendee mtu jambo ambalo wenyewe wasingalipenda kutendewa. Yesu aligeuza kuwa jambo lolote jema ambalo twapenda kutendewa, hilo tumtendee mwingine. Bila shaka yapo mengi ambayo twapenda kutendewa. Ni njia ya upendo, si ya sheria, maana sheria haiwezi kuwekwa kwa kutenda mema, mema hauna mpaka.

### 7:13·27 Maonyo juu va uanafunzi usio wa kweli

7:13-14 Njia mbili
Uzima haupatikani kwa kufuata umati wa watu ila kwa kukata shauri gumu la kuishi maisha membamba, maisha yaliyobanwa, maisha ya kufanya apendavyo Mungu. Mlango ni mwembamba, twaingia uzimani pale msalabani tunapotubu dhambi zetu na kumkubali Kristo. Wengine hawakati shauri lolote, waendelee wapendavyo bila kujali. Kuwa Mkristo ni kuwa kinyume cha wengi, ni kuwa katika "kundi dogo la Baba". Kila njia ina mwisho wake. Yesu hakusema wote watafika uzimani; tujitahidi kufika uzimani (Lk. 13:24).

k.15-20. Wa uongo. Wakati wa Agano la Kale walikuwepo manabii wa uongo, na baadaye katika Kanisa walitokea (2Pet. 2:1; 1 Yoh.4:1-3; Ufu.2.20) Yesu alitoa onyo juu yao (Mt.24:11, 24). Watatoa mafundisho mepesi ya kuepa njia nyembamba, hivyo wataonekana kama "kondoo" kumbe ni "mbwa mwitu". Lazima kiwepo kitu cha kuwapima maana hawatambulikani mara. Kipimo ni matokeo kimaisha, matunda ya kazi na mafundisho yao.

Iwapo watu waweza kuiga maisha ya kikristo kwa muda, wakati utafika utakaodhihirisha hali yao halisi. Kudai kuwa Mkristo ni rahisi na kujifanya kuwa Mkristo pia ni rahisi, ila kuishi kweli ni vigumu. Asiye Mkristo wa kweli atakataliwa.

k.21-23. Sehemu hiyo yafunua zaidi juu ya kukataliwa kwa wale ambao ukiri wao wa Kikristo hauwi kweli (k.19). Haitoshi kumwita Yesu "Bwana" na kutaja matendo kadha waliyoyatenda, kwa kuwa Yesu hutazama maisha mazima ya mtu, nia na sababu zake na hasa ushirikiano kibinafsi kati yake na yule mtu.

7:22. "siku ile" ni ile ya mwisho, siku ya hukumu (k.23). Neno la ajabu ni kwamba Yesu ndiye Mhukumu katika siku ile. Bila shaka watu walitazamia atasema ni Mungu. Tena alisema bila kuomba radhi, wala kujadili, wala kusitasita. "ondokeni Kwangu" hawakuwa na uhusiano wa binafsi na Yeye.

7:24-27 Mfano wa wajenzi wawili na misingi miwili
Yesu alifunga sehemu hiyo na mfano wa wawili waliojenga juu ya misingi miwili tofauti, mwamba na mchanga. Wajenzi hao ni wasikilizaji wa hotuba hiyo. Wote wawili walisikia yale yale, ila tofauti, yaani msingi, ni katika maitikio yao. Mmoja aliitika kwa kufanya k.24, yaani kujenga maisha yake juu ya mafundisho ya Yesu. Wa pili aliitika kwa kutokufanya k.26, alikataa kufuata mafundisho ya Yesu maishani mwake. Katika mafundisho ya Yesu mkazo ni juu ya utendaji.

Nyumba zote zilionekana imara mpaka mvua iliponyesha, maji yakafurika na pepo zikavuma. Ndipo ilipoonekana tofauti katika misingi. Aliyejenga juu ya mwamba aliweza kustahimili shida na magumu ya maisha, alishinda upinzani na mateso aliyoyapata kwa ajili ya Kristo. Aliyejenga juu ya mchanga hakuweza kustahimili magumu yaliyompata, akashindwa, tena sana, maana Yesu alisema anguko lake lilikuwa kubwa. Katika maisha ya kiroho ni bure kusikia bila kutenda. Msingi imara ni kujenga maisha juu ya mafundisho ya Yesu.

**7:28-29 Kujumlisha**

"Yesu alipoyamaliza maneno hayo" maneno hayo yamerudiwa kila baada ya kumaliza fungu kubwa (11:1; 13:53; 19:1; 26:1). Halafu mwandishi aliendelea na habari nyingine. Makutano walionaje hotuba hiyo? Walishangaa mno. Si kwa sababu ya mafundisho tu, bali kwa jinsi Yesu alivyoyatoa kwa mamlaka. Alionekana zaidi ya marabi. Tena alidai itikio la kimaisha kwa mafundisho yake na kuonyesha kwamba hayo mafundisho yatakuwa kipimo kitakachoongoza hukumu ya mwisho. Mamlaka ni ya yule aliyetumwa kutimiza torati na manabii.

*MASWALI: HOTUBA YA MLIMANI*

*Hasa hotuba hiyo ni kwa watu gani na ni akina nani ambao watazamiwa wataishika? Unazionaje "heri" zilizotajwa? unakubaliana nazo?*

*Tutapatanishaje heri hizo na maendeleo ambayo watu wanayatafuta? Utawasaidiaje watu wako ili wakubali mapinduzi hayo ya Bwana Yesu kupongeza wale wa hali fulani ambazo ni vigumu tufikiri ni heri?*

*Katika matendo ya dini kama kuomba, kufunga, na kutoa ni rahisi kufanya kwa desturi. Hata Wakristo wengine na madhehebu mengine wameingia hatari ya kufanana na Mafarisayo kwa kuweka visheria juu ya mavazi, kama mwanamke kuvaa kofia, na urefu wa nguo n.k. Hasa twahitaji kukaza nini kwa Wakristo wetu?*

*Kuhusu utoaji waonaje desturi ya wengine kudhihirisha wazi utoaji kwa kuorodhesha majina na kiasi walichotoa watu, pia kuweka kima fulani? Waonaje jinsi wengine wanavyofanya mnada baada ya ibada, pia makanisa mengine yana desturi ya kuweka fungu la mwaka n.k. Je! ni sawa kwa wote kuwekewa kima kimoja huku mapato yao hutofautiana? Eleza.*

*Utafanya nini kwa Mkristo aliye na ugomvi na mwenzake, na watu wanaoleta fitina Kanisani, na wale wasiojitahidi kuuhifadhi umoja wao katika Kristo? Mara nyingi shida zatokea kati ya watu wa kabila mbalimbali ndani ya shirika moja, kiongozi afanyaje? Utawaachilia kwa kusema ni shauri lao? au utachukua jukumu gani?*

*Utawafundisha Wakristo kufanya nini ili wayatekeleze mafundisho ya Yesu juu ya mali na dunia na nia yao ya kutoka maendeleo katika hali ya maisha yao, hasa kwa sababu mkazo wa nchi ni maendeleo ya usitawi wa jamii, afya, elimu, n.k. Wafanye nini ili wajali maonyo ya Yesu, pia wajiendeleze?*

*Ni ipi iliyo tofauti kubwa kati ya maadili ya Yesu na torati na mapokeo ya waandishi na Mafarisayo? Je! Kanisa kweli limeepa hali za Kifarisayo au vipi? na kama halikuepa, limeshindwa kwa mambo gani?*

*Yesu alitoa mfano wa wawili waliojenga tofauti. Kujenga juu ya mwamba ni kujenga juu ya Hotuba hiyo.*

*Je! umewahi kufundisha Wakristo Hotuba hiyo? Kama jibu lako ni bado, sababu*

*yako ni nini? Umeona kazi yako ni Kuihubiri Injili tu? Kama unaona ni vema kufundisha hiyo Hotuba ni wakati gani ambapo ni vema kufanya? Siku ya Jumapili au katika Darasa la Kikristo au Mtaala wa Biblia?*

*Wakristo waitwa kuwa Chumvi na Nuru katika ulimwengu. Kwa kutimiza wajibu huo utawashaurije kuhusu maisha yao kazini, vijijini au mjini mahali wanapoishi, pia maisha yao nyumbani n.k? Wapige vita juu ya mambo gani yaliyo kinyume cha mapenzi ya Mungu na yasiyo haki kwa wananchi?*

## MIUJIZA MBALIMBALI YA YESU: 8:1-9:34.

Baada ya fungu kubwa la kwanza la mafundisho Mathayo alilifuata na fungu la matendo makuu ya Yesu. Miujiza 10 iliyopangwa kwa mafungu matatu 8:1-17; 8:23-9:8; na 9:18-34. Kati ya fungu la kwanza na la pili aliweka habari ya wawili waliotaka kumfuata Yesu na kati ya fungu la pili na la tatu aliweka habari za wito wake.

Shabaha ya Mathayo katika kuikusanya miujiza hiyo na kuiweka kalika fungu moja kubwa ni kuonyesha mamlaka ya Yesu kama ilivyoonekana katika mafundisho yake. Alifunga sehemu hii kama alivyofanya kwa mafundisho 7:28 akionyesha ushangao wa watu 9:33.

Mamlaka ni ya Yesu Masihi, miujiza ni ishara yake 11:5. Masihi mwenye uwezo wa kushinda ugonjwa, pepo, dhoruba, upofu, ububu n.k. Mathayo anataka kuonyesha Yesu kuwa nani.

**i: Mwenye ukoma 8:1-4**:

Huenda Mathayo alipoweka habari ya mwenye ukoma kwanza alikuwa na shabaha ya kuonyesha jinsi Yesu alivyotenda hali akijua yaliyoandikwa katika Agano la Kale. Wenye ukoma walikuwa chini ya sheria za Lawi 13-14.

i. Waliwekwa nje ya kambi wasishirikiane na jamii ya watu kwa sababu ya hatari ki-afya ya kuambukizana.
ii. Mara nyingi hawakuwa na "uvutano" miili yao iliharibika.

iii. Walihesabiwa kuwa "wanajisi" kwa upande wa dini. Pia ukoma ulifikiriwa ni ugonjwa ulio vigumu kuponyeka, hivyo wenye ukoma walijisikia shida pande zote, kimwili, kijamii na kidini.

k.2."akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia akisema Bwana ukitaka waweza kunitakasa" "akaja" inaonekana huyo mtu alimjia Yesu, ishara ya mamlaka ya Yesu, bila shaka amesikia habari zake. Hakuwa na mashaka juu ya uwezo wa Yesu ila aliona shaka juu ya utayari wa Yesu kumpokea. Si ajabu kwa kuwa amezoea kuwa "nje ya watu" na "kukataliwa" Je, huyo Yesu pia atamkataa? "akamsujudia" dalili ya huyo mtu kumwaza Yesu ni zaidi ya mtu wa kawaida.

k.3. Yesu "alinyosha mkono akamgusa akisema "nataka, takasika". Kumbe Yesu kwa tendo hilo **dogo** la kunyosha mkono na kumgusa alifanya tendo

**kubwa** la ajabu. Aliruka mapokeo ya miaka mingi. Tendo hilo lilitenda zaidi ya maneno yo yote yatakayosemwa. Kisheria ilikuwa marufuku kwa mtu kumgusa mwenye ukoma, akifanya atanajisika pia. Waonaje, mtu huyo alisikiaje alipoguswa kwa mara ya kwanza baada ya muda mrefu? Yesu alivunja sheria juu ya unajisi ya Lawi 5:3. Kwa Yesu "sheria" ya upendo na huruma ilizidi ile ya andiko. Kwa kumgusa Yesu alifanya "uponyaji" mwingine, alimrudisha katika jamii, pia aliuondoa unajisi wake.

"nataka" Nia ya Yesu na mamlaka yake inaonekana katika neno hilo, akijibu "ukitaka" wa mwenye ukoma. "takasika" ukoma ulimtia mtu unajisi na uponyaji ulielezwa kuwa "utakaso".
Mara ukoma ulimwacha - neno "mara" ni ishara ya mamlaka na uwezo wa Yesu.

k.4. "usimwambie mtu" Yesu alitambua kwamba ipo hatari ya watu kumfuata kama mtenda miujiza tu. Vilevile ipo hatari ya watu kumwaza kuwa Masihi, Masihi wa siasa atakayewaondoa Warumi. Hayo yote ni kinyume cha Utume wake. "ujionyeshe kwa Kuhani...toa sadaka...iwe ushuhuda kwao" Iwapo Yesu alivunja sheria iliyoandikwa juu ya unajisi, kanuni ya nje, (ya ndani ya upendo na huruma aliitimiza) alilisimamisha juu ya kutoa sadaka ya shukrani Lawi 14:10, kwa sababu shukrani kwa Mungu ndiyo sheria ya ndani pia. "ujionyeshe" kwa kuuhakikishia utakaso wake. Pengine pia ni ushuhuda kuwa Yesu hapingi sheria za kale. Itakuwa vigumu kuwaza ni kuushuhudia uwezo wa Yesu kwa kuwa Yesu ameisha kumkataza asimwambie mtu. Yesu aliweza kufanya lile ambalo sheria kamwe hakuliweza, yaani kumtakasa mwenye ukoma.

**ii. Mtumishi wa akida 8:5-13 (Luka 7:1-10).** Yesu alimponya mwenye ukoma mtu aliyetengwa na jamii ya watu kwa sababu ya hali yake kimwili. Habari hiyo yafuatwa na habari ya mtu aliyetengwa kwa sababu ya Utaifa wake.

Akida alikuwa ofisa katika jeshi la ulinzi. Luka ametuambia alilipenda taifa la Israeli na kwa sababu ya rafiki zake walio Wayahudi alituma habari kwa Yesu. Ni mtu aliyempenda sana mtumishi wake, alikuwa tayari kumshughulikia.

Alifanya kazi Kapernaumu mahali alipokuja Yesu kuishi 4:13. Kutokana na kazi yake alikuwa mtu aliyefahamu sana neno la mamlaka. Mwenyewe alikuwa chini ya maofisa walio juu yake, lazima awatii mara, vile vile kama ofisa aliweza kutoa amri kwa walio chini yake nao lazima wamtii.

Kwa hiyo, alimwonaje Yesu? Alimtambua kuwa "mwenye mamlaka na uwezo" juu ya ugonjwa n.k. Mamlaka kuu ambayo akisema neno tu jambo latendeka, hata kwa mbali. Yesu hatakuwa na haja ya kuingia nyumbani mwake, wala kumwona, wala kumgusa mtumishi wake; yatosha atamke neno tu.

k.7 "nitakuja nimponye" Tukumbuke kwamba Wayahudi hawakuingia nyumba za Wamataifa, ili wasinajisike. Huenda maneno ya Yesu ni kama swali "Je! nije nyumbani mwako nimponye?" kama ni hivyo Yesu alitaka akida atambue ni nini analomwomba, aingie nyumba ya Mmataifa?" Kama si swali ni itikio lake kwa taarifa ya akida kuhusu mtumishi wake kuwa mgonjwa.

k.8. Akida alikuwa mnenyekevu sana na mwenye imani kubwa. Alikiri kwamba kibinafsi hastahili Yesu aingie nyumbani mwake si kwa sababu ni Mmataifa ila kwa sababu kimaisha hastahili. Yesu hana haja ya kuingia nyumbani mwake, neno tu, la mbali, litatosha. Kwa nini ni hivyo ni kwa sababu Yesu anayo mamlaka kuu kuliko yake. Neno la wakuu wa jeshi lilikuwa na nguvu, si zaidi neno la Yesu!!!

k.10 Ni mtu wa Wamataifa ambaye ni wa kwanza kutambua mamlaka ya Yesu. Yesu Mwenyewe alistaajabu (taz. Mk.6:6 Yesu alistaajabu kutokuamini kwa watu wake). Imani ya akida ilizidi ya ye yote katika Israeli.

k.11. "imani ya namna hiyo" ina maana gani kuhusu ufalme wa mbinguni? Ndipo Yesu alitamka kwa mamlaka ya KiMasihi maana yake mpya. "Nami nawaambieni":
i. Kwanza ufalme sio kwa Wayahudi peke yake;
ii. Neno la ajabu: WaMataifa wamwaminio wataingia;

iii. Neno la ajabu zaidi: Wayahudi wasiomwamini watatupwa nje "wataketi pamoja na" Wayahudi hawakuketi kula na WaMataifa maana kufanya hivyo watanajisika. Kumbe Wamataifa wataketi na baba zao, akina Ibrahimu, Isaka na Yakobo.!!!

"wana wa ufalme" ambao hasa ufalme ni wao watatupwa nje, kwa sababu walitegemea "uzao wao" tu, tena watapatwa na adhabu ya wasiomcha Mungu.

Kwa hiyo mapinduzi makubwa kuhusu ufalme yanatokea - walio ndani watatupwa nje, walio nje wataletwa ndani - na yote hayo hutokana na itikio lao kwa Huduma ya Yesu Masihi.

Kwa hiyo kanuni ya kuuingia ufalme wa Mungu ni IMANI katika Yesu. Yeye ndiye mwenye kuyafunua mapenzi ya Mungu kuhusu wokovu wa wanadamu wote, na ndivyo alivyofanya kwa tendo la kumponya mtumishi wa akida aliye Mmataifa na kwa tamko lake juu ya imani ya akida.

k:13.Ndipo Yesu alimponywa mtumishi aliye mbali kwa neno tu.

**iii. Mkwewe Petro** 8:14-15 (Mk.1:29-31 Luka 4:38-39) Petro alikuwa na nyumba Kapernaumu. Mk.1:38 wasema ni ya Simoni na Andrea. Huenda ilikuwa kubwa yenye nafasi kwa mkwewe Petro. Yawezekana Yesu aliishi humo. Kama ni hivyo ilikuwa mahali pa shughuli nyingi za Yesu: 9:10,28; 13:1,36; Mk.2:1 9:33. Yesu alikuwa mtu wa kwenda hapa na pale, na kama hakuwa na nyumba yake alihitaji nyumba za rafiki kuwa mahali pa kutua L.10:38-42.
Mkwewe Petro aliumwa homa kali, akashindwa kazi za nyumbani.
Yesu alimponya kwa kumgusa na mara aliweza kuendelea na shughuli zake, dalili ya uhakika wa kuponywa kwake.

iv: **Kujumlisha huduma ya uponyaji wa Yesu** 8:16-17: Mathayo kama
alivyopenda kufanya mara kwa mara alijumlisha "uponyaji wa Yesu" "wengi wenye pepo" walitolewa; na "wote waliokuwa hawawezi" aliwaponya. Pepo

walitolewa kwa neno si kwa kugusa, na bila itikio la imani. Wagonjwa waliponywa kwa neno au kwa kuguswa, na karibu mara zote kama itikio kwa imani ya mgonjwa.

Kwa Mathayo shughuli hizo hasa ni dhihirisho la Utume wa Yesu. Ni kutimiza Neno lililosemwa na Nabii Isaya; Is.53:4 neno la kuhusu Mtumishi atakayeteswa. "aliutwaa udhaifu wetu - aliyachukua magonjwa yetu" kwa kuyaondoa. Baadaye atazichukua dhambi zetu nafsini mwake na kutukomboa.

**v. Wawili waliotaka kumfuata** 8:18-22 (Luka 9:57-62).
k.18: Yesu alitaka kuvuka Bahari ya Galilaya ili awe mbali na makutano, maana ilikuwa rahisi kwao wasielewe shabaha kamili ya Utume wake.

k.19: Mwandishi mmoja - hatujui kama alikuwa mwanafunzi au bado. Ila alijitoa kwa bidii kumfuata Yesu.

k.20. Yesu alimwonya juu ya ugumu atakaoupata. Ugumu wa kukosa malazi na riziki watakapotembea hapa na pale bila mpango wa mahali pa kukaa n.k. Yawezekana alikuwa amevutwa sana alipoona umati wa watu na kuona matendo makuu ya Yesu na kusikia mafundisho yake. Ameona hayo mazuri ila bado hajauona ugumu wa maisha ya Yesu. Alimwita Yesu "mwalimu" pengine amemwaza kama marabi wengine.

k.21. Huyo wa pili ameitwa "mwanafunzi" na alimwita Yesu Bwana. Huyo hakutaka kuvuka bahari na kuendelea na Yesu wakati huo. Alitoa sababu ya "kumzika baba", kama kweli baba alikuwa amefariki dunia ni ombi la halali tena ilikuwa wajibu wa mwana kufanya yaliyotakiwa. Huenda maana yake ni baba alikuwa mzee ambaye yu karibu na kufa, kwa hiyo alitaka kurudi nyumbani na kungoja hadi afe, ndipo atasikia uhuru wa kumfuata Yesu sawasawa. Labda pia aliwaza urithi wake, ila si lazima tufikiri hivyo.

Yesu alikataa ombi lake kwa nguvu na ukali. Alimfahamisha kwamba mambo ya Ufalme wa Mungu yana haraka na umuhimu, madai yake hayachanganyiki na kitu kingine, hata mambo ya familia. Mambo ya nyumbani hayakosi watu kuyatimiza, ila ya ufalme wa Mbingu yafanyika na wale tu walio "hai kiroho" wafu ni wale walio nje ya kundi la wanafunzi.

Yesu alipenda kujiita Mwana wa Adamu na hapa ni mara ya kwanza kukuta amejiita hivyo. Ni Yeye tu aliyetumia maneno hayo. Hatujui kwa nini alipenda jina hilo, pengine ni kwa sababu lilionyesha dhati zake mbili, ubinadamu wake Zab.8. na Uungu wake Dan.7:13-14.

Hatujui hao wawili waliitikaje. Ila twaona Yesu alijibu kila mmoja kulingana na hali yake. Alitaka wa kwanza afikiri-fikiri kwanza ndipo amfuate, ila asimfuate kwa kuchukuliwa tu. Alitaka wa pili asiendelee kufikiri-fikiri hali za nyumbani kiasi cha kushindwa kumfuata. Afadhali afikiri juu ya umaarufu wa Ufalme na shughuli zake zinazohitaji haraka.

**vi. Kutuliza dhoruba** 8:23:27: (Mk.4:36-41 Luka 8:22-25).
Mathayo alitaka kuonyesha mamlaka ya Yesu juu ya pepo na bahari k.27, mamlaka ya kipekee inayozidi kuonekana. Wanafunzi waliogopa sana, tukumbuke wengi wao walikuwa wavuvi waliozoea maisha ya baharini. Bahari ya Galilaya ilijulikana kwa jinsi dhoruba kubwa ziliweza kutokea kwa ghafula. Kuvuka Bahari ilichukua kama saa 1 au 2, kumbe Yesu ameisha kushikwa na usingizi mzito hata hakuamshwa na dhoruba. Kwa sababu walikuwa katika hatari ya kuangamia wanafunzi walimwamsha. Usingizi wa Yesu ni ishara ya ubinadamu wake wa kweli na kuonyesha jinsi alivyochoka kwa sababu ya shughuli nyingi kila siku.

k.26a Aliwakemea kwa uhaba wa imani yao, wameona miujiza n.k. hata hivyo walishikwa na hofu. Yesu hakuwadharau iwapo imani yao ilikuwa haba alikubali kuwasaidia.

k.26b: "akazikemea bahari na pepo" kwa mamlaka yake Mwenyewe kama mkuu wa Maumbile na Mwumba wake.

k.27. Watu waliuliza "huyu ni mtu wa namna gani?" Katika Agano la Kale dalili ya mamlaka ya Mungu ilikuwa utawala wa Bahari - Ayubu 38:8-11; Zab.65:5-8; 89:8-9; 107:23-32. Yesu ameonyesha uwezo na mamlaka ya "Mwumba", amefunuliwa kuwa Masihi na zaidi ya Masihi.

**vii: Wenye pepo wa Gadara** 8:28-34 (Mk.5:1-20 Luka 8:26-37)
Gadara ilikuwa maili 6 kutoka pwani na eneo lake lilifika mpaka pwani. Hao wawili waliishi maisha ya upweke na watu waliwaogopa sana na kuwaepa. WaMataifa wengi waliishi sehemu zile, na walifuga nguruwe - mwiko kwa Wayahudi. k.29: Yesu hakuwahofu alipitia pale walipo - labda walikuwa wamewaona wakati wa dhoruba. Walimtambua kuwa Mwana wa Mungu na hao waliozoea kuwaogofya wengine walijaa hofu.

"umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?" Walijua Yesu ni Mhukumu wao, ni Yule wa kushindana na uovu na kuushinda. Kumbe walifikiri amewahi kuja kuwaangamiza, walijua makubwa yatatokea watakapokutana na Yesu.

Kwa hiyo walimwomba Yesu asiwaangamize bali awaruhusu kuingia nguruwe, ili wapate "kikao". Yesu aliwaruhusu, ila labda kwa kelele au vipi hatujui, nguruwe walishtuka, na kwa sababu walikuwa kwenye telemko walikimbia kwa haraka na kupotea majini.

Wenyeji walipata hasara ya nguruwe, ila kwa upande wa pili wanadamu wenzao wawili walipona, wakaweza kurudi makwao kwa familia zao na kuishi maisha ya kawaida. Pamoja na hayo wenyeji waliondolewa hofu wakaweza kupitia po pote pale walipotaka. Kwa hiyo kweli hasara ya nguruwe ilitokea lakini vile vile faida kubwa zilitokea. Yesu hakuwaharibu nguruwe, ni pepo waliosababisha vifo vyao. Kwa kuwahurumia wale wawili Yesu aliruhusu pepo wawatoke na kuingia nguruwe.

Wenyeji walionaje? Kweli walithamini nguruwe zao kuliko kuwepo kwa Yesu kati yao, walimwomba aondoke. Hawakufikiri ni baraka zipi watakapozipata akizidi kukaa nao! Walipenda nguruwe kuliko Yesu.

Kwa hiyo tumeona mamlaka ya Yesu juu ya "enzi" za Shetani. Amedhihirika kuwa Mwana wa Mungu ambaye amekuja kumfunga Shetani na kuwaacha wafungwa wake huru 12:22-29. Ishara ya kuwa uovu utashindwa kabisa kabisa baadaye.

**viii: Aliyepoozwa: 9:1-8:** (Mko 2:1-12 Luka 5:17-26)

Walirudi Kapernaumu, mjini kwao, 4:13. Yesu alipoona imani ya rafiki za mwenye kupoozwa aliitambua ni imani ya kweli. "jipe moyo mkuu, mwanangu" maneno ya kumtia moyo na kumtazamisha atapona ila maneno yaliyofuata bila shaka mgonjwa hakuyatazamia "umesamehewa dhambi zako" - yalihusu ugonjwa wake kwa njia gani? Kwa nini Yesu atangulize maneno hayo? Wayahudi walizoea kufikiri kwamba ugonjwa unaletwa na dhambi Yoh.9:2. Hatuwezi kujua kama kweli huyu mtu amefanya dhambi fulani ambayo imesababisha ugonjwa wake wa kimwili.

Pengine Yesu kwa kujua mtindo wao wa kuwaza alichukuliana na mawazo hayo ili amsaidie. Alikuwa na haja mbili, ya kusamehewa, na kupona.

Tangazo la Yesu la msamaha ni kubwa sana, maana ni kazi ya Mungu peke yake kusamehe dhambi. Yesu hakusema "Mungu akusamehe" la! - alisema kwa mamlaka yake Mwenyewe. Tena kwa uhakika wa tendo lenyewe kuwa limetendeka tayari "umesamehewa" si utasamehewa.

k.3 Waandishi waliokuwepo walianza kumpinga Yesu. Kwao Yesu amekufuru. Ni mara ya kwanza tusikie habari za upinzani, nao umetoka kwa waandishi, kundi moja lenye sauti na madaraka katika Israeli, watu walioyashughulikia Maandiko na kutoa uongozi katika mambo ya imani.

k.4."Yesu hali akijua mawazo yao" 12:25; 22:18. Alijuaje? hatuna haja ya kufikiri alifunuliwa kipekee na Baba yake, huenda alijua kutokana na wepesi wake wa kutambua hali za ndani za kiroho. "mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu?" Yesu alikuwa tayari kuushambulia msimamo wao.

k.5. "rahisi ni lipi, ni kusema umesamehewa, au ondoka uende?" Kwa kweli rahisi ni kusema "umesamehewa" maana hakuna atakayeweza kuthibitisha kama msamaha umetokea au siyo; ila kusema "ondoka, uende" kutathibitishwa kwa tukio litakaloonekana, na kama halionekani basi kusema kwake kutapuuzwa. Kwa hiyo kama Yesu akimwambia mwenye kupoozwa "ondoka, uende" naye anaondoka na kwenda, basi hawataweza kukana neno la msamaha. Litakuwa na nguvu ile ile. Na kama kweli kuna uhusiano kati ya dhambi na ugonjwa wake, atakuwa ameponyeka mambo hayo mawili.

k.6. Ndipo Yesu alitoa amri kwa mgonjwa kuondoka na kurudi nyumbani kwake. Na amri hiyo alitoa ili wapate kujua "Yeye anayo amri duniani ya kusamehe dhambi." Amri duniani, yaani hapa hapa wakati huo huo.

k.7 Mara mgonjwa aliponywa.

k.8. Itikio la waliokuwepo: walishikwa na hofu na kumtukuza Mungu. Waliona Yesu ni tofauti sana na wengine. "aliyewapa watu amri ya namna hiyo" neno "watu" ni la ajabu, maana watu hawakuweza kusamehe dhambi, ila baadaye Yesu aliwashirikisha wanafunzi wake amri hiyo 16:19; 18:18.

Mathayo aliendelea kujenga picha ya mamlaka ya Yesu kuzidi: 7:28-29 mamlaka katika kufundisha: 8:1-17 mamlaka juu ya magonjwa aina aina, ukoma, kupooza, homa n.k. 8:18-22 mamlaka ya kuita watu na kudai wampe utiifu wao wote; 8:23-27 mamlaka juu ya maumbile; 8:28-34 mamlaka juu ya pepo, enzi za kiroho; 9:1-8 mamlaka ya kusamehe dhambi.

**ix: Wito wa Mathayo:** 9:9-13: (Mko 2:13-17 Luka 5: 27-32)
Mathayo baadaye aliitwa na Yesu kuwa Mtume 10:3. Marko na Luka wamemwita Lawi. Aliishi Kapernaumu kwa hiyo haikosi amesikia habari za Yesu. Alifanya kazi ya mtoza ushuru, akiketi forodhani penye Ziwa la Galilaya na kutoza ushuru kwa bidhaa iliyosafirishwa. Watoza ushuru hawakupendwa na wenzao kwa sababu walikuwa wakiwasaidia Warumi walioitawala nchi. Yawezekana walifanya waliposhindwa kupata kazi nyingine. Ilikuwa rahisi wadhulumu watu wakitoza zaidi ya kiasi cha halali.

"wenye dhambi" ni wale ambao hawakushika sheria ndogondogo za mapokeo kama Mafarisayo walivyofanya. Wengine ni wale walioshindwa maisha. Ila Mafarisayo na wenzao walijumlisha aina zote mbili kuwa mamoja.

Yesu aliketi mezani pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi asisikie shida yo yote katika kushirikiana nao. Mathayo kwa furaha ya kuitwa na Yesu aliandaa karamu kubwa akitaka rafiki zake wakutane na rafiki yake mpya.

Kuketi nao ni dalili ya urafiki na ushirikiano. Ni ishara ya utayari wa Yesu kujihusianisha nao. Luka 15:1-2 na 19:1-10 aliitwa "rafiki yao"

k.11 Mafarisayo walipoona hayo walianza kumpinga wakiwauliza wanafunzi wake "mbona mwalimu wenu?" Mbona maana yake Yesu amekosa katika kula na watu wa namna hiyo.

k.12. Kwa jibu lake Yesu alionyesha kwamba kitu cha kwanza katika mapenzi ya Mungu ni watu na haja yao ya kupewa msaada. Kwa Mafarisayo kitu cha kwanza ni sheria zao ndogo ndogo, na nyingi nyingi, zisizo na msaada, zilizolemea watu. Yesu ametumwa kwa ajili ya kuwasaidia watu, "sheria" yake ni upendo uliojaa huruma ya kuwahurumia watu. Ndivyo alivyoona Nabii Hosea zamani Hos.6:6. Mafarisayo walisimamia dini ya nje, yenye visheria vingi badala ya amri kuu ya upendo. Kwa hiyo dini ya Mafarisayo ni kinyume kabisa ya mapenzi ya Mungu. Kumlaumu mgonjwa kwa sababu eti ni mgonjwa ni msaada gani kwake? kutokumshughulikia kibinafsi kutamsaidiaje?

13b. Neno "sikuja kuwaita wenye haki bali wenye dhambi" ni kama maneno ya 8:11-12 - ni maneno ya upinduzi. Wenye kuitwa karamuni bila shaka ni "wenye

haki" lakini Yesu afanya upinduzi na kuwaita "wenye dhambi". Mafarisayo machoni pao walikuwa wenye haki Fil.3:5 lakini machoni pa Yesu haki yao haitoshi 5:20: 5:6,10 wenye kiu na njaa ya haki wako karibu zaidi na "haki" kuliko Mafarisayo ambao wameshibishwa na haki yao na hali yao.

Pamoja na hayo wote ni wenye dhambi Rumi 3:10. Wasio tayari kuungama hawana sehemu katika rehema za Mungu. Hamna dini wala sheria iwezayo kuleta "haki ile izidiyo" 5:20, inayodaiwa na Mungu. Haki hii hutokana na uhusiano mwema na Mungu kwa njia ya Yesu.

**x: Maulizo juu ya kufunga** 9:14-17 (Mk.2:18-22 Luka 5:33-38)

Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji walimlaumu Yesu juu ya kufunga na jinsi ambavyo Yeye na wanafunzi wake hawakufunga. Katika dini ya Kiyahudi ni siku moja iliyowekwa kwa watu kufunga, Sikukuu ya Upatanisho. Ila wakati wa Yesu Mafarisayo walifunga siku mbili za juma n.k. Lu.18:12. Hasa sababu ilikuwa "ya huzuni" ila Mafarisayo na wanafunzi wa Yohana wengi wao walifanya kwa desturi tu.

Yesu amekuja na kuleta "dahari mpya", ni jambo la furaha kuu Ufalme wa Mungu umekuja. Kwa hiyo wanafunzi hawawezi kuhuzunika. Wayahudi waliwaza Nyakati za Masihi ni kama Arusi, ni wakati wa Karamu Is.25:6-9; 35:1-10. Yesu alifananisha huduma yake kuwa arusi na Yeye ni Bwana Arusi.

15b. Ila siku itafika na bwana arusi ataondolewa. Ni mara ya kwanza Yesu kudokeza kwamba atauawa, na dalili zipo katika upinzani kuzidi. Atakapoondolewa ndipo wanafunzi watashikwa na huzuni kubwa nao watafunga. Ni muda wa tangu alipouawa hadi alipofufuliwa Yoh.16:16-21. Yesu alijua kuna utofauti usiopatanishwa kati ya Israeli ya zamani na Israeli mpya, na kati ya haki ya sheria na msamaha wake kwa imani.

k.16-17: Neno kuu liletalo furaha ni kwamba Imani mpya ya Kikristo itashika mahali pa imani ya Kiyahudi iliyotangulia, ambayo "imezeeka". Imani hiyo mpya huleta uzima mpya wa kiroho. Yesu ameleta kitu kipya "divai mpya" nacho hakiingizwi katika viriba vikuukuu vya Kiyahudi. Kitu kipya chahitaji viriba vipya, yaani "sheria mpya na tabia mpya" upendo na huruma zilizoonyeshwa katika Hotuba ya(Mlimani. Roho wa Mungu atakuwa badala ya "andiko liualo" 2 Kor.3:6. Si kwamba divai mpya ni uhuru wa kufanya asikiavyo mtu, la! viriba vipya vyahitajika kuhifadhi divai mpya bila kuibana.

Katika Kanisa wakristo walifunga wakati wa kuamua mambo makubwa n.k. Mdo.13:2-3; 14:23; 9:9.

Katika fungu hilo la tatu la miujiza Yesu ameonekana kuwa Yule wa kurudisha uzima na uwezo wa kuona na wa kunena.

**xi. Binti wa mkuu wa sinagogi na mgonjwa wa kutoka damu** 9:18-26: (Mko 5:22-43 Luka 8:40-56).

Mathayo amefupisha sana habari hii tukilinganisha na Marko na Luka. Pia amechanganya habari mbili, ya binti WA Yairo na ya mama mgonjwa. Jumbe mmoja - mkuu wa sinagogi, jina lake Yairo Mk. 5:22, alikuwa na binti wa umri wa miaka 12 aliyeugua kisha akafa. Yairo alipoona hali ya binti imezidi alimwendea Yesu na kumwomba aje. k.18 "sasa hivi amekufa" maana yake hali yake ni mbaya yu karibu kufa Mk.5:23,35. Yesu alichukua Petro, Yohana na Yakobo pamoja naye. Walipofika nyumbani, hakika amekufa, wapiga filimbi wamefika, hao walioajiriwa kuongoza maombolezo, pamoja na umati wa watu.

k.24. "ondokeni, kwa maana kijana hakufa amelala tu" si kwamba kweli hakufa ila kifo chake ni kama usingizi kwa vile karibuni hivi "ataamka" yaani Yesu atamfufua kutoka wafu.

k.24b. "walimcheka sana" Luka 8:53,55. kwa kweli watu walihesabu maneno ya Yesu "amelala tu" ni mzaha, ila pia ni dalili ya ukweli wa kufa kwake.

"ondokeni" mamlaka ya Yesu juu ya umati wa watu ilionekana, ni nani ambaye angethubutu kuondoa watu wakati wa kilio?!!

k.25. Halafu mamlaka yake juu ya mauti ilionekana, adui wa mwisho mauti ilishindwa, ililazimika kutoa mtu wake.

Ni ishara ya umasihi wake 11:5, baadaye wanafunzi walishirikishwa mamlaka hiyo.10:8.

Mwanamke wa kutokwa damu 9:20-22. Huyo mama alikuwa ameumwa siku nyingi, ametafuta msaada kwa madaktari na wa dawa, bila mafanikio yo yote. Yesu alipokuwa akienda nyumbani kwa Yairo huyo mama aliamua kuchukua nafasi hii njema ili aponywe Watu wengi walimsonga Yesu, na huyo mama aliamini kwamba hana haja ya kusema lo lote, mradi tu aliguse pindo la vazi lake tu, itatosha. Kufuatana na neno la Lawi 15:25 amenajisika.

Yesu alimgeukia na kumtia moyo "jipe moyo mkuu binti yangu" Imani ya namna hiyo ilimfurahisha Yesu. Ni Yesu aliyemponya na imani yake ilikuwa kama ufunguo wa kufungulia hazina ya uwezo wa Yesu Mk.5:30. Yesu alipenda kuchochea imani za watu na kuwatia moyo. Habari za Yesu zilizidi kuenea.

**xii: Vipofu wawili** 9:27-31:
Yesu alimrudishia binti uhai wake, sasa atawarudishia hao vipofu wawili uwezo wa kuona.

k.27: Inaonekana Yesu hakuitika mara moja walipokuwa njiani bali aliendelea mpaka alipofika na kuingia katika nyumba fulani, ndipo akawajali. Huenda alikuwa akipima ukweli wa imani yao.

"uturehemu Mwana wa Daudi" Kurehemu ni kutenda jambo si kuliwaza tu. "Mwana wa Daudi" ni jina la Masihi 15:22; 20:30-31. Isaya alitabiri kwamba Masihi atawaponya vipofu Is.35:5-6. Pia Masihi atakuwa mwenye rehema Is.61:1, Math.11:4-5.
k.28: Yesu aliendelea kuwahoji juu ya imani yao, wapaswa kuikiri wazi.

Imani iliyo na matumaini katika uwezo wa Yesu kutenda jambo. Katika miujiza ya sura hizo imani imekazwa sana, mwenye ukoma, akida, rafiki za aliyepooza, binti wa Yairo, na mama mgonjwa.

k.29: Yesu aliwaponya kwa kuwagusa na kwa kutamka maneno kama alivyofanya kwa mgonjwa wa kutoka damu.

k.30: Yesu aliwakataza wasiseme habari zake. Hakutaka kuamsha watu wamfuate bila kuelewa au watamwaza isivyo na kumtazamia yale yaliyo kinyume cha wito wake. Umasihi wake si wa siasa, hakuja kuipindua serikali ya Kirumi.

Lakini kwa hao wawili waliopata kuona kweli, ilikuwa vigumu wanyamaze, wakaenda na kueneza habari zake sehemu ile yote.
**xiii: Mtu bubu:** 9:32-34.
k.33 Inaonekana ni pepo aliyesababisha huyo mtu kuwa bubu. Math.12:22 Mk.9:17. Yesu alitoa pepo ndipo mtu akanena.
Hatusikii habari za imani, wala hatuoni kwamba Yesu alimgusa.

Twaona itikio la makutano walioona jambo hilo: "Hayakuonekana hivi katika Israeli, yaani katika taifa letu, wakati wo wote" waandishi walifundisha lakini hamna matokeo, ila Yesu anena na pepo hutoka, dhoruba hutulia, dhambi husamehewa, wafu hufufuliwa - dalili za kuwako kwa Ufalme wa Mungu.

k.34. Itikio la Mafarisayo ni tofauti, hawakupenda kusikia jinsi watu walivyosema, walipinga, na kuzidi kupinga, k.3,11,14. na upinzani huo utazidi 12:24.

*MASWALI:*

*Katika sura hizi tuna habari ya Yesu akiwahudumia wagonjwa Unapofikiri juu ya jinsi Yesu alivyohudumia watu mbalimbali wenye mahitaji mbalimbali, umejifunza nini ambayo itakusaidia wewe kuwahudumia watu mbalimbali?*

*Twaona jinsi Yesu alivyowajibu wawili waliotaka kumfuata, kila mmoja na tabia yake. Kijana akija kwako akisema anataka kuwa pasta/mtumishi utafanyaje? Itakubidi kutambua nini? utataka kuona nini kwake?*

## HUDUMA YA WANAFUNZI 9:35 - 11 :1.

Fungu hilo la pili ni kama hati au mwongozo kwa wanafunzi wa Yesu alipowatuma kufanya kazi.

i. **Kujumlisha na utangulizi:** 9:35-38 Katika sehemu hiyo Mathayo ametazama nyuma na kujumlisha shughuli za Yesu, pia ametazama mbele na kuonyesha shughuli zitakazoendelea kufanyika na wanafunzi wake atakapowatuma 10:1.

k.35: Kama alivyofanya 4:23 alijumlisha huduma ya Yesu mpaka wakati huo. Picha ni kwamba Yesu alikuwa amefanya kazi nyingi sana akizunguka-zunguka mijini na vijijini vya Galilaya. Miujiza 10 ya sura za 8 na 9 ni michache tu

ambayo Mathayo aliichagua ili aonyeshe matendo yake makuu. Yesu alifanya aina tatu za shughuli hasa, kufundisha, kuhubiri, na kuponya.

k.36: Alikuta nini katika kuzunguka kwake? Alikutana na umati wa watu waliokosa "mtu wa kuwachunga na kuwatunza" Hali yao ilikuwa mbaya "wamechoka na kutawanyika" maana ya maneno yaliyotumika ni "wameraruliwa na kutupwa chini" Wachungaji wao walikuwa wakali wasiostahili kuitwa wachungaji.

Huenda ni hukumu juu ya viongozi wa dini. Katika 10:6 na 15:24 ni "kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" wasio na viongozi waliotumwa na Mungu Hes.27:16-20, 1 Waf.22:17, Ez. 34:5. Wahitaji Masihi Mchungaji Mik. 5:4; Ez. 34:23.- ni Yesu.

Yesu alisikiaje alipoona hali yao? Aliguswa sana ndani, alisikia huruma kubwa, huruma ya kufanya neno la kukabili shida zao, atawaletea msaada. Haitoshi kuona shida kubwa na kuwahurumia kimawazo tu au kukata tamaa na kuacha kufanya 10 lote lile la kuwaletea msaada.

k.37-38: Atafanyaje? Mara atatuma watu kwao, watu ambao amewashirikisha uwezo na mamlaka yake 10:1,5-8. Kama haja ni kubwa vilevile nafasi njema ni kubwa. Mavuno ni tayari na ni mengi.

Kwa sababu ya shida zao watu huwa tayari kuitika Yoh.4:35 ila wavunaji ni wachache kulingana na nafasi zilizopo. Wafanyaje ili wavunaji wapatikane? Wamwombe Mvunaji Mkuu azidishe watenda kazi. Huduma hiyo ina Mungu, na Yeye ni kiongozi wake.

Sura ya 10 yaonyesha huduma ya waliotumwa jinsi ilivyo na mambo yaliyomo ni nini kwa wale wa kuifanya.

ii: **Mitume 12** 10:1-4: (Mk.3:14-19; Luka 6:13-16; Yoh. 1:40-49)

Yesu alisema juu ya haja ya kupata watumishi maana alifahamu ya kwamba Yeye Mwenyewe hataweza kufikia kila mahali, kwa hiyo alichukua hatua ya kutuma wanafunzi 12. Aliwapa amri ya kufanya kama alivyofanya Mwenyewe 4:23 9:35. Mtume ni mtu aliye na mamlaka ya yule anayemtuma. Walikuwa wanafunzi waliojifunza kwa Yesu ndipo walistahili kutumwa. Walipewa mamlaka kwa Huduma si kuwekwa kama viongozi wa chama.

Katika orodha zote Petro ametajwa kwanza. Bartholomayo ni Nathanieli aliyetajwa na Yohana Yoh. 1:45. Mathayo ameitwa Lawi katika Marko na Luka. Thadayo ni Yuda Luka 6:16. Simoni Mkananayo ameitwa Zelote na Luka. Wazelote walitaka kuipindua serikali ya Kirumi. Hivyo Yesu alimwita Mathayo aliyekusanya kodi kwa Warumi na Simoni aliyetaka kupindua serikali. Yuda Iskariote amewekwa mwishoni, kama yule wa kumsaliti Yesu. Yawezekana ameitwa "Iskariote" kama alitoka mji wa Kerioth, kama siyo, maana ya neno ni msaliti au mwongo. Yadhaniwa ni yeye tu aliyetoka kusini ya nchi.

iii: **Maagizo kwa huduma yao:** 10:5-16:
k.5-6:Waliambiwa wasiende kwa Wamataifa na Wasamaria ila wawaendee Waisraeli tu. 15:24. Kwa nini? kwa sababu hawatakuwa na nafasi ya kwenda kwa hao wote. Vilevile afadhali wawaendee wale wa taifa lao, maana watawaelewa vizuri. Hasa katika mpango wa Mungu kihistoria, Injili ni kwa Wayahudi kwanza Rumi 1:16; 11:13ku. Mdo.13:46.

Baada ya kufa na kufufuka kwa Kristo watatumwa kwa WaMataifa Math.28:18-20. Mathayo amekwisha kuonyesha kwamba Wamataifa wataingizwa katika Ufalme wa Mungu - 8:11-12; 21:43; 25:32 na katika habari za 2:1-12; 4:14-16; 24:25 dalili zipo, kwa hiyo isiwazwe kwamba kuna hali ya kupinga WaMataifa, la hata kidogo, ila kimipango, na kihistoria Wayahudi hutangulia.

k.7-8. Ujumbe wao ni ule ule wa Bwana Yesu 4:17 na watatenda yale yale 4:23 9:35. Matendo yao ni ishara ya kufika kwa Ufalme wa mbinguni na wenye macho watatambua ni majira ya Masihi. Wamepewa amri na uwezo bure, nao watende kazi yao kwa ukarimu sana, bila malipo, na bila kutoza fedha.

k.9-10: Wachukue mahitaji ya lazima tu, wasijilemee bali wawategemee wale wanaoendewa kwa riziki na malazi. Hivyo watakumbushwa daima umuhimu wa kazi yao, haraka yake, na jinsi iwapasavyo kuiweka mbele. Vilevile hali zao za kujitoa zitavuta usikivu wa watu na kuwasaidia kuutambua umuhimu wa ujumbe wao. Ilitegemewa watatunzwa "mtenda kazi astahili posho lake".

k.11: Yesu aliwaambia wakae na watu wenye sifa ya kuwa waaminifu, walio tayari kuwapokea vizuri na kuupokea ujumbe wao. Huenda sababu ni wasiwazwe kwa mashaka, pia waonyeshe tabia ya kutulia na kuridhika, wasihame-hame kama watu wasiotosheka na utunzaji wao.

k.12-13: Watoe salamu ila salamu hizo ni zaidi ya maneno tu. "amani" itawafikia wale tu ambao watawakaribisha vema, kama siyo "amani" itawarudia wale walioitoa.

k.14: Yesu alitazamia baadhi ya watu watawapokea ila baadhi watawakataa, na kwa hao ni jambo kubwa la hatari, kwa hiyo watapewa ishara nzito kwa kukataa kwao "kukung'uta mavumbi". Bila shaka ishara hiyo ilieleweka na kutumika siku zile. Ilikuwa ishara ya nini? ishara ya hukumu kali ya Mungu, izidiyo ile ya Sodoma na Gomora zamani Mw.19:4-9.

Kwa nini izidi? Kwa sababu wameitwa kutubu, Habari Njema ni neno la mwisho kutoka kwa Mungu, kwa kuwa katika Yesu Mungu amepatanishwa na wanadamu, yu tayari kusamehe dhambi. Kwa hiyo kukataa ni kufunga njia pekee ambayo kwayo mtu aweza kumkaribia Mungu na kupata msamaha na msaada wa maisha.
Kukataa ni dhambi kubwa, itikio la ajabu kwa upendo wa Mungu.

Wasikae mahali wasipotakiwa, maana nafasi ni tele. Kwa jumla twaweza kusema kwamba hali yao yote ionyeshe kuwa wametumwa na "Mfalme Mkuu" wakiwa na ujumbe muhimu kabisa juu ya wokovu wa watu nao unahitaji itikio la mara moja. Kwa vyo vyote hali zao ziwe msaada kwa watu ili watambue

kwamba Masihi amefika na ni Yeye aliyewatuma. Ishara wanazozifanya ni ushuhuda wa Kufika Kwake, na maisha yao ni uthibitisho wa umuhimu wake.

k.16. Hayo yote yalihusu safari iliyo mbele yao, halafu Yesu aliendelea kuzungumza habari za mateso. Wao ni wana-kondoo kati ya mbwa-mwitu, wako katika hatari, hawana ulinzi ila kumtegemea Mchungaji wao. Ila wasiwe kondoo tu, bali wafanane na nyoka kwa busara, watumie fahamu zao, wawe macho. Pia wafanane na hua kwa upole, wawe na nia safi, watu wa kweli. Hivyo kwa kutumia busara na upole na kuwa watu wa kweli watajihifadhi ili waendelee na kuitimiza huduma yao.

iv. **Maonyo juu ya upinzani na mateso** 10:17:
k.17. Yesu aliwaonya juu ya maudhi na mateso watakayopata kwa ajili yake katika kuitimiza
huduma yao. Wasiwaamini watu "wanadamu" watawashtaki na watapigwa n.k. k.18: maneno "maliwali na wafalme, WaMataifa" huenda Yesu amewaza ya mbele watakapokwenda kwa WaMataifa. k.19-20:

Wachukue nafasi hizo kwa kumshuhudia Kristo, na Roho atawasaidia na kuwapa maneno ya kuyajibu mashtaka. k.21: Injili italeta matengano katika familia. k.22: "mtachukiwa na watu wote" mateso yatatoka kwa watu, kwa serikali, kwa familia, maana yake wasitumaini kuwa salama. Wadumu kuwa waaminifu, wasikate tamaa, wala wasiache kumshuhudia Kristo, ndipo wataokoka. Ajabu ni kwamba chuki ndiyo itikio la watu kwa pendo la Kristo kufa kwa ajili yao!

k.23: Ipo nafasi tele kuendelea na utume wao, wasikae mahali pamoja, wasipotakiwa, kama watu hawautaki ujumbe waende penginepo. "hata ajapo Mwana wa Adamu" ni nini maana ya maneno hayo"? Wengine huwaza ni mpaka Yesu amekufa na kufufuka - mpaka ametukuzwa na ushindi umepatikana na kuthibitishwa na Mungu katika kumfufua. Wazo lingine ni mpaka Kuanguka kwa Yerusalemu BK.70 Mungu alipolihukumu taifa la Israeli kwa kumkataa Mwana wake, na baada ya watu kupewa muda wa miaka kama 40 kubadili uamuzi wao juu yake. Ni thibitisho la maneno ya Yesu kuhusu Yerusalemu Math.24.

Mkazo ni waendelee na ushuhuda wao katikati ya vipingamizi vingi na maudhi mengi hali wakijua Yesu atatukuzwa.

k.24-25: Chuki hasa ni kwa Yesu Kristo. Wamepata heshima ya kushirikishwa kazi yake na kuwa wajumbe wake, na watashirikishwa mateso yake.

k.26-33: Neno kubwa la sehemu hiyo ni "kuogopa". waliposikia maneno ya Yesu kuhusu kuchukiwa na kuteswa bila shaka walianza kuogopa, na hofu hiyo ingaliweza kuwakatisha tamaa wasiendelee na huduma. Wapaswa kuendelea kumshuhudia Kristo hadharani - Rumi 10:9-11, watangaze wazi "juu ya

nyumba" yale waliyoyasikia kwa Kristo sirini, na Mungu atathibitisha ujumbe wao.

Wamwogope Mungu, wasiwaogope wanadamu? Kwa nini? kwa sababu kuna mpaka katika uwezo wa wanadamu kuwaudhi - waweza hata kuwaua kimwili bila kugusa uhusiano wao na Mungu na maisha yao ya baadaye. Tena ni Mungu aliyestahili kuogopwa, Yeye ndiye Mhukumu wa wote, na ni afadhali kuuawa kwa ajili ya Kristo kuliko kumwasi Kristo na kukataliwa na Mungu.

Wakiogopa watu watashikwa na woga ndipo watamkana Kristo, watamkana kwa kunyamaza tu.
Mungu Baba aliye Mhukumu wa wote ni Mhifadhi kwa wale wamchao. Yeye huangalia hata mambo madogo madogo, ndege, na nywele za vichwa!!! maana yake hakuna kitu kilicho nje ya ufahamu wake. Yeye hujua mambo yetu ya ki-binafsi. "bora ninyi kuliko mashomoro wengi" mashomoro ni ndege wadogo tena ni wengi, waliuzwa kwa bei rahisi k.29, chakula kwa maskini.

k.32-33: Kwa hiyo Baba anayeangamiza mtu Yehanamu ni yuleyule wa kuangalia ndege kwa hiyo wasiogope, ni Baba wa upendo kwa wote wanaomtegemea. Watakufa wakati ulioamriwa na Mungu, na kuna tukio baya kuliko kuuawa kwa ajili ya Kristo nalo ni kukanwa na Kristo mbele za Baba na kukataliwa.

Kwa hiyo tunalotenda wakati huo ndilo linaloongoza tutakalotendewa baadaye.

Bwana wao kamwe hawatawakana walio wake, waliompa Yeye utiifu wao wa kwanza. Itakuwa heshima kupita zote kumsikia Yesu akinikiri mbele za Baba wazi, katika siku ile kuu ya mwisho, vilevile itakuwa aibu kupita zote na hasara kuu kumsikia Yesu akinikana mbele za Baba. Maneno hayo yatusukume tumkiri Kristo wakati wote na mahali pote, potelea mbali tutapokelewa au kukataliwa na watu.

Kitu kikubwa ni uhusiano wetu na Bwana Yesu. Kama Yesu hakuwa Mwana wa Mungu na Masihi wa kweli aliyetumwa na Baba, kwa kweli alijaa "umimi" na kuwa mdanganyifu wa kwanza, maana alidai makubwa mno. Kwa hiyo wachague wawe pamoja na Yesu au pamoja na watu.

k.34-35:"Msidhani nalikuja kuleta amani duniani; la! sikuja kuleta amani, bali upanga" Maneno hayo yaonyesha matokeo ya Kuja kwake si sababu yake. Wayahudi walikuwa na mtindo wa kuonyesha matokeo kama ni sababu, mtindo huo huonekana mara kwa mara katika Agano la Kale. Iliandikwa kwamba Masihi ataleta amani Is.9:5-7; 11:1-9; Zek. 9:9-10 na Luka 2:14. Kwa nini "upanga" umetajwa, ni dalili ya nini? Ni dalili ya utengano utakaotokea, utakaosababishwa na watu kumwamini. Ni kuhusu itikio la watu. Yesu hudai kuwa wa kwanza katika maisha ya mtu, kabla ya jamaa zake na kabila lake, na serikali yake n.k. Madai hayo ni "upanga", yahusu utiifu wetu. Kama familia watanidai kinyume cha mapenzi ya Mungu au kutanguliza mapenzi yao,

napaswa kutii mapenzi ya Mungu kwanza. Vilevile kwa serikali, kwa kabila, kwa cho chote kile kitakachodai utiifu wangu.

Tuangalie Yesu alisema "kuliko" si badala, hasa ni kuhusu ni nani aliye wa kwanza(katika maisha yangu - na Yesu hakubali kuwa wa pili au wa tatu! 6:33.

"kuchukua msalaba" ni kukana nafsi. Kweli nitaumizwa kama matakwa yangu au ya familia yatakuwa kinyume cha anayotaka Mungu. Ni kusema "la" kwa mapenzi yangu na "ndiyo" kwa mapenzi ya M}ngu.
k.40-42. Iwapo Yesu ameonyesha "hasara" ya kumfuata, hasara ya maudhi na mateso, hasara ya kujikana nafsi, hata hivyo, si hasara tupu. Faida zipo. Faida ya heshima ya hali ya juu ya kushirikishwa baraka za kuwa pamoja na Kristo. Na wale watakaowapokea watakuwa wamempokea Kristo, na wale wa kufanya jambo dogo, la kawaida kabisa, kama kumpa mtu maji kwa sababu ni mtumishi wa Kristo, watahesabiwa kuwa wamempa Kristo hayo maji. Nao wote watapata thawabu ya milele, kushirikiana na Kristo katika uzima wa milele kwa kuwa walikubali kuwa naye duniani kwa njia ya kumkiri.

Kwa hiyo tangu mwanzo wa sura hiyo tumeona ya kuwa jambo kubwa ni uhusiano wa wale waliotumwa na Bwana wao. Wameshirikishwa amri na uwezo wake, watashiriki kupokelewa ni kukataliwa kwake, watashiriki mateso yake, watashiriki uhifadhi wa Baba yake, watashiriki heshima zake na hasa heshima ya Yeye kuwakiri mbele za Mungu, na mwishowe watashiriki thawabu ya milele, kuwa pamoja naye katika utukufu wa milele. Hivyo wasiwaogope wanadamu, wamwogope Mungu Baba yao, waendelee kumshuhudia Kristo kwa wazi.

11:1: Hapo Mathayo afunga fungu hilo kwa kujumlisha 7:28-29: ili aendelee na habari zingine.

## MAITIKIO MBALIMBALI KWA HUDUMA YA YESU: 11:2 - 12:50.

Katika sehemu hiyo Mathayo amekusanya pamoja mambo mbalimbali yanayoonyesha ukweli wa Umasihi wa Yesu na aina yake na maitikio mbalimbali ya watu.

i. **Yohana Mbatizaji** 11: 2-19. Yohana alitiwa gerezani 4:12. Yosefu (Josephus) mwalimu wa historia ya Kiyahudi alisema alifungwa katika gereza la Machaerus, mashariki ya Bahari ya Chumvi. Baadaye aliuawa kwa agizo la Herode Antipa 14:1-12.

Bila shaka alipofungwa alisikia shida sana kwa sababu ya ugumu wa maisha uliozidi sana ugumu wa kuishi jangwani alipokuwa akihubiri. Pia hali ya kutokujua na kutokuona matendo ya Yesu ilimsumbua. Kwa kuwa alikuwa amembatiza Yesu na kumtangaza kuwa "yule ajaye" akiamini ni Masihi, bila shaka angalipenda kujua vizuri zaidi jinsi Yesu alivyokuwa akifanya na kufundisha, lakini ilibaki asikie kidogo kidogo tu, kwa hiyo ilikuwa vigumu apate picha kamili ili aweza kuamua vema juu yake. Alikuwa mwanadamu mwenye kusikia hali ya mashaka na kukata tamaa, huenda alijiuliza kama Yesu ni

Masihi mbona amemwacha gerezani n.k. Hivyo Yohana aliamua kutuma wanafunzi kadha kumwendea Yesu na kumwuliza moja kwa moja juu ya Umasihi wake.

k.2-3: Swali lake lilikuwa "wewe ndiye yule ajaye au tumtazamie mwingine?" Mashaka yake yaonekana wazi, Je, Yesu ndiye Masihi au yuko mwingine? Inaonekana matendo ya Yesu hayakutoboa wazi kwa Yohana Umasihi wa Yesu. Yohana alipombatiza alimkiri Yesu kuwa mkuu kuliko yeye 3:14-15 pia aliwashuhudia watu waliomwendea kwamba Yesu anayo nguvu kuliko yeye, naye atafanya hukumu "atabatiza kwa Roho na kwa moto" pia pepeto li mkononi mwake - atausafisha sana uwanda wake" 3:11-12. Mashaka ya Yohana yalihusu matazamio yake juu ya "matendo ya Yesu". Yesu haonekani kama mfalme waliomtazamia yeye na watu. Ni mpole si mkali, mbona hajisukumi, mbona Mfalme Herode na Herodia "mkewe" wangali hai wakiendelea na maovu yao? Yohana alipotafakari hayo yote ilimbidi atume watu kumwuliza Yesu swali hilo.

k.4-5: Yesu hakuudhika na swali la Yohana, bila shaka alimhurumia na kujiweka mahali pake na kufahamu sababu za swali lake. Yesu alitoa jibu rahisi, alimwelekeza katika "matendo yake", matendo ya huruma si ya hukumu, kuwahubiri maskini na kuwashughulikia wanyonge. Upole wake ulidhihirika na huruma zake, na hayo yote ni matimizo ya Maandiko kuhusu Masihi
Is. 61:1-2; 35:5ku. 29:18. Luka 4:18. Kweli watu wapaswa kuyatazamia matendo kama hayo.

k.6. "heri awaye yote asiyechukizwa nami" Yesu alifahamu kwamba huduma yake ya kuwashughulikia wanyonge, kuwaponya wagonjwa, kuwakaribisha wenye dhambi, kushirikiana na wasiopendwa na walio "nje" haiwapendezi wakuu, wala kuridhisha wale waliotazamia Masihi wa kuipindua serikali.

Mara nyingi mashaka yalizuka kuhusu mafundisho yake juu ya Wamataifa kupokelewa na Wayahudi kuwekwa nje ya Ufalme wa Mungu. Bila utambuzi wa kiroho ilikuwa vigumu kuwahakikishia wengine juu ya ukweli wa Umasihi wake. Ni baraka ikiwa watatambua wapaswa kuamini iwapo ufalme haujaja bado kwa ukamilifu, na hukumu atakayofanya ni ya baadaye.

k. 7-15: Wanafunzi wa Yohana walipoondoka Yesu alizungumza habari za Yohana na makutano wa watu waliokuwepo akionyesha umaana wake na mahali pake katika mpango na makusudi ya Mungu.

Alianza kwa kuwakumbusha kwa nini wengi walikwenda jangwani kumwona, maana alipotokea watu walishtuka sana, kila mahali habari zake zilienea, na watu walikuwa katika hali ya msisimko wakitazamia yatakayotokea.

Hawakumwendea kwa sababu alikuwa mnyonge, mtu asiye na msimamo, (nyasi iliyotikiswa), la, hata kidogo; walimwendea kwa sababu alikuwa imara, mwenye nguvu, asiyejali mtu yeyote hata wakuu. Je! walimwendea eti, alivaa mavazi mororo? la, hata kidogo; kinyume chake alivaa mavazi magumu ya nabii 3:4.

Alikuwa tofauti sana na wakuu, mtu asiyejali mawazo ya watu.

Kweli watu walimwaza kuwa nabii katika mfuatano wa manabii wa kale, na wa kwanza kutokea tangu Malaki aliyeishi miaka mia nne kabla yake.

k.9-10: Lakini haitoshi wamkubali kuwa nabii, na mkuu katika manabii wote, na wa mwisho, maana waliomtangulia walitabiri habari za Masihi kwa mbali, ila yeye alihubiri habari zake hali akimwona kwa macho yake mwenyewe. Tena haitoshi wamwaze kuwa nabii mkuu kuliko wote. Yohana alikuwa zaidi - alikuwa "mjumbe" wa Masihi aliyetajwa na Malaki Mal.3:1 atakayetayarisha njia ya Kuja kwa Mungu kwa kuhukumu. k.10 Yesu alibadili maneno ya Malaki, badala ya "uso wangu" ni "uso wako" na "njia yangu" alibadili kuwa "njia yako" Kumbe Yesu anadokeza kwamba kwa Kuja Kwake Mungu amekuja.

k.11: Kwa hiyo kutokana na mahali pake katika mpango wa Mungu kuleta Ufalme wake kwa njia ya Yesu, Yohana Mbatizaji alikuwa na heshima ya hali ya juu, wala hakuna mwingine aliyempita. Ila Kuja kwa Masihi katika makusudi ya Mungu ni kuleta hali mpya, dahari mpya, na Yohana ni mjumbe tu, mtangulizi wa kutangaza habari zake, ila hayumo katika Ufalme huo, atakufa kabla hajapata kuzishiriki baraka zake.

Siyo kusema kwa kuhusu wokovu wake kibinafsi ataukosa, la, kama mababa na watumishi wa Mungu wa zamani ataushiriki pamoja na akina Abramu, Musa, Amosi, n.k. Ila aliye mdogo katika Ufalme wa Yesu ni mkuu kuliko Yohana kwa vile Agano Jipya ni bora, ahadi zake na baraka zake ni nzuri zaidi 13:16. Ukuu wa Yohana ulitokana na mpango wa Mungu wa kuleta Ufalme wake, si ukuu kibinafsi au kimaisha.

k.12. Ni vigumu kuelewa maana ya kifungu hicho kwa sababu chasema juu ya ufalme wa Mungu "kupatikana kwa nguvu" na "wenye nguvu kuuteka". Huenda maneno hayo ya Yesu yahusu jinsi Kuja kwa Ufalme katika Yeye kumesababisha watu kuitika kwa utofauti. Iwapo baadhi wamemkubali wako wengi waliompinga kwa nguvu, nao wazidi kumpinga. Hao mara nyingi hujitahidi kuwazuia watu wasimfuate Kristo. 9:11. Vilevile kanuni za Ufalme siyo rahisi 8:20;, hivyo mtu lazima ajitahidi ili apate kuingia, apaswa kukata shauri bila kusita-sita Luka 13:24, 16:16, awe tayari kwenda kinyume cha jamaa 10:34ku. Kwa kukazana mtu ataupata.

Huenda maana nyingine ni kwamba ufalme unaingia kwa nguvu, Yesu ameushambulia ufalme wa Shetani kwa kutoa pepo, na kuponya watu, na kusamehe dhambi. Madai yake makubwa na uwezo wake umeoonekana katika miujiza. Ametikisa misingi ya Wayahudi na imani yao, divai mpya huhitaji viriba vipya!

k.14-15: Wakati wa Yesu wengi walitazamia Eliya atarudi 16:14; 17:11-14, 27:47. Yesu hakusema Eliya mwenyewe amerudi ila ya kuwa Yohana Mbatizaji ni mfano wa Eliya aliyehesabiwa nabii mkuu. Malaki alitabiri Mal. 4:5-6 ya kuwa Eliya atarudi na Yesu alithibitisha unabii huo kuwa umetimizwa na Yohana

Mbatizaji Luka 1:17 Yoh.1:21. Watu wapaswa kuwa na utambuzi wa kiroho ili wayatambue hayo yote, na wawe tayari kukubali.

k.16-19: Yesu aliwakemea watu kwa sababu hawakuwa tayari kuwapokea waliotumwa na Mungu, yaani Yohana na Yeye. Hawakujali ujumbe wao, hawakuwa tayari kusikiliza neno ambalo Mungu alitaka walisikie. Yesu aliwafananisha watu wa "kizazi hiki" na watoto waliocheza michezo mbalimbali. Baadhi walipenda michezo ya furaha, kama arusi, huku wengine walipenda michezo ya huzuni kama mazishi. "kizazi hiki" ni wale waliomsikia Yohana Mbatizaji, na baadaye walijaliwa kumsikia Masihi Mwenyewe, yaani Yesu.
Yohana alikuwa mtu mzito, aliishi maisha magumu ya porini, mbali na watu, si mtu wa kucheka-cheka; na ujumbe wake vilevile ulikuwa wa toba, wa kuita watu watengeneze maisha yao kwelikweli, na aliwaonya juu ya hukumu kali ya Mungu. Wengi walimwendea ila baadaye walipoa na kufikiri ana pepo.

Yesu alikuja, alijaa huruma, wanyonge walitiwa moyo, wagonjwa waliponywa, wenye pepo waliondolewa mapepo, watu wa kawaida walihubiriwa habari za upendo wa Mungu - kweli ilikuwa kama "arusi" watu wakijaa furaha 9:10-13; ila baadhi walimwona ni mtu mlegevu, rafiki wa wasio na sifa nzuri, mtu asiyefunga, asiyejali sabato n.k.

Ajabu ni kwamba watu hawakuridhika na mtu mzito wala na mtu mwepesi, mtu aliyewaonya juu ya hukumu ya Mungu na mtu aliyekaza rehema za Mungu. Hayo yote yaonyesha ya kuwa hamna ya kuwaridhisha. Huduma zote mbili, ya Yohana na ya Yesu, zilikuwa na maana katika makusudi ya Mungu, na maitikio ya watu kwa huduma hizo hayatazuia mapenzi ya Mungu yasitendeke. "Kizazi hiki" walijaliwa kuona Matendo makuu ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, iliwapasa waitike vema, lakini wengi wamekosa kuelewa. "hekima imejulikana kuwa ina haki kwa kazi yake" Yohana Mbatizaji na Yesu wamedhihirishwa kuwa walifanya iliyo sawa na watu wema watatambua hivyo. Iwapo huduma zao zilitofautiana hazikupishana.

ii **Miji iliyomkataa Yesu** 11:20-24. Yesu aliendelea kwa kuikemea miji na vijiji vya Galilaya, mahali pa huduma yake, mahali alipofanya miujiza aina aina, mahali alipofundisha makutano makubwa ya watu. Miji iliyojaliwa kuona maajabu mengi, yasiyotendeka kamwe hapo nyuma. Itikio lao limekuwaje? Wengi hawakutubu, iwapo ni itikio lililotakiwa, maana shabaha ya matendo hayo ilikuwa kuleta watu kwenye toba ili wasamehewe dhambi zao na kuletwa kwenye uhusiano mwema na Mungu.

Yesu aliwakemea kwa sikitiko na kwa huruma, si kwa kulipiza kisasi. Korazini - Bethsaida. Korazini ilikuwa maili kama tatu kutoka Kapernaumu, na Bethsaida maili chache magharibi yake. Hatuna habari ya miujiza iliyofanyika Korazini dalili ya kuwa waandishi wa Injili walichagua michache kati ya miujiza mingi aliyoifanya Yesu.

Yesu alipambanisha miji hiyo na miji ya zamani ya kipagani, ya Tiro na Sidoni, iliyojulikana kwa uovu uliofanyika ndani yake. Miji iliyokemewa na manabii

Is.23; Ez.26-28; Am. 1:9-10 Yesu alisema kwamba kama hiyo miji ingalijaliwa kuona miujiza yake watu wangalitubu kwelikweli.

k.23. Halafu Yesu alikemea mji wa Kapernaumu, mahali pa kikao chake 9:1. alipofanya miujiza mingi. Wenyeji walikuwa na kiburi kingi, watu walijiona wako salama katika maendeleo na mafanikio yao, hawakuhitaji kitu kingine. Yesu alitabiri kwamba kuinuka kwao kutafuatwa na kuanguka kwao, anguko kubwa la hukumu ya Mungu. Sodoma ilijulikana kwa uovu wake na kwa kuukataa ujumbe wa Mungu Mw.19:1-29; Math.10:15. Adhabu ya miji hiyo ya zamani itakuwa ndogo kulingana na adhabu ya miji ya Galilaya, wamejaliwa kuona makuu nao wapaswa kuitika vema, wala hawakujali Luka 12:47-48.

Neno ambalo haliwezi kusameheka ni la kukataa "msamaha wa Yesu" Yohana Mbatizaji alisema Masihi atafanya hukumu, ila wakati huo Yesu hakutekeleza hukumu ila aliwaonya itakuja.

iii. **Itikio la kweli kwa wito wa Yesu** 11:25-30: Siku za Yesu kupendwa na watu na watu kumfuata kila mahali zilianza kupita. Wengi hawakutubu na wakuu walizidi kumpinga. Alionaje hali hiyo? Je! ataudhika na kukata tamaa? k.25: Yesu alijibu hali hiyo kwa kumshukuru Baba yake na kujitia kwa moyo chini ya mapenzi yake. Baba ni juu ya mbingu na nchi naye amemkabidhi yote k.27: 28:18.

Baba ndiye asili ya wale wengi kukosa kumtambua "Baba amewaficha" hawawezi kufahamu bila kufunuliwa: na hawatafunuliwa wasiponyenyekea na kuwa kama "watoto wachanga" 18:3 walio tayari kujifunza. Shida yao ni kujiona kuwa wanafahamu Is.29:14, I Kor. 1:18ku. Mambo ya Mungu hayaeleweki kama mambo ya dunia, ufahamu wa kiroho hautegemei akili na uwezo wa kibinadamu I Kor.2:6-16. Hasa Yesu alimshukuru Mungu kwa wale "wachanga" waliomwamini, na kuitika wito wake na kumfuata, ila ni wachache waliotoka kwa wakuu. 16:17, Mdo.16:14, 25b. Mungu ndiye mwenye madaraka ya kuwafunulia watu. Yeye huwaficha wengine na kuwafunulia wengine kufuatana na mapenzi yake.

k.26 "Naam Baba ndivyo ilivyopendeza mbele zako" Yesu hakusikia shida yo yote, iwapo bila shaka hakufurahi kuona watu wakikataa wito wake. Yu radhi na mapenzi ya Baba.

k.27. Uhusiano kati ya Baba na Mwana ni wa kipekee - wao hufahamiana kikamilifu, hamna siri kati yao, Baba amemkabidhi Yesu "vyote" yaani ufahamu wote wa kweli. "Hakuna amjuaye Mwana ila Baba wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana" kujua ni "ushirikiano wa kibinafsi" si ujuzi tu.

Yoh.17:3 Ushirikiano wao wa kipekee ni wao kwa wao. Kamwe mwingine hana haki kuushiriki. Si jambo la kawaida kwa wanadamu. "na ye yote ambaye Bwana apenda kumfunulia" Ila wako wenye kuchaguliwa na Mwana, mwenye kujaliwa, ndio hao ambao watausiriki kwa mapenzi ya Baba na Mwana I

Ilimpendeza Baba kwamba Mwana awe juu ya yote na kuwa njia pekee ya watu kumwendea Yoh. I:18; 14:6. Hakuna mwingine awezaye kumfunua Baba. Katika Injili hiyo Mathayo amekaza Yesu kuwa Mwana wa Mungu; 2:15, 3:17; 4:3,6; 8:29; 14:33; 6:16-17; 17:5; 21:37.

k.28-29: Yesu aliwaita "wote" waliosumbuka na kulemewa na mzigo Kuja Kwake Is.55:1-3. Wako chini ya Nira ya Torati. Mafarisayo na waandishi walikuwa wamezidisha uzito wa Torati kwa kudai watu washikilie kila neno na vilevile wayashikilie mapokeo yao mengi mengi na madogomadogo, kiasi cha kuwalemea watu sana 23:2-4 "nitawapumzisha" wakija Kwake watasikia nafuu, watawekwa uhuru mbali na madai mazito. Badala ya nira ya Torati watapewa Nira yake laini. Kweli madai yake huzidi ya Torati, kama tulivyoona katika sura za 5-7: ila tofauti ipo katika nira hizo kwa sababu ya tabia yake. Ni nira "yake" wakiunganika naye Yeye atakuwa pamoja nao, njia ni nyepesi, badala ya sheria zilizoandikwa ni Yeye Binafsi, Yeye aliye mpole, mnyenyekevu, asiyevunja mwanzi uliopondeka Is.42:2-3; 53:1-2; Zek.9:9. Madai yake ni makubwa ila kwa sababu ya Yeye Mwenyewe na tabia yake watasikia raha nafsini mwao badala ya masumbufu na kulemewa.

"Jifunze kwangu" nira ilifunga ngombe wawili pamoja ili wavute plau kwa pamoja. Vilevile mtu akienda pamoja na Bwana Yesu atasikia msaada mkubwa. Hasa iliyotakiwa si utii kwa sheria bali ni utiifu kwa Yesu binafsi. Ni rahisi zaidi kufanya kama atakavyo mtu kuliko kutii "andiko" la sheria lililo baridi, halina "nafsi" Nira ipo, mzigo upo, ila ni ya tofauti sana. Ni njia mpya ya kumtumikia Mungu katika uhusiano mwema na Yeye.
Kweli Yesu aliendelea kudai makubwa.

*MASWALI:*

*Yesu alipowachagua Mitume 12 alikuwa na shabaha gani? Wafikiri walipewa "cheo" au hasa mkazo ulikuwa huduma na kazi? Unaonaje! Kanisa limepata shida kwa sababu ya kuweka kama "vyeo" k.m. lina maaskofu, mapasta, wainjilisti, maruraldean, maarchdeakoni, n.k. Si afadhali ziwepo huduma mbalimbali bila majina hayo yote ya "vyeo"? Toa mawazo. Taz. 1 Tim.3:1 "mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema" - mkazo ni kazi au cheo!!*

*Math: 11:28: Wito wa Yesu wa Kumjia unadhihirisha utofauti mkubwa kati ya dini ya Kikristo na dini zingine; Utofauti gani hasa?*

iv. **Yesu kupingwa juu ya Sabato:** 12:1-14; (Mk.2:23-28 na Luka 6:1-5)

12:1-8: Kuvunja masuke: Kumb. 23:25 iliruhusu watu kuvunja masuke. Mafarisayo walifundisha katika mapokeo yao kwamba ni "kazi" na kwa sababu hiyo atakayefanya atakuwa amevunja amri ya sabato "usifanye kazi" - walikuwa wameongeza "amri" kwa kutoa visheria vingi vingi, vidogo vidogo, kutokana na ufafanuzi wao. Nira ya Torati ilizidishiwa uzito kwa njia hiyo hasa juu ya Sabato.

Wayahudi walitumaini Sabato kuwa baraka na furaha, ushuhuda wa uumbaji wa Mungu, na uhusiano wao na Mungu kwa njia ya Agano lake, na ishara ya furaha za baadaye. Ila waandishi na Mafarisayo kwa ufafanuzi wao wa sheria na kwa kuyaweka mapokeo yao kuwa sawa na Torati yenyewe wamegeuza sabato kuwa "mzigo" kuliko baraka. Badala ya mtu binafsi aamue ni ipi iliyo "kazi" hao viongozi waliwaambia na kuwatisha!

k1. "wanafunzi wakaona njaa" hawakuvunja masuke ili wachokoze wakuu na kugombana nao. la! ila kwa kuwa walisikia njaa. k.2. Yesu aliwatetea akiyajibu mashtaka ya Mafarisayo. Neno la kwanza, aliwakumbusha jinsi Mfalme Daudi alivyofanya (I Sam.21:1-6) wakati yeye na watu wake waliposikia njaa. Alifanya isivyoruhusiwa. Iwapo walifahamu habari hiyo wameshindwa kuelewa maana yake kiroho "hamkusoma" Haja ya wanadamu hupita madai madogo madogo ya sheria.

k.5. Halafu makuhani katika huduma yao kila wakati huvunja sabato, kwa hiyo ni wazi kwamba Mungu hakukusudia watu wafungwe kama kwa minyororo na visheria vidogo vidogo vingi vingi, alipotoa amri juu ya sabato.

k.6. Ndipo Yesu alisema kwa mamlaka ya Ki-Masihi kwamba Yeye ni mkuu kuliko hekalu - watu waliamini "Mungu" yumo katika hekalu, ni mahali pa Kuwemo Kwake ki-pekee. Yesu ni Mungu aliyefanyika mwili, Mungu yumo katika Kristo zaidi ya Alivyo ndani ya Hekalu. Sheria za hekalu juu ya utendaji wa ibada na dhabihu zilimlenga Kristo, nazo zimefikia mwisho wao na matimizo yao katika Kristo, kwa kifupi hekalu halina kazi kama hapo nyuma Rumi 10:4 Gal. 3:24.

Yesu alisema wanafunzi wake hawakuwa na hatia. Yeye anayo mamlaka ya kutafsiri maana ya torati na jinsi ya kuishika, si ya kuiondoa. Jinsi hiyo ni tofauti sana na ya Mafarisayo na waandishi. Njia ya Yesu ilitikisa mapokeo yao k.7: Jambo moja kubwa ni "rehema" kama Hosea alivyosema Hos.6:6. Mungu ni mwenye rehema na hupenda rehema iongoze maisha ya watu, rehema inatangulia hata mambo ya ibada na kutoa dhabihu. Dhabihu nyingi hazitoshi kama rehema imekosekana.

k.8: Bwana Yesu alidai makubwa - Yeye ni Bwana wa Sabato, aweza kuamua juu yake. Ikiwa Daudi alikuwa na "haki" ya kuvunja sheria si zaidi Yeye aliye Mwana wake, Masihi?

12:9-14: Kumponya mtu mwenye mkono uliopooza: (Mk.3:1-6 na Luka 6:6-11). Habari hii ni ya pili katika Yesu kugongana na Mafarisayo. Utengano kati yao unazidi. Yesu aliruhusu kazi ya lazima itendeke siku ya sabato na katika habari hiyo aliruhusu kazi ya huruma itendeke siku ya sabato. Inaonekana kwa maneno ya Luka 6:7 Mafarisayo wamepanga jambo hilo litokee kwa kusudi la kumvizia Yesu na kuona atafanyaje.

k.9 "akaingia sinagogi lao". Neno "lao" huenda ni dalili ya utengano unaozidi. Swali lao "Je! ni halali kuponya watu siku ya Sabato?" ni kama kumpima Yesu.

Yesu alipojibu hakutumia mamlaka yake, wala Maandiko, ila aliwatazamisha katika kawaida yao ya kutenda.

Kuhusu wagonjwa walifundisha kwamba mgonjwa asishughulikiwe isipokuwa yu katika hali ya kufa. Kwa mali yao walifanya tofauti. Wengine walifundisha kwamba mnyama asishughulikiwe kama ni kufa, basi na afe. Ila wengine walisema kitu fulani chaweza kushushwa shimoni ili mnyama asaidiwe kutoka, pia aweza kulishwa hadi kesho yake. Wengine walitoa tu wakisema hali ni mbaya iwapo siyo. Kumbe waliruhusu sheria ziachwe kwa ajili ya mali yao ila kwa wanadamu siyo! Yesu alijua hakika jinsi walivyofanya, hawataweza kujitetea - taz. k.11 "ni mtu yupi miongoni mwenu .... ?" kwa kuwa mtu alikuwa ni mmoja tu, kwa ajili ya mmoja tu yu tayari kuvunja torati.

Kwa kweli yule mgonjwa wa kupooza mkono asingalikufa siku ile, angaliweza kushughulikiwa kesho yake, ila Yesu aliona kumwacha kwa siku moja ni kukosa huruma. Kwake :Yesu ni "halali kufanya mema siku ya Sabato" k.12. Yesu alikasirika alipoona hali ya "ugumu wa mioyo yao "Mk.3:5 na jinsi walivyothamani mnyama kuliko wanadamu. Yesu aliwathamini wanadamu sana 6:26, 10:31. k.13 ndipo Yesu alimponya yule mtu.

k.14. Itikio la Mafarisayo ni kufanya shauri la kumwangamiza. Tofauti zao na Yesu hazitengenezeki, hawawi tayari kumpokea kuwa Masihi wao, na badala yake wataendelea na shughuli zao za kuzidisha mapokeo yao na kuuzidisha uzito wa mzigo kwa watu na kufanya nira ya Torati kuwa ngumu zaidi.
Marko alisema Maherode walijiunga na Mafarisayo katika shauri la kumwangamiza Yesu, watu wa siasa wakijiunga na Mafarisayo watu wa dini, kwa kawaida hawakupendana.

v. **Itikio la Yesu kwa upinzani huo:** 12:15-21.
Yesu alifahamu Mafarisayo wameondoka hali wakitaka kufanya mpango wa kumwondoa. Yesu hakutaka kuwachokoza zaidi, iwapo alijua wengi watamtetea. Kwa hiyo aliondoka pale alipokuwapo nao wengi walimfuata, akawaponya wote waliokuwa wagonjwa. Ila aliwakataza wasiseme lolote ili awe na uhuru wa kuendelea na huduma mpaka atakapotimiza yote yaliyotakiwa.

Ndipo Mathayo alitumia Maandiko kuonyesha jinsi hayo yote yalivyolingana na picha ya "Mtumishi" iliyotajwa na Isaya, Is.42:1-4. Wapinzani watatumia nguvu ili wamwondoe, ila Mtumishi wa Mungu atadumu kuwa mpole na mnyenyekevu. Mathayo alikaza tabia ya Mponyaji kuliko uponyaji alioufanya Amekwisha kuonyesha uponyaji wa aina mbalimbali. Sura 8 - 9.

k.18: Maneno hayo yatukumbusha ubatizo wake wakati alipokubali wito wa KiMasihi wa kuwa Mtumishi atakayeteswa, na kupewa Roho ili autimize huo wito. Ndipo alianza huduma kwa wanyonge na wasio na sauti, waliokosa haki zao. n.k.

k.19-20: Yesu hatatumia mabega, hataipindua serikali, bali ataonyesha huruma na upole "mwanzi uliopondeka" na "utambi utokao moshi" yaani kwa wanyonge

mpaka apate ushindi ndipo hao kwa ushindi wake watapatiwa haki zao. Ila huduma yake haitakamilika mpaka ameteswa. "atakuwa kimya" Is.53:7-8, hatatafuta ugomvi na wapinzani wake. Mungu atamfufua katika wafu na kumpa Jina lipitalo kila jina, ndipo ufalme wake utafunguliwa wazi na wanyonge wataingia.

vi. **Yesu kushtakiwa amefanya patano na Shetani na jibu lake** 12:22-37. (Mk.3:23-30 Luka 11:17-23 12:10 6:43-45)

22-24: Yesu alifanya mwujiza wa ajabu akimponya mtu mwenye pepo, kipofu na bubu. Inaonekana asili ya ugonjwa wake ni pepo. Watu walishangaa sana kiasi cha kujiuliza "huyu siye Mwana wa Daudi?" yaani Masihi. Ni kama mwujiza imewafanya wamwona Yesu ni Masihi ila mashaka ni kwamba haonekani kuwa na heshima za Kifalme.

k.24. Mafarisayo waliposikia maoni hayo walijitokeza mara na kutoa maoni yao ya tofauti. Hawakuweza kuukana ukweli wa tendo lenyewe, ila watajadili asili yake. Walisema Yesu amepatana na Shetani, amefanya kwa Beelzebuli, mkuu wa pepo! 10:25, 2 Waf. 1:2. mungu wa Ekron. Shetani na Beelzebuli ni mamoja 12:24,26. Yaani shtaka lao ni kwamba Shetani amemtuma Yesu kufanya kazi yake, na ndiyo sababu aweza kutoa pepo. Yesu alijibu kwa kutoa sababu nne za kuwapinga.

k.25-26: Ni upuuzi mkubwa kusema hivi, maana vita ya ndani ni hatari sana, na kwa kweli Shetani hawezi kujiangamiza. Shetani anao watumishi - mapepo wengi, anayo nyumba, anao ufalme. Yeye na walio wake wameunganika pamoja kwa kusudi la kumpinga Mungu. Haiwaziki kwamba wataachana na kufitinika wao kwa wao - upuuzi mtupu.

k.27. Yesu alionyesha unafiki wao (Mdo.19:13-16) Kwa nini wamlaumu Yeye huku wakiwasifu wa kwao wanaotoa pepo? Imekuwaje Yeye akifanya amefanya kwa Beelzebuli na hao wakifanya wamefanya kwa Mungu. Sharti waufuate uamuzi mmoja wa haki si wa upendeleo. Yawezekana wengine wali-toa pepo, ila si mara nyingi na bila shaka si kama Yesu alivyofanya, hasa kwa huyu kipofu na bubu, maana watu walishangaa sana kama hawajaona kitu cha namna hiyo. Wengine wamewaza maneno ya Yesu "Je wana wenu huwatoa kwa nani?" kuwa kama ubishi "wana wenu hawawezi kutoa pepo"

28-30: Yesu alionyesha asili ya mamlaka yake juu ya pepo. Kama si Shetani lazima ni Mungu. Hamna awezaye kumshinda Shetani ila Mungu. Katika huduma Yesu ameendelea kumshinda Shetani kwa miujiza yake, ameteka "vyombo vyake" na ni wazi Yeye anayo nguvu zaidi Is.49:24-26. Anazidi kumfunga, ila bado hajamfunga kabisa asiweze lo lote. Anazidi kumzuia hadi atakapoingia utawala wake wa mauti na kuwafungulia wateka wake Ebr.2:14ku.

k.28 "ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia" ufalme umeisha kuja katika Yesu, ila mpaka atakapokufa msalabani na kumponda kichwa Mw.3:15 na Kufufuka, uwezo wa ufalme hautakuwa dhahiri. Mungu anafanya kazi akionyesha madaraka yake juu ya uovu na mkuu wake.

k.30: 23-24: Shetani lengo lake ni kuwazuia watu wasimwamini Kristo. Adui ni Shetani, si serikali ya Rumi. Miujiza ni utangulizi wa tendo kuu la Ukombozi kutoka utumwa wa dhambi na Shetani. Zamani mapigo kwa Wamisri yalitangulia ukombozi wao kutoka utumwa wa Misri.

Katika mashindano hayo mtu hana budi achague upande wake, hawezi kukaa kati, asiye upande wa Yesu humsaidia Shetani.

k.31-32 Yesu alitoa onyo kali juu ya dhambi isiyosameheka. Ni nini dhambi hiyo? Ni kuzidi kuukana ukweli ulio dhahiri na kuita lililo jema kuwa "uovu" na kinyume chake kuuita uovu kuwa "jema". Is.5:20. Ndivyo Mafarisayo walivyofanya waliposema Yesu ametoa pepo kwa Beelzebuli, walionyesha kwamba wamekwisha kuamua kumpinga Mungu na Kazi yake, wamefanya mioyo yao kuwa migumu. Kwa hiyo potelea mbali Yesu afanye nini, hawamtaki, basi. Wamekaidi mpaka wamepotoka kabisa. Yoh.3:19 Wamejiweka katika hali isiyo na msamaha.

Kama mtu hatatubu atawezaje kusamehewa?" Kama dhambi yake siyo dhambi kwake ataitubuje?" Kama mtu ni kipofu kwa sababu ya ukaidi wake atawezaje kuona vizuri lipi ni jema na lipi ni baya?". Ni Mungu peke yake awezaye

kutambua wakati ambapo mtu amefikia hatua ya mwisho katika kukaidi imfanyayo asiweze kuacha upinzani wake.

k.32 Petro alinena neno juu ya Yesu 16:23 na kumkana baadaye kwa kuwa hakuutambua udhaifu wake, ila moyoni mwa ndani alimpenda Yesu. Yuda alikuwa ameendelea kwa muda sirini kumpinga Yesu na hakudhihirika wazi mpaka baadaye Yoh.12:6.

Aliye na mashaka kuwa amemkufuru Roho Mtakatifu ni dalili ya kuwa hajafanya maana kuwa na mashaka inaonyesha kwamba yu tayari kujihoji wala bado hajakaza nia yake.

Kwa nini yasema ni "kumkufuru Roho"? Ni kwa sababu ni kazi ya Roho kutuleta kwenye toba, akifanya kazi mioyoni mwetu.

k.33-35: Kwa nini Mafarisayo wampinge Yesu? Kwa sababu ni "wazao wa nyoka" 3:7 23:33 Yoh.8:47. Lazima mti uwe mzuri ndipo matunda yatakuwa mazuri. Mafarisayo walijaribu kufanya matunda kuwa mazuri bila kuuangalia mti. Waliposema "amefanya kwa Beelzebuli" si kosa dogo la kusema kwa haraka, bila tahadhari, la! Ni ufunuo wa hali halisi ndani yao. Itakuwa vigumu wabadilike, maana badiliko lililohitajika ni kubwa kabisa la ndani, la kuzaliwa upya Yoh.3:3. Maneno yao mabaya yalitokana na tabia yao mbovu.

k.36-37: Yesu aliendelea kuonyesha uhusiano kati ya maneno ya mtu na tabia ya ndani. Maneno hufunua jinsi alivyo mtu kwa ndani, kwa hiyo maneno yake yatahukumiwa. Mara nyingi "neno lisilo la maana" neno dogo mtu asemalo bila kufikiri humfunulia alivyo. Maneno ya Mafarisayo kumhusu Yesu yatasababisha hukumu yao.

vii: **Hukumu ya Yesu kwa kizazi hiki:** 12:38-45.
Miujiza mingi aliyoifanya Yesu haikutosha kuwaridhisha wakuu, walitaka "ishara ya kutoka juu" 16:1 Luka 11:16 yaani ishara isiyoanzia Kwake Yesu, ishara isiyoelezeki. Yesu alikataa kuwapa ila alisema watapewa moja baadaye Baba atakapomfufua kutoka kwa wafu, wala hawataiamini Luka 16:31.

Kwa nini wasipewe? kwa sababu ni kizazi kibaya na cha zinaa hawakuwa waaminifu kwa Mungu, wamemwasi Yak.4:4 Mathayo ametumia maneno "kizazi hiki" mara nyingi 11:16-19, 16:4, 17:17, 23:29-36, 24:34.

Nabii Yona aliokolewa na hatari ya mauti, Yesu ataokolewa na mauti yenyewe. Kuokolewa kwa Yona kulikuwa ishara ya yeye kutumwa na Mungu, na alipowahubiri Waninawi walio wapagani habari za toba, walitubu kuanzia kwa Mfalme hata na wenyeji wote Yoh.3:2-10. Yesu amefanya makubwa kupita Yona kwa mahubiri na mafundisho na kwa miujiza mingi, na Waisraeli wateule wa Mungu hawatubu.

"siku tatu usiku na mchana" Yesu hakukaa kaburini kwa siku tatu nzima, ni "msemo" wa Wayahudi waliohesabu hata masaa machache ya siku kuwa siku nzima.

Malkia wa kusini alisafiri mbali sana aliposikia habari za Mfalme Sulemani na hekima yake I Waf.10: 1-10.

Si kwamba Waninawi walitubu na wa kizazi hiki hawatubu, kosa hasa ni kumkataa Masihi Mwenyewe aliye mkuu kuliko nabii Yona na Malkia wa kusini. Ukuu wake ni ameuleta Ufalme wa Mungu ambao hao wote waliutazamia. Itikio la Waninawi na Malkia litakuwa ushuhuda wakati wa kuwahukumu wa "kizazi hiki".

Katika habari hiyo Mathayo amepambanua tena kati ya Wayahudi wasioamini na wapagani walioamini.

12:43-45: Katika mfano huo Yesu alisema juu ya hatari ya mtu au taifa kujitengeneza au kutubu nusunusu. Wengi walimwamini Yohana Mbatizaji, walibatizwa ubatizo wa toba. Yesu akaja na wengi walisaidiwa kwa kutolewa pepo na kuponywa. Lakini wasipojitoa kikamilifu Kwake na kumpokea, hali yao ya mwisho itakuwa mbaya kuliko ya kwanza kabla kuja kwa Yohana na Yeye.

Katika kuomba ishara wameonyesha toba lao kuwa si la kweli. Wasipompa Yeye utiifu wao Shetani atauchukua.

k.43 Jangwani ilidhaniwa kuwa mahali palipopendwa na mapepo. Mtu aliyetolewa pepo, au aliyetubu kwa kuacha ubaya fulani, apaswa kujaza lile pengo kwa kumpokea Yesu na Roho Mtakatifu. Kuitikia wito wa Yohana Mbatizaji na kutubu bila kuendelea kwa kumpokea Yesu ni bure, tena ni hatari.
viii: **Yesu na jamii yake ya kweli:** 12:46-50.

Mathayo ametupasha habari juu ya upinzani wa watu, hasa wa wakuu, hata hivyo walikuwapo wale waliompokea Yesu kwa dhati.

Hao Yesu aliwatambua kuwa ndugu zake wa kweli, watoto wa Baba yake, wa familia moja. Twakuwa karibu na Yesu kiroho si kimwili. Uhusiano tulio nao ni wa ukaribu kuliko ule wa ki-familia.

Mama na ndugu zake walikuwa wamesimama nje wakitaka kumwona. Hatujui jinsi walivyomwamini huenda bado hawajajitoa Kwake kikamilifu Yoh.7:5. Ndugu zake ni wale waliozaliwa baada ya Yesu kuzaliwa Mk.6:3. Wanafunzi ni wale walioyafanya mapenzi ya Baba yake, walikuwa na heshima kuu ya kuwa katika familia yake ya kiroho Yoh.1:11-13. Yesu alitafuta watu watakaouitika wito wa kufanya mapenzi ya Baba yake.

Kwa hiyo iwapo Yesu amekataliwa na wengi wa kizazi chake, Mathayo alifunga sehemu hiyo kwa kuonyesha Yesu hali amezungukwa na kundi la watu wateule walio jamaa yake kweli.

*MASWALI:*

*Katika sura hii twaona upinzani umezidi. Kwa nini wakuu walizidi kumpinga Yesu?*

*Je! katika Kanisa wivu upo? kama upo, unasababishwa na nini? Utafanyaje unaposikia uvumi wa mambo fulani juu ya mtumishi fulani? utaukubali mara kuwa kweli? utawaambia wengine kabla ya kuuhakikishia? au utafanya uchunguzi kwanza?*

*Kama utasikia watu wanaeneza habari fulani juu yako isiyo kweli utachukua hatua zipi?*

## MAFUNDISHO YA YESU KWA NJIA YA MIFANO 13:1-53

Maelezo machache kuhusu mifano Tukumbuke kwamba mara nyingi mfano ulilenga kufundisha jambo moja tu la maana au kujibu swali moja tu, kwa njia ya hadithi. K.m. Luka 10:29 swali liliulizwa na Yesu alilijibu kwa Mfano wa Msamaria Mwema. Katika mfano wa wakili mdhalimu ni busara yake iliyosifiwa si udhalimu wake.

Yesu alikuwa wa pekee kabisa kama mwalimu aliyefundisha kwa mifano. Hakukuwa mwingine aliyekuwa mstadi kama Yeye.
Mifano ya Bwana Yesu ilikuwa juu ya Ufalme wa Mungu uliokuja katika Yeye, kwa hiyo mifano huelezwa kwa kuihusianisha na Nafsi yake na Huduma yake. Tukitazama Luka 8:10 na Math.13:34 Yesu hakufundisha watu bila mifano. Hiyo mifano haikueleweka kwa urahisi, hata kwa wanafunzi Math.13:36 na 15:15, Mk.7:17-18 na Yoh.16:29. Yesu aliwaelezea wafuasi Math.13:10,11,36.

Katika sura za 11 na 12 tumeona upinzani ulizidi na watu waliachana katika maitikio yao. Yesu alipambanua kati ya ndugu zake wa kweli na ndugu zake wa kimwili 12:46-50. Halafu alianza kuwageukia wanafunzi wa kweli 13:11,16 na kuwaacha wengine 13:11,13, Yesu alifanya hivyo kwa kuitumia mifano na kuitafsiri kwa wanafunzi tu. Alikuwa na kusudi la kupambanua kati ya

wasikilizaji wa kweli "wana wa ufalme" (ngano) na wale wa nje (magugu). Alitaka kuvuta waliotatuta ufalme kwelikweli, walio na ufahamu wa kiroho, waliotiwa nuru na Roho Mtakatifu Math. 11:25ku. 16:1; ili hao wazidi katika ufahamu wao wa Ufalme 13:11,12 na 25:29.

Ufunuo wa kipekee ulitolewa na kuthibitishwa na miujiza n.k. hata hivyo wengi hawakuguswa wala kujali - kwa hiyo "siri" ipo na siri hiyo ni nini? (a) ufalme umekuja katika Yesu aliyeonekana mtu duni, asiye na maana, hata akasulubiwa. Yesu hakutenda kama Wayahudi walivyotazamia, alionekana mpole na mnyenyekevu. Kwa hiyo ilikuwa vigumu kwa watu kutambua ya kuwa katika Yesu ufalme ulikuwa "katikati yao".

(b) Siri ya ufalme ilihusu wokovu wa Wamataifa na kukataliwa kwa Wayahudi "wana wa ufalme". Yesu aliwaonya Wayahudi wasipomwamini na kumpokea kwamba watakataliwa Math.8:11-12 na Wamataifa watakaomwamini watapokelewa katika ufalme

**i. Mfano wa Mpanzi 13:1-9 na Tafsiri yake 18-23**: Mfano huo ulitolewa kwa mkutano hadharani, maana twasoma kwamba Yesu aliondoka nyumbani k.1. Iwapo tumezoea kuuita Mfano wa Mpanzi, hasa neno la kuangaliwa si mpanzi ila ni mbegu na hasa udongo. Wasikilizaji wote wasikia neno lile lile ila matokeo hutokana na udongo. Neno ambalo lasikiwa tu ni mateka rahisi kwa adui wa neno, yule Mwovu. Tena kulipokea kwa furaha bila kulitekeleza kimaisha halitadumu, mtu ataliacha mara apatapo shida na mateso. Wengine wangeweza kulipokea vizuri na kuzaa ila wameisha kushikwa na shughuli za dunia na kuvutwa na mali, hivyo hawawi tayari kulishikilia kama iwapasavyo, kwa hiyo hawazai. Ila wako walio tayari kulipokea kwa moyo na kwa dhati, ndio hao ambao huzaa matunda. Kwa hiyo mtu anayesikia Neno la Ufalme ametikishwa kwenye shauri kuu la maisha, na hukumu ya Mungu hufuata itikio lake. Ndivyo ilivyokuwa Yesu alipofika na kuleta ujumbe wa kuhusu Ufalme Wengine hawakutambua na kuelewa kwamba Yesu ameuleta Ufalme wa Mungu kati yao, wengine wako tayari kumfuata kwa muda ila ikitokea mateso kwa ajili yake watamwacha, na wengine kwa kutaka mambo ya dunia hiyo hawawi tayari kuacha vyote kwa ajili yake. Kwa kutokuelewa, na kwa kukosa kina, na kwa uvutano wa mengine, ujumbe haupokelewi. Nyuma ya hayo yote ni yule Mwovu. Ajabu ni kwamba hata hivyo wako walio tayari kujitoa kabisa na kumfuata. Mfano huo ndio kiini cha mifano yote Mko:4:13.

**ii. Shabaha ya mifano 13:10-17** Hapo twakuta kipengele kati ya Mfano wa Mpanzi na tafsiri lake. Kwa nini mifano itumiwe? Inaonekana ni tangu hapo katika huduma yake Yesu ameanza kuitumia kwa watu k.34. Kutokana na maneno ya Yesu inaonekana ni njia yake ya kuwaficha watu ukweli huku akiwafunulia wanafunzi wake - walio na "kitu wataongezewa" na wale wengine watanyimwa k. 11,12,16,17. Kufahamu Yesu ni Masihi, Mwana wa Mungu, ambaye ameuleta Ufalme wa Mungu ni kujua ·"siri" - kwa wengine mifano ni kama hadithi nzuri tu. Mifano ni njia nzuri katika kipindi hicho cha huduma ya Yesu, ni picha ya mambo yalivyo, kama ilivyokuwa wakati wa Nabii Isaya.

Yeyote aweza kusikia ila ni mwanafunzi wa kweli anayetambua na kuelewa. Faraja ni kwamba wako wanaofahamu na kuitika.

iii. **Mfano wa Ngano na Magugu:13:24-30 na 36-43**:

Wengi wamesumbuliwa na kuwepo kwa uovu ulimwenguni, nao wauliza, "mbona Mungu hauondoi?" "Je! ameshindwa kuuondoa?" Wayahudi waliwaza kwamba atakapotokea Masihi makubwa yatatokea. Masihi amefika na kumbe mambo kwa jumla yaendelee kama kawaida. Yesu licha ya kuwahukumu watoza ushuru na wenye dhambi huwakaribisha, na badala ya kuwaangamiza WaMataifa huonyesha utayari wa kuwapokea.

24-28a. Bwana hawezi kulaumiwa kwa sababu ya magugu yaliyomo kondeni mwake, ila kwa nini ayaachie yakue?

Jibu la Bwana lina sehemu mbili: (a) ni vigumu kupambanua kati ya ngano na magugu mpaka yote imeiva, kwa hiyo wakati wa kubagua haujaja bado, maana yake wana wa ufalme na wana wa yule Mwovu hawatambulikani vizuri wakati huo (b) siku ya mwisho ni Kristo Mwenyewe atakayepambua bila makosa. Ameitwa Mwana wa Adamu, Yeye anayo mamlaka ya kutoa hukumu kwa kuwa alikuwa mwanadamu kweli, ameelewa vema hali yetu, ila amri yake ni ya ki-Mungu.

k.38b. Mfano huhusika na hali ya ulimwengu si ya Kanisa, ni juu ya wema na waovu waliomo ulimwenguni.

Mwovu na enzi za uovu zajitahidi kuuzuia Ufalme wa Mungu, lakini mwishoni jitahada zao zote zitakuwa bure, ila mpaka huo mwisho zaruhusiwa kufanya upinzani wao.

Kwa mfano huo Yesu alionyesha kwamba wafuasi wake watahitaji subira na kuwa na uhakika wa ushindi wa Mungu na ufalme wake kutimilika. Kutenganisha si kazi yao, Mungu atakufanya siku ya mwisho, utengano utakaowafanya wasio wa kweli kutaabika mno na wa kweli kufurahi furaha kubwa na kung'aa kama jua.

iv. **Punje ya haradali na chachu: 13:31-33**:

Watu walizoea kutumia mithali au usemi kama "punje ya haradali" walipotaka kuelezea kitu kilicho kidogo sana. Punje ya haradali ilikuwa ndogo sana, ila siyo ndogo kuliko zote. Ilikua mpaka kama futi tatu, si mti hasa bali ni kama kijiti. Mfano huo unahusu jinsi Ufalme wa Mungu hukuavyo na kuenea ulimwenguni, watu wa aina zote na hali zote wakiuingia na kuokoka. Ila jambo kubwa si ukuaji wake bali ule utofauti kati ya unyonge wa chanzo chake kidogo (yaani Yesu kuzaliwa bila fahari, dhiki na shida za maisha yake, kifo chake cha aibu, wanafunzi wake wanyonge - wavuvi ambao hawakusoma katika shule za marabi, na neno lao la upuzi I Kor. 1:18 n.k.) na ukubwa wa hali yake ya mwisho (utakaotokea kotekote ulimwenguni). Kwa hiyo wana wa ufalme wasikate tamaa, maana Injili ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, ni ufalme utakaoshinda kabisa mwisho wa dahari.

"ndege katika matawi" ishara ya Wamataifa kupokelewa na kuwa salama ndani ya ufalme huo.

Ndiyo siri ya ufalme, ufalme utakua sana iwapo kwa wakati ule chanzo chake hakitumainisha ndivyo itakavyokuwa.

13:33: Chachu: Mfano huu pia wahusu kukua kwa Ufalme toka chanzo kidogo mpaka mwisho wa ajabu. Ila ukuaji ni wa ndani. Chachu inayowekwa katika unga ni kidogo lakini huchachisha donge zima, ikikolea kila sehemu. Katika Biblia "chachu" imetumiwa kama ishara ya uovu, lakini sivyo ilivyo hapa. Neno kubwa ni chachu huchachisha donge zima. "akaisitiri" ni mkazo jinsi chachu hufanya kazi kwa siri na kwa ndani, bila kuonekana. Ufalme wa Mungu unagusa maisha ya ndani na kupenya hata mazingara ya uovu. Mungu ataushinda uovu wote ndani ya mtu na ndani ya ulimwengu.

Mifano hiyo ya ukuaji ni jibu la Yesu kwa wale waliotazamia matukio makubwa yatatokea mara, walioshindwa kuona Kuja Kwake kumeleta mabadiliko waliyotazamia. Kumbe Mungu alikuwa akifanya kazi kwa wale wenye macho ya kutambua, njia zake si zetu. Kwa sababu neno limepandwa na chachu imewekwa, hakika mavuno yatapatikana, ila ni subira inayohitajika.

**v. Shabaha ya Mifano 13:34-35**: Hiki ni kipengele cha pili kuhusu shabaha ya mifano k. 10 ku. Lengo halikuwa kufundisha kinaganaga habari za Ufalme wa Mungu. Ila kwa wanafunzi ambao wamejikabidhi Kwake, atawaelezea "siri" ya Ufalme. Neno hilo ni timizo la Zab.78:2. Wengi hawawi tayari kujitoa Kwake vizuri, hivyo kwa mafumbo ya mifano ataachana nao.

**vi. Mifano 3 - hazina, lulu nzuri, na juya: 13:44-50**:
Mifano ya hazina na lulu nzuri inafundisha mamoja. Ufalme wa Mungu ni wa kudumu milele, vyote vingine vitatoweka, kwa hiyo ni wa thamani kuu isiyohesabika. Yeyote atakayeukuta atasikia furaha sana, tena atakuwa tayari kuuza au kuacha vyote alivyo navyo ili aupate 10:37-39 19:27-29. Wala hatahesabu ni hasara kufanya hivyo, maana apata kitu cha thamani izidiyo. Wengine hupata kuisikia Injili kama kwa bahati, kama yule aliyeikuta hazina iliyositirika, hakuitafutia. Wengine hutafuta sana kujua ipi ni kweli, wakitaka sana kujua shabaha ya kuishi hapa duniani, hao wajaribu filosofia na dini na imani mbalimbali, mpaka baada ya kutafuta-tafuta wasikia habari za Kristo. Hao ndio mfano wa mfanyi biashara aliyetafuta-tafuta lulu zuri, ndipo alipoliona akawa tayari kuuza alivyo navyo vyote na kulipata Luka 14:33: wasio tayari kuacha vyote hawawezi kuingia.

Juya:47-50: Mfano huu unafanana na wa Ngano na Magugu. Wakati huo wema na wabaya huendelea pamoja, ila kwa uhakika, watatenganishwa siku ya mwisho, hukumu itafanyika, na wasiofaa watatupwa nje, watapatwa na dhiki kuu. Wana wa ufalme watakaribishwa kwenye raha ya milele. Katika Ufalme wa Mungu hamna nafasi kwa waovu. Kwa hiyo wakati huo yule mwovu na wafuasi

wake huendelea pamoja na Yesu na wafuasi wake pia huendelea pamoja. Mambo yataiva na kuufikia upeo wakati Mungu atakapofunga nyakati hizi za sasa. Hakuna haja ya kukata tamaa, iliyopo ni kuhakikisha kwamba wamo katika Ufalme wake kwa kutubu na kumwamini Kristo. Sasa ndio wakati wa kukata shauri vizuri na kujiweka upande wa Kristo.

**vii: Mfano wa mtu mwenye nyumba: 13:51-53:** Yesu ametilia mkazo wa wanafunzi kuwa na ufahamu na utambuzi wa kiroho, wasipime mambo kwa jinsi yaonekanavyo kwa nje. Taz. k.13, 14, 15, 19, 23. Wawe kama waandishi waliopewa mafundisho ya kuwasaidia kuelewa. Hao ni kama wenye nyumba walio na wajibu wa kutumia "Hazina ya mafundisho waliyopokea" na kuwapa wengine ili hao nao waelewe siri ya ufalme. "vitu vipya na vya kale" "Vya kale" ni kweli za Mungu zilizowekwa tangu awali. I Kor 2:7 Ef. 1:3-12; 3: 9-11; na manabii walizitabiri pia ni "vitu vipya" kwa sababu sasa Kristo anayafunua, akiingiza ufalme wake kwa uwezo: Ef. 3:4-5; Ebr. 1:2.
*MASWALI:*

*Je! Mifano hiyo imekusaidiaje katika kufahamu hudumu yako? Yamerekebisha mawazo yako kwa njia gani hasa kuhusu Ufalme wa Mungu na kuja kwake?*

*Kutokana na mfano wa Mpanzi na Mbegu umetiwa moyo na neno gani na umepewa onyo kwa neno gani, unapofikiri mafanikio ya huduma yako?*

## MAITIKIO MBALIMBALI KWA MAFUNDISHO NA MIUJIZA YA YESU: 13:54-16:20.

**i. Mji wa Nazareti kumkataa 13:54-58:** Mko 6:1-6

Tumeona ya kuwa Yesu anazidi kupingwa. Pale Nazareti alikataliwa na wenyeji waliomfahamu tangu utoto wake. Mahali ambapo mama na ndugu zake wangali wakiishi. Katika Luka 4 kuna habari ya Yesu kuwa Nazareti, ila pengine wakati ulikuwa mwanzoni mwa huduma, ila hatuna uhakika. Iwapo walishangazwa na mahubiri na hekima yake, hawakuwa tayari kukubali kwamba ametoka kwa Mungu. Walimdharau wakisema "huyu si mwana wa seremala" - walishindwa kwa sababu walimtafakari kwa kimwili tu. Waliona kwamba ni jambo geni kabisa kwa mtu aliyelelewa kati yao, na kufanya kazi ya useremala tu, mtu ambaye hakuelimishwa katika shule za marabi, amethubutu kufundisha kama rabi aliye hitimu pia kuonyesha uwezo wa kipekee katika kuponya watu na kutoa pepo n.k. Walifikiri wamemfahamu ya kutosha, ila hawakuelewa siri ya asili yake.

k.58: Mathayo alisema hakufanya miujiza mingi kwa sababu ya kutokuamini kwao - Marko alisema "hakuweza kufanya" Pia Marko aliandika kwamba Yesu alistaajabu kwa ajili ya kutokuamini kwao.

Yesu hakujitetea, aliona chuki yao ni kubwa, ni ukuta usiorukwa. Hatawalazimisha kumwamini kwa kufanya miujiza. Twasoma walichukizwa, bila shaka walitaka maelezo ambayo yatawaepusha na haja ya kujitoa Kwake.

Jambo muhimu ni imani. Neno linalozuka katika habari hizo ni Yesu ni nani? Ni mara ya mwisho kusikia habari za Yesu kuwa sinagogini.

ii: **Herode Antipa kumwaza Yohana Mbatizaji amefufuka na Yesu kuwa ndiye yeye:** 14:1-12:

k.3-12 Vyasimulia habari ya mambo yaliyokwisha kutendeka zamani kidogo. Herode Antipa alikuwa mwana wa Herode Mkuu, alipewa kutawala Galilaya na Perea. Wenyeji walimwita "Mfalme" lakini siye. Alimchukia Yohana Mbatizaji kwa sababu mara nyingi Yohana alimkemea kwa kumchukua mke wa ndugu yake Filipo. Hakuchukua hatua ya kumwua kwa sababu aliwaogopa watu, pia inaonekana dhamiri yake ilimshtaki na aliguswa na mahubiri ya Yohana Mk.6:20. Ndipo alibanwa bila kutazamia, wakati wa sikukuu ya kuzaliwa kwake. Alimwahidi binti yake cho chote atakachopenda - kumbe, kwa kuchochewa na mamaye aliomba kichwa cha Yohana. Herode alisikitika, ila hakutaka kuaibishwa mbele za wageni wengi akakubali apewe. Ni tendo lililo kinyume cha sheria za Kiyahudi, maana Yohana hakuhukumiwa kwanza, tena Wayahudi hawakukata kichwa kama adhabu ya kumwua mtu. Twajifunza kwamba chuki ni hatari sana.

Bila shaka Yesu alipopata habari hizo alikumbushwa kwa nguvu "mwisho" wake mwenyewe, maana wakuu walikuwa na chuki kubwa Kwake, dalili zipo za kifo chake cha mbeleni.
Kama tulivyosema, tendo hilo limekwisha kutendeka muda uliopita. Kwa nini ziandikwe hapo? Jibu ni katika k 1,2. Herode alikuwa akisikia habari za matendo makuu ya Yesu na jinsi umati wa watu humfuata, alishikwa na wasiwasi alidhani kwamba Yohana amefufuka kutoka kwa wafu na yeye ndiye anayefanya hayo yote. Twajifunza kwamba amemwondoa kimwili lakini bado anasumbuliwa naye katika dhamiri na mawazo yake, hata amekosa amani. Ndipo katika k.13 twaona kwamba Yesu alipofahamu jinsi Herode anavyomwaza kuwa Yohana aliondoka mahali alipo na kwenda pasipo na watu.

iii. **Alilisha mkutano mkubwa:** 14:13-21:

Habari hii imeandikwa katika Injili zote nne, kwa hiyo inaonekana ni jambo lenye maana kubwa kwa wanafunzi. Mko 6:3lku. Luka 10ku. Yoh.6:1 ku. Yesu aliondoka eneo la Herode akitafuta nafasi ya utulivu na wanafunzi wake, kwa hiyo walivuka Bahari mpaka Bethsaida Luka 9:10, lakini wengi walimfuata wakija kwa miguu.

Badala ya kunung'unika aliwahurumia k.14,16. maana walileta wagonjwa, na Yesu aliwaponya na kuwafundisha. Siku ilipoendelea wanafunzi walimwomba awaage watu ili wapate nafasi ya kujitafutia chakula. Yesu alisukumwa na huruma alipowaona hawana "mchungaji mwema" ndipo aliamua kutumia uwezo wake na kuwalisha. Ila hana budi kufanya wanafunzi wake watambue ya kuwa Yeye amewaita wawe wachungaji wa Israeli mpya, kundi lake la KiMasihi, ila wito huo hawataweza kuutimiza kwa nguvu zao wenyewe. Watahitaji uwezo

wake. Ndiyo sababu aliwaingiza kabisa katika huduma ya kuwalisha. Kwanza aliwaambia "hawana haja ya kuondoka, wapeni ninyi kula" Ni kuwalazimisha watazame walicho nacho ili wakiri ya kuwa hakitatosha hata kidogo. Aliwaagiza wakilete hicho kidogo walicho nacho Kwake, ndipo akamshukuru Baba kwa ajili yake, akakibariki, ndipo akawarudishia ili wakigawe kwa watu, kumbe! kwa njia hiyo kilienea na kuwashibisha wote hata kubaki. Twajifunza kwamba kile kidogo tulicho nacho Yesu hatakidharau, na ni hicho kidogo kitakachotumiwa sicho kingine!! Mabaki ni ishara kwamba maadamu haja ipo "kile kidogo" kitaenea. Ila hasa Masihi amekuja kuleta baraka za kiroho, tukitazama Yoh.6:26ku. alitoa mafundisho kuhusu "chakula cha uzima".

Yoh. 6:15: Watu walitaka kumshika Yesu na kumweka kuwa Mfalme wao, bila shaka walikumbushwa Musa na "mana" ya zamani pia juu ya Elisha 2 Waf. 4:42-44. Yesu alipotambua hayo aliwaondoa wanafunzi iwapo wao hawakutaka na Yeye Mwenyewe alijitenga, akapanda mlimani na kuomba. Bila shaka alisikia nguvu ya kujaribiwa kama zamani jangwani, Shetani alipomwonyesha njia za mkato, Shetani akitaka kumwondoa asiende msalabani.

Hakudanganywa na watu, alijua wamefurahiwa kwa kulishwa "kimwili", wengi hawakuwa na mzigo wa mambo ya kiroho. Twakumbushwa juu ya Ushirika Utakatifu, kila Injili ina habari hiyo; zikitaja mambo manne: "alitwaa, akabariki, akamega, akawapa" Ni karamu kuu Taz. I Kor. 11:23-24.

### iv. Kutembea juu ya maji 14:22-33

Yesu alilazimisha wanafunzi waondoke kwa chombo na kuvuka bahari bila Yeye.

Bila shaka waliwaza atakuja kwa miguu kwa nchi kavu. Labda walishiriki matakwa ya watu katika kumshika kuwa Mfalme. Yesu hakutaka waguswe na mawazo na msisimuko wa watu. Baharini walipigwa na dhoruba kali na kwa muda mrefu walitaabika k. 25. Mwishowe Yesu aliwaondoa hali akitembea juu ya maji, huku mawimbi yalikuwa makubwa na upepo ulivuma sana, akataka kuwapita Mk. 6:48. Kwa nini afanye hivyo? hatujui; labda alitaka wajifunze kwamba baadaye hatakuwa nao hali ya kuonekana ila kiroho atakuwa nao daima.

Alipojitambulisha kwao waliogopa sana, ila Yesu aliituliza mioyo yao kwa maneno aliyoyazoea kuyatumia "jipeni moyo, Ni Mimi (Kut. 3.14) msiogope". Kwa nini alifanya kama atawapita, ndipo twakuta ameingia chomboni? Ni kwa sababu ya Petro. Alipoisikia sauti ya Yesu na kuona kwamba hana nia ya kujiunga nao chomboni aliamua kwenda Kwake kwa kutembea juu ya maji. Yesu akamwita "njoo" Petro aliitika kwa kuanza kwenda - ujasiri ulimwacha alipoyaondoa macho yake kwa Yesu na kuyatazama mawimbi - akaanza kuzama. Kwa hofu kuu akamwita Yesu amwokoe. Yesu akamhurumia na kumshika mkononi, na kumkemea kwa imani yake haba. Walipoingia chomboni,

mawimbi yakapungua, upepo ukaacha kuvuma; wanafunzi wakamsujudia na kumkiri kuwa Mwana wa Mungu. Yesu ni mtawala wa bahari na upepo.

**v. Yesu kupendwa kwa uponyaji alioufanya 14:34-36:**

Genesareti lilikuwa eneo chini ya utawala wa Herode Antipa. Hapo nyuma Yesu aliondoka katika sehemu iliyotawaliwa naye 14:13, kwa hiyo ni vigumu kuelewa sababu ya kurudi. Watu waliamini kabisa Yesu atawaponya wagonjwa wao, wakatangaza kufika kwake na kumletea wote waliokuwa hawawezi. Walikuwa wakiridhika kwa kuligusa pindo la vazi lake tu, labda habari ya yule mama imewafikia 9:20. Watu wangali wakimpenda Yesu kwa huruma zake za kuwaponya wagonjwa wao ling. na 4:23-24; 8:16; 9:35; 12:15 15:30-31 akipona watu wote si mmoja mmoja tu. Iwapo ni kwa jumla siyo kusema kwamba hakuidai imani, maana waliionyesha imani kwa kuligusa pindo tu, wala siyo kusema hawakuhusika ki-binafsi.

*MASWALI:*

*Umepata funzo gani kubwa kwa kuona jinsi Yesu alivyowalisha watu wengi kwa mikate na samaki chache?*

*Je! ne vema kushirikisha wengine katika huduma yako? faidi yake ni nini? Je, katika huduma yako ni nini inayokupa mashaka? Ni wakati gani unapojaribiwa kuondoa macho yako kwa Yesu? Unafanyaje wakati wa mashaka ili imani yako yapate kujengwa kwa upya?*

**vi. Majadiliano na Mafarisayo na Waandishi juu ya unajisi: 15:1-20:**

Ni hatua ya mbele katika upinzani wa wakuu. Majadiliano yalihusu "dini ya kweli". Inaonekana hao Mafarisayo na waandishi ni kama wajumbe kutoka Yerusalemu waliotumwa rasmi ili wampeleleze Yesu na kuona kama anashika Torati au vipi. Wasiwasi ilizidi pale Yerusalemu waliposikia habari za wengi katika Galilaya kumfuata Yesu, nao waliogopa upinduzi.

Walipoona kwamba wanafunzi hawakunawa mikono kabla ya kula walimshambulia Yesu na swali "mbona wanafunzi wako huyahalifu mapokeo ya wazee ..... ?" Yesu akajibu kwa swali "mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?" Katika Agano la Kale haimo amri juu ya kunawa mikono. Iliingizwa na Mafarisayo na waandishi kwa njia ya mapokeo. Jambo la "kunawa" si jambo la afya bali la kunajisika, maana walifundisha kwamba kwa kugusa kitu fulani au mtu fulani kama Mmataifa waweza kunajisika kwa sheria yao. Mwanzoni bila shaka nia ya wale walioandika mapokeo ilikuwa safi wakitaka kuwasaidia watu kuelewa maana ya amri ya Mungu vizuri zaidi - k.m. amri ya Mungu ilisema "usifanye kazi siku ya Sabato" basi walifafanua maana ya neno "kazi" ni kazi zipi zilizokatazwa n.k Shida ni kwamba baadaye walizidi mpaka na kutoa visheria vingi vidogo vidogo mpaka badala ya kuifunua sheria ya asili wameifunika. Zaidi ya kuifunika wameitangua amri ya Mungu. Kwa swali lake, k. 3. Yesu alitoboa wazi utofauti uliopo kati ya

Amri ya Mungu na Mapokeo ambayo yametungwa na wanadamu. Ipi ina mamlaka? Ndipo Yesu aliendelea kuonyesha jinsi ambavyo wameitangua amri ya Mungu akisema juu ya desturi ya Korbani. Kwa mapokeo yao waandishi walisema kwamba mtu aweza kuapa kwamba mali fulani ni Korbani, yaani imewekwa kwa hekalu n.k. kwa hiyo mali hiyo haiwezi kutumika kuwatunza wazazi wake wazee.

Lakini mali hiyo hakuitoa kwa hekalu, aliendelea kuitumia. Hivyo aliepa **amri ya Mungu** iliyosema "waheshimu baba yako na mama yako". Yesu alihesabu wameyapinga mapenzi ya Mungu kwa mapokeo hayo - ni "wanafiki" k. 7; kwa sababu walidai kuwa watu waliotaka kumpendeza Mungu huku walikuwa wakipinga mapenzi yake yaliyo dhahiri katika amri za Mungu. Mathayo waliona wamefanana na watu wa siku za Isaya nao walistahili laumu zile Isaya alizozitoa kwa watu wa wakati wake Is. 29:13. Dini ya namna hiyo ni bure, haifanyiki kwa moyo. Tangu sura ya tano tumeona mkazo wa Yesu ni juu ya "undani wa mtu, moyo na nia na sababu zake".

k. 10 Yesu aliona mafundisho yao ni ya hatari, yaharibu uhusiano wa mtu na Mungu, kwa hiyo aliwaita watu ili awafundishe zaidi. Aliyatumia maneno ya fumbo, baadaye aliwafunulia wanafunzi maana yake k.15-16. Kitu cha maana si cha nje bali cha ndani - uovu umo moyoni mwa mtu, chakula hakiwezi kumnajisi mtu. Kwa hiyo fundisho la Yesu lilitikisa kabisa mafundisho ya viongozi, na mengine katika Agano la Kale. Mafarisayo na waandishi walichukizwa na mafundisho hayo ya Yesu, na wanafunzi walimweleza Yesu hivyo. Ndipo Yesu alisema mambo magumu kuwahusu: wamekataliwa na Mungu kuwa viongozi; hawakufaa kuwa waalimu wa kufundisha mapenzi ya Mungu; hawamo katika Ufalme wa Mungu; hawakupandwa na Baba yake, maana yake hawakuwekwa na Mungu; nao wataondolewa. Wanapodai kuwa viongozi ni viongozi vipofu, na ni hatari kabisa kipofu akithubutu kumwongoza mwenzake kwa hiyo waachwe k.14 waendelee katika upofu wao.

15:17-20: Halafu Yesu alirudia kuukaza umuhimu wa "undani" wa mtu, moyo wake. Kama uovu umo ndani (Yer. 17:9) ni kwa jinsi gani kula na mikono isiyonawiwa kwaweza kumnajisi mtu? Dhambi haitokani na mazingara ya nje, bali hutoka kwa ndani. Yesu aliorodhesha dhambi kadha za ndani. Mafundisho hayo ya Yesu yatasababisha kuondolewa kwa "miiko ya chakula" na kufanya chakula chote kuwa safi - Mko:7:19b. Pia yatafungua njia ya Wakristo wa WaMataifa kula pamoja na Wakristo wa Wayahudi - meza moja, familia moja, Kanisa moja, Imani moja.

### vii. Imani ya mwanamke wa Ki-mataifa: 15:21-28:

Yesu alijitenga na makutano na hao Mafarisayo na waandishi waliotoka Yerusalemu, akaenda sehemu ya kaskazini magharibi, pande za Tiro na Sidoni. Mwanamke alikuwa Mkananayo, mwenyeji wa asili, watu hao walikuwepo wakati wa Yoshua kuingiza Waisraeli nchini baada ya kutoka Misri. Mwanamke alimtambua Yesu ni Masihi, alimwita "Bwana, Mwana wa Daudi" akaja akamlilia

Yesu kwa ajili ya binti yake. Tumeona huruma za Yesu, ila katika habari hiyo alikuwa mzito hakumsaidia huyo mama mara. Kwa mara nne ombi la huyo mama halikujibiwa Kwanza Yesu alikuwa kimya k.23; pili, wanafunzi walimnung'unikia k.23; tatu, Yesu alitumia maneno kuhusu shabaha ya huduma yake kuwa kwa Wayahudi tu k.24; kisha alitumia lugha ngumu juu ya WaMataifa k.26. Maneno ya wanafunzi katika k.24 yaweza kumaanishwa kwamba walitaka Yesu amponye binti mara moja ili wasicheleweshwe zaidi na huyo mama.

Huyo mama alikubali kwamba hakustahili kuzishiriki baraka za Ki-Masihi "si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa" akasema "ndiyo Bwana" - alijinyenyekeza, hakubisha, kwa upande wake binti yake anahitaji msaada, ni hilo tu analotaka, mengine yote si kitu. Alionyesha imani kubwa kwa kutaja "makombo anayokula mbwa mezani pa bwana wake" Kweli Wamataifa hawastahili kuketi mezani pa Masihi, lakini hata hivyo yawezekana wapate "makombo" sawa na mbwa!!!

Bila shaka Yesu aliutambua ukweli na imani ya huyo mama, na alizidi kuivuta na kuikuza. Kumbe "makombo" ya Masihi ni uponyaji wa binti yake, makombo mazuri ajabu!!!

Yesu aliisifu sana imani yake, mara kwa mara WaMataifa waliwazidi Wayahudi kwa imani, nao watakuwemo katika Ufalme wake 8:10-11; Yesu akamponya binti yake.

**viii. Huduma ya Uponyaji kati ya Wamataifa: 15:29-31:** Yawezekana Yesu alikaa sehemu zile kwa muda akiwafundisha wanafunzi. Alipata utulivu huo kwa kuwa walikuwepo katika nchi ya Wamataifa. Walipoondoka wakaelekea upande wa mashariki ya Bahari ya Galilaya Mko:7:31, wilaya ya Dekapoli palipo na Wamataifa wengi. Huko aliwaponya wengi, viwete, vilema, vipofu na mabubu, wengi wao wakiwa Wamataifa, nao wakamtukuza "Mungu wa Israeli" lugha ambayo ni dalili ya Wamataifa kuwepo. Kwa hiyo, iwapo maneno ya 15:24 ni mwongozo kwa huduma yake, Yesu hafungwi na mwongozo huo, na baadaye mlango utafunguliwa wazi kwa Wamataifa 28:19-20.

**ix. Kulisha umati wa watu tena 15:32-39**:
Baadhi ya wataalamu wasema kwamba Mathayo ameandika kwa mara mbili habari za kuwalisha watu elfu tano. Ni vigumu kukubali, kwa sababu Yesu Mwenyewe alitaja kuwalisha watu elfu 5 na elfu 4-16:9. tena zipo tofauti nyingi katika idadi ya watu na kiasi cha chakula kilichotumiwa na kilichobaki, na mahali na aina ya vikapu; pia katika chanzo chake, maana wanafunzi walimwambia Yesu awaage watu, halafu kwa watu elfu nne ni Yesu aliyeleta neno hilo mbele ya wanafunzi. Huenda Wamataifa wengi walikuwepo na kama ni hivyo ni ishara kuwa hao nao watashirikishwa baraka za Masihi. 15:32 Watu walikuwa wamekaa siku tatu wakimsikiliza Bwana Yesu labda walitazamia matukio makubwa. Yesu aliwahurumia hali alifahamu watakuwa na njaa na watataka kula. Alisema na wanafunzi juu ya kuwapatia chakula - tusisahau

amekwisha kulisha watu elfu 5 nao waliingizwa kabisa wakati ule. Hata hivyo wangali wakiwaza kama kawaida, kile walicho nacho tu. Wakasema "tupate wapi" labda ni njia yao ya kukiri kushindwa kwao. Pengine hawakusikia huruma kwa Wamataifa na Yesu alitaka kuamsha mawazo ya kuwahurumia Wamataifa, maana baadaye watatumwa kwao.

*MASWALI:*

*Katika sura hii tunafunuliwa wazi ule utofauti mkubwa kati ya Yesu na wakuu wa dini ya Kiyahudi? Hayo yakusaidiaje katika huduma yako? Ujihadhari na nini? Je! Kanisa li katika hatari ya kuweka sheria zake kuwa sawa na Neno la Mungu? waonaje? Ukifikiri "ndiyo" taja ni katika mambo gani.*

**x. Yesu kuwakemea Mafarisayo na waandishi: 16:1-12:**

Kwa kawaida watu hawa hawakupendana, Masadukayo si watu wa Kiroho, hasa walihusika na siasa, walipenda mali na vyeo, na makuhani walitoka kwao. Mafarisayo walishughulika mambo ya dini, Torati, ibada za masinagogini n.k. Ila ajabu ni kwamba walijiunga pamoja ili wamshambulie Yesu na kumpinga. Ni mara ya pili Yesu ameombwa kufanya ishara ya kipekee 12:38-39. k.1 "wakamjaribu" Ombi lao halikutoka katika nia safi, na Yesu alikataa kama hapo nyuma. k.2-3: waliweza kutambua hali ya hewa, pia walidai kuwa viongozi wa kiroho, kumbe ishara za maana za kumhusu Masihi na nyakati zake (11:4-5) wamekosa kuzitambua. Hasa umuhimu wa kuukubali wito wa Yesu "tubuni, maana ufalme wa Mungu umekaribia". Wamekosa kuelewa kwamba katika Kuja kwa Yesu, Ufalme wa Mungu umekuja nao upo kati kati yao, sababu ni kwamba wamemwasi Mungu k. 4a. Ishara itakayotolewa baadaye ni kufufuka kwake Yesu.

Masadukayo hawakuamini kwamba kuna ufufuo wo wote, na Mafarisayo waliamini utakuwepo ufufuo wa wenye haki tu mwisho wa mambo yote. Yesu aliwaacha.

5-12. Yesu aliwaonya wanafunzi juu ya upinzani wa hao ambao hawakutoa mafundisho ya kweli. Aliwakemea wanafunzi juu ya uhaba wa imani yao. Iwapo walishirikiana naye katika kuwalisha umati wa watu mara mbili, walipokuwa wamesahau kuchukua mkate walihangaika sana. Ndipo Yesu alisemea hatari ya mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo kwa kutumia lugha ya "chachu" na kama chachu huchachisha donge zima ndivyo mafundisho yao yaweza kuwakolea wasipojihadhari nayo. Kwa hiyo Mathayo ameonyesha jinsi upinzani wa Mafarisayo na Masadukayo unavyozidi, wakiwa tayari kujiunga pamoja.

**xi. Yesu ni Masihi: 16:13-20**:
Yesu amefika njia panda katika huduma yake, mawingu meusi ya upinzani yazidi kuzuka. Hana budi kuwaandaa wanafunzi kwa kuuawa kwake, ila kwanza ni vema awapeleleze ili aone wamefikia wapi katika kumtambua. Hivyo aliwachukua mpaka Kaisaria-Filipi, mbali na Wayahudi, karibu na chanzo cha

mto Yordani. Hapo alitulia nao na kuzungumza nao. Yeye ni nani? neno hilo limezidi kuzuka, kila mara baada ya kufanya mwujiza n.k. watu na wanafunzi waliitika kwa kusema "huyu ni nani?" Wanafunzi walikuwa wamepiga hatua katika ufahamu wao 14:33. Yesu alitaka wamkiri wazi. Aliuvuta usikivu wao kwa kuanzia mbali kwa kuwaulizia swali "watu wanena Mwana wa Adamu ni nani?"

Wakajibu kwa kuwataja manabii kama Eliya na Yeremia, pia Yohana Mbatizaji; hawakufikiri ni zaidi ya nabii hawakumwona kuwa wa kipekee. Yohana aliwatayarisha watu kwa ufalme ila hakuwaweza kuwaingiza, aliweza kuwaleta mlangoni ila ni Yesu aliye Mlango Yoh. 10:7. Eliya na Yeremia walikuwa watu wa maombi, na Eliya alifanya miujiza hata hivyo aliweza kukata tamaa. Yeremia alifanana na Yesu zaidi kwa uvumilivu wake na mateso yake. Alitabiri habari za Agano Jipya ila ni Yesu atakayezitimiza ahadi zake za msamaha wa dhambi. Kisha Yesu aliwageukia wanafunzi na kuwauliza "nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?" Petro aliyekuwa na tabia ya kujibu kwa haraka, pia alikuwa kama kiongozi kati yao (10:2, 14:28ku 15:15 17:24-27 18:21)alimjibu "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai"

Kwa nini Petro na wenzake wamemtambua hivyo na wengi walishindwa? ni kwa sababu alifunuliwa na Mungu k.17 ling. na 11:25. k.18: Petro ni "Petros" kwa Kiyunani na mwamba ni "Petra" kwa Kiyunani. Aliitwa Petro zamani 10:2 Mk. 3:16 Yoh. 1:42 ila sasa Yesu alifunua sababu ya kupewa jina hilo. Atakuwa na kazi ya kuwa msingi wa mwamba kutokana na ukiri wake. Ndivyo alivyokuwa katika Kanisa siku za kwanza, akiwa kiongozi kati ya Mitume. Katika Nyaraka Kristo Mwenyewe ameitwa msingi na jiwe kuu I Kor. 3:10-11; I Pet. 2:6-8. Petro kwa tabia hakuwa imara kama mwamba, alijikwaa mara kwa mara 16:22-23; 26:52, 56, 74, 75. Gal. 2:11-14 na katika Mdo. 15 alijitia chini ya uamuzi wa Yakobo na Kanisa zima. Ukweli wa ukiri wake ulimstahilisha kuitwa Petro. Katika Ef. 2:20 na Uf. 21:14 Mitume wote wameitwa msingi ila hasa ni ile kweli waliyokuwa nayo ambayo ndiyo neno la maana.

k.18b. "Milango ya kuzima haitalishinda" Is. 38:10: Kanisa halitakufa, ni jamii ya watu wa Mungu ambao watadumu milele.

k.l9: "funguo za ufalme wa mbinguni" ni mamlaka kuu na mitume wote wameikabidhiwa, si Petro peke yake 18:18. Taz. Yoh. 20: 22-23: Ni kuhusu uwezo wa kusamehe na kutokusamehe dhambi. Funguo zatuelekeza kuwaza mambo mawili: funguo za kufungua nafasi ya kuingia mlangoni, mfano wa mlinzi mlangoni. Kama ni hivyo maana yake ni kwa kuihubiri Injili watu watapewa nafasi ya kutubu na kumpokea Kristo, kama Petro alivyofanya Siku ya Pentekoste, watu elfu tatu waliuitika wito wake wa kutubu na kumwamini Kristo. Waliokosa kuitika watakuwa wamekosa nafasi ya kuingia. Wazo la pili ni kwamba funguo ni za "uongozi" Is. 22:22, mamlaka ndani ya Kanisa ya kuongoza na kupanga mambo kama wakili, akiamua linalokubalika na lisilokubalika yaani kufunga na kufungua. Lugha hiyo ilitumika na marabi wakiruhusu au kukataa mambo. Petro alifanya hivyo Wamataifa walipoingizwa katika Kanisa bila tohara Mdo. 10:11:18. Kwa hiyo lo lote watakalofanya kwa

kupatana na mapenzi ya Mungu litakuwa na mamlaka. Maneno ya Yesu kwa Petro hayaonekani katika Injili ya Marko Mk. 8:27-30 ambayo imedhaniwa kuwa na uhusiano mkubwa na Petro na Rumi, mji mkuu wa Dola.

k.20. Yesu aliwakataza wasimtangaze kuwa Kristo - kwa nini? Sababu moja ni kwamba ni juu ya kila mtu kutambua habari hiyo mwenyewe; pili, hata iwapo wamemkiri kuwa Kristo na kuamini kwa dhati ni kweli, hata hivyo wamekosa kuelewa aina ya Umasihi wake 16:21-23, Petro atakemewa vikali sana mara baada ya kumkiri kuwa Masihi. Hawajafahamu bado kwamba lazima ateswe na kuuawa. Kama hao walio karibu naye daima wameshindwa kumwelewa kikamilifu, sembuse walio nje.

Wakidaka neno Masihi bila kuelewa watamshangulia kwa mawazo ya siasa siyo ya kiroho na kumletea shida katika kuendelea na huduma.

## MAFUNDISHO JUU YA HUDUMA YAKE: 16:21-17:27:

### i. Tangazo la kwanza kuhusu Mateso na Kifo chake 16: 21-23:

k.21 "tangu wakati huo Yesu alianza" yaani tangu Petro kumkiri kuwa Masihi, Mwana wa Mungu - Yesu alianza neno "anza" laonyesha ni hatua mpya. Ling. na 4:17 Yesu alipoanza huduma yake huko Galilaya, huduma ya kuhubiri na kupona n.k. Katika hatua hiyo mpya Yesu alijifunua zaidi kwa wanafunzi wake kuhusu Umasihi wake na wito wa kuwa Mtumishi ateswaye atakayekataliwa na watu, na kwa njia hiyo alizidi kuwaandaa kwa kuondoka kwake.

Maneno ya 16:21-23 yafuata ya 16:13-20 nayo yafahamika kutokana na hayo yaliyotangulia. Umasihi alioukiri Petro utakuwa na utofauti mkubwa na alivyodhani.

Petro alikuwa mbele katika kuukiri na katika sehemu hiyo Petro ni mbele katika kutokuelewa aina ya Umasihi alioukiri. Wanafunzi wote walikuwa pamoja naye ila ni yeye aliye msemaji wao. Kama hao waliokuwa karibu na Yesu kila siku wamekosa kuelewa vema, Je! umati wa watu wameelewaje? wameelewa vema? la! hata kidogo! Ilikuwa vigumu kwa Myahudi ye yote kuuelewa ulazima wa Masihi wao kuteswa na kuuawa, iwapo katika Maandiko unabii ulionyesha hivyo.

k.21 Yesu aliwapasha habari ya jinsi mambo yatakavyokwenda watakapofika Yerusalemu - "imempasa kwenda Yerusalemu" Yesu hakutoboa wazi sababu zake ila ameona "imempasa" kutokana na jinsi alivyofahamu wito wake. Ilikuwa vigumu aishike njia ya kwenda Yerusalemu kwa kuwa alielewa kabla ya kwenda ni nini yatakayompata. Alitaja "wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi" vikundi vitatu katika Baraza Kuu la Wayahudi lililoitwa "Sanhedrin", ambao watamhukumu afe. Uadui umezidi na utengano kati yao na Yesu hautengenezeki.
Ila neno la mwisho si lao, Mungu atamfufua katika wafu siku ya tatu. Bila shaka Petro na wenzake waliposikia habari za kuuawa kwake waliduwaa, kiasi cha kutokushika neno la kufufuka.

Petro aliposikia habari hizo alimhurumia Yesu na alitaka kumzuia asipatwe na hayo. Hakuelewa ni mapenzi ya Mungu, hivyo alimkemea Yesu kwa nguvu sana akitumia neno "hasha". Yesu alisikia kujaribiwa vikali sana kama alivyojaribiwa jangwani, ila wakati huo Shetani amejificha akimtumia Petro, rafiki yake mpendwa sana, kusudi apenye mawazo ya Yesu kwa hila. Shabaha ya Shetani ilikuwa ileile ya wakati wote, amwondoe Yesu asiende msalabani. Ila wakati huo majaribu ni makali zaidi kwa kuwa mambo yameiva, yamekaribia, kwenye njia panda hana budi aichague njia ipi ya kuifuata. Je! ni kweli Baba anampenda huku anakubali auawe? Je! ni kweli kufa ndiyo njia ya hekima ya kuwaokoa wanadamu? Bila shaka Shetani alijitahidi kupandikiza mawazo kama hayo ndani yake.

Yesu alitambua hila ya Shetani, akamkemea Petro akamwonyesha wajibu wake ni kumfuata siyo kumpinga, pia, anayowaza ni kinyume cha mapenzi ya Mungu. Kweli Petro hakuelewa mpango wa Mungu kuhusu wokovu wa wanadamu. Mwamba umegeuka kuwa jiwe la kujikwaa.

Katika sehemu hiyo twaona ubinadamu wa kweli wa Yesu, akisikia kujaribiwa kwelikweli na kusikia ugumu wa njia iliyo mbele yake. Kwa kujua mapema kuliongeza shida. Je! ni rahisi kwa mtu kujua mapema juu ya kufa kwake au kuugua kwake?

Wewe na mimi tutaishije kama tutakuwa na uhakika wa kufa mwezi ujao? sidhani kujua kutaleta msaada. Yesu alijua tangu mwanzo, tena kifo chake kitakuwa kibaya mno.

Tunapounganisha ukiri wa Petro na ufunuo wa Yesu juu ya kifo chake twaona kwamba ni Mwana wa Mungu atakayekwenda Yerusalemu ili auawe na kufufuka - si nabii fulani - ni jambo la kipekee kabisa litakalofanyika Yerusalemu, jambo ambalo halijatokea kabla wala halitatokea tena baada ya hapo. Twaona ujasiri na uthabiti wa Bwana Yesu, iwapo njia zote zi wake Kwake, ni ile iendayo Yerusalemu ambayo yampasa akanyage, na tangu hapo ndiyo ni ile atakayoikanyaga.

ii. **16:24-28: Kumfuata kutaleta mateso:**

Kwa hiyo wanafunzi ni wafuasi wa mtu atakayesulibiwa, nao watashiriki mateso katika kumfuata. Kujikana, maana yake mtu hukana haki yake ya kuishi, hupaswa kunia na kukata shauri kumtanguliza Kristo na mapenzi yake katika maisha hata ikisababisha apatikane na shida, mateso, na hata kifo. Mtu atakayekataa kufuata njia hiyo ngumu atapata hasara kubwa mno, atapoteza nafsi yake. Hata kama mtu atapoteza maisha ya hapo duniani hana hasara kwa kulingana na hasara atakayeipata kwa kuishi maisha ya kujisalimisha tu na kupoteza uzima wa milele. Apime ni lipi la maana, la Mungu, au la dunia 6:24. Mwanafunzi wa Kristo budi akate shauri kuwa upande wa Kristo.

k.27. Uzito wa uchaguzi huo utaonekana katika siku ya hukumu Yesu atakapokuja tena. Ni ajabu jinsi Yesu alivyokuwa na uthabiti wa ushindi wake,

alijua hakika atashirikishwa mamlaka na utukufu wa Baba yake baada ya mateso yake. Kama ni hivyo ni vema, tena ni hekima, kwa wanafunzi wake kukata shauri kuwa upande wake, iwapo watapata dhiki na mateso.

k.28 Tumeona katika k.27 Yesu atakuja kama Mhukumu, na katika k.28 atakuwa kama Mfalme. Kuna neno moja lililo vigumu kuelewa katika k.28 ni kuhusu baadhi ya "waliopo" ambao watamwona atakapokuja. Kwa hiyo maana ya "Kuja Kwake" ni nini, na ni lini "Kuja Kwake"? Pengine maana yake ni Yeye kuja kwa Baba ili aupokee ufalme wake Dan. 7:13-14 Ling. na Math. 10:23. Atakapofufuka ataanza kumiliki ulimwenguni mwote na kwa njia hiyo kweli atakuwa amekuja katika ufalme wake, na wengi wa wale waliomsikia wataona jambo hilo katika Kanisa kuzaliwa na Injili kuenezwa.

Watalaamu wamewaza alikuja katika Kufufuka na Kupaa Kwake, pia katika mwaka BK.70 Yerusalemu ulipohukumiwa kama alivyosema, hekalu lilipobomolewa pamoja na mji mkuu kuanguka.

*MASWALI:*

*Waonaje wale wasemao kwamba si neno mtu awe anaamini nini kumhusu Yesu mradi tu anaishi vizuri? Iliwabidi wanafunzi wamkiri Yesu kuwa nani? Kama ni neno muhimu watu wamkiri Yesu kuwa Mwana wa Mungu, wewe unafanya nini ili watu wako wamwelewe Yesu vema?*

*Wanafunzi walishtushwa sana Yesu alipowafunulia kwamba yampasa aende Yerusalemu ili auawe. Halafu aliendelea kuwaambia kwamba wao pia watapaswa kuubeba msalaba wa mateso wakitaka kumfuata vizuri.*

*Kama hatusikii kukwazwa na habari hiyo. Je! kweli tumeelewa vizuri maana ya kuwa mwanafunzi wake? Utawafundisha Wakristo jinsi inavyowapasa kukubali mateso mbalimbali kwa ajili ya Kristo? Wataweza kupata mateso ya aina gani?*

iii. **Yesu alionekana katika utukufu** 17:1-13.

Jambo hilo lilitokea siku 6 baada ya Ukiri wa Petro pale Kaisaria-Filipi na baada ya furaha yao kuzimishwa Yesu alipowaambia juu ya kifo chake, na baada ya Yesu kuwaambia jinsi ambavyo wao wenyewe watateswa kwa ajili yake. Yesu alipanda mlima pamoja na watatu wa wanafunzi wake, Petro, Yakobo na Yohana - hao walikuwa naye alipomfufua binti Yairo, na watakuwa karibu naye zaidi ya wengine katika Bustani ya Gethsemane. Kutaja kwa usahihi wakati kuwa baada ya siku 6 ni kuuonyesha uhusiano na yaliyotangulia pale Kaisaria-Filipi. Twakumbuka kwamba Musa alipopanda mlima mtakatifu alichukua watatu pamoja naye Kut. 24:1; vilevile uso wa Musa uling'aa Bwana alipozungumza naye. Vilevile wakati huo uso wa Yesu uling'aa kwa sababu na utukufu wake Mwenyewe wa asili akionekana kama alivyo hasa.

Musa na Eliya walitokea katika utukufu. Kwa nini? Ni kuuthibitisha ukweli wa ukiri wa Yesu na Ufunuo wake juu ya mateso - walizungumza nini na Bwana Yesu? Luka ametuambia ni "kufariki kwake atakakotimiza" yaani msalaba ni

kiini cha mazungumzo yao, hatakufa kwa bahati mbaya bali kwa kutimiza mapenzi ya Mungu juu ya wokovu wa wanadamu, mpango ulioanzia zamani sana ambao Mungu ameutekeleza katika historia ya Israeli, Musa kama mwakilishaji wa Torati na Eliya kama mwakilishaji wa Manabii ni thibitisho. Hao wawili waliteswa na kukataliwa na watu kwa sababu ya huduma zao, hali wametumwa na Mungu - Ling. Luka 9:31 na 24:27. Yesu atatimiza yote ambayo waliomtangulia walitumwa kutayarisha, kazi yao imekwisha, ya Kwake itaendelea na kudumu.

Petro alijitoa kujenga vibanda vitatu, hali ametekewa, hakujua la kusema, lakini Musa na Eliya hawawi sawa na Yesu, budi waondoke na Yesu akae na kupata usikivu wao na ibada yao. Petro amesahau au pengine hakutaka kukumbuka, neno la Yesu juu ya kwenda Yerusalemu. Ndipo kabla hajamaliza kusema lilikuja wingu jeupe na kuwatia uvuli (wingu katika Agano la Kale lilikuwa ishara ya Kuwepo kwa Mungu), na kutoka wingu sa uti ya Baba ilisema naye, nalo lilithibitisha ukweli wa ukiri wa Petro na kumtia Yesu moyo wa kuendelea katika njia iendayo msalabani. Alikuwa ameisikia sauti hiyo alipobatizwa wakati alipojitwika wito na kuanza huduma,sasa sauti imekuja tena anapokaribia kumaliza huduma. "ninayependezwa sana" ni mapenzi ya Baba aende Yerusalemu na kuteswa. "msikieni Yeye" Kum.18:15,18. Wanafunzi wapaswa kumsikiliza Yesu anapowafunulia juu ya Kuuawa Kwake, ni kama kemeo kwa Petro. Kwa hiyo mateso na kuuawa na utukufu ni sehemu mbili katika jambo moja; moja halipo bila la pili.

Si ajabu wanafunzi walisikia hofu kuu walipotokewa na hayo yote. Kwa upole Yesu aliwagusa na kuyatumia maneno aliyezoea kusema nao "msiogope" na walipotazama walimwona Yesu tu, Musa na Eliya wametoweka na huenda Yesu alionekana kama kawaida yake.

k.9: Yesu aliwaagiza wasitangaze habari hizo - bila shaka wanafunzi walitaka kuwaambia wengine makuu waliyoyaona hasa kwa sababu watu wangefurahi kusikia habari za Musa na Eliya. Waliruhusiwa kusema habari hizo baada ya Yesu kufufuka.

Sababu ni kwamba Yesu hakutaka watu kuinuka na kumfuata hali ya kutaka aipindue serikali ndipo auawe kwa sababu ya siasa. La! kweli atakufa, ila sababu itakuwa ya kuwaokoa wanadamu na dhambi zao, yaani aukomboe ulimwengu.

k. 10: Watu walitazamia Eliya atarudi kabla ya Masihi kuja. Pale mlimani Eliya alikuja, kwa hiyo, kwa nini wasiruhusiwe kuutangaza Umasihi wa Yesu. Pia Eliya atapata nafasi lini kama Yesu atafufuka katika wafu, atatengeneza nini na lini? Lakini Yesu alijibu kwa kuonyesha kwamba iwapo ni kweli waandishi wamefundisha kuwa "Eliya atakuja kwanza na kutengeneza yote" Ma1.3:1 na 4:5-6 Mathayo 11:14. Wamekosa kuelewa kwamba "huyo Eliya" ni Yohana Mbatizaji ambaye ameisha kuja na kutengeneza yote tayari kwa Masihi. Kwa sababu hawakumtambua vema wamemwua Yohana, vilevile kwa

kutokumtambua Masihi, Yeye naye atauawa. Shida imetokea kwa sababu Mtangulizi wa Masihi na Masihi Mwenyewe hawakuwa kama watu walivyodhani.

iv. **17:14-20: Nguvu ya Imani:**

Wanafunzi tisa walibaki wakati Yesu alipopanda mlimani na Petro. Yakobo na Yohana. Mlimani imani ya wale watatu ilijengwa, huko nyuma imani ya wale tisa ilipungua. Waliletewa mvulana aliyesumbuliwa na pepo, mwenye kifafa, ambaye babaye aliwaomba wamponye.

Wakashindwa, iwapo kutokana na habari katika sura ya 10:1,8, wangaliweza. Wakamsubiri Yesu na wenzao watatu washuke mlimani. Yawezekana Yesu alikumbuka wakati wa zamani Musa aliposhuka mlimani akakutana na uasi mkubwa wa Waisraeli Kut.32. Yesu aliwakemea kwa kutokuamini kwao.

Twaona ya kuwa Yesu alichoshwa na watu wasio tayari kumwamini. Akamponya kijana. "Kuondoa mlima" ulikuwa msemo wa Kiyahudi ulio na maana ya kushinda shida au jambo gumu. Maana ya Yesu ilikuwa imani itaweza kufanya makubwa kwa sababu si kiasi cha imani kiletacho uwezekano ila kwa imani mtu hujiunga na uwezo wa Mungu, ni kumtegemea Mungu. Ni uwezo wa Mungu unaofanya makubwa kwa hiyo imani ndogo kama punje ya haradali itatosha kama imeungana na uwezo wa Mungu ambao ni mkubwa. Bila shaka Mathayo alikuwa mmojawapo wa hao tisa waliokemewa.

v. **Tangazo la pili kuhusu mateso na kifo chake** 17:22-23: Ling. na Mk.9:30-32 na Luka 9:44-45: Kwa mara ya pili walipokuwa wangali huko Galilaya na kabla ya kuja Yerusalemu (19:1 safari ilianza) Yesu aliwaambia wanafunzi kwa wazi kwamba atauawa na siku ya tatu atafufuka. Wakati huo Petro hakumpinga ila wote walisikitika sana maana bado hawajaelewa ki-ndani; na ndiyo sababu Yesu alihitaji kutilia mkazo neno hilo. Mk.9:32 neno jipya lilitajwa "atatiwa" katika Kiyunani ni lilelile la kueleza Yuda kumsaliti 26:15-16,21. Walisikia kama tayari wamefiwa na rafiki yao, na ahadi ya kuwa atafufuka haikuwasaidia. Huzuni hiyo haikuwaacha iwapo Yesu aliisemea usiku wa mwisho Yoh.16:6.

vi. **Swali kuhusu kodi ya hekalu:** 17:24-27:

Kila Myahudi alitoa nusu shekeli kila mwaka kusaidia gharama za ibada za hekalu, hali wakiona fahari juu ya taifa lao Kut.30:11-16. Baadhi hawakupenda kuitoa, kama Masadukayo na wengine, kwa hiyo waliilipa mara moja tu maishani mwote.

Je! Yesu alionaje? Aona Yeye ni tofauti na Wayahudi wengine. Ajibague na kuwakwaza? Jibu alilolitoa lilikuwa la pekee.

Alisema kwamba hakusika wajibu wa kulipa, ila yu tayari kusudi asiwakwaze na kufanya huduma yake idharauliwe.

k.24: Ni mara ya mwisho kusikia Yesu kuwa Kapernaumu, huenda wamekaa nyumbani mwa Petro k.25: 4:13; 8:14-15. Wakusanya kodi walimwendea Petro kama kichwa cha nyumba. Yesu ametambulikana kuwa mwalimu na kiongozi

wao Marabi hawakulipa kodi hiyo wala makuhani walioishi Yerusalemu. Je! Yesu adai asiilipe kama wao? Ni wazi Yesu amezoea kulilipa. Watu waliweza kulipa pale Yerusalemu wakati wa Sikukuu ya Pasaka, maana lazima ilipiwe kwa fedha ya kipekee isiyotumika kila siku, ndiyo sababu wavunja fedha walikuwepo 21:12, ila mwezi kabla ya Pasaka katika maeneo mbalimbali na katika nchi za ng'ambo nafasi ilitolewa kwa watu kulipa.

k.25-26: Yawezekana Yesu alisikia swali likiulizwa nje ya nyumba, na alifahamu Petro alikuwa akiwaza habari hiyo. Yesu alihesabu kwamba kawaida ni kodi hulipwa na waliotawaliwa kwa watawala wao, na mtawala hatozi kodi kwa jamaa zake.
Kodi ya hekalu ni kodi ya Mungu kwa hiyo Mwana wa Mungu hana wajibu
wa kulipa, vilevile wafuasi wake waliofanyiwa kuwa wana, watoto wa Baba, hawana wajibu pia.

Wayahudi walimtumikia Mungu kama watumwa ila wafuasi wa Yesu wamewekwa huru mbali na sheria Gal.4:4-7. Ndani ya habari hiyo bila shaka Yesu alifahamu Kanisa litakuwa Israeli Mpya badala ya Israeli ya kale na watu wake ni Jamii mpya na hekalu la Roho. Ibada na taratibu za kale zitapita atakapofufuka na kusimamisha hekalu la Roho Yoh.2:19-22.

Yesu hakutaka kuleta shida kwa wale ambao bado hawajafahamu ya kuwa kumfuata Yeye ni kuachana na. hekalu na ibada zake na taratibu za mapokeo yao. Hivyo alimwongoza Petro jinsi ya kupata hiyo shekeli moja kwa Yeye na Petro. Hatusikii kwamba kweli Petro alikwenda na kukuta fedha mdomoni mwa samaki ila twaweza kuamini ndivyo ilivyotokea. Huu ni mwujiza wa pekee kati ya yote aliyoifanya Yesu na hasa kwa sababu alifanya kwa ajili yake Mwenyewe na bila shabaha kubwa ya maana.

*MASWALI:*

*Je! kuna wakati wo wote twaweza kupata kumwona Kristo kama amegeuka sura mbele yetu, iwapo si kama ilivyokuwa mlimani kwa wanafunzi wale watatu? Nyakati hizo zina msaada gani?*

*Je! imani na maombi yana sehemu gani katika huduma yako? Katika shirika lako una mpango wa wakristo kuja pamoja kuomba? Utaijengaje imani yao?*

## MAFUNDISHO KUHUSU UHUSIANO WA WANAFUNZI WAO KWA WAO: 18:1-35:

Katika sura ya 18 tunalo fungu kubwa la mafundisho likifungwa na maneno aliyozoea Mathayo kutumia baada ya kila fungu kubwa 19:1. Fungu hilo lahusu uhusiano wa wanafunzi wao kwa wao, Yesu akiwawaza kama shirika maalumu 16:18. Katika shirika nafasi zipo za kusaidiana na kujengana, na za kuumana na kudharauliana. Kwa hiyo jinsi watakavyowawaza na kuwafanya wenzao ni

muhimu, kwa hiyo hapo ni mkusanyo wa tabia zitakikanazo, ni mwongozo kwa maisha yao ya pamoja.

i. **Ukubwa wa kweli** 18:1-5:

Mara kwa mara walijadiliana wao kwa wao kuhusu ni nani atakayekuwa mkubwa wao. Mk.9:33-34; Luka 9:46; 22:24. Yesu ameutaja "ufalme" kwa hiyo Je! vyeo na madaraka vipo? tena kama vipo, vina nguvu na maana gani, ni vya aina gani? Katika dunia vyeo n.k. ni vya maana sana, Je! katika jamii ya Mungu ni vivyo hivyo? Yesu alijibu kwa kupindua kabisa mawazo ya kawaida, pia alijibu kiutendaji kwa kuita mtoto na kumweka katikati yao. Katika Wayahudi watoto hawakuthamanika, walikuwa chini ya mamlaka ya wakubwa walitunzwa ila hawakutazamiwa kitu. Kwa hiyo kugeuzwa kuwa mtoto ni upinduzi mkubwa, mtu akubali kuwa "si kitu" asishindanie ukubwa wale vyeo - ndiyo maana ya "kuongoka" hapo neno hilo halihusika na wokovu kiroho bali laeleza hali ya badiliko kimawazo lililohitajika. Yesu alionyesha "cheo" kwa maana ya mahali pa mtoto si kwa tabia za mtoto, si kwamba tuwe na mambo ya kitoto - la!

k.4 Ukubwa wa kweli ni katika kuwa "mdogo" kuwa "nyuma" kuwa "chini" k.5 "mtoto mmoja mfano wa huo kwa jina langu" ni ye yote aliye mfuasi wa Yesu ambaye amekubali kuwa "mtoto mdogo" ukubwa wao ni katika uhusiano wao na Bwana wao Yesu. Neno hilo ni kubwa na lahitaji kufikiriwa sana na viongozi wa Kanisa wanapowaza "wakristo wa kawaida".

k.6,10,14: "wadogo hao" si watoto tu bali ni neno kueleza wakristo waliokubali kuwa kama "watoto wadogo" wasiotafutia cheo au kuhesabiwa ni wa maana, kwa hiyo katika Ufalme wa Mungu ni wanyenyekevu si wajisukumao ambao ni wakubwa wa kweli. Yeyote aliye mwaminifu kwa "Mfalme" ni wa thamani sana, potelea mbali watu wamemtambua au siyo.

ii. **Vikwazo** 18:6-9:

Kikwazo ni kama kitu kinachowekwa njiani na kumwangusha mtu. Tumeona kwamba ni wale wajionao ni wadogo ambao wamejihesabu ni watoto, ambao Mungu huwathamini sana. Hivyo wengine hupaswa kuwaona kama ambavyo Mungu huwaona na tutahukumiwa kufuatana na tunavyowatendea k.16: 10:40-42 25:31-46 I Yoh.4:20. Mafundisho hayo juu ya kukosesha Paulo alikaza katika nyaraka zake kwa Wakorintho na Rumi I Kor.8:9-13 Rumi 14:13-21 hasa k.15. Ni kosa kubwa kwa wenye nguvu ki-imani kudharau walio dhaifu na kuwaumiza moyoni na kuwafanya wakate tamaa katika kumfuata Kristo. Vikwazo vyaweza kuwa kukosa mzigo, kutokumjali ndugu, kukataa kumsamehe mtu, kudharau n.k. "Wadogo hao" ni sawa na "mtoto" wa k.2. Yesu alitumia lugha hiyo kwa wanafunzi wake 10:42, 11:25; 25:40,45 kwa sababu machoni pa dunia wanafunzi huonekana kama hawana maana, ni wadogo, ni "maskini wa Roho, wanyenyekevu, wateswao" 5:3-12.

Kwa hiyo "wadogo hao" si walio dhaifu wa imani tu, bali ni waamini wote ila hapo Yesu amesema hasa juu ya wadhaifu. Anayemkwaza ndugu kwa hali ya

kumwangalia au kumtendea au hata kwa kutokumsaidia afadhali afe haraka kwa kuzama majini. Hata hivyo vikwazo vitadumu kuwepo ulimwenguni mpaka mwisho na wavileta o watakuwa na hatia.

k.8-9. Maneno kama hayo yapo katika 5:29-30. "Jehanum" "moto" 25:41 10:28. Ni onyo juu ya "dhambi" katika maisha ya Mkristo ambayo itamwangusha mtu. Katika sura hiyo neno linalozungumzwa ni uhusiano wa waamini wao kwa wao kwa hiyo yawezekana maana ni kwamba dhambi katika maisha ya mtu fulani yaweza kusababisha mwingine kuanguka dhambini pia. Kukata mkono n.k. maana yake ni mtu aishi maisha yaliyopungua badala ya kufanya dhambi, ni kushika njia nyembamba, pia yaweza kuwa na maana ya kumtenga mtu katika shirika, asishirikiane naye, au wao waepukane naye. Kwa vyo vyote jambo hilo ni kubwa katika jamii ya watu wa Mungu ambao huitwa kuishi maisha ya pamoja ya kupendana na kujengana kama watoto wa Baba mmoja wenye tabia yake.

iii. **Utunzaji wa "wadogo" 18:10-14**:
Wayahudi waliamini kwamba kila mtu anaye malaika wake mwenyewe, mjumbe wake mbele ya kiti cha Mungu Dan.10:13,20 ku. Ufu. 1:20: Neno hilo si wazi katika Biblia. Kwa Mkristo ni Kristo Mwenyewe aliye mjumbe na mwombezi mbele ya Baba. Ila malaika huwahudumia watu wa Mungu - taz. Ebr. 1:14; Mdo.12:15, Zab.34:7; na 91:11. "huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni" maana yake hata "wadogo hao" waweza kumkaribia Mungu wakati wote ni mboni wa jicho lake. Kila Mkristo huhitaji utunzaji wa ndugu na pia utunzaji wa Mungu ampendaye kila mmoja, ndiyo sababu "mwana kondoo mmoja aliyepotea" ametajwa hapo kuuonyesha mzigo wa Mungu Baba juu ya kila mwamini. Kondoo mmoja akipotea juhudi zote zifanyike kumridisha zizini. Ni rahisi kwa wenye nguvu ya imani kujiona kuwa wana nguvu na kudharau walio dhaifu na kufanya watakavyo bila kuwajali wengine.

**iv. Ndugu kukosana: 18:15-20:**
Iwapo wengi wamefikiri maneno hayo ni kuwasaidia viongozi wa Kanisa katika kuwarudi wakristo wao, lakini maneno "ndugu yako **akikukosa hasa** yamhusu Mkristo mmoja kwa mwenzake. Lengo si kumhukumu na kumrudi mtu ila hasa ni kumwokoa "ndugu" ambayo dhambi yake imemtia hatarini. Ni njia kwa Mkristo kufanya akifuata kielelezo cha Baba kwa kondoo anayepotea. Mkristo asimwachilie katika kosa ambalo ameliona kwake bali aseme naye kwa tumaini kwamba atalitubu ndipo "atampata". Ni kati ya mtu na mtu na wengine hawaingizwi mpaka jambo limeshindikana. Wakikwama basi wawili au watatu waitwe pengine kwa kusaidia maelewano na kumshawishi.

k.7 Mwishowe na kama ni lazima Kanisa liambiwe, jamii wa waamini washirikishwe, shabaha mkosaji awasikilize, neno la adhabu halitajwi, ni kama kumsihi atubu. Kama hamna matokeo mema basi yule Mkristo aliyemwita mwanzoni aepukane naye, ndiyo maana ya "awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru" watu ambao Wayahudi hawakushirikiana nao. Kwa kweli atashindwa kushirikiana naye vema kama amekataa msaada. Kwa hiyo mkosaji

apewe nafasi za kutosha kuonyesha kwamba kosa lake ni la muda, yu tayari kulitubu, kwa sababu wakristo waishi kwa neema si kwa sheria.

18:18-20: Maneno hayo si kwa mtu mmoja "nawaambieni yo yote mtakayofunga .... :." maneno hayo yafanana na yale ambayo Yesu alimwambia Petro 16:19b - mamlaka si kwa Petro peke yake bali kwa jamii ya waamini. Waamini wana haki ya kuamua ni lipi lililo sawa au lisilo sawa kwa Mkristo. Neno la kutokumwachilia ndugu aendelee katika kosa limetoka "mbinguni". Ni "yo yote" ni kuhusu kosa - si "yeyote" iwapo mtu na kosa huandamana, mkazo ni juu ya kosa, si juu ya kumwadhibu au kumsamehe mtu. Mamlaka ya aina hiyo budi itumiwe kwa uangalifu mkubwa na katika huruma.

19-20: "wawili, watatu" wametajwa kama hapo juu, pia jambo la hapo duniani kutiwa sahihi huko mbinguni. "wamekusanya katika Jina langu" idadi si kitu, la maana ni kwamba "wamekutana katika jina la Yesu" yaani wana shabaha ya kutafuta na kufanya mapenzi ya Mungu kwa hiyo Yesu yu kati yao 1:23, 28:20. Hivyo Yesu amewahakikishia Kuwepo Kwake hata wakiwa wawili tu. Bila shaka Yesu alisema hayo kuhusu wale wawili waliokutana kutengeneza kosa k.15-17; ila pia ni ahadi kuhusu wakati wote ambapo wakristo hukutana na kuomba neno lipatanalo na mapenzi ya Mungu.

**v. Kusameheana. 18:21-35:**

Ufalme wa Mungu umejengwa juu ya msamaha, ni waliosamehewa ambao ni raia wake kwa kupitia mlango wa msalaba, mahali walipopatanishwa na Mungu. Kwa hiyo neno la kusameheana ni kubwa kati wa wana wa ufalme.

Marabi walijadili habari ya msamaha na kufikiri mara tatu zatosha kumsamehe mtu. Petro alipotaja mara 7 alipita kawaida ya mawazo ya watu, pengine kwa sababu alifahamu Yesu yu "mkarimu" wa msamaha. Jibu la Yesu liliondoa kabisa neno la "kufanya hesabu" akikataa kuwekwa kwa mpaka. Kwa njia ya mfano Yesu alionyesha msamaha usio na mpaka wala hesabu.

Katika mfano, wa kwanza alikuwa na deni kubwa mno lisilopimika (talanta ilikuwa sarafu iliyo kuu kuliko zote) na elfu kumi tarakimu kubwa kuliko yote katika alfabeti ya Kiyunani. k.32 "deni ile yote" maneno ya kuonyesha ukubwa wake. Hicho ndicho kiasi cha msamaha Mkristo ameupokea kwa Mungu, amesamehewa dhambi zake zote - deni lisilopimika. Kama ni hivyo haiwaziki kwamba Mkristo aliyesamehewa na Mungu ataweka mpaka katika kumsamehe ndugu yake! Tena deni la mwenzake ni "dogo mno" linapolinganishwa na deni alilosamehewa na Mungu, kwa hiyo ni ajabu kumwona akidai haki ya kulipiwa bila kukawia.

Pengine wazo limezuka, ilikuwaje apate kuwa na deni hilo kubwa mno? Yawezekana Yesu amewaza jinsi waziri mkuu alivyokuwa na wajibu wa kutoa kodi ya eneo lake na ombi la kupewa nafasi pengine ni aruhusiwe kuendelea kuikusanya mpaka mwaka kesho. Hata hivyo itikio la Mfalme lilikuwa kuifuta kabisa siyo kuliahirisha, picha ya msamaha kamili wa Mungu msamaha wa bure kutokana na huruma zake k.27.

Jambo jingine katika habari hiyo ni kufikiri jinsi ambavyo Mungu aliye Mtakatifu, asiye na haja ya msamaha huwa tofauti na mwanadamu ambaye daima huhitaji msamaha wa Mungu na pia wa wenzake, ni mwenye dhambi kwa wenye dhambi wenzake.

k.35 Mafundisho ya Yesu ni kwamba asiye tayari kusamehe hawezi kutazamia asamehewe na Mungu. Neno "deni" kwa dhambi limetumika mara kwa mara k.24,28, 30, 32, 34 kama katika Sala ya Bwana 6:12,14-15. Kanisa ni jamii ya waliosamehewa, kwa hiyo kati ya wakristo budi hali ya kusameheana iwepo kiutendaji si katika maneno tu. "kwa mioyo yenu" k.34 maneno hayo yafuta hali ya kuweka mpaka au kufanya hesabu na kuwa na sheria kuhusu msamaha. Tukitambua "ukubwa" wa deni letu kwa Mungu, basi tutaufurahia sana msamaha uliopatikana kwa Yesu kumwaga damu yake. Wala tusingesikia shida kumsamehe watu "makosa madogo" tunayofanyiwa, kwa sababu kwetu ni nia ya kusamehe inayotakikana siyo kumwaga damu, na hata neema ya Mungu ipo ya kutusaidia kutaka kusamehe.

*MASWALI:*

*Katika sura hiyo unyenyekevu na msamaha umekazwa sana. Twaona wanafunzi walisumbuliwa sana na kutaka ukubwa. Je! Kanisa linasumbuliwa na watu wanaotaka ukubwa? dawa yake ni nini?*
*Kwa kuhusu msamaha Je! Utakaza sana jambo hilo kati ya wakristo wako? Utawasaidia kwa njia gani?*

## NJIANI KWENDA YERUSALEMU - 19:I-20:34.

i. **Utangulizi: 19:1-2**

Hapo nyuma tuliona Yesu akiwa angaliko Galilaya akiwatayarisha wanafunzi kwa shindano kubwa la mwisho na wakuu, ambalo mwisho wake ni katika Yeye kukataliwa nao na kuuawa. Sasa katika sehemu hiyo twaona Yesu ameukaribia Yerusalemu, mahali atakapoweka madai yake wazi na kutenda kwa mamlaka ya Ki-Masihi.

Yesu alikuwa amekwenda Yerusalemu mara kwa mara, habari ya safari hizo iko katika Injili ya Yohana, ila Mathayo hakusema juu yake mpaka safari hiyo ya mwisho ..

Yesu alikuja kusini kwa kupitia ng'ambo ya Mto Yordani na kwa kupitia Yeriko 20:29.

**ii. Ndoa na Talaka:** 19:3-12.

Neno la talaka lilijadiliwa sana na marabi. Walikuwepo mashauri wawili waliotofautiana katika mafundisho yao, na kila mmoja alikuwa na wafuasi wake. Mmoja aliitwa Hillel na mwingine wa pili aliitwa Shemmai. Hasa majadiliano

yalikuwa juu ya maana ya "neno ovu" Kumb. 24:1. Hillel alifundisha kwamba hilo "neno ovu" ni "uasherati" tu, huku Shemmai aliona neno ovu laweza kuwa mambo mbalimbali yanayofanya wawili wasiishi vema pamoja, hata kama mama kuunguza chakula!. Yesu alikuwa amekwisha kutoa mawazo yake katika Math.5:31-32. Mafarisayo hawakuwa na nia safi walipomwuliza Yesu habari hiyo, walitaka kumtega si kujua hasa. Walitaka kuona kama amempita Musa kwa ukali. Tukumbuke kwamba talaka haikuwa kama ilivyo leo. Kwanza wakati ule ni mwanamume tu aliye na haki ya kuachana na mkewe, mwanamke hakuwa na haki hiyo. Walitaka kumbana Yesu, akiwa mkali wengi hawatampenda nao watasema amezidi Musa kwa ukali. Akiwa mlegevu watasema hatilii uzito mafunzo ya Kumb.4:1-4. Tumeona kwamba shida ni katika maana ya maneno "neno ovu" sehemu ile ya Kumb. 24 haitoboi wazi maana yake. Tangu dhambi ilipoingia ulimwenguni kwa anguko la Adamu mambo kati ya wanaume na wanawake yalizidi kuharibika, kwa hiyo Musa aliingiza talaka kwa kusudi la kuzuia mambo yasiharibike zaidi, ili waume wasiachane na wake zao bila sababu maalumu. Ilikuwa njia ya kutengeneza siyo ya kulegeza.

Alipojibu Mafarisayo Yesu alirudi nyuma ya ruhusa ya talaka iliyoingizwa na Musa mpaka asili ya ndoa. Mungu alifunua mapenzi yake wakati alipoumba wanadamu wanaume kwa wanawake. Mapenzi hayo ni mwanaume mmoja kuungana na mwanamke mmoja kimwili na mwungano huo kuendelea mpaka kifo. Shabaha iliyowekwa ilikuwa "waambatane" neno la kuzaa watoto na mengine hayakuwekwa. Wawe "mwili mmoja" kwa hiyo kuachana ni kinyume cha mapenzi ya Mungu. Fundisho gumu kwa wanadamu walioanguka. Uhusiano huo hauwekwi katika ibada ya Kanisa bali katika kuungana kwao Mw. 2:24. Mapenzi hayo ya Mungu ni kwa wanadamu wote, ila kwa sababu ya Anguko la Adamu wengi hushindwa, ni Wakristo walio na neema ya Mungu maishani mwao ambao hutazamiwa kutimiza ndoa ya mume mmoja na mke mmoja, ndiyo sababu twaiita "ndoa ya Kikristo" lakini hasa ndoa ni moja potelea mbali iitwaje.

k.7-8: Yesu alikaza Maandiko ya Mw. 2:24, kwa hiyo tayari Mafarisayo wamemnasa akisema wazi msimamo wake. Ila ilikuwa katika Maandiko ya Kumb. 24:1-4 talaka iliruhusiwa. Je! Yesu alikuwa amempinga Musa? Yesu alijibu kwa kuonyesha kwamba ni ugumu wa mioyo ya wanadamu iliyokataa kukubali mapenzi ya Mungu uliomfanya Musa atoe nafasi ya talaka, ila bado kusudi la Mungu limesimama. Yesu alikataa kuweka "ruhusa ya talaka" kuwa sawa na mapenzi ya Mungu ya asili. Maandiko hayapingani ruhusa ni kwa ajili ya udhaifu wa wanadamu, mapenzi ya Mungu yangali yamesimama kwa wale wenye neema ya kuyatimiza. Tena ruhusa ya talaka ni kwa "uasherati" peke yake, kwa uasherati walioungana wamekwisha kuvunja umoja wao wa kimwili. Wanaume walizuiliwa wasiachane na wake zao kwa mambo madogo-madogo.

Kwa talaka taabu za wanawake zilipungua, kwa walioachwa, waume zao walilazimishwa wawakatie hati ya talaka yenye nguvu ya sheria.

k.9 "isipokuwa kwa "uasherati" Kwa uasherati mtu tayari ameivunja ndoa, ameuharibu uhusiano na uambataji wake wa kimwili ambao ndio kiini cha ndoa na mapenzi ya Mungu. Talaka hutambua "uvunjaji" huo. Yesu kwa mafundisho hayo ameunga mkono mafundisho ya Rabi Shemmai kinyume cha Rabi Hillel 5:32.

Mpaka leo ndoa ya Kikristo, talaka, n.k. lasumbua Kanisa na watu huwa na mafundisho tofauti tofauti. Kuna mawili ya kusema kwa uhakika. I. Yesu alitilia mkazo kwamba hali bora ya ndoa ni kwa mume mmoja na mke mmoja kuisha pamoja maisha yao yote, hayo ndiyo mapenzi ya Mungu hasa. 2. Tusisahau "ugumu wa mioyo ya wanadamu" tu wenye dhambi, tu dhaifu sana, kwa hiyo baadhi watashindwa katika ndoa zao, na Kanisa lina wajibu kuwahurumia na kuwasaidia. Wakati wote twapaswa kukaza mapenzi ya Mungu, tusiyabadili, ila pia tuwahurumie walioshindwa.

k. 10-12. Mafundisho hayo ya Yesu yaliwashangaza hata wanafunzi wake. Waliona ni afadhali kutokuoa. Si kwamba waliona kutokuoa ni hali bora kuliko kuoa, la, hali zote zahitaji neema ya Mungu, ila ni itikio lao waliposikia hayo mafundisho magumu. Halafu Yesu alionyesha kwamba wako wasioweza kuoa kutokana na hali ya asili kimwili, na wengine kwa sababu wamejeruhiwa na wengine, na wengine wamejifanya kwa sababu ya wito wa kazi ya Mungu, kwa mfano, walioitwa kwenda mahali pagumu au mbali, na wale wenye shughuli zisizowapa nafasi ya kushughulikia mambo ya unyumba. taz. I Kor. 7:8,32,33. Kwa hiyo kuoa na kutokuoa, hali zote ni kipawa cha Mungu I Kor. 7:1 ku. Hamna sababu yo yote ya kusema "haifai kuoa" I Tim. 4:3.
iii. **Baraka kwa watoto** 19:13-15:
Wayahudi hawakujali watoto, na wanafunzi walifanana na Wayahudi wenzao katika hali hiyo. Huenda waliwaza kwamba Yesu ana mambo makubwa kuyaangalia kuliko kuwashughulikia watoto. Ila Yesu aliwathamini sana, aliwabariki, akihesabu kwamba hao waweza kuwemo katika ufalme wake. Alitoa nafasi, aliwakaribisha na kuwapokea. "Wanafunzi waliwakemea" - walikemea akina nani? watoto? au mama zao? Basi kama waliwakemea watoto wamekuwa tofauti sana na Yesu. Yesu aliyapindua mawazo ya kawaida ya watu "ufalme wa Mungu ni wao" ni kurudia na kukaza neno la "ukubwa" lililozungumzwa 18:1-5 ku. Katika Orodha ya ukubwa ya Yesu wamo wasio na uwezo, wasiopendwa na watu, walio chini - wanawake, watoto, WaMataifa, watoza ushuru n.k. Hao watoto walipata "kibali" chake, na kupewa "thamani" na kuhesabiwa wa "maana". Bila shaka hayo yote ni mafundisho kwa wanafunzi kwa huduma yao baada ya Yeye kuondoka, ni kuwapa "mwongozo" kwa maisha ya Kanisa. Kanisa wakati wote imejitahidi kuwahudumia watoto ..

iv. **Kijana tajiri** 19:16-22 (Mko 10:17-31 Luka 18:18-30).

Wayahudi walifikiri utajiri ni ishara ya baraka za Mungu. Lakini Yesu na wanafunzi wake waliishi maisha magumu ya kutegemea walichopewa. Kwa hiyo uhusiano kati ya "utajiri" na "uanafunzi wa Yesu" ulikuwa neno la maana. Ni kijana aliyemjia Yesu k.20,22. (Luka 18:18 "mkubwa"). Swali lake lilihusu

uzima wa milele, swali la maana sana, wala hakuna sababu ya kufikiri hakuwa wa kweli. Alifikiri ni katika kutenda, **"nifanye** nini?" si katika hali na tabia "niwe mtu wa namna gani?" Pengine alitaka kutenda tendo moja kubwa, la kipekee, la kuvuta kibali cha Mungu. Yeye alitaja jambo jema na Yesu alidaka neno "jema" na kuonyesha ya kuwa utu wema hauwi katika mambo ya wanadamu bali ni katika Mungu, kwa hiyo kuingia uzimani ni katika kuzishika amri za Mungu ambazo ni ufunuo wa tabia ya Yeye aliye Mwema Mkamilifu.

k.18-20: Yesu alitaja zile amri zilizohusu jinsi ya kuwatendea watu "kupenda jirani" na ilikuwa rahisi kupima hayo kwa matendo ya nje ( ila tukumbuke ya kwamba katika 5:21-28 Yesu alionyesha kwamba kushika kwa nje haitoshi). Ndiyo sababu kijana alisema "hayo yote nimeyashika". Amezishika juujuu tu, kwa sababu alisikia kupungukiwa. Yesu hakutaja amri ya kumi kuhusu choyo, na kutamani. Labda kijana aliwaza kwa nini ameiacha hiyo ya kumi? ila hatujui. Yesu alifahamu anayo mali nyingi na anaipenda.

k. 21-22. Yesu aliendelea kwa kutaja "ukamilifu" Ni haki ile izidiyo ile ya Mafarisayo 5:20. Kwa kuchimba chini ya sheria na kupenya mpaka mapenzi na tabia ya Mungu aliye mkamilifu 5:48 mtu hufikia ule "utu wema" wa kweli. Ni wote wanaoitwa kuwa wakamilifu, si wachache tu. Ndipo Yesu alimgusa kijana kwenye kile kilichomtawala, mali imemkamata na kumtawala, kwa hiyo ilidhihirika wazi kwamba kule kuzishika amri kadha hakuwa kitu cha kwanza maishani mwake.

Hakumpenda jirani kwa kutumia mali yake. Alishindwa kuitika wito wa Yesu kutoa mali yake, na Yesu alimwacha aondoke. Hatusikii kwamba alirudi tena. Atawezaje kumfuata Yesu ambaye msingi wa maisha yake ni "bora kutoa kuliko kupata" na kijana amejenga maisha yake juu ya msingi "ni bora kupata kuliko kutoa". Tusitenge mawili aliyoyasema Yesu kwa kijana "enenda ukauze .. wape maskini. .. " "kisha njoo unifuate" Jambo kubwa hasa ni kumfuata Yesu ila kuuza alivyo navyo ni njia ambayo kwayo atawekwa huru ili amfuate. Kuuza alivyo navyo peke yake hakutamfanya kuwa mkamilifu wala kumpatia ule uzima alioutafuta. Ukamilifu una maana ya kutimiza shabaha ya kuishi kwake, na kijana alikataa shauri la Yesu na hivyo alikosa shabaha ya kupata uzima wa milele.

Je! ni lazima tuwe maskini au bila mali ili tumfuate Yesu? 19:26. Kifungu hicho chaonyesha kwamba matajiri waweza kumfuata na baadhi ya wafuasi walikuwa matajiri. Yesu humdai kila mtu tofauti na kila mmoja hutakiwa kumtii katika 10 lote Yesu atakalomwambia.

**19:23-30 Utajiri na thawabu:** Kinyume cha mawazo ya kawaida Yesu alionyesha kwamba utajiri ni kizuizi si msaada kuhusu Ufalme wa Mungu kwa jinsi kijana alivyoshindwa kutoka katika utumwa wa mali. Yesu aliwaambia wanafunzi wazi kwamba ni kazi ngumu kwa tajiri kuuingia ufalme wake. Tena aliuelezea huo ugumu kwa mfano wa ugumu wa ngamia kupenya tundu la sindano! Ila Yesu hakusema "haiwezekani" Zakayo, Yusufu wa Arimathea, Nikodemo na wengine walikuwa wenye mali nao walimtumikia Mungu kwa mali

yao. Walipoyasikia maneno hayo wanafunzi walishangaa sana, wakamwuliza "ni nani basi awezaye kuokoka?" Yesu akawajibu "hakuna, bila uwezo wa Mungu" ni Mungu peke yake awezaye kumsaidia tajiri aachane na mali yake.

Petro alipoona kijana ameondoka kwa huzuni alichukua nafasi hiyo ya kumkumbusha Yesu jinsi yeye na wenzake walivyoacha vyote kwa ajili yake. Yesu hakumkemea kwa kuuliza hivyo bali aliwaahidi heshima ya kipekee na kusema juu ya thawabu watakayoipata. Watashirikiana naye katika kuuhukumu ulimwengu kwa sababu neno lao ni lile la Yesu Mwenyewe. Ila si wao tu watakaopata thawabu kwa kujitoa wote wataushiriki huo uzima wa milele. Waamini wote watajaliwa thawabu ya kiroho.

k.29 Wale watakaoamini baadaye watahesabiwa sawa na walioamini mapema. Ndipo aliwaonya juu ya kujivunia uaminifu wao k.30 I Kor.10:12.

k.28 Mbingu mpya na nchi mpya vitatokea Yesu atakapotokea mara ya pili. Ni onyo kwa Wayahudi wanaokataa neno lake na kwa wale watakalolikataa neno la Mitume litakalohubiriwa mbeleni. Neno litarudi kuwahukumu.

*MASWALI:*

*Kanisa limejaa watu walioshindwa katika ndoa zao. Utatoa mashauri gani kwa vijana wanaotaka kuoana, utawapa mafundisho mapema? kwa wale ambao unafahamu wanayo shida katika ndoa zao utangoja mpaka wameshindwa au utawahi kuwaita na kuwashauri?*

*Waonaje shida ya vijana wengi wasioweza kuoa/kuolewa na yule wa mapenzi kwa sababu ya kiasi cha mahari wazazi wanachodai? Utajiingiza katika mazungumzo yao?*

*Katika makanisa mengi kazi ya Shule ya Jumapili imepoa sana hasa kwa sababu watu hawajitoi kuwa waalimu, na walio tayari hawapati msaada wa mafundisho kwanza. Je! Unathaminije kazi ya Shule ya Jumapili? Je! Umebuni njia nyingine ya kuwasaidia watoto?*

vi. **Mfano wa Walioajiriwa kwa kazi:** 20:1-16.
Watafsiri wa Biblia ya Kiswahili walifanya vizuri walipoweka mfano huu katika aya moja na maneno yaliyotangulia. Maana mfano huo waeleza maana ya neno fupi la Yesu katika 19:30 lililotumiwa tena mwishoni mwa mfano. Angalia "Kwa maana ... " 20:1 na "vivyo hivyo" 20:16. Mfano huu hufundisha juu ya neema ya Mungu ambayo wanadamu hawaistahili. Ni desturi ya watu kutafakari kustahili kwao 19:27 na pia watu hupenda sana kufanya ulinganifu. Lakini Mungu, katika ufalme wake, haangalii kustahili kwetu. Wakulima walitazamia kupokea mishahara mbalimbali kwa kipimo cha masaa ya kazi waliyoifanya, kumbe! walipewa wote mshahara mmoja. Hii ndiyo neema ya
Mungu ambaye alimwahidi mnyang'anyi aliyetubu saa ya mwisho uzima wa milele. Sawa na Petro na Paulo ambao watataabika sana, kwa sababu Mungu huwafanyia watu kulingana na haja yao ya uzima wa milele.

Mungu ni mwema kamili naye huwahesabia haki wote wamjiao. Yesu alikuwa amekwisha kuonyesha kwamba wote waitikiao wito wa kumtumikia na kukubali magumu yatakayowapata watapata thawabu, ila hawana budi kufahamu kwamba thawabu hiyo hutokana na neema yake si kwa kustahili kwao kama Petro alivyofikiri alipomwuliza swali "na sisi tutapata nini?"

Mfano huo unahusu Ufalme wa Mungu, usitumiwe kuhusu watu kuajiriwa na mpango wa malipo kwa wafanyakazi. Neno kuu ni katika wema na ukarimu wa Mungu, na mwajiri katika mfano alifanana na Mungu kwa wema na ukarimu wake kwa jinsi alivyowahurumia wale waliokuwa wamekosa kazi. Alituma watu kufanya kazi shambani zaidi ya alivyohitaji, tena aliwalipa mshahara wa kutwa iwapo baadhi hawakufanya kazi kutwa nzima.

Hao walionung'unika walionyesha wivu, maana walipata haki, walilipiwa kufuatana na patano kati yao na mwajiri, hawakudai wapewe zaidi ila walinung'unika wenzao walipolipiwa sawa na wao, hawakufurahia wema na ukarimu wa mwajiri katika kufanya hivyo. Waliotumwa baadaye hawakufanya patano, walitegemea wema wa mwajiri aliyewahurumia, waliamini atawatendea vizuri. Twajifunza hakuna apokeaye chini ya astahilivyo, ila baadhi hupokea zaidi sana kuliko wastahilivyo, kama mwana mpotevu. Ukarimu waweza kuongezwa juu ya haki.

vii. **Tangazo la tatu kuhusu Kito chake** 20:17-19 (Mko 10: 32-34 Luka 18:31-34)

Hapo Yesu kwa mara ya tatu (16:21 17:22-23) aliwaelezea wanafunzi mengi zaidi kuhusu mateso yatakayompata kwa Wayahudi ambao watamhukumu barazani na kumkataa rasmi kuwa Masihi wao, nao watamtia mikononi mwa Wamataifa, liwali na maaskari wa Kirumi, nao pia watamkataa wakimpiga na kumsulibisha. Kwa hiyo Yesu alitoboa wazi zaidi juu ya aina ya mateso na kuuawa kwake kwa kusulibishwa. Hatakufa kama mfia dini bali atakufa katika aibu mkubwa na kwa maumivu makali mno. Ila ajabu ni kwamba siku ya tatu atafufuka.

Maneno "angalieni tunapanda kwenda Yerusalemu" si taarifa kwa wanafunzi, maana walifahamu wanakwenda Yerusalemu ila ni thibitisho la nia yake kukazwa kwenda, na dalili ya vita yake ya ndani, maana ni vigumu aende kwa sababu alifahamu kikamilifu yote yatakayompata huko.

viii. **Ombi la Mama wa Yakobo na Yohana - jibu la Yesu kuhusu ukubwa katika utumishi** 20:20-28 (Mk.10:35ku Luka 22:24ku). Iwapo Mathayo amesema ni mama aliyemwomba Yesu, ndugu hao walishirikiana naye k.20,22; wanafunzi kumi waliwakasirikia hao ndugu si mama yao k.24.
Mara Yesu alisema juu ya mateso si heshima. Katika ufalme wake mateso hutangulia utukufu Ru. 8:17. "Kikombe" "ubatizo" Mk.10:38 ni lugha ya
kueleza mateso. Baadaye hakika watakinywea kikombe - Yakobo aliuawa na Herode Agripa wa kwanza Mdo. 12:2. Katika uzee wake Yohana alifukuzwa mpaka Patmo Uf. 1:9. Ila ni Baba atakayewapa watu viti vya heshima, wao

hawapaswi kuviwaza. Ndipo Yesu aliwaita Kwake wanafunzi wote, k.25; maana wote walikuwa na tabia ya kuwaza ukubwa, akawafundisha tena juu ya ukubwa wa kweli. Huo ukubwa katika ufalme wake ni tofauti sana na wa dunia hii. k.26. Wao wote huitwa kutumika, wala hamna wa kutumikiwa. Wafuate kielelezo chake. Upeo wa Yesu katika kututumikia ni Yeye kutoa maisha yake mpaka kifo, kifo cha kufidia, kifo cha kuwa badala yetu na kuwa mahali petu, kifo kwa dhambi zetu, kifo cha ukombozi Neno "fidia" kwa Kiyunani hupatikana hapo tu katika Agano Jipya lote, ila liko neno katika I Tim. 2:6 lililotafsiriwa "ukombozi" lililo karibu na hilo "fidia".

Katika maisha yake vote Yesu alikuwa akiwatumikia wanadamu, na kufa kwa ajili yao ni upeo wa maisha hayo. Atafanya lile asiloweza mwanadamu awaye vote kufanya kwa ajili ya ndugu yake Zab.49:7.naye atafanya kwa wengi. Alipozaliwa alipewa jina la Yesu maana yake "atawaokoa watu na dhambi zao" 1:21; karibuni hivi atatimiza neno hilo. Baadaye Mitume walipoeleza maana ya kifo chake walisema kilikuwa kwa ajili yetu, akichukua mahali petu, dhambi zetu na kuadhibiwa badala yetu. I Yoh.2:2 I Petro 2:24,3:18 Ga1.3:13 Rum.3:25.

Iwapo Yesu yu karibu na kuuawa na kuwaacha ni wazi kwamba wanafunzi bado hawajaelewa vizuri aina ya Umasihi wake, ilimbidi achukuliane nao na kuwafundisha kila wakati, maana hadi usiku wa mwisho waligombana wao kwa wao juu ya ukubwa Luka 22:24.

ix**. Vipofu wawili 20:29-34** (Mk.10:46ku Luka 18:35ku).

Marko na Luka wametaja kipofu mmoja tu na Marko alisema jina lake aliitwa Bartimayo. Kwa nini Mathayo ametaja kwamba walikuwa wawili. Wataalamu hufikiri kwamba wawili waliponywa ambaye mmoja alikuwa Bartimayo aliyejulikana na Petro na ndiyo sababu Marko na Luka walimtaja huyo mmoja iwapo ni wawili walioponywa. Kwa kumwita "Mwana wa Daudi" walionyesha kuwa wamemkubali kuwa Masihi na Mfalme wa nyumba ya Daudi. Kwa nini Yesu aliwauliza "mnataka niwafanyie nini?" Yawezekana alitaka waukiri wazi Umasihi wake hadharani mwa watu. Karibuni hivi atakapoanza kuingia Yerusalemu umati wa watu watamshangilia hivyo naye hatawakemea. Pia Mungu hufahamu mahitaji yetu kabla ya sisi kumwambia, ila apenda kutufanyia mema kama jibu la maombi yetu; na kutuvuta kuwa watu wapendao kumwomba ili ushirikiano wetu na Yeye ujengwe.

Kwa kuwagusa machoni Yesu alionyesha huruma zake kwao. Bila shaka walifurahi sana walipomwona Yeye aliyewapona mara baada ya kuguswa, wakamfuata bila kukawia.

k.31-34. Twaona ya kuwa hata katika kuitwa Masihi angali tayari kuwatumikia hao vipofu, iwapo mkutano wa watu waliona si heshima afanye hivyo. Yesu alipindua mawazo ya kawaida ya watu. Wao waliona ni aibu kwa Masihi wao kucheleweshwa na vipofu hao waombaji. Ila Yesu aliwajali, alisimama, akawaita waje Kwake, si rahisi hali amezungukwa na umati wa watu. Alitawaliwa na huruma kwa wengine, iwapo ingalikuwa rahisi ashikwe na mawazo ya kujihurumia akitafakari mateso yaliyo karibu kumpata na mashindano na

wakuu, na udhaifu wa wanafunzi watakaomwacha saa ya dhiki kuu.
Uzuri ni kwamba vipofu hawakuwajali wale watu, walikataa kunyamaza, walikazana kupata kile walichotaka, yaani kuona. Ni akina nani walio vipofu? si umati wa watu wasiomtambua Yesu vema.

*MASWALI:*
*Yesu aliwafundisha wanafunzi wake mambo gani kwa kutaja "kikombe" na kuhusu "ukubwa". Ilimbidi Yesu arudie-rudie mambo fulani kwa wanafunzi, dalili ya kuwa mengine hawakuweza kupokea mara. Je! sisi nasi twahitaji kujifunza nini tena na tena? Vilevile inatusaidia kuelewa kwamba wakristo wetu watahitaji kuambiwa mengine tena na tena. Je! Wajikuta kwamba unachoka na watu wasioelewa mambo? Na unafanya nini kwa ajili yao?*

## KUFIKA YERUSALEMU 21: 1-22.

**i. Kuingia Mjini** 21:1-11 (Mk. 11:1-11, Luk. 19:28ku Yoh.12:12ku)

Tumeona ya kuwa Mathayo ametutayarisha kwa habari hiyo tangu 16:21. Hakutaja hapo nyuma habari za Yesu kuwa Yerusalemu iwapo katika 23:37 na 26:55 amedokeza hivyo. Ni Yohana katika Injili yake ambaye ametaja Yesu kuwa Yerusalemu mara kwa mara.

Yesu na wanafunzi hawakuja peke yao. Kwa kuwa Sikukuu ya Pasaka ilikuwa karibu wengi kutoka mahali mbalimbali walisafiri mpaka Yerusalemu kwa kuiadhimisha, na picha tuliyo nayo ya tuliyo nayo ni ya wengi kusafiri kutoka Galilaya.

Yesu alifanya kila jambo kwa kusudi maalumu ya kuwapa watu nafasi ya kumpokea kama Masihi wao. Atakapofika Yerusalemu itambidi apambane na wakuu wa taifa wasio tayari kukubali madai yake. Aliingia kama Mfalme wa Israeli ambaye manabii walitangaza habari zake. Kweli enzi yake haionekani wazi, hana mapambo ya nje ya Kifalme, hakupanda farasi kama Mfalme na Jemadari Mkuu apiganaye vita kama wafalme wa dunia hii.

Hakuja kama walivyomtazamia - Ye ye ni Mfalme mnyenyekevu. Ametembea kwa miguu kutoka Galilaya, hakuwa na haja ya kupanda punda, ilibaki maili mbili tu mpaka mjini! Alipanda punda kwa kusudi la kuutimiza unabii wa Zakaria aliyemwambia Binti Sayuni afurahi maana Mfalme wake amekuja kwake mwenye haki na wokovu. Yawezekana alipanga na mtu ili punda awe tayari, na kama hakupanga alifahamu watamkuta punda pale.

Walimletea mama punda na mtoto pamoja. Marko 11:2 na Luka 19:33 walitaja mwana punda tu. Yesu alipanda mwana punda ambaye alikuwa hajapandwa bado, (punda atatulia kwa mama kuwa pamoja naye) k4-5:
Yawezekana Yesu alitamka maneno hayo kwa wanafunzi. Kwa vyo vyote Mathayo anataka kukaza ya kuwa Yesu aliingia Yerusalemu kama Masihi aliyeahidiwa katika Maandiko Is.62:11 Zak. 9:9-10.

Wanafunzi walitandika wanyama nguo zao kwa kumheshimu Yesu na watu walitandaza nguo zao njiani na kukata matawi ya mitende wakimshangilia na kumpokea. Watu walikuwa wengi sio wachache, wakiwa na msisimko wa kutazamia makuu yatatokea atakapofika Yerusalemu, bila shaka walikuwa tayari kuipindua serikali. Walipaza sauti wakisema kwa sifa "Hosana, Mwana wa Daudi.." Hosana, maana yake "Utuokoe" Zab.1I8:25-26. Walipofika mjini, mji wote ulitaharuki, bila shaka watu walishikwa na mawazo mbalimbali, wasiwasi, dharau, chuki, n.k. wakiwa na matazamio mbalimbali, wasijui mwisho wa mambo hayo yatakuwa nini.

Kwa hiyo Yesu aliingia Yerusalemu hali ya kuonekana wazi pamoja na umati wa watu walioandamana naye hali wamemkubali kwa kitambo kama nabii 21:46. Wakuu hawataweza kumwepa, ama wamkubali au wamkatae –
mambo yameiva - ni juu yao ni nafasi yao.

ii. **Kutakasa hekalu** 21:12-17 (Mko 11:15-19 Luka 19:45-46)
Tendo hilo lilikuwa la maana kubwa, likifuata tendo maalumu la Yesu kuingia Yerusalemu katika hali ya kudai kutawazwa kuwa Masihi wao. Hekalu lilikuwa mahali pa kwanza katika maisha ya taifa. Alifanya kwa kusudi akijiingiza katikati ya shughuli zao na kuonyesha kwamba Ufalme wa Mungu umeletwa karibu nao kwa njia yake. Malaki alitaja kwamba Mjumbe atalijia hekalu kwa shabaha ya kuitakasa ibada MaI. 3:1-5. Zakaria pia aliahidi siku ambayo hamtakuwepo mfanyi biashara nyumbani mwa Bwana wa Majeshi - Zak. 14:21. Katika maono ya Ezekieli, Ez. 40 - 48 na Zek. 6:12-13 lilitajwa tazamio la Masihi kuleta uamsho wa kutakasa hekalu ambalo zamani lilitiwa unajisi na watawala wa kipagani, pia kutengeneza ibada zisizo kweli ya watu wa Mungu.

Kwa hiyo Yesu aliamsha matumaini mengi alipolitenda tendo hilo. Alionyesha mamlaka yake ya Ki-Masihi maana hakuomba ruksa ya wakuu wala kuomba radhi. Pia kwa tendo hilo alihukumu ibada za wakati ule.

Marko alisema usiku mmoja ulipita kabla ya Yesu kufanya jambo hilo. Mk. 11:11,15. Kwa hiyo ni wazi Yesu hakufanya kwa hasira ya mara moja ila kwa nia na kwa kusudi.

Lilitokea katika Ua la Wamataifa, ua kubwa lililozunguka hekalu lenyewe, mahali ambapo soko la kuuza wanyama kwa dhabihu lilikuwepo pamoja na mahali pa kubadili pesa, sarafu za kipekee zilitumika badala ya za kawaida. Hayo yote yaliwasaidia watu hasa waliotoka mbali, wasiwe na haja ya kuleta wanyama pamoja nao.

Hasa kitu kilichomkasirisha Yesu ni jinsi wakuu wa hekalu walivyoruhusu jambo hilo kuwa "biashara kubwa" Inaonekana Yesu ameona mkazo umezidi kuhusu utoaji wa dhabihu za wanyama. Pia yawezekana dhuluma imeingia, watu wakitozwa gharama kubwa - ila ni vema tuone ya kuwa Yesu alitoa wanunuzi pamoja na wauzaji.

Wakuu wamekubali hayo yote yatendeke katika Ua la Hekalu. Ni dhahiri kwamba Yesu kwa tendo hilo alijiweka juu ya wakuu hao na kudai haki ya kuhukumu taratibu ya ibada za kidhabihu, iwapo taratibu hiyo ilikuwa na asili katika Maandiko ni kama Yesu amehesabu kwamba imezidi hata isikubaliwe na Mungu. Hapo amedai haki ya Ki-Masihi, kweli Yeye Ndiye ni mkuu kuliko Hekalu 12:6.

k.13 "Nyumba yangu itaitwa nyumba ya Sala" Is.56:7 Mungu aliahidi kuwa wageni na Wamataifa watapata nafasi ya kumwabudu Mungu pamoja na watu wake, na biashara hiyo imewazuia nafasi hiyo.

Daudi aliamuru vipofu na vilema wasikaribishwe katika nyumba ya Mungu 2 Sam. 5:8, lakini Yesu, "Mwana wa Daudi" aliwapokea na kuwaponya.
k.15-16: watoto waliendeleza sifa walizozisikia kwa wengi k.9. Wakuu walikubali kelele za biashara huku wasizipende sifa za watoto. Makuhani wakuu walijiunga na waandishi kumwendea Yesu na kumkemea. Kawaida ilikuwa kwa Mafarisayo na waandishi kumpinga, ila sasa Yesu ameingia kiwanja cha Makuhani nao wakampinga pia. Yesu aliwatetea watoto akitumia maneno ya Zab.8:2 yaliyosema juu ya sifa za Mungu Je! alikuwa akidai kuwa Mungu siye Masihi tu? Alionyesha kwamba sifa za watoto ni hukumu kwa wakuu wa dini.

k.7. Katika juma la Pasaka wengi walipaswa kujitafutia malazi nje ya mji na Yesu na wanafunzi vilevile Luka 22:39.

iii. **Mtini kulaaniwa na mafunzo juu yake:** 21:18-22 (Mko 11: 12-14, 20-25).

Kulitakasa hekalu lilikuwa tendo la ishara la kuhukumu ibada ya Israeli vivyo hivyo kukausha mtini lilikuwa tendo la ishara la kuhukumu taifa la Israeli, taifa teule. Vote mawili yakaza jambo moja, bila kuzaa matunda ya ibada ya kweli yote ni bure!

Ule mtini ulionekana wa kufaa kuridhisha njaa yake, vivyo hivyo Israeli lilionekana kama litatimiza lile ambalo Mungu alilokusudia katika kuliteua. Kwa nje dini ilisitawi sana, ibada, sikukuu, sheria, zote zilishughulikiwa vya kutosha, lilionekana lina afya tele. Kumbe, sivyo ilivyo, li katika hali ya kufa, limepoteza shabaha ya kweli, yote yafanyika bila upendo wa kweli wa ndani kwa Mungu 15:1 ku. Waliteuliwa ili Masihi atakapokuja apokelewe kwa mikono miwili, kumbe tayari wakuu wamempinga, na karibuni hivi watamwua - linalowabakia ni hukumu. Matunda waliyotakiwa kuzaa hawazai, kwa hiyo hukumu itakayowapata yalingana na kosa lao, hawatazaa tena, nafasi ya kuieneza Injili itapewa "Israeli Mpya" yaani Kanisa, jamii mpya ya watu wa Mungu.

Wanafunzi walishangaa nguvu ya maneno ya Yesu na jinsi mtini ulivyokauka mara. Walipomwuliza sababu waliambiwa kwamba katika ulimwengu wa kiroho "wakati" hauwi kama hapa duniani. Kwa njia ya imani na kuomba makubwa yatatokea wasiyotazamia, watashinda "milima" yaani shida kubwa 17:20.

Katika habari hiyo mambo ambayo Yesu alitaka kuyakaza kwa wanafunzi ni imani na maombi, kwa sababu kwa Mungu hakuna lisilowezekana. Imani

inayotakiwa ni ile ya kumwamini na kujikabidhi kwa yule wanayemwomba. 8:10;12,22,29; 15:28.

## MASHINDANO KATI YA YESU NA WAKUU 21:23-23:39.

i. **Swali kuhusu Mamlaka yake:** 21: 23 - 27:

Bila shaka hayo yote yaliyotokea yaliwapa wakuu wasiwasi nyingi - hao wakuu wameelezwa kuwa wakuu wa makuhani na waandishi k.15 na wazee wa watu k.23, Mafarisayo k.21 na 22:34,41. Maherode wametajwa 22:15-16 na Masadukayo 22:23. Vikundi hivi mbalimbali wenye uongozi katika mambo mbalimbali walitofautiana wao kwa wao ila katika kumpinga Yesu walijiunga pamoja.

Yesu amefanya makubwa bila idhini yao, amewashambulia penye enzi yao - ameingia Yerusalemu akizipokea sifa za KiMasihi, akajiingiza kwa nguvu katika shughuli za kawaida za hekalu, humo hekaluni alizikubali sifa za watoto akiwatetea, pamoja na kuwaponywa vipofu na vilema. Kwa hiyo si ajabu viongozi walipomkuta akiwafundisha watu hekaluni wakamwendea na kumwuliza juu ya amri ya kufanya hayo yote.

Yesu hakuwajibu moja kwa moja ila aliwauliza swali, nao watapata jibu la swali lao watakapolijibu swali lake. Hakufanya kwa ujanja maana kazi ya Yohana na kazi yake ziliingiliana, na aliyemtuma Yohana ndiye aliyemtuma Yeye. Yohana alimtangaza Yesu kuwa "yule ajaye" kwa hiyo wakiupokea ushuhuda wa Yohana kweli watampokea Yesu.

Si kama hawakujua asili ya "ubatizo wa Yohana" ila shida yao ni kwamba hawakukubali ametumwa na Mungu - Luka 7:29,30, kwa hiyo walijibu kwa werevu wasitake kunaswa. Lakini katika kukataa kujibu swali la Yesu walionyesha kuwa hawana haki ya kumwuliza tena juu ya mamlaka yake. Walikuwa wakienda kinyume cha mawazo ya watu waliomwona Yohana kuwa nabii, na hata Yesu pia 21:26, 46 na 22:33.

Yesu aliwashinda naye akaendelea kuwashambulia katika mifano mitatu ifuatayo iliyowasema.

ii. **Mifano mitatu:** Wana wawili, Shamba la Mizabibu, na Arusi ya Mwana wa Mfalme: 21:28 - 22:14.

Mfano wa wana wawili: 21: 28 - 32.

Mfano huo ni wazi na rahisi na fundisho lake ni dhahiri. Ya maana si ahadi ya mtu bali utendaji wake. Neno ambalo tumeliona mara kwa mara katika mafundisho ya Yesu.

Yesu aliwalenga wakuu akiwapambanisha na watoza ushuru na wenye dhambi, ambao hao wakuu waliwadharau na kuwahesabu kuwa mbali na Mungu. Bila shaka kuna ukumbusho jinsi Yesu alivyowapokea 9:9-13 na jinsi wakuu walivyochukizwa. Katika Luka 15 iko mifano mingine inayotoa mafundisho yayo hayo pia iliyosababishwa na hali hiyo 15:1-2.

Yohana alipohubiri ujumbe wa toba na kufanya haki hao watoza ushuru na wenye dhambi waliupokea ujumbe wake na kuuitika wito wake wa kutubu na kubatizwa, tofauti na wakuu Luka 7:29.30. Wakuu walishindwa kumtambua Yohana, hata walipoona mabadiliko katika maisha ya hao wengine hawakutubu wala kuamini. Wote wapaswa kutubu na kumwamini Kristo wakitaka kuingia ufalme wake.

Kwa hiyo Yesu alijiweka pamoja na Yohana tena kama alivyofanya katika swali lililotangulia, wakimwamini Yohana watampokea Yeye.
Shamba la Mizabibu: 21:33-46 (Mko 12:1-12; Luka 20:9-19)
k.33 Mfano huu ulifuata mara ule wa wana wawili. Shamba ni Israeli - Is.5:1-2; Mwenye shamba ni Mungu Mwenyewe Zab.80ku Yer. 2:28; Ez. 19:10 ku.
Wakulima ni viongozi wa Israeli, na waliotumwa kupata mazao ni manabii. Mwana wa Mwenye shamba ni Yesu, Masihi.

Yesu alionyesha kwamba alijifahamu kabisa kwamba Yeye ndiye Mwana wa Mungu mwenye shamba na ya kuwa atakataliwa na wakulima na kusulibishwa. Kabla yake manabii walitumwa na Baba yake, nao wakakataliwa na wakulima. Yeye ni wa mwisho katika mfuatano huo, ila Yeye ni tofauti nao maana Yeye ni Mwana na wao walikuwa watumishi waliotumwa na Baba. Kwa hiyo Yesu alidai kuwa Mwana wa Mungu, hawana udhuru maana Mwana anaye mamlaka yote ya Baba. Ebr.1:1-2.

k.38 Ujinga wao ni katika kufikiri kwamba wakimwua Mwana watalirithi shamba, Mwenye shamba angaliko!! kwa hiyo atafanya nini?

k.40-41 Kwa njia ya kuwauliza swali alivuta wapinzani wake wautoe uamuzi wao ambao ndiyo hukumu juu yao wenyewe. Nabii Nathani alitumia njia hiyo kwa Daudi 2 Sam.12:1-7.

k.42 Jiwe lililokataliwa ni Yesu. Katika Zab.118:22-23 jiwe lilikuwa Israeli, kila wakati Mungu aliwaokoa na adui zao, lakini Yesu alijichukulia Kwake neno "jiwe" maana Yeye binafsi ni Israeli wa Kweli akifanya mapenzi ya Mungu kwa ukamilifu. Atakapokataliwa na watu Mungu atamwokoa, atamfufua katika wafu na kumwadhimisha juu na kumweka kuwa Jiwe Kuu katika hekalu, ambalo ni mwili wake, kwa njia yake Mungu ataabudiwa katika Roho na kweli Mdo. 4:11, I Petro 2:4,7 Yoh. 4:24; 2:19; 14:6. Hapo Yesu ametabiri kufufuka na kupaa kwake - jambo la ajabu k. 42b.

k. 43 Yesu alitoa uamuzi mzito, litatokea taifa lingine, watu wapya wa Mungu. Ufalme wa Mungu utaondolewa kwa taifa la Israeli na kupewa wengine I Pet.2:9. Mungu atatekeleza makusudi yake kwa njia ya taifa jipya - taifa hilo si taifa moja fulani, bali ni "taifa" la mmoja mmoja kutoka mataifa yote ambao watampa Yesu utiifu wao ila wapaswa kuzaa matunda Msingi ni katika kuzaliwa upya, kiroho, si kuzaliwa Myahudi kama hapo nyuma. Bila shaka neno hilo liliwakwaza sana, kwanza kwa sababu wataondolewa shamba, na pili wengine watapewa. k.45-46 Wakuu walitambua ya kuwa mfano umewasema, ila badala ya kujihoji na kuwaza "mwisho" wao waliendelea kuufuliza mpango wa

kumwondoa ila shida moja ni watu, itawabidi watafute njia ya kuwavuta upande wao, wasipofaulu hawana budi kufanya kwa chinichini na kwa hila.

Arusi ya Mwana wa Mfalme: 22:1-14 (Ling. na Luka 14:16-24 unaofanana kwa mengine na kutofautiana kwa mengine). Tumeona ya kuwa mfano uliotangulia ulisema juu ya upungufu wa Wayahudi na kwa sababu hiyo wengine watawekwa badala yao. Karamu ya Arusi ni ishara ya baraka za Mungu 8:11. 25:1 ku. Ling. na Is.61:10, 62:5 Uf.21:27. Arusi ni picha iliyotumiwa kwa ushirikiano kati ya Masihi na watu wake. Walioitwa wamekwisha kuupokea mwaliko na kuuitika wito wa kuhudhuria.
Baadaye walipashwa habari tena juu ya saa ya karamu k.3-4. wito wa pili. Kwa hiyo walikwenda kinyume cha ahadi - ling. na mwana katika 21:30, na waliopangwa shamba 21:35-36.

Waalikwa hao si walio nje, ni wapenda dini, ila walithamini shamba na biashara kuliko Mungu - ni kama Yesu alivyosema haiwezekani kumtumikia Mungu na mali 6:24.

6-7: Ni utabiri wa Anguko la Yerusalemu kama hukumu ya Mungu kwa uasi wa Israeli, nalo lilitokea BK.70.

k.8-10: Jambo la wengine wasiotazamiwa kuchukua nafasi ya wateule walioitwa limekwisha kuonekana katika mifano miwili iliyotangulia 21:31-32 na 41:33. Na Injili itakapohubiriwa kwa wengi zaidi itawavuta wema kwa wabaya, nalo ni tatizo.

k. 11-13.Vazi la arusi huenda si vazi la pekee ila ni nguo safi, pengine nyeupe, ambayo watu walizoea kuvaa wakati maalum. Kuja katika nguo chafu kulimwaibisha sana mwenye karamu. Ni wajibu wa aliyealikwa kuvaa vizuri.

Fundisho ni kwamba wokovu ni bure kwa kila mtu ila ni wa kuthamaniwa si wa kudharauliwa au kuchezewa, eti ni bure! kwa kuwa Kristo alimwaga damu yake ili atuokoe. Vazi la Arusi ni maisha mapya, 7:13-27, Is.61:10, Uf.21:27:

Ni hukumu ya mwisho itakayoonyesha walio wageni wa kweli. k.14: Wote waliitwa ila ni wachache walioitika wito na kuwa katika kundi la "wateule".

Kwa hiyo Yesu katika mifano hiyo mitatu ameonyesha ya kuwa hawatazuia mapenzi ya Mungu kwa njia ya kukataa kwenda shambani kama mwana wa kwanza, wala kwa kumwua "Mwana" aliyetumwa kwa mazao, wala kwa kukataa mwaliko wa kuja karamuni. Mungu atawafungulia wengine nafasi na Ufalme wake hautakosa kujaa wageni wa kila aina. Ila iliyopo ni kwamba wote waingiao budi wavae vazi la arusi, wafanane na mwana wa pili ambaye baadaye alikwenda shambani, na wapangaji wapya watakaleta mazao. Kwa hiyo mifano yote miwili iliingiliana.

Injili itahubiriwa kwa WaMataifa baada ya Wayahudi kupewa nafasi ya kwanza 22:15-46 (Mk.12:13-37 Luka 20:20-44) Mfululizo wa Maswali. (Kuhusu kodi - Ufufuo wa wafu - Amri kuu - Masihi)

iii. **Swali la kuhusu kodi** 22:15-22.
Wakuu mbalimbali walitumia njia ya maswali ya hila ili wapate kumshinda Yesu ambaye amewashambulia na mifano mitatu juu yao.

Kwanza Mafarisayo, viongozi wa dini walijiunga na Maherode, viongozi wa siasa, kwa kawaida hawakupatana. Pia waliuliza swali kuhusu kumpa Kaisari kodi - swali lililojadiliwa sana na Wayahudi ambao kamwe hawakupenda kutoa kodi, hawakuona ni halali kwa wateule wa Mungu kutoa kodi kwa Kaisari mpagani.
Walihesabu ni kinyume cha sheria ya Mungu. Hata hivyo wamekubali kwa kuitumia sarafu ya fedha yenye sanamu na anwani yake. Nyakati zile po pote ambapo fedha zenye sanamu ya mtawala fulani zilitumiwa ilihesabiwa wa Herode Mfalme aliyewekwa na Warumi walikubali kodi ilipiwe, ila Mafarisayo kwa ndani hawakupenda. Katika chuki yao kubwa kwa Yesu walijiunga na Maherode ili wamnase Yesu na kupata neno la kumshtaki, ndiyo hila yao.

Walimjia Yesu kwa upole na kwa kumpaka mafuta! k.l6 ila Yesu aliwajibu kwa ukali k.18. Aliutambua unafiki na hila yao wamejifanya kuwa rafiki ambao wamheshimu, kumbe sivyo, na swali lao ni la hatari kabisa. Walidhani kwa jinsi walivyotunga swali itambidi Yesu ajibu "ndiyo" au "siyo". Kwa "ndiyo" watamnasa na kwa "siyo" watamnasa. Akijibu ni halali kumpa Kaisari kodi Mafarisayo wataweza kumsema kwa watu ambao wangali wakimpenda na kugeuza mawazo yao wakionyesha ya kuwa Yesu hafai kuwa Masihi wao, atapinduaje serikali ikiwa amekubali kodi ilipwe?!! Kwa njia hiyo watawaondoa watu kwa Yesu. Maherode wasingekuwa na shida yo yote kwa kulisikia jibu hilo.

Akijibu si halali, iwapo kwa ndani Mafarisayo watafurahi, kwa nje watakuwa wamepata neno kamili la kumshtaki kwa liwali. Na kwa vyovyote Maherode watamshtaki. Ndiyo hila yao kwa kuja pamoja, makundi mawili yaliyo tofauti. Lakini Yesu hakudanganywa nao wala kuwaogopa. Akatoa jibu kamili lenye kugusa eneo lote la maisha ya mtu, si eneo la uhusiano wake na serikali tu. Hakujibu moja kwa moja ila aliwaomba wamletee sarafu ya fedha, nao wakamletea dinari yenye sanamu na anwani ya Kaisari. Wao wenyewe wameukubali utawala wa Kaisari kwa kuitumia fedha hiyo. Kisha akawaambia "mlipeni Kaisari iliyo yake" maana yake mlipeni kodi - neno "Lipeni" ni neno la kuonyesha wana wajibu kufanya hivyo, ni kama deni kwake kwa baraka zipatikanazo kwa utawala wake. Ila Yesu hakusimama kwa Kaisari, akaendelea "na mlipeni Mungu iliyo yake" maana wanadamu wameumbwa katika sura na mfano wa Mungu, ni mali yake, ni wajibu wao, ni kama deni lao, la kutoa maisha yao yote kwa Mungu kwa baraka zote za maisha, kwa uhai na kila kitu. Wanadamu huishi duniani chini ya enzi fulani, pia wanadamu ni raia wa Ufalme wa Mungu, kwa hiyo wana wajibu kwa sehemu zote mbili na utiifu wa serikali ni sehemu katika utiifu mzima kwa Mungu. Ru.13:1-7 I Pe.2:13-17. Ingawa Yesu alijibu hivi, alipohukumiwa walimshtaki kwa liwali kwamba aliwafundisha watu wasilipe kodi! Luk. 23:2.

iv. **Swali kuhusu Ufufuo wa Wafu:** 22:23-33:
Inaonekana Masadukayo walimjia Yesu na swali lao siku ileile baada ya Mafarisayo na Maherode kumwuliza swali lao la kodi. Shabaha ya Masadukayo ilikuwa kumfanya Yesu aonekana kuwa si mtaalamu wa theologia na kuonyesha jinsi isivyowezekana kuamini neno la Ufufuo wa wafu kama Mafarisayo walivyoamini. Walitunga swali ambalo walidhani litalipuuza neno la ufufuo. Ila msingi wa kuwaza kwao haukuwa wa kweli. Waliwaza kwamba lipo la kimwili tu, kwa hiyo kama upo ufufuo wa aina yo yote hali za hapo, za kimwili, zitakuwepo. Na kama ni hivyo swali lao "atakuwa mke wa yupi?" lingefaa, maana katika siku ya ufufuo waume saba wangekuwepo mbele yake!! Ila swali halipo kwa sababu ulimwengu ujao ni wa kiroho si wa kimwili. Neno ambalo Masadukayo hawakuwa tayari kulipokea Mdo.23:8.

Yesu alikataa mawazo yao, aliyaona kuwa yanayapinga Maandiko na kumbana Mungu na uwezo wake.

Masadukayo walithamini vitabu vitano vya kwanza vya Musa na mfano waliouleta ulitoka Kumb. 25:5-6. Yesu alikubali kwamba desturi hii ipo kwa sababu mauti hutokea na wanadamu huendelea kuwepo kwa njia ya watoto kuzaliwa. Ila katika ulimwengu ujao mauti haipo, watu huishi milele, hakuna haja ya kuendeleza kuwepo kwa wanadamu, wala hakuna haja ya kuzidisha uzao wa wanadamu. Uzima wa milele utatofautiana sana na maisha ya hapo duniani, si maendeleo ya maisha ya hapo, kwa hiyo uhusiano wa kipekee wa mume na mke katika kuzaa watoto hautakikani. Sio kusema hatutashirikiana na wale ambao tumewapenda ila ushirikiano wetu utakuwa tofauti, utakuwa wa hali ya kuruhusu waliooa au kuolewa mara mbili na zaidi kushirikiana kwa kiroho si kimwili.

Kwa kusema "Mimi ni Mungu wa Ibrahimu na Isaka na Yakobo" Kut.3:6 Mungu alithibitisha kwamba uhusiano wake nao ungali unaendelea iwapo hao wamekufa zamani kabla ya Yeye kusema maneno hayo kwa Musa. Ni vigumu kufikiri kwamba Mungu aliye hai aliyeanzisha ushirikiano nao utaukomesha mara watakapofariki dunia.

Bila shaka Masadukayo waliaibika kwa jibu hilo, wakanyamaza! ila watu walishangaa mafundisho ya Yesu. Kadiri wakuu walivyojitahidi kuondoa watu Kwake ndiyo kadiri walivyoshindwa.

Kama Mafarisayo walikuwepo Yesu alipowajibu Masadukayo kweli kwa ndani wangalilifurahia jibu la Yesu, maana ameusimamia ufufuo wa wafu ila ajabu ni kwamba twasoma kwamba mara walithubutu kujiunga na wanasheria na kuleta swali lingine la kumwangusha Yesu.

v. **Amri iliyo kuu** 22: 34-40:

Swali lililetwa na mwanasheria aliyekuwa Farisayo. Walikuwa wameshauriana baada ya kuona jinsi Yesu alivyowanyamazisha Masadukayo. Lilikuwa swali la kumjaribu k.35. Shabaha ni kumfanya Yesu aseme neno la kushangaza,

lisilopatana na mafundisho yao ya kawaida, litakalowapa neno la kumshtaki kwamba amekufuru torati yao.

Yesu alitoa jibu sahihi kabisa kulingana na Torati. Kwake amri iliyo kuu ni ile ya kwanza, ya Kumb. 6:5, ya kumpenda Mungu kikamilifu kwa hali zote. Wayahudi walioishika imani yao vizuri walisema maneno ya Kum.6:5-9 kila siku mara mbili Halafu Yesu aliendelea kusema kwamba iko amri nyingine inayofanana na hiyo ya kwanza, nayo yapatikana katika Lawi 19:18 ni mtu kumpenda jirani kama mwenyewe. Ni vigumu mtu ampenda Mungu kiutendaji bila kumpenda jirani aliyeumbwa katika mfano wa Mungu. Ling. na 5:43-47. Maana ya "kufanana" ni kuwa pamoja na Kum.6:5 kama uongozi kwa amri zingine zote za Torati, zasimama pamoja kwa sababu zategemeana. Yesu alisema kwamba Torati yote na Manabii vyasimamisha amri hizo mbili, kila neno la torati na manabii limejengwa juu ya kumpenda Mungu na kumpenda jirani. Ling. Luka 10:25-28; Rumi 13:8-10; Gal.5:14; Yak. 2:8. Kwa maneno hayo hawakuweza kumshtaki ameziacha amri zingine, zote zadumu kuwa amri za Mungu ambazo twaitwa kuzitii katika hali ya kumpenda Mungu na kumpenda jirani.

Mathayo hakuonyesha itikio la mwana sheria kwa jibu la Yesu, ila twaweza kufikiri kwamba aliondoka bila raha.

Katika sehemu hiyo yote ya maswali twaona neno la Zab.2:2 limetimizwa, kweli wakuu walifanya shauri pamoja kumjaribu na kumtega Masihi wao.

vi. **Swali kuhusu Masihi** 22: 41-46:

Baada ya maswali yao Yesu alichukua nafasi ya kuwauliza Mafarisayo swali kuhusu Masihi ambaye ni Yeye Mwenyewe. Swali lake ni kubwa kabisa na la maana sana kwao. Tukumbuke Yesu ameingia Yerusalemu hali akishangiliwa kuwa Mwana wa Daudi 21:9,15 na hata watoto waliendeleza sifa hizo hekaluni na Yesu alikataa kuwakemea. Mara nyingi ameitwa Mwana wa Daudi 9:27; 12:23; 15:22; 20:30 Watu walitamani sana Masihi aje na wengi walimdhani Yesu kuwa Ndiye Yeye; hakuoana ila Mwenyewe hakutumia jina hilo. Ila ameingia Yerusalemu na hekaluni kwa mamlaka yake Mwenyewe bila idhini na ruksa ya wakuu, mamlaka ambayo ni ya KiMasihi. Amepata wapi mamlaka yake? Je! ni mkuu kuliko Daudi 12:6,41,43, na 12:3-4?

Kwa hiyo, ni swali tu ila ni zaidi ya swali tukikumbuka mazingira hayo. Tena aliwauliza wao wenyewe, "mwaonaje?" Alilenga kutoboa kosa lao kubwa, maana wao waliwaza Masihi atakuwa Mpiga Vita kama Daudi aliyewashinda adui zake - wao hutaka mtu wa kuwatoa kutoka utawala wa Warumi. Hawakumwaza kama Mwokozi, Mwana wa Mungu, atakayewaokoa na dhambi zao. Kwa hiyo, swali "ni Mwana wa nani?" wakajibu "ni wa Daudi". Ndipo kwa kutumia Maandiko aliwafunulia kuwa Masihi atamzidi Daudi, na hata Daudi alikiri hivi alipomwita Bwana Zab. 110:1

Masihi ni Mwana wa Daudi kimwili na Mwana wa Mungu kwa asili Hapo ndipo penye kosa lao. Hivyo aliwalazimisha kutafakari kwa kina zaidi juu ya Masihi na

kukata shauri juu yake.

Mafarisayo walishindwa na pamoja na wengine wote wakaacha kumhoji. Iliyobaki watumie nguvu za kimwili za kumpata na kumwua.

*MASWALI:*

*Watu walimbishi Yesu sana, Yesu hakuogopa kujadiliana nao. Je! katika huduma yako u tayari kuipigania Injili kwa kujadiliana na watu? Utafanya hivyo kwa kusudi la kuchokoza watu? au kwa wakati ambapo watu wamekushambulia? Wewe mwenyewe utawashambulia ukiona nini?*

vii. **Makosa ya Waandishi na Mafarisayo** 23: 1-36. Ling. na Mk. 12:38-40 na Luka 11:39-50 13:34-35:
Sura ina sehemu tatu. Katika sehemu ya kwanza 1 - 12 Yesu aliwaonya makutano waliomfuata na wanafunzi juu ya "unafiki" wa waandishi na Mafarisayo. Yawapasa kuyaheshimu mafundisho yao yaliyopatana na torati ya Musa, ila wasifuate kielelezo chao. Kwa nini? kwa sababu (a) hawakuyatimiza kimaisha mafundisho waliyowafundisha wengine: "hunena bali hawatendi"

k.3b. (b) kwa sababu waliwatwisha watu "mzigo" wa mapokeo yao yasiyo na mamlaka kama Torati, bila kuwahurumia wala kuwasaidia k4. Maneno "kufunga mzigo" huonyesha kwamba waliongeza vilivyokatazwa bila kuwaonyesha watu vya kufanya ili wampendeze Mungu - twakumbushwa maneno ya Yesu Math. 11:28-30 "njooni kwangu ... nami nitawapumzisha .... nira yangu ni laini. .. " (c) 5-12 Walikuwa na kiburi na kujiona kuwa bora, walifanya matendo ya dini kwa shabaha ya kutazamwa na watu, na kuheshimiwa kuwa wazuri, bila nia ya ndani ya kumpendeza Mungu. Walipenda kuwa mbele, penye heshima, na walifurahia majina ya heshima kama "Rabi" "Baba" "Bwana" "Kiongozi" Walijikweza. Huku hawakuwa na uwezo wa kuwawezesha watu kuyatimiza waliyowaambia, walikosa huruma na unyenyekevu.

k.5 "hirizi" zilikuwa visanduku vya ngozi ambazo ndani waliweka vikaratasi vyenye maneno ya Torati kama Kutoka 13: 1-10; 11-16; Kum.6:4-9 11:13-21. Taz. Kum.6:8 walizifunga mkononi mwa kushoto na kichwani.

"Matamvua" yaliwekwa kwenye pindo la vazi kuwakumbusha Torati - taz. Hesb. 15:37ku. Shida yao ilikuwa waliongeza ukubwa wa vitu hivyo ili watu wavione.

k.8 "bali ninyi msiitwe" ni kwa wanafunzi wake kuhusu vyeo na madaraka katika Kanisa. Tunaye mmoja tu aliyestahili kuitwa "Rabi" "Bwana" n.k. aliye na haki ya "Kiti cha Musa" Kanisa lahitaji sana kuangalia hali yake kuhusu vyeo na kutumia majina makubwa kwa viongozi wake na kukaza "kisomo" na hali za nje za watu, tusije tukaanguka katika makosa ya hao waandishi na Mafarisayo. Yesu alimaliza sehemu hiyo ya kwanza ya maonyo kwa wito wa kutumika na kunyenyekea.

vif. 13:26 Katika sehemu hiyo Yesu alitoa ole 8 ila hasa ni 7 maana lile la k.14 halionekani katika nakala za zamani sana. Maana ya neno "ole" ni kama neno lenye hukumu pamoja na sikitiko ndani yake. Ni kinyume cha zile "heri" za sura 5.

Ole la kwanza: k.13. Walimkataa Kristo aliyeleta njia ya Uzima na waliwaudhi wote waliomkubali. Walifanya njia ya wokovu kuwa vigumu kwa watu, na wao wenyewe hawakuiingia

k.14. Maneno hayo yaonekana katika Mk.12:40 Luka 20:47 Walijifanya kuwa na mzigo juu ya wajane huku walitafutia vipawa kwao.

k.15: ole la pili: Kwa bidii walitafuta kuvuta watu kuwa Mafarisayo hata kuwafanya wayashikilie mambo yao kuliko wao wenyewe. Kumbe wao wamepotea na watakaowafuata watapotea Neno "mwongofu" lina maana ya aliyegeuka kuwa Farisayo.
k:16: Walionyesha unafiki wao kuhusu viapo, wakibagua kati ya vitu mbalimbali wakiapa kwa kitu kidogo na kisicho na maana kwa kulingana na kitu kingine. Vitu vyote vina Mungu kwa hiyo mwishowe wakitambua wasitambue wameapa kwa Mungu na kufungwa na viapo vyao. Ni vipofu!
k.23-24. Walikaza mambo madogo-madogo na kuyaachilia makubwa. Walishindwa kutambua yapi ni makubwa na ya kutangulia. Siyo kwamba madogo si kitu, wasishikilie, la! ila wayatanguliza ya maana. "mbu" ni mfano wa madogo na "ngamia" ni mfano wa "makubwa" Kwa lugha hiyo ya kichekesho Yesu alitoboa wazi hali yao.

k.25-26: Kosa lao lingine kubwa lilikuwa la kuangalia sana mambo ya nje bila kuzijali hali za ndani za moyoni. Ni dhambi ya ndani imtiayo mtu unajisi si mambo ya nje Sura 15. Kila mara amewaita "wanafiki" na "vipofu"

k.27 -28: Ni sawa na kosa lililotangulia. Kwa nje walionekana kuwa wazuri sana wa dini, wenye kuipenda na kuishikilia, ila ndani mioyo yao ni mbali na Mungu. Hawakufanya kwa shabaha njema ya kumpenda Mungu, nia yao ilikuwa wao wenyewe wasifiwe

k.29-36: Wamekuwa katika safu ya waliowatangulia waliowatesa na kuwakataa manabii wa kweli. Wakati huo walikuwa na mpango wa kumwua Mwana wa Mungu aliyetumwa kwao na Mungu. Kwa maneno makali sana Yesu alitaja hukumu itakayowapata k.33. Wafanye watakavyo k.32 "kijazeni kipimo cha baba zenu" pamoja na kuwaita wanafiki alitumia maneno "nyoka, wana wa majoka" kama Yohana Mbatizaji alivyotumia Sura ya 3. Habeli (Mw. 4:8) alikuwa wa kwanza kuuawa kwa imani yake ya kumpendeza Mungu na Zakaria (2 Nyak. 24:20-22) alikuwa wa mwisho. Wa mwisho kwa sababu Biblia ya Kiyahudi ilimalizika na kitabu cha 2 Nyakati. Inaonekana mwandishi alichanganyiwa kimawazo maana Zakaria aliyeuawa kati ya patakatifu na madhabahu alikuwa “bin” yaani “mwana” wa Yehoyada. Nabii Zakaria wa baadaye alikuwa mwana wa Barakia. Waliowaua walikuwa na hatia ya damu yao.

35-36: Tendo lao la kumwua Masihi wao, Mwana wa Mungu litaleta hukumu kali ya Mungu juu ya taifa zima, na hukumu hiyo ilitokea mwaka BK.70 Yerusalemu ulipotekwa na Warumi. Subira ya Mungu iliufikia upeo wake. Wataadhibiwa kwa dhambi hiyo na dhambi za wale waliowatangulia. "kizazi hiki" kimetajwa mara kwa mara na Mathayo 11:16-19:12:38-45: 17:17.

Tusifikiri kila mwandishi na kila Farisayo alikuwa mbaya la! sivyo! ila kwa jumla wamefanya kosa kubwa la kuwapotosha watu wa Mungu, hawakuwasaidia kuelewa mapenzi ya Mungu, walikuwa wameifanya dini kuwa kitu cha nje, ya kuyashikilia maagizo madogo-madogo waliyoyatunga wenyewe bila kufundisha watu kuishi katika hali ya kumpenda Mungu kwa moyo na kwa kushirikiana naye ki-binafsi.

Kwa hiyo kama ambavyo tumeona mara nyingi Yesu ameyapindua mawazo yao kabisa. Onyo ni kwamba sisi tusiufanye Ukristo kuwa dini ifananayo na "Ufarisayo". Kwa hiyo Yesu alitoa maonyo rasmi juu ya dini ya Kiyahudi, ni kama maneno yake ya mwisho kwa watu wake.

viii. **Unabii juu ya Yerusalemu kuanguka** 23:37-39:

Katika sehemu hiyo ya mwisho Yesu aliuombelezea Mji wa Yerusalemu na kuonyesha hukumu itakayoupata. Kwa kweli Yesu mara nyingi alikuwa amewasihi wampokee kuwa Masihi wao wa kweli aliyetumwa na Baba - "mara ngapi" ni dalili ya Kuja Kwake Yerusalemu mara kwa mara kama Yohana aonyeshavyo katika Injili yake. Alikuja kwa upole na kwa upendo, kwa kusudi la kuwaokoa, mfano wa kuku ahifadhiye vifaranga wake. Alitaka kuleta Israeli kwenye toba ili wasiadhibiwe kwa mwenendo wao wa muda mrefu k.35-36. Hawakumtaka! Walitaka Masihi wa vita atakayewaokoa na Warumi, kumbe vita wataipata, Warumi watachoka nao ndipo Hekalu lao na taifa litaangamizwa.

k.38: "nyumba yenu" hasa ilikuwa Yake na ya Baba ila kwa sababu wamemkataa Yeye na Baba wataiacha, nayo itakuwa "ukiwa" ukiwa ulio mzito wa kukosa Mwenyewe!! Kweli hekalu na taifa litaendelea mpaka BK.70, lakini kuanguka kwake ni tendo la nje ambalo halina budi litokee kama timizo la tendo la ndani la kuachwa na Mungu. Hekalu lilikuwa "ishara" ya nje ya uhusiano wa ndani, wa Agano lao na Mungu, uhusiano huo utakapovunjwa ndipo jengo, ishara ya nje, litaachwa.

39: Hali mpya inaanza kutokea, hawatamwona tena kama walivyozoea kumwona, wala hawataweza kumwona tena mpaka waitimize sharti moja ya "kusema amebarikiwa ajaye .... " hatuambiwi kwamba sharti hiyo itatimizwa au siyo. Pengine haitatokea au pengine mwisho wa mambo yote itatimizwa Yesu atakapokuja kwenye utukufu mwingi na enzi kuu na kuwaadhibu adui zake wote Mk.14:62. Ni wazi kwamba Yesu alitumia lugha kali hata hivyo alifanya kwa uzito wa hali, na kwa ombolezo lililojaa huzuni nyingi na upendo mwingi. Hakufurahia kuwaambia hayo yote, ila kwa sababu ni kweli yenyewe budi waambiwe ili wajihoji kabla ya kumwua. Vote watakayoyapata yatokana na

kumkataa. Shabaha yake ilikuwa kuwaokoa, kumbe wale ambao alikuja kuwaokoa watakapomkataa watapatwa na adhabu kali.

*MASWALI:*
*Katika sura hiyo Yesu amesema sana juu ya unafiki wa wakuu wa dini. Je! kama Yesu angefika leo na kutazama Kanisa la wakati wetu, wafikiri angetaja mambo gani yaliyo kinyume chake? Kanisa la leo lifanye nini ili limpendeze Bwana Yesu?*

## MAFUNDISHO YA YESU KUHUSU MATUKIO YA BAADAYE 24:1-25:16.

Neno kuu la sehemu hiyo ni hukumu. Hukumu juu ya Yerusalemu 24:1-35 na hukumu iandamanayo na Kuja Kwake 24:36-51; ndipo yafuata mifano miwili kuhusu hukumu 25:1-30; na mazingara ya hukumu ya mwisho 25:31-46. Sura 23 pia ilihusu hukumu juu ya waandishi na Mafarisayo na dini ya Kiyahudi. Tofauti ni kwamba mafundisho ya sura 23 yalitolewa kwa watu wazi, hayo ya sura za 24 na 25 yalitolewa kwa wanafunzi faraghani.

Sura ya 24 inatatiza kwa sababu si rahisi kujua kwa uhakika ni lipi linalozungumziwa, Anguko la hekalu au Kuja Kwake Yesu mara ya pili. Mwanzoni yaonekana ni kuhusu Yerusalemu na mwishoni ni kuhusu Kuja Kwake. Wanafunzi walipomwuliza swali lililosababisha Yesu atoe mafundisho hayo walitaja yote mawili katika swali lao k.3. Upo uhusiano mkubwa kati ya hayo mawili, maana iwapo yatatokea kwa wakati tofauti, yote ni hatua katika Yesu kuitekeleza na kuitimiza Huduma yake, yote yahusu Hukumu zimshuhudiazo Yeye kuwa kweli Neno la mwisho la Mungu kwa watu.

Kuna hali ya kupunguza msisimko ya watu kuhusu Kuja Kwake, taz. vif. 4,5,6b,8,14,23-28,36. Pia ni kama kupooza tazamio la Kuja Kwake kuwa mapema. Yesu Mwenyewe alisema hakujua siku wala saa ya Kuja Kwake k.36.

Inaonekana k.29 na k.34 vyahusu Kuanguka kwa Yerusalemu na k.36 ni chanzo cha Yesu kujibu swali la pili la wanafunzi kuhusu Kuja Kwake.
i. **Yerusalemu kuanguka:** 24:1-2:

Yesu alipoondoka hekaluni ilikuwa hatua maalumu ya kuonyesha kwamba Mungu hakuwa na makusudi nalo tena. Walipotoka wanafunzi walimwonyesha majengo yake, bila shaka katika hali ya kushangaa kwamba Yesu ameliacha, pamoja na ushangao juu ya maneno juu ya anguko lake. Yesu aliwathibitishia kwamba iwapo ni jengo kuu hata hivyo halitasalia jiwe juu ya jiwe!!! Wayahudi wakati wa Yesu walidhani kwamba hekalu haliharibikani.
ii. **Maonyo juu ya kufikiri mengine yatatokea mapema** 24:3-14:

Yesu alionyesha kwamba Kuanguka kwa Yerusalemu na Kuja Kwake ni matukio mbalimbali. Yawezekana wanafunzi waliwaza la pili litafuata la kwanza mara kwa vile Anguko la Yerusalemu ni jambo kubwa mno mawazoni mwao, budi lifuatwa na "mwisho" Yesu alitaka kuyapanua mawazo yao ili wafahamu ya

kuwa mambo yataendelea baada ya hekalu kubomolewa na taifa kutawanyika. Mwisho wake si mwisho wa mambo yote!!

k.4-5. Yesu aliwaonya juu ya kudanganywa. Yeye ndiye Kristo wa kweli ila wengine watatokea wakitaka kuchukua mahali pake lakini hao si wa kweli. Kati ya Wayahudi waliinuka "Masihi" wa uongo" wakitaka kuipindua serikali na kuvuta watu wawafuate Mdo.5:36-37 21:38.

k.6-8: Vilevile vita na misiba mbalimbali itatokea na watu watadhani ya kuwa ndiyo dalili za "mwisho" kumbe sivyo. Hizo zisitumiwe kwa kufanya hesabu ya wakati. Neno "utungu" lina maana ya kwamba kutoka dhiki mbalimbali kitu kipya chazaliwa yaani ufalme wa Mungu na dahari mpya.

9-13: Ndipo Yesu alisemea mateso ya wafuasi wake ambayo hayatatoka kwa Wayahudi tu bali yatatoka kwa mataifa yote. Kwa mateso hayo wengine watarudi nyuma na kupoa, na kwa sababu yake upendo wa wengi utapoa, hata wakristo wao kwa wao watasalitiana. Watakaovumilia shida zote ndio watakaookolewa na kuzishiriki baraka za dahari mpya.
k.14. Budi Injili ihubiriwe katika dunia nzima kati ya vipingamizi vingi vya mateso, chuki, maasi, waamini kupoa na manabii wa uongo kutokea. Yesu aliongoza wanafunzi kuwaza kuwa Injili itahubiriwa kwa watu wote mahali pengi ndipo "mwisho" utatokea. Ni vigumu kuweka "wakati" kwa neno hilo kutimia! Wengine hufikiri kwamba maana ya k.14 ni "huo mwisho" ni wa Yerusalemu kuanguka na Habari Njema kuhubiriwa kwa "mataifa yote" kulitimizwa katika uenezi wa ajabu uliotokea katika miaka thelathini baada ya Yesu Kufa Mdo.2:5 Rum. 1:8; Kol. 1:6,23. Mawazo yetu yamepanuka juu ya "ulimwengu wote" kutokana na nchi mbalimbali kugunduliwa baadaye.

iii. **Shida zitakazotokea karibuni hivi katika Yudea** 24:15-28.

Sehemu hiyo yahusu Anguko la Yerusalemu lililotokea BK.70. Vita na Warumi ilianza BK.66 na kuendelea hadi Yerusalemu kuanguka. "chukizo la uharibifu" lilikuwa madhabahu ya kipagani aliyoisimamisha Antioko Epifani hekaluni KK.167. Patakatifu paweza kuwa si pale tu bali patakatifu po pote. Katika Mk.13:14 "pasipolipasa" na Luka 21:20 ni Yerusalemu kuzungukwa na majeshi walioinua bendera za Kaisari wa Kirumi zenye sanamu yake. Yatakapoonekana hayo basi watu wasiweke tumaini lao katika Yerusalemu, budi wakimbie haraka kabisa bila kuchukua cho chote. Pia waombe kwamba hayo yatokee wakati wa hewa nzuri, wasicheleweshwe na mvua na baridi n.k.

Pia isiwe siku ya sabato yenye katazo la kwenda zaidi ya mwendo wa sabato. Majeshi ya Kirumi watafanya uharibifu mkubwa ila Mungu katika rehemu zake na kwa kuwakumbuka wateule wake atapunguza muda wa dhiki zao. Wenye kupata shida zaidi watakuwa wenye mimba na wanyonyeshao. Ni picha ya shida kubwa na Yosefu, mwandishi wa historia ya Wayahudi katika maandishi yake amezitaja. Yasemekana kwa sababu ya njaa kali wazazi walikula watoto wao, na wengine walijilaza katika masanduku ya maiti wakielekezwa kutazama hekalu wakitumaini Masihi atakuja na kuwaokoa. Warumi walizunguka mji kwa

muda mwingi, wakizuia watu na vitu kutokuingia wala kutoka. Wakristo waliotia maanani maneno ya Yesu walikimbia mapema mpaka Pella, ng'ambo ya Yordani. Wayahudi waliotumaini sana kupata Masihi wao, ambao hawakumkubali Yesu ndiye Yeye, hao walizidi kumtazamia wakati huo wa dhiki. Pia wengine walitumia nafasi hiyo kwa kuamsha uvumi kwamba Masihi yuko jangwani, au yuko mahali pa siri. Yesu aliwaonya wanafunzi wake kwamba wakati wa dhiki hizo si wakati wa Kurudi Kwake.

Yeye atarudi wazi na bila taarifa na ishara. Itawapasa watu wastahimili dhiki maana ni hukumu ya Mungu juu ya hao waliomkataa Masihi wao wa kweli. Si wakati wa Yeye kuja kuwalipiza kisasa Warumi.

k.28 Pengine kifungu hicho kina maana kwamba "tai" ni mfano wa majeshi ya Kirumi na bendera zao wakija kwenye Yerusalemu ulio mfano wa "mzoga" - au pengine maana yake ni kwamba kama kuwepo kwa tai kwahakikishia kuwepo kwa mzoga, vivyo hivyo Kuwepo kwa Kristo kutahakikishiwa kwa kuwako kwa watu wake.

iv. **Upeo wa shida katika "kizazi hiki"** 24:29-35. k.29.

Kifungu hicho chatuelekeza kuwaza kwamba hayo yaliyoandikwa katika sehemu hiyo yahusu Anguko la Yerusalemu iwapo wengi wamewaza yahusu Kuja kwa Yesu mara ya mwisho.
Yameandikwa kwa lugha ya ki-picha kama Wayahudi walivyozoea kuandika kwa unabii. Kwa nini tufikiri yahusu Anguko la Yerusalemu? ni kwa sababu ya kusema "mara baada ya siku zile ... " pamoja na maneno ya k.34 "kizazi hiki hakitapita ... " Tukisema yahusu Kuja kwa Kristo mara ya pili inaonekana
hata Yesu Mwenyewe hakujua vizuri, kwa sababu hakuja mara baada ya Anguko la Yerusalemu. Pia k.36 alisema hakujua siku wala saa ya Kuja Kwake; pia k.27 chatufikirisha kwamba hazitakuwepo ishara za kututayarisha kwa Kuja Kwake. Kwa hiyo ni vema tutafsiri lugha hiyo ya ki-picha ni kuhusu dhiki za Anguko la Yerusalemu, zikielezwa katika hali ya mashairi na kwa lugha ya ki-picha Ndiyo kawaida ya waandishi kuandika wakati wa shida kubwa na mabadiliko makubwa. Ni kueleza hukumu zitokeazo mara
kwa mara kwa mataifa mbalimbali ambayo huanguka mara kwa mara.
Tukumbuke kwamba Mji Mtakatifu ulipoangamizwa milioni moja ya watu
walipotea na bila shaka si ajabu jambo kuu la kiasi hicho lielezwe kwa kuona "jua kutiwa giza" "mwezi kukosa kutoa mwanga" "nyota kuanguka" n.k. Siyo kusema nyota zilianguka n.k. la! ni lugha tu ya kueleza tukio kuu na badiliko kuu, hasa Mungu alipojiingiza kwa nguvu kwa kuwahukumu watu wake ling. na Is.13:1,10 kuhusu Anguko la Babeli; Is.34:4 - Anguko hasa la Edomu; Amosi 8:9, Ez.32: 7-8; Yoeli 2:28-32.

Waandishi wa historia wa siku zile, km. Yosefu na Takito ("Josephus" na "Tacitus") waliandika hivyo pia "Majeshi yapiganayo yalionekana mbinguni, silaha zikametameta, hekalu likatiwa nuru ya moto uliotokea na mawingu kwa ghafula .. "

Hayo yote yaweza kuelezwa kuwa "kuja kwa Mwana wa Adamu" "ishara ya Mwana wa Adamu" ni ishara ya mamlaka yake katika hukumu itakayotendeka.

Tafsiri nzuri ni "kabila zote za nchi" badala ya mataifa yote. Ling. na Zek.I2:10-14, ni itikio la Wayahudi watakapoona yule waliyemwua amepewa mamlaka ya kufanya hayo yote. ling. Math. 16:28; Is.19:1 Zab.97:2,3 104:3.

k.34 Kuwakusanya wateule wake kulitimia wakati mitume walipoanza kuwahubiria Wamataifa na Kanisa kupata nguvu zaidi lilipowekwa uhuru na uhusiano wake na Wayahudi baada ya hukumu la B.K.70. Hekalu litakapobomolewa na taratibu za dini ya Kiyahudi zitakapoondoka ndipo Kanisa litasimama peke yake. Parapanda ya Injili k.31 italia na kuwakusanya wateule kutoka kila mahali. Katika Kiyunani ni neno moja tu kwa malaika na wajumbe.

"Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu" ling. na Dan. 7: 13-14. Maneno ya Danieli si kuhusu Yesu kuja ulimwenguni bali Yesu kwenda, yaani Kuja kwa Baba kupata madaraka na enzi.

k.32-35: Mfano wa mtini waonyesha ya kuwa dalili dhahiri zitatangulia jambo hilo - k.15. k.33 chasema juu ya ukaribu wa mambo hayo. k.34 chasema ni "kizazi hicho" yaani wale walioishi wakati Yesu alipokuwa akisema hayo ambao wataona hayo yote. Kwa hiyo jambo ni la hakika sawa na mtini unaochanua majani na kuzaa matunda. Tena Yesu alitilia mkazo kwa maneno ya mamlaka yake "amin, nawaambieni.." Neno lake ni imara na la kuaminika.

v. **Mwana wa Adamu kutokea wakati usiodhaniwa** 24:36-25:13.

k.36 Sasa Yesu asema juu ya Kuja Kwake mara ya mwisho "siku ile na saa ile" Haitanguliwi na dalili na hata Yesu katika hali ya kufanyika mwili hakujua ni lini. Alisema hivi akimtaja Baba na kuonyesha uhusiano wa ukaribu mno alio nao na Baba pamoja na kukiri hali ya kumtegemea kwa yote.

Watu hawawezi kujitayarisha kwa siku ile, isipokuwa budi wawe tayari kila siku. Wengi hawatakuwa tayari kama vile wakati wa Nuhu wengi hawakuwa tayari. Mambo yatatokea ghafula. "Siku ile" ni ya hukumu 7:22 na ni lugha aliyotumia Mathayo mara kwa mara taz. 11:22-24 12:36. Ni siku ya hukumu k. 43, 48-51. Kwa wengine ni siku ya wokovu. Fundisho ni kwamba Yesu atakuja ghafula, wakati asiyetazamiwa, na bila ishara maalumu, mfano wa mwivi asiyeleta tangazo la kuwa ataivunja nyumba fulani. Watu watakuwa wakiendelea na shughuli zao za kawaida, kikazi, kifamilia.

k. 4I-51. Watu watafanana kwa kufanya kazi n.k. ila pia upo utofauti mkubwa kati ya wale walio tayari na wale wasio tayari, ila utofauti hautaonekana mpaka Kristo atokee, ndipo utengano utatokea, mmoja atachukuliwa na mmoja ataachwa. Kuwa tayari ni kuwa mwaminifu na wa kukesha. Kukesha siyo kukaa na kusubiri tu, bali ni kuendelea katika utumishi kwa uaminifu, kuwapatia wa nyumba mahitaji yao. Na thawabu kwa waaminifu ni kupewa wajibu ulio mkubwa zaidi. Kujitayarisha ni kutumika kwa uaminifu si kufanya hesabu ya wakati.

25:1-13: Mfano wa Wanawali 10: Mfano huo hukaza neno lile lile la kuwa tayari kwa Mwana wa Adamu wakati usiojulikana. Bwana Yesu ni Bwana Arusi. Wanawali kumi walifanana katika mengine, wote waliondoka kwenda kumlaki Bwana Arusi, wote walichukua taa zao, ila walitofautiana sana katika kujiandaa kuwa tayari. Watano walioitwa wapumbavu walikosa kuchukua mafuta kwa taa zao, huenda kwa kudhani Bwana Arusi hatakuja usiku wa manane.

Yesu alifundisha kwamba ni jambo muhimu kabisa kuwa tayari. Kutokuwa tayari kutasababisha kukosa uzima wa milele. Watu waweza kukawia kumpokea nafsini mwao, kwa hiyo akija bado hawajampokea hawatapata nafasi ya kumpokea wakati ule wa Kuja Kwake, watakuwa wamechelewa, mlango utafungwa, maneno ya kuonyesha kwamba hamna kumbembeleza wakati huo. Tena neno "siwajui" laonyesha kwamba kitu kikubwa ni uhusiano wa ki-binafsi na Yeye - ling. na 7:21-23.

Kukawia kwa Bwana Arusi si udhuru wa kutokujiandaa. Mfano huu wahusu Kanisa ambalo wengi ndani yake hawajampokea Yesu bado. Ni hatari kutokuwa tayari.

vi. **Mfano wa Talanta** 25:14-30:

Neno "mara" laonyesha uhusiano uliopo kati ya mfano huo na ule wa wanawali kumi, hasa kuhusu kuwa tayari k.13. Kuwa tayari kwataka nini? Bwana Yesu alisema juu ya kipindi kile kati ya Kuondoka Kwake ambako ni karibu, na Kurudi Kwake ambako ni baada ya siku nyingi k.19, k.5.
Watumishi wake watapewa talanta, vipawa vya Roho Mtakatifu, na nafasi za kumtumikia. Kila mtu atagawiwa kufuatana na hali yake "kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake" k.15 ili wasio na uwezo wasilemewe na wenye uwezo wasidharauliwe - Mungu humfahamu kila mtu na hali yake na kumgawia vivyo hivyo. Talanta zilikuwa mali ya yule Bwana, nazo zilitolewa ili zitumiwe kwa kuleta faida.

Kwa hiyo katika kipindi hicho ni dhahiri kila Mkristo apaswa kumtumikia Bwana wake kwa moyo wote na kwa uwezo alio nao na kwa uaminifu. Ni wajibu wake pamoja na furaha yake. Kukesha si kumngojea tu, bali ni kumngojea kwa kumtumikia na kwa kujua hakika anaye Bwana ambaye atarudi na kufanya hesabu juu ya utumishi wake, ndipo kila mtu ataipata thawabu aliyostahili. Kwa wafanyao vema 'nafasi za kutumika zitapanuka, Uf. 7:15 pamoja na kushirikiana kwa ukaribu zaidi na Bwana wao na kumfurahia.

Katika mfano, wawili walifanya vema na iwapo walikuwa na talanta tofauti, wote walipata thawabu iliyofanana. Mmoja hakufanya vizuri, alibadili shabaha ya Bwana wake na badala ya kuitumia talanta akaifukia chini, alii"salimisha" badala ya kuitumia. Tangu mwanzo alimtazama Bwana wake kwa jicho baya. Siyo kusema kwamba alivyotamka juu yake ilikuwa kweli, la! sivyo! Bwana wake si mgumu, ila kwa kuwa yeye alifikiri hivyo ilimpasa afanye kulingana na mawazo yake, na kwa vyovyote kutafuta kumletea faida, ikiwa si kwa kuitumia, afadhali angaliiweka kupata riba. Kwa kukosa kutumia nafasi aliyopewa

atakosa kupata nafasi tena, atanyang'anywa talanta na yule aliye nazo atazidishiwa - 13:12.

Uvivu na kutokujali ni makosa makubwa katika maisha ya Mkristo. Yaonekana hakuwa Mkristo wa kweli, alifanana na wale waliotajwa 24:48-51 na 25:12 na mwisho wake ni sawa na mwisho wao, ni kukataliwa.

vii. **Hukumu ya mwisho** 25:31-46:

Neno la hukumu lililoanza katika sura ya 23 sasa hufikia upeo wake katika hukumu ya mwisho. Katika 16:27 na 24:30-31 Yesu alitabiri juu ya Kurudi Kwake katika utukufu, na hapo Yesu alieleza habari hiyo kwa lugha ya ki-picha. Ataonekana katika utukufu kama Mfalme k.34 akitumia cheo na mamlaka yake ya Ki-Mungu k.32 (Yoh. 5:19-29) na kufanya hukumu ya mataifa yote. Si kadhi mkali, amejaa huruma, ameguswa na udhaifu wetu, ni Mwana wa Adamu ambaye ameonja maisha ya wanadamu hali amefanyika mwili na kuishi kati yetu. Ndiyo imfanyayo kustahili kuwa mhukumu wetu.

Twaona ni mataifa yote watakayokusanyika mbele zake. Yeye atawagawa katika vikundi viwili - wa "kondoo" wenye haki k.37 hao watakuwa upande wa kuume, hao ni wateule" k.34 wametoka pande zote za dunia kutokana na Injili kuhubiriwa ulimwenguni mwote. Wameuhakikishia uteule wao, si kwa kusema "Bwana, Bwana", wala kwa maneno yao tu, bali kwa kujitoa katika kuwatumikia wenzao, kuwatendea mema kila wakati, bila kujionyesha. Hao waliotendewa mema Yesu amewaita "ndugu" amesikia umoja nao katika dhiki na shida zao k. 40.
Ling. na 12:48-50 na 28:10 ni neno kwa wanafunzi wake. "Wadogo hao" walitajwa 10:42 na 18:6,10,14. Dhiki zilizotajwa zimetajwa kuwa zile watakazozipata wafuasi wake katika sura ya 10. Kwa kuwahurumia wenzao na kuwatendea misaada mbalimbali itahesabiwa wamemfanyia Bwana Yesu Mwenyewe. Walifanya kwa upendo na furaha, si kwa shabaha ya kupata kibali cha Bwana Yesu, hivyo wameonyesha wanayo tabia za "wana wa Baba", wamefanana na Baba yao, kwa hiyo Yesu amewaita waliobarikiwa, naye amewaita kuja na kuurithi uzima wa milele, urithi kwa sababu ni wana, urithi uliotayarishwa tangu awali.
Kwa upande wa "mbuzi" hao ni "waliolaaniwa" - neno gumu kwao ni "ondokeni kwangu mwende katika moto wa milele" wataondoshwa machoni pa Mfalme, hawatazishiriki baraka za familia ya Baba, maana hawakuonyesha tabia za kuwa "wana wa Baba" hawakufanana na Baba yao, walijipenda, hawakuwa na mzigo juu ya wenye shida. Hao waliuliza kama wenzao walivyouliza k.44 "lini tulipokuona?" kumbe jibu ni kwamba kutokumtendea mmoja aliye na shida ndiyo ni sawa na kutokumtendea Kristo Mwenyewe. Kwa hiyo hali yetu ya kawaida, yale tufanyayo bila kupima ni ishara kamili ya hali yetu ya kweli.

Katika sura hii yote hukumu kali ipo kwa wale wote ambao **hawakufanya ilivyowapasa** - kukosa kutenda mema kwaleta hukumu kali kuliko kufanya makosa - wanawali watano walifungiwa mlango kwa kuwa walikosa kuleta

mafuta kwa taa zao - mtumishi aliyefuka chini talanta asiitumie alitupwa nje, na mbuzi wa mkono wa kushoto walipelekwa kwenye moto wa milele kwa vile hawakufanya 10 lote la kuwasaida wenzao katika shida zao. Uzima wa wenye haki utadumu na adhabu kali ya waliolaaniwa itadumu, utengano utakapotokea ni wa kudumu. Urithi wa wabarikiwa ulitayarishwa kutoka awali kwa ajili yao, ila moto wa milele ulitayarishwa hasa kwa Ibilisi na malaika zake, kwa hiyo waliolaaniwa watakwenda kwenye mwisho ambao hasa sio wao, ila wataushiriki kwa sababu walijiweka upande wa Ibilisi wala si upande wa Kristo.

Kwa juujuu inaonekana Yesu anafundisha tutaokolewa kwa matendo mema, ila tukifikiri kwa ndani sivyo ilivyo. Kama ambavyo tumeona "ndugu" ni wanafunzi wake na neno urithi pamoja na lugha "ondokeni kwangu" ni lugha ya uhusiano na uhusiano huo hutokana na kumwamini Yeye Mwenyewe.

*MASWALI:*

*Je! Wakristo wamepoa katika habari ya kutazamia Bwana Yesu atakuja tena? Unawakumbushaje habari hiyo? mara moja Wakati wa Kuja, au mara kwa mara katika mwaka? hasa wawe tayari kwa namna gani?*

## MATAYARISHO KWA MATESO 26:1-46.

Sasa twafikia mambo makuu ambayo Yesu ameyatabiri kwa mkazo tangu Ukiri wa Petro 16:21.ni upeo wa huduma yake na shabaha kamili ya Kuja Kwake. Katika habari hizo Mathayo ameifuata Injili ya Marko isipokuwa kwa machache tu - ling Mko sura 14 na 15. Yesu hafundishi tena, wakati wa kufundisha umekwisha na nafasi ya watu kuitika imepita. Iliyobaki ifanyike ile kazi ya ukombozi iliyomleta hapa duniani. Nyuzi mbili zimefumwa pamoja katika sehemu hiyo; kwa upande mmoja Yesu amtii Baba na mapenzi yake, yuaenenda kwa Kifo Chake kama "impasavyo" kwa kuyatimiza Maandiko. Kwa hiari Mwana wa Mungu atatimiza mapenzi ya Babaye. Hashikwi kwa nguvu kana kwamba hakuwa na uwezo wa kuwaepa au kuwashinda adui zake, hafi kwa bahati mbaya, hafi kutokana na kigeugeu cha watu n.k. la!

Ila kwa upande wa pili alikufa kutokana na nia mbaya, chuki, na wivu wa viongozi wa Wayahudi ambao kwa vyo vyote hawakumtaka, pamoja na umati wa watu waliolia "msulibishe" pamoja na usaliti wa Yuda.

Kwa hiyo nyuzi hizo mbili zimefumana, mapenzi ya Mungu ya kukomboa ulimwengu kwa kifo cha Yesu, na pia mbaya ya wanadamu waliomwondoa pasipo kutambua ya kuwa watatimiza mapenzi ya Mungu. Wao huwa na hatia ya dhambi hiyo, na Mungu aliigeuza kuwa njia na sababu ya wokovu. Mdo.2:28.
i. **Utangulizi:** 26:1-2:

Fungu kubwa la tano la mafundisho limekoma Mathayo akitumia maneno aliyoyazoea 7:28; 11:1; 13:53; 19:1 na 26:1 ila aliongeza neno "yote" kuonyesha kwamba mafundisho yamekwisha.

Yesu aliwakumbusha wanafunzi juu ya mateso yake - kila wakati amefanya hivyo ila sasa mambo yameiva, karibuni hivi, baada ya siku mbili atauawa 16:21; 17:22-23; 20:18-19.

Alifahamu kwa ukamilifu yote yatakayompata, hata ya kuwa atauawa katika Sikukuu, akiwa Mwana Kondoo halisi wa Mungu. Ila sivyo walivyokusudia wakuu k.5. Mpango wa Mungu utasimama, mpango uliopangwa kabla ya Anguko na kabla ya wakuu kufanya mipango yao.

Sikukuu ya Pasaka ilikuwa kumbukumbu la Waisraeli kuokolewa mikononi mwa Wamisri chini ya uongozi wa Musa na kwa mkono hodari wa Mungu kwa matendo makuu. Kwa hiyo ulikuwa wakati uliofaa kwa ukombozi mkuu zaidi, wa wanadamu kuokolewa na utumwa na dhambi na Shetani. Sherehe mbalimbali ziliendelea kwa juma lote. Kwa kalenda ya Kiyahudi Sikukuu yenyewe ni 14 Nisani, wakati wanakondoo walipochinjwa ndipo jioni yake waliita Pasaka, hiyo jioni ni 15 Nisani, maana wao huanza siku zao jioni. Taz. Kutoka 12 kwa habari za Pasaka.

ii. **Mpango wa hila juu ya Yesu:** 26:3-5:

Makuhani wakuu na wazee walikusanyika pamoja na Kayafa, Kuhani Mkuu (alikuwa Kuhani Mkuu BK.I8-36). Hao walikuwa viongozi rasmi wa taifa, na sasa kwa mara ya mwisho wamkataa Yesu. Katika sehemu hiyo Mafarisayo na waandishi wametajwa mara chache tu.

Viongozi waliogopa watu wakikumbuka jinsi walivyomshangilia Yesu alipoingia Yerusalemu 21:8-11, 15-16, pamoja na jinsi walivyomsikiliza alipokuwa akifundisha kila siku hekaluni. Wamekwisha kukata shauri kabisa kwamba watamwua, ila tatizo ni lini? watawezaje kumkamata bila kuleta fujo ndipo Warumi watakuja juu yao kwa nguvu. Wakikawia Yesu atakuwa ameondoka Yerusalemu pamoja na watu. Wakimkamata kabla ya Sikukuu ni shida maana wengi wamefika na kila siku huwa wakimsikiliza.

Wafanyaje? Wafanye kwa hila, kwa siri, wakiwindawinda nafasi huenda mara baada ya Sikukuu. Ndipo Yuda akajitokeza kwao na kujitoa kuwafahamisha mahali pa kumpata Yesu usiku.

Mradi wamlipe kwa tendo hilo. Bila shaka walifurahi sana walipotatuliwa tatizo hilo k.14-16.

Kwa hiyo picha tuliyo nayo ni kwamba hakika Yesu atauawa hata bila Yuda kumsaliti, wakuu wamekwisha kukaza nia zao, ni utekelezaji tu uliobaki. Yuda alirahisisha kazi yao ya kumkamata Yesu, na bila shaka kwa kutokea kwake walibadili mipango na kuileta mbele, hata wakawa tayari kuishughulikia usiku wa Pasaka! hivyo mapenzi ya Mungu yalitimia!!

iii. **Yesu kupakwa mafuta huko Bethania** 26:6-13, Mk. 14:3ku na Yoh. 12:1-8:

Katika sura hizo twakuta Yesu akifanyiwa mengi mabaya ila hapo twaona alitendewa jambo jema la upendo, la nuru, la kumfariji sana. Katika kumpaka

mafuta mama huyo aliukiri Umasihi wa Yesu na kumtia mafuta kama Mfalme. Alitayarishwa kwa Kufa Kwake kutakakotimiza wito wake. Nyuma ya hila za wakuu na usaliti wa Yuda Yesu ametwisha kabisa wito wa kuwa Mtumishi Ateswaye (Is. 53).

Habari hiyo ilitokea Bethania, mahali pa rafiki wapendwa wa Yesu na mahali alipozoea kukaa. Simoni alijulikana kwa jina Simoni Mkoma, yawezekana Yesu alikuwa amemponya, hatujui, ila asingaliruhusiwa kukaribisha watu nyumbani mwake kama bado angalikuwa ana ukoma.

Yohana amesema huyo mwanamke ni Mariamu, dada wa Martha na Lazaro. Marhamu ilikuwa ghali sana, Marko na Yohana walisema ilikuwa nardo safi, iliyotumiwa kupaka mafuta kichwani. Kwa nini huyo mama ampake Yesu mafuta? Yawezekana ametambua kwamba Yesu ataondolewa karibuni hivi, kwa hiyo achukue nafasi hiyo ya kuuonyesha upendo wake Kwake, na pengine kumwonyesha kwamba ametambua yatakayompata. Hatujui kama alifikiri atakufa kwa ajili yake, yawezekana hilo amelitambua pia.

Kama alifahamu Yesu atakufa kama mhalifu wa hali ya juu na mwili wake utaumizwa sana, hatujui, ni vigumu kufahamu kiasi cha kufahamu kwake.

Tujualo ni kwamba Yesu alitafsiri tendo lake ni matayarisho kwa maziko yake, amewahi kumpaka mwili kabla ya Kufa na mwilini kuwa maiti, kwa kuwa baadaye nafasi haitapatikana kwa watu kumshughulikia kufuatana na mila zao.

k.8-9: Itikio la wanafunzi halikuwa zuri. Yohana ametaja choyo ya Yuda, mtunza fedha wao, na Marko amesema juu ya wanafunzi wengine, ila Mathayo amesema wanafunzi kwa jumla walishirika mawazo ya kumlaumu.

Waliona tendo lenyewe ni bure, na fedha nyingi zilizotumika kwa marhamu zingaliweza kuwasaidia maskini wengi.
k. 10-11: Yesu aliyarekebisha mawazo yao. Alisema wazi kwamba mama huyo amemtendea tendo jema, maana ameutambua wakati ni wa maana sana ambao hautapatikana tena. Nyakati zi tele kwa watu kuwasaidia maskini ambao hawakosi kuwepo wakati wote, ila Yeye hatakuwa nao tena.

k.12: Ndipo Yesu alitafsiri maana halisi ya tendo lake, ameutayarisha mwili wake kwa maziko. Halafu akatamka neno la imani thabiti juu ya Injili kuhubiriwa ulimwenguni mwote, hafi bure, atafufuka na kupewa madaraka yote. Ajabu ni kwamba Injili itakapohubiriwa ndipo na tendo la huyo mama litatajwa kwa kumbukumbu lake. Yeye alijitoa kwa mali na kwa moyo, ila Yesu atajitoa zaidi, hata mpaka kufa, kwa kusulubiwa, ili tuokolewe. Yohana katika Injili yake aonyesha kwamba Yuda alichukizwa na tendo la huyo mama. Alitamani fedha, na huyo mama alileta kibwete cha marhamu, tena Yesu amemkubali kabisa na kuwakemea wanafunzi.

iv: **Yuda alijiingiza katika mpango wa hila:** 26: 14-16:

Injili hazitoboi wazi sababu ya Yuda kuchukua hatua hiyo mbaya ya kumsaliti Yesu, isipokuwa kwa kutaja choyo yake na wizi; hasa Yohana ametaja hayo Yoh. 12:6; 13:29. Mathayo pia ametaja tabia ya Yuda kuhusu fedha kwa kusema kwamba Yuda aliwauliza wakuu juu ya kiasi cha fedha watakachompa, huenda ndani ya kuwauliza ana maana ya kuonyesha kwamba asipopewa cha kutosha hatamtia mikononi mwao. Pia Mathayo ametaja kiasi walichokubaliana naye 26:15; sawa na alivyotabiri Zekaria (Zek. 11:12).

Wengine huwaza kwamba Yuda alikuwa amekata tamaa kwa sababu Yesu hawi kama alivyodhani atakuwa wakati alipoitika wito wake. Kama aliwaza ufalme wa namna ya dunia hii na ukubwa wa hapa duniani, ni wazi kwamba Yesu si Mfalme wa namna hiyo. Upeo ulifika Yesu alipomwunga mkono huyo mama na kusema juu ya kifo chake. Hayo yote ni makisio, hatuna uhakika, ni fumbo - Luka alisema - "Shetani alimwingia - Luka 22:3

Kwa jinsi Mathayo alivyopanga mambo amepambanisha kati ya Yuda na tendo lake baya, la chuki, lililokosa shukrani na utambuzi wa kiroho na tendo jema la yule mama, la shukrani na lenye utambuzi wa kiroho. Yohana amemtaja huyo mama kuwa Mariamu, dada wa Lazaro na Martha.

Ni wazi Yuda kwa tabia ya kupenda fedha na kutaka kupata aliachana kabisa na Yesu ambaye msingi wa maisha yake ni kutoa, tabia ambayo Mariamu pia anayo. Ubaya wa Yuda ni katika kumsaliti Yesu, mbona asimwache tu kama wengine walivyofanya, tena ubaya ulizidi katika kutaka fedha kwa kazi hiyo mbaya; pia kwa kumsaliti aliye rafiki.

Yesu hakufa kwa sababu ya Yuda kumsaliti. Kwa siku nyingi wakuu wametaka kumwua, ila wamekosa nafasi nzuri. Hata tumeona wameamua kabisa kumwua wakati huu, wakisubiri nafasi ya kufanya bila kuleta ghasia; Yuda alirahisisha mambo na kwa ahadi ya kuwa ataweza kuwajulisha mahali alipo wao watamkamata Yesu mapema kuliko walivyodhani 26:3-5 iliyobaki Yuda aitafute nafasi hiyo.
Ndani ya mipango hiyo yote ya wanadamu Mapenzi ya Mungu yatatendeka - Yesu kama Mwana Kondoo wa Pasaka atakufa wakati wa Pasaka.

v: **Chakula cha Mwisho:** 26:17-30: (Mko 14:12ku. Luka 22:7ku. Yo.13:1 ku.) Dhabihu ya Yesu yahusiana na Sikukuu ya Pasaka. Mathayo, Marko, na Luka wakaza habari za Chakula cha Pasaka kilichotangulia siku ya Yesu kusulibishwa. Yesu alikuwa ametamani kula chakula hicho na wanafunzi wake - Lu. 22:15. Alikuwa amewahi kupanga na mfuasi wake mmoja aliyeishi Yerusalemu, maana kupata chumba wakati wa Sikukuu haikuwa rahisi. Tena alificha mpango huo hali akijua hila ya Yuda, kusudi apate utulivu pamoja na wanafunzi kabla ya mambo kwenda haraka usiku na kesho yake atakapokamatwa na kuuawa.

Aliwatuma wanafunzi wawili kwenda kuandaa mahali akiwapa ishara ya kumfuata mtu aliyebeba mtungi wa maji (ni wanawake waliobeba mitungi ya maji) Iwapo huyo mtu hatajwi kwa jina ni wazi alijulikana kwa sababu mgeni asingaliutambua ujumbe wala kuelewa lugha "mwalimu asema majira yangu ni karibu ... "

Sikukuu hiyo iliitwa Sikukuu ya Mikate isiyotiwa chachu iliendelea kwa siku saba - siku ya kwanza walichinja wanakondoo wa Pasaka Luk. 22:7 ili jioni waile hiyo Pasaka hali wakikumbuka jinsi mababa zao walivyookolewa utumwani mwa Misri - ishara ya ukombozi wao. Kila Myahudi lazima akae nyumbani na kuila Pasaka.

Yesu alionyesha umuhimu na haraka kwa kusema "majira yangu ni karibu" mipango ya hila na uovu wa wanadamu itaungana na mpango mwema wa Mungu wa kuukomboa ulimwengu; mpango ulioanza hata kabla ya Anguko la Adamu. Wanadamu wafanya kwa hiari na bila kufahamu wanatimiza mapenzi ya Mungu.

Kwa maneno na matendo Yesu aliwafunulia wanafunzi umaana wa Kifo Chake na kuwaachia njia ya kumkumbuka, ambayo kizazi kwa kizazi wafuasi wake wataifuata mpaka atakapokuja tena.

Katikati ya chakula Yesu aliwaambia waziwazi habari ya kusalitiwa kwake na mmoja wao vi.20-25. Angalia jinsi alivyokaza hayo yote kuwa yanapatana na mapenzi ya Mungu aliyekusudia k.21 na 24a na kwa upande wa pili hiari ya msaliti k.24b. Katika mahubiri Mitume walizikaza sehemu zote mbili - taz. Mdo:2:23; 4:28; Yoh. 17:12.

Wanafunzi walishtuka mshtuko mkubwa waliposikia habari hiyo. Hawakuhisi ni Yuda, ila kila mmoja kwa mfuatano alimwuliza Bwana Yesu "ni mimi Bwana?" Yuda alichelewa kumwuliza Yesu, tena hakumwita Bwana ila Rabi tu. Katika pendo lake Yesu alikuwa amemficha ili wenzake wasigundue hali yake na hata ile ishara aliyotoa Yesu haikumdhihirisha wazi, maana wote walikuwa wakiweka mkono katika kombe, na katika mahangaiko yao bila shaka hawakusikia yote yaliyosemwa. Kwa kweli kama wanafunzi wangalijua mapema huenda wangalimpiga. Mpaka dakika ya mwisho Yesu alijaribu kumvuta auache mpango wake lakini ameisha kuteleza siku nyingi.
k.26-30: Ndipo Yesu aliendelea kwa kuweka "chakula kipya" badala ya Pasaka ya zamani kuwa kumbukumbu la "ukombozi mpya" badala ya "ukombozi wa zamani". k.26 "akabariki" maana yake alitoa shukrani - hakuubariki mkate kwa sababu vitu haviwezi kubarikiwa. "huu ndio ... " maneno hayo hayasemi lolote kuhusu jinsi mkate ulivyo mwili wa Yesu. Haukuwa mwili wake halisi kwa maana bado alikuwa katika mwili. Mara nyingi twasema kitu fulani "ni" kitu kingine ikiwa ni mfano au ishara yake. "akaumega" dalili ya mwili wake kuvunjwa pale msalabani. Kwa tendo hilo Yesu aliwafunulia wanafunzi juu ya Kuuawa Kwake - atauawa kwa ukatili mkubwa. Kama walikuwa na matumaini kwamba hayo hayatatokea, hapo kwa mara ya mwisho aliwahakikishia kwamba

yatatokea hakika. Kwa kuwaagiza kula na kunywa ni kuonyesha watashiriki kabisa Kito Chake na baraka zake. Baraka hasa ni kupatanishwa na Mungu na kusamehewa dhambi zao. Vilevile wote watakaowafuata watashirikishwa baraka hizo.

k.28. Kwa maneno hayo Yesu aliwakumbusha habari za Agano Jipya lililotajwa na Yeremia Yer. 31:31-34. Pia Kutoka 24:8. Yesu ni Musa mpya mwenye kutengeneza Agano Jipya. Sawasawa na lile la Agano la Kale lahusu ondoleo la dhambi na kuwekwa kwa damu Kut. 24:8 Ebr. 9:18-22.

Kwa Agano Jipya Yesu alifaulu kufanya lisilowezekana katika Agano la Kale, yaani kuondoa dhambi kwelikweli.

Maneno "kwa ajili ya wengi" yanatukumbusha Isaya 53:10-12 kuhusu Mtumishi Ateswaye. Isaya alitabiri kwamba huyo Mtumishi atateswa kwa ajili ya dhambi za watu wake na badala yao. Neno "agano" lahusu shirika/jamii - Agano hilo litazalisha Israeli Mpya.

k.29. Hapa Yesu amewatazamisha mbele baada ya Kito Chake, Ufalme wake utazidi kusimamishwa, ila ni mwisho wa kushirikiana naye kimwili.

k.30. Wimbo wa Pasaka ulikuwa Zab.1l6-118 Ndipo Yesu alitoka pamoja nao tayari kukabili magumu yaliyo mbele yake,na kwa kuweka ibada hiyo ya Ushirika Mtakatifu ameonyesha imani thabiti ya kuwa atashinda.

**vi. Yesu kutoa habari ya Petro kumkana:** 26:31-35:

Mazungumzo hayo yalitokea walipokuwa njiani kwenda Mlima wa Mzeituni. Yanaonyesha mzigo mkubwa aliokuwa nao Bwana Yesu kwa ajili yao. Iwapo mbele yake ni mateso makali sana alifahamu hao nao watapitia katika hali gumu watakapomwona akikamatwa na kuhukumiwa. Kwa hiyo aliendelea kuwaonya na kuwaelezea mambo ili wajiandae tayari. Mwanzoni watakimbia na Petro atamkana. Kama kawaida yake Petro alikuwa wa kwanza kuanguka, wa kwanza kusimama imara tena, na wa kwanza katika kumtumikia vema baadaye.

k.31: "mtachukizwa kwa ajili yangu" maana yake ni kwamba Yesu kukamatwa na Kuuawa ni kikwazo, wataanguka, si kwa kuogopa tu - bali kwa sababu wamekosa kutambua makusudi ya mateso ya Yesu. Bado hawajaelewa **yampasa** Masihi kupatwa na hayo yote. Ndipo Yesu aliwakumbusha unabii wa Zekaria 13:7 "nitampiga Mchungaji na kondoo watatawanyika" Mungu ndiye asili ya mambo hayo.

k:32: Ila hayo si mwisho - atafufuka; nao watamwona, wote isipokuwa aliyemsaliti. Watakapoondoka Yerusalemu kwenda Galilaya hawataiacha maiti yake kaburini bali watamkuta huko hali yu hai. Bwana asifiwe!!!

k:33-35: Petro alidhani haitakuwa vigumu kumtetea Yesu; hakutambua vibano vitakavyokuwepo; ujasiri wake wa kimwili hautamtosha; baadaye atakuwa na ujasiri wa Roho. Mdo.4:7,l3.

vii: **Maombi ya Yesu Gethsemane:** 26:36-46:

Kwa habari hiyo twafunuliwa jinsi Yesu Mwenyewe alivyojisikia rohoni mwake alipokaribia "ile saa yake" saa ambayo alikuwa ameitaja mara kwa mara. Twaona uhusiano wake na Baba, pia gharama ya kuutimiza wito wa kuwa Mtumishi ateswaye atakayebeba dhambi za wanadamu wote na kuvumilia adhabu ya Baba juu ya dhambi hizo. Ukweli wa ubinadamu wake umeonyeshwa kwa jinsi alivyomwomba Baba akiondoe "kikombe" kama ikiwezekana, pamoja na kuonekana kuwa Mwana wa Mungu kweli.

Twaona pia udhaifu wa wanafunzi walioshindwa kukaa macho na kushiriki naye taabu yake, iwapo kwa kweli hawakuweza kuwa karibu kabisa, ilimbidi ajitenge kiasi fulani, maana njia hii ataikanyaga peke yake kama nabii Isaya alivyotabiri Is. 63:3.

Angaliweza kuepa mambo hayo kwa kwenda mahali pengine ili Yuda asimpate, ila alifahamu kabisa ni mapenzi ya Baba na matimizo ya Maandiko.

Wale watatu waliokwenda naye ndani zaidi bustanini walikuwa naye mlimani alipogeuka sura.

k.38.Moyo wake ulikuwa karibu na kuvunjika alipokabili mateso yake. Bila shaka alipowaza mateso ya kimwili alifadhaika, ila zaidi ilikuwa dhiki ya rohoni iliyomsumbua alipowaza kutwishwa dhambi na kufanywa kuwa dhambi 2 Kor:5:2l.na kutengwa na Baba; hali mpya kabisa kwa Yeye asiyejua dhambi wala kamwe kuifanya. Yeye asiye na mawaa atahesabiwa mwenye dhambi. Hayo ndiyo asili ya dhiki yake kuu.

k.39. Katika dhiki yake alianguka kifudifudi na kuomba. Kama siku zote alimwita Mungu "Baba" ndipo alitaja "kikombe" lugha ya kujumlisha mateso yote atakayoyapata. Maneno aliyotumia yaonyesha utii wa Mwana kwa Baba pamoja na kuonyesha ugumu wake. Alitaka kuhakikishia kwamba hamna njia nyingine. Kama hamna yu tayari kukinywea hicho kikombe, kama alivyoomba aliporudi kwa mara ya pili na ya tatu.

Katikati ya vipindi vya kuomba aliwarudia wanafunzi, akawakuta wamelala. Hao walikwa wamezoea kufanya kazi usiku walipokuwa wavuvi. Bila shaka asili ya kushindwa kwao ni kwa sababu hawakuomba. Tangu hapo Yesu yu tayari kukutana na watesi wake; ushindi ameupata katika kukaza nia yake kwa njia ya kuomba na kushirikiana na Baba. Yatubidi pia kumwaza Baba
atakayemtazama kwa huruma Mwana wake katika dhiki kuu, asiweze kufanya lolote kumsaidia kwa kuwa ni njia ambayo kwayo ulimwengu utakombolewa, dhambi itashindwa, Shetani atashindwa, na laana za Anguko zitageuzwa kuwa baraka; na wanadamu wataokolewa.

k.45-46: Yawezekana Yesu aliziona taa za adui zake wakisogea kumkamata wakiongozwa na Yuda. Saa ya kukesha pamoja na Yesu imepita, hawawezi kumsaidia zaidi; kwa ujasiri Yesu alikwenda kukutana na Yuda na wenzake

## YESU KUKAMATWA NA KUHUKUMIWA 26:47-27:26.

i: **Yesu kukamatwa:** 26:47-56:

Katika sehemu hiyo Yesu anatawala - taz. k.46,50,53,56; hatawapinga, hivyo wataweza kutekeleza mipango yao. Kwa kawaida mwanafunzi hakumbusu Rabi wake ila kwa wakati maalum ya kumheshimu. tena kwa kuitwa kufanya hivyo. Yesu akaitika kwa kumwita rafiki, pengine ukumbusho wa kula naye mezani. Halafu Yesu akamwambia afanye alilokusudia. Yesu hakushtuka kumwona Yuda, ila alishangaa kuona waliokuja naye, wamekuja na silaha kama wamekuja kukamata mtu mkatili: aliwafunulia kwamba wasingaliweza kufanya lolote juu yake hata kwa silaha zao kama si mapenzi ya Mungu na matimizo ya Maandiko.

Petro alijitahidi kumlinda Yesu kwa upanga, Yesu akamzuia na kumkemea. Walipoona Yesu amekamatwa wakakimbia wasije wakakamatwa pia. Yesu aliwalinda akikubali kushikwa bila vita. taz. Yoh.18:1 ku. Msingi wa maisha yake ulikuwa Maandiko; hayo yaliandikwa humo.

ii. **Hukumu mbele ya Wayahudi:** 26:57-68:

Injili nne zatoa habari za hukumu mbalimbali. Alipelekwa kwa Anasi aliyeendelea kuitwa Kuhani Mkuu iwapo Kayafa mkwewe hasa alikuwa Kuhani mkuu. Inaonekana Anasi bado alikuwa na sauti kuu katika mambo - taz. Yoh. 18:13.

k.57: Wakuu wamekwisha kukutanika, bila shaka kwa kuandaa mashtaka yatakayoweza kusimama mbele za liwali ya Kirumi Pilato. Kwa hiyo walikuwa wametafuta mashahidi wenye ushuhuda wa kufaa, maana Pilato hatajali mambo yao ya dini. Baadaye walifaulu kupata wawili walioshuhudia kwamba Yesu alidai kusema juu ya hekalu. Kwa sheria yao lazima wawili wapatane katika ushuhuda wao. Yo.2:19. Yesu alikuwa na maana ya mwili wake kuwa hekalu, si jengo lenyewe. Hukumu hiyo ya kwanza haikuwa haki, maana wamekwisha kuamua lazima afe.

k.62-63: Yesu alinyamaza, aliachia mambo yaendelee hivyo hali akifahamu mapenzi ya Baba yatatimizwa.

k.63: Kisha Kuhani Mkuu kwa kiapo alimwuliza Yesu kama kweli Yeye ndiye Masihi, kama alivyodai kwa kusema ataharibu hekalu na kulijenga upya; maana hakukana mashahidi walipotoa ushuhuda huo - Zek. 6: 12. Yesu alilazimika kujibu Kuhani Mkuu alipomwapiza kwa jina la Mungu. Katika kujibu ni sawa na kutia sahihi kwenye hati ya kufa.

k.64. Mara nyingi Yesu alikuwa amedai kuwa Masihi bila kusema waziwazi. Sasa alikubali, atakufa kwa kuwa ni Masihi wao wa kweli, lakini si wa siasa. Ndiyo sababu aliendelea kuwaambia hali halisi ya Umasihi wake; ni ya Mungu mwenye mamlaka ya juu. Kumbe! atatawazwa juu mbinguni: Dan. 7:13. Kutoka huko juu atakuja kuhukumu.

k.65: Hayo yaliwatosha kabisa - amekufuru, na kwa sheria yao alistahili kabisa kuuawa. Ila kwa Pilato watabadili mashtaka Hawakujihoji itakuwaje kwao watakapomwua ikiwa kweli Yesu ndiye Masihi wao. Wamekaza nia zao kwa muda mrefu kwamba hawamtaki. Ndipo wakamchezea vibaya. Hayo ndiyo walimfanyia Mungu aliyefanyika mwanadamu ili atukomboe.
Yesu alikuwa mjasiri akikiri wazi Umasihi na asili yake.

iii: **Petro kumkana:** 26:69-75:

Sasa Mathayo baada ya kuonyesha ujasiri wa Yesu mbele ya washtaki wake waliokuwa na madaraka ya kumwua ameonyesha udhaifu wa Petro aliyeshindwa kabisa kumkiri hata mbele ya kijikazi mmoja. Kwa nini amkane? Huenda hakujiandaa kwa maombi alipokuwa bustanini; alijitegemea; alidhani ataweza kuwa imara. Pengine alihofu kwamba watamtambua kuwa yule aliyekata sikio la mmoja aliyekuja kumkamata Yesu. Jogoo alipowika Petro alijua maneno ya Yesu yalikuwa kweli, akatoka na kulia sana.

*MASWALI:*

*Twaona Yesu alikubali kwa furaha kupakwa mafuta na yule mama. Je! uko tayari kutoa nafasi kwa akina mama katika huduma yako? Wataweza kusaidia kazi ya Kanisa kwa njia zipi? Unawathamini sawa na jinsi Yesu alivyowathamini au bado unasikia shida kuwahesabu ni wa maana?*

*Kuhusu Ushirika Mtakatifu unawasaidia Wakristo kuthamini ibada hiyo kuliko ibada zote? Unawashaurije kuhusu kuikaribia Meza ya Bwana? Kwa nini inatupasa kuiheshimu ibada hiyo?*

*Tunapomtazama Bwana Yesu huko Gethsemane twajifunza nini kuhusu Mateso yake na Kifo Chake? Pia twajifunza nini kuhusu Maombi katika kumtii Mungu. Mtumishi wa Bwana apaswa kuwa mtu wa Maombi - Je! unakubali? Je! unafanyaje ili uilinde nafasi ya Utulivu na Maombi katika shughuli nyingi za kila siku?*

*Twajifunza nini kutokana na kuanguka kwa Yuda na kuanguka kwa Petro? Lazima tujihadhari na nini ili sisi nasi tusianguke? ikiwa tutaanguka tufanyaje tukikumbuka Yuda alipotea na Petro aliponywa?*

iv: **Kuletwa mbele ya liwali ya Kirumi:** 27:1-2:

Sasa iliwabidi viongozi Wayahudi wapate njia ambayo kwayo uamuzi wao utekelezwe na Warumi maana wao wenyewe hawakuwa na ruhusa kum-sulibisha mtu. Walifahamu liwali hatajali mashtaka ya kufuru. Hivyo asubuhi mapema, wakati ambapo wajumbe wengi wamefika, Baraza lao kuu liitwalo "Sanhedrin" lilikutana. Walishauriana kwa namna watakavyomweza Pilato, maana yeye hakuwa mwepesi wa kuchukuliana nao. Budi wageuze mambo kuwa ya siasa. Kwa maneno ya kwanza ya Pilato k.11 inaonekana walikubaliana kukaza madai yake ya kuwa Mfalme wa Wayahudi.

v. **Yuda alijiua:** 27:3-10:

Mathayo ameingiza hapa habari ya Yuda kujiua. Yeye ametaja mambo yake kuliko wainjilisti wengine. Yesu aliwahi kuwaambia wanafunzi kwamba Petro atamkana na mmoja wao atamsaliti 26:24,34. Ila baada ya kuanguka Petro alisikitika mno na kutubu; Yuda hasa alijuta, hakutubu kweli, hakusubiri nafasi ya kumwona Yesu. Yeye aliwarudishia wakuu wa makuhani fedha walizompa, na walipokataa kumjali akazitupa chini hekaluni, akatoka kwenda kujinyonga. Hakutaka kuwa na hatia ya damu ya Kristo, lakini kurudishia fedha hakutamsalimisha Yesu. Wakuu walilazimika kuchukua fedha hiyo - hao nao watakuwa na hatia ya damu ya Kristo.

Ajabu ni kwamba hawakuogopa kuondoa fedha katika hazina ya hekalu, lakini waliogopa kuirudisha!!! Ndipo wakaitumia kununua mahali pa kuzika wageni; yaani WaMataifa waliokufa wakati wa kuwa Yerusalemu, neno la kumfurahisha Bwana Yesu, (Tukilinganisha na Mdo:I:18 inaonekana habari zinapishana ila huenda siyo, angeweza kujinyonga, ndipo kuanguka chini na kupasuka) Mwisho wake ulikuwa mbaya sana, mwisho wa asiye tayari kutubu, mtu aliyemwasi Mwana wa Mungu hali ametembea naye siku kwa siku na kuona maajabu mengi.

vi. **Yesu kuhukumiwa na Pilato:** 27:11-26:

Hapa tuna habari ya Hukumu rasmi ya Yesu mbele ya Pilato aliye na madaraka ya kuamua kuwa anayo hatia au hanayo, pia akiwa na hatia apewe adhabu gani. Lakini katika hukumu hiyo wakuu wa Wayahudi walikuwa wakimsukuma-sukuma Pilato asifanye alivyotaka kufuatana na ushuhuda uliopo.

Akateleza-teleza akitafuta njia ya kuepukana na wajibu wa kutoa uamuzi, mwishoni walimbana kabisa. Ni vema kusoma Injili ya Yohana 18:28-19:16 kwa habari zaidi.

Hukumu ilianza na swali la Pilato juu ya Yesu kuwa Mfalme wa Wayahudi. Kwa ujanja kabisa wakuu wameingiza siasa ndani ya Umasihi wa Yesu - kweli Yesu ni Masihi wao na Mfalme wao lakini si katika maana ambayo Pilato anawaza Ufalme. Pia kwa mashtaka ya aina hiyo lazima Pilato ayashughulikie, walifanya Yesu aonekane ni mpinduzi wa serikali. Ling. na Luka 23:1-5, Yesu hakumjibu Pilato, ni kama nusu amekubali na nusu amekana maana pasipo kutoboa zaidi Pilato hataelewa matumaini ya Wayahudi kupata Masihi na mapenzi ya Mungu kumhusu. Katika Yoh. 18:33-37 walipokuwa peke yao Yesu alijaribu kumsaidia Pilato aelewe kwamba Ufalme wake si wa dunia hiyo. Taz. Is. 53:7 kuhusu ukimya wa Yesu. Pilato alishindwa kujua afanye nini, ndipo akakumbuka desturi ya kuwafungulia mfungwa mmoja kwa kuwatuliza wakati wa Sikukuu walipowaka na kutaka uhuru. Haki iko wapi?

Yesu amehukumiwa kosa gani? Ana hatia gani? Kama Pilato angesimama imara ilimbidi atoe hukumu ya kuwa hana hatia na kumfungulia - kumbe asema haoni hatia, ndipo aliamua apigwe mijeledi n.k. Hii ndiyo haki?

Wakati wa kungojea uchaguzi wa watu, kama ni Baraba au Yesu mkewe Pilato alituma mjumbe kumwambia bwana wake asimhukumu Yesu, maana usiku amesumbuliwa na ndoto. Yawezekana iwapo ni mpagani huyo mama amesikia habari za Yesu, labda wamepata taarifa kwamba wakuu wanayo mipango ya hila juu yake, labda walikuwa wamezungumzia habari zake wao kwa wao. Hata hivyo Pilato ameisha kuteleza katika kumfungulia, na wakuu wamekwisha kumsoma ni mwoga, basi wakaendelea kumbana vibaya mpaka walipofaulu na Pilato alikubali auawe. Kwa namna alivyoandika inaonekana Mathayo anataka Wayahudi wawekewe lawama ya kifo chake.

k.20. Waliporudi baada ya kupitapita kati ya watu na kuwashawishi wamchague Baraba wakuu wakafika tena mbele ya Pilato - Pilato akawauliza wote waliokuwapo walimtaka yupi. Akashangaa na kuogopa walipomtaja Baraba. Akawauliza amfanyie Yesu nini? Kumbe wakamjibu "asulibiwe". Atawezaje kumsulibisha Yesu ambaye bado halijaonekana kosa lake? Ndipo wakapiga kelele sana na kumtisha Pilato, naye aliogopa ghasia kwa sababu ni wakati wa Sikukuu na watu wengi wamefika Yerusalemu. Ni wakati wa Wayahudi kusikia uamsho wa kutaka uhuru wao na hali ya utaifa iliwaka; basi Pilato akajiondoa katika kesi na kuwaachia nafasi ya kufanya walivyokusudia. Hatia ya damu ya Kristo hakuitaka iwe juu yake, ila iko juu yake maana ndiye yeye peke yake mwenye mamlaka ya kumwadhibu au kumwachilia. Kweli Pilato alikuwa mwoga. Ila watu hawakujali, wakaitika kwa kukubali damu ya Kristo iwe juu yao, maana yake wao watabeba wajibu huo. La ubaya ni kwamba iwapo ameshuhudia Yesu hana hatia kumbe hata hivyo aliamuru apigwe mijeledi. Wengi waliumizwa vibaya kwa kupigwa mijeledi, hata wengine walikufa kabla ya kusulibishwa. Yawezekana ndiyo sababu Yesu hakuchelewa kufa msalabani.

## YESU KUSULIBIWA 27:27-56:

i. **Yesu kudhihakiwa na maaskari** 27:27-61:

Dhihaka hizo zililingana na mashtaka ya kuwa Mfalme, bila shaka ndani yake ni dharau kwa Wayahudi na tumaini lao la kupata Masihi wa kuwaokoa mikononi mwa Warumi. Zilianza katika dharau ila baadaye maaskari walitumia nguvu za kimwili na kumpiga Yesu. Kisha wakamvika nguo tena, maana walifahamu Wayahudi walichukizwa wakimpeleka mtu kusulibishwa hali yu uchi.

ii. **Yesu kusulibishwa:** 27:32-44:

Wayahudi hawakukubali kumwadhibu mtu afe kwa kusulibishwa, hata hivyo waliona wengi wakiuawa kwa njia hiyo. Hasa Warumi walitumia njia hiyo kwa walioshtakiwa kuwa wapinduzi wa serikali na kwa wakosaji wakuu, hasa kwa shabaha ya kuzuia wengine. Ilikuwa kifo kibaya mno cha ukatili sana. Katika kuandika habari hizo Mathayo hakukaza maumivu makali n.k. hasa alitaja dhihaka za wakuu jinsi walivyomdhihaki Bwana Yesu alipokuwa msalabani.

k.32: Yesu alishindwa kuubeba mbao wa msalaba, alikuwa amedhoofika kwa kupigwa mjeledi na kuchezewa vibaya. Warumi wakamkamata mtu aliyekuwa akipita njiani na kumlazimisha aubebe, Yawezekana huyo mtu aligeuka kuwa Mkristo baadaye Mko:15:21 wana wake wawili watajwa.

k.34. Wakampa divai - na Yesu aliikataa: Divai hiyo ilikuwa kama dawa ya kupunguza maumivu: Yesu alitaka kuwa na akili timamu ili afanye yampasayo katika Kufa Kwake hali akielewa anayofanya - yaani kufidia dhambi, kuchukua mahali petu na kufa badala yetu. Yampasa akili zake ziwe sawa. Pia atashuhudia katika Maneno Saba maana ya mateso yake.

k.35: Kugawa nguo zake, timizo la unabii wa Zab.22:18. Maneno ya k.35b
hasa yalitoka Injili ya Yohana Yoh. 19:24b.

k.36: Maaskari walimlinda wasije watu kuja kumwokoa, ila kwa Mathayo ni kututayarisha kwa ushuhuda wao Yesu alipokata roho k.54.

k.37:Anwani yake: Kwa kawaida wafungwa walizungushwa mjini hali wamevaa mashtaka yao kusudi wawe fundisho kali kwa wengine. Mathayo aona ya kuwa Yesu hupata Ufalme kwa njia ya Kufa Kwake, Yeye ni matimizo ya Masihi ya Isaya 53, Mtumishi Ateswaye. Wawili wengine walisulubishwa pamoja na Yesu, Yesu akiwa katikati yao IS.53:12. Pengine Baraba angalikuwa wa tatu, ila sasa Yesu ndiye:,badala yake.

Yesu aliendelea kudhihakiwa na waliopita: k.39-40; na wakuu k. 41-43: na wanyang'anyi k. 44. Kwa dhihaka aliitwa majina makuu; Mfalme wa Wayahudi; Mjenzi wa hekalu; Mwana wa Mungu. Katika sehemu hiyo vote twakumbushwa Zaburi 22.

k. 40b "shuka msalabani" Kwa kumwita Mwana wa Mungu na kumwambia ashuke msalabani Shetani aliwatumia akijitahidi tena kumwondoa asitimize mapenzi ya Mungu kama alivyojitahidi jangwani zamani alipoanza huduma yake. Pale Gethsemane ameshindana kiasi cha kutoa matone ya damu kwa kudumu kuwa mwaminifu kwa Baba. Hapo ajaribiwe tena, kwa mara ya mwisho Kweli angaliweza kushuka msalabani, lakini kwa sababu ni Mwana Mtiifu wa Baba hawezi kushuka - lazima akae, awe fidia ya dhambi, awaokoe wenye dhambi kwa kumwaga damu yake kama Kondoo wa Pasaka.

k. 41-43: Kwa kutaja Wakuu wa Makuhani, Wazee, na Waandishi Mathayo ameonyesha kwamba Yesu alikataliwa rasmi na taifa zima la Wayahudi.

iii: **Yesu kufa:** 27:45-56: k. 45:
Kwa mara ya kwanza Mathayo ataja saa "sa a sita" wakati wa giza kufunika nchi - ling. na Mko 15:25 Yoh. 19:14. Giza hilo kuu lilisababishwa na nini? Bila shaka lililetwa na Mungu Mwenyewe maana lilitokea wakati ambapo mwanga ni mkubwa katikati ya mchana. Twaweza kulipa maana mbalimbali. Kwanza Mungu alitaka kuuvuta usikivu wa watu ili watambue ya kuwa jambo kuu latendeka pale msalabani - jambo la ukombozi wa ulimwengu na dhambi zake

kuhukumiwa mwilini mwa Yesu. Pia ni jambo la kutisha hata kiasi cha uumbaji kushindwa kutazama, Mwana wa Mungu alipoteswa vikali, ni kama uumbaji umejiunga naye, giza la nje likilingana na giza lake la rohoni. Lilikuwa ishara ya Mungu kutengana naye alipobeba dhambi za walimwengu wote, maana maovu yetu vote yaliwekwa juu yake Is.53:6; alifanywa kuwa dhambi 2 Kor.5:21 alichukua laana Gal. 3:13; taz. Is. 59:2; Amosi 8:9. Habari hiyo pia yatukumbusha pigo la tisa pale Misri kabla ya Waisraeli kutoka utumwani Kutoka 10:22.

k. 46: Hicho ni kilio cha kutisha cha Bwana Yesu aliposikia kuachwa na Mungu, dhambi ilipoadhibiwa; Yesu hakumwita Mungu "Baba" hata hivyo aliweza kusema Mungu **wangu,** wakati huo akinywea "kile kikombe cha Baba" kile kilichomsumbua sana alipokiwaza Bustani ya Gethsemane.

k. 47-49: Waliokuwepo hawakuelewa kilio chake wakadhani anamwita Eliya amsaidie; pengine walitazamia tukio la ajabu litatokea. Mmoja alimletea msaada wa kinywaji kwa sababu taabu moja ya kusulibishwa ilikuwa kuishiwa maji mwilini, na kwa kufungiwa mtu alishindwa kujipatia msaada. Yoh. 19:28. Zab.69:21. Kwa msaada wa kinywaji hicho Yesu aliweza kupaza sauti yake tena, pengine wakati huo alilia "Imekwisha" Yoh. 19:30.

Ushuhuda wa kushinda: ameukomboa ulimwengu, amefidia dhambi: ushindi utakaodhihirika Siku ya Kufufuka Kwake.

k.50: Yesu aliitoa roho yake, akaikabidhi kwa Baba Lu.23:46. Alikuwa na mamlaka ya kuitoa hali akifahamu nafsini mwake ya kuwa yote aliyotakiwa kuyafanya amefanya, hana haja ya kuteswa zaidi. Alikufa hali akimwita Mungu "Baba".

k.51-56: Maajabu yalitokea: k.51: Pazia la hekalu lililotenganisha Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu lilipasuliwa kutoka juu, mahali pale pote palikuwa wazi. Dalili ya kuwa mtu yeyote aweza kuingia kwa damu ya Yesu. Hapo nyuma ni Kuhani Mkuu tu aliyeruhusiwa kuingia, tena mara moja kwa mwaka, Sikukuu ya Upatanisho, tena kwa damu ya Mwana Kondoo. Tangu wakati huo mpango huo hauhitajika tena. Taz. Ebr. 6:19; 10:19. Njia ni wazi.

Ndipo tetemeko la nchi lilitokea, miamba ikapasuka na makaburi yakafunuka, ndipo baada ya Yesu kufufuka watu wa Mungu wa zamani walitoka makaburini na kuwatokea watu. Maaskari waliguswa sana na matukio hayo, waliogopa sana kwa kuwa ni hao waliompigia misumari na kumweka msalabani. Walimkiri kuwa Mwana wa Mungu!!! tofauti na dhihaka zao za hapo nyuma. Hao ni Wamataifa, ishara ya Wamataifa wengi watakaomwamini Kristo Injili itakapohubiriwa baadaye. Jina la "Mwana wa Mungu" laheshimiwa tena baada ya kutumiwa vibaya k. 40,43

k.55-56: Wanawake waaminifu walikuwa mashahidi wa yote yaliyotendeka, walidumu waaminifu; nao waliona na kupahakikishia mahali pa Yesu kuzikwa ili baada ya Sabato waje kumalizia kuiweka maiti yake vizuri zaidi.

## YESU KUZIKWA NA KUFUFUKA - 27:57 - 28:20:

i. **Yesu kuzikwa** 27:27-61:

Hakika Yesu alikuwa amekufa - ling. na Yoh. 19:33-37. Watu hawaziki mtu mpaka wana hakika amekufa kweli. Kinyume cha kawaida kwa wale waliosulubiwa maiti ya Yesu haikutupwa ovyo bali iliheshimiwa na kuzikwa katika fahari impasavyo Mfalme. Ilipakwa manukato mengi na kutiwa katika sanda ya kitani safi na kuwekwa katika kaburi jipya. Kweli Yusufu wa Arimathea na Nikodemo hawakuwa na muda mrefu kwa sababu ya kuanza Sabato kuu jioni ile, vilevile hawakuwa na taarifa ya mapema ile waandae, hata hivyo juhudi zao zilitosha kumzika Yesu vema: Ling. na Yoh. 19:38ku.

ii. **Walinzi kuwekwa kaburini kulilinda:** 27:62-66:

Wakuu wa Makuhani walijiunga na Mafarisayo ambao hawakutajwa katika habari zilizotangulia wakimwomba Pilato walinzi wawekwe kwenye kaburi. Iwapo Yesu ni mfu hawawezi kutulia, maneno juu ya kufufuka yaliwatia mashaka eti! wanafunzi waweza kuja kuiba maiti - kumbe! wanafunzi wamejificha kwa hofu ya kuwa watakamatwa, wala hawatumaini maneno ya Yesu aliyowaambia mara kwa mara kwamba atafufuka. Wakuu walikuwa tayari kushughulikia neno hilo siku ya Sabato. "Yule mjanja" udhaifu wa mawazo yao yaonekana katika kufikiri hata ikiwa maiti itaibiwa itakuwa vigumu kuificha, na maiti ikipatikana neno la kufufuka litakomeshwa mara. Mungu aliruhusu hayo yote yatendeke kusudi Yesu atakapofufuka itakuwa vigumu kutoa maelezo mengine.

k.65-66: Basi walinzi waliwekwa, pamoja na jiwe lililotiwa muhuri. Hayo yote hayatamzuia Yesu asitoke siku ya tatu!

*MASWALI:*

*Siasa ya Warumi na siasa ya Wayahudi zilikutana na kusababisha Yesu auawe. Siyo kusema siasa ni mbaya kwa kuwa siasa ni mpango wa kuongoza mambo ya nchi. Siasa ni hatari wakati gani? Je! ni vema wakristo wajitenge kabisa na siasa au afadhali wajiingize? Toa sababu kama ukiona wajitenge, vilevile ukiona wajiingize toa sababu.*

*Utawasaidiaje wakristo ambao kazi zao zahusika na serikali? Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote. Neno hilo linakusukuma kufanya nini katika huduma yako? Je! unakaza Neno la Msalaba katika mahubiri yako?*

iii. **Kaburi kuwa wazi na Yesu kuwa hai** 28:1-10:

Hakuna maelezo kuhusu Yesu hali akifufuka, ila iliyopo ni maelezo ya kaburi kuwa wazi na tupu na wanafunzi kukutana naye hali akiwa hai. Hasa mkazo ni jinsi wanafunzi walivyoshtushwa na kubadilishwa, ni wazi hawakutazamia watamwona tena kiasi cha wengine kusita kupokea habari hiyo mara moja.

k.2: tetemeko la nchi tena, pengine kwa kuliondoa jiwe, ndipo ataja "malaika wa Bwana" mara ya kwanza baada ya 1:20, 2:13, 20. Ameelezwa kuwa zaidi ya mjumbe, utukufu wake wafanana na ule wa Mungu. Walinzi wakahofu sana, na wanawake vilevile waliogopa, ila hao hawana sababu ya kuogopa, wakaitwa kupatazama mahali alipolazwa. Yeye Mwenyewe hayupo, amefufuka. Kwa hiyo uaminifu wao umepata thawabu; wanawake walikuwa wa mwisho msalabani - wa kwanza kaburini - wa kwanza kupashwa habari za Kufufuka Kwake - hao ndio watakaowaambia wanafunzi wake.

Mathayo alitaja Galilaya kuwa mahali wanafunzi watakapomwona k.7, 10,16. Yesu alipoanza huduma alianzia Galilaya, mahali mwanga mkuu utakapozuka 4:12-16. Wanawake walipoondoka kaburini wakakutana na Yesu njiani, Yesu akawasalimia, nao wakamsujudia na kumshika miguuni, ushuhuda wa ukweli wa mwili wake, iwapo ni "mwili wa ufufuo" mwenye uwezo mpya.

LU.24:39-43. Yesu akawaagiza wawaambie wanafunzi waende Galilaya, maana watakutana naye huko. Mathayo hakusema juu ya Yesu kuwatokea Yerusalemu. Taz. Injili ya Yohana kwa habari hizo.

iv: **Walinzi kutoa ripoti** 28: 11-15:
Jiwe liliondolewa ili wafuasi wake wapate kuingia humo na kujihakikishia maiti haipo, ila Yesu aliwaachia ushuhuda wa sanda na vitambaa. Yeye alipitia mwambani wala hakuna aliyemwona akifufuka. Walinzi walipoona jiwe limeondolewa na maiti haimo wakaogopa sana maana wameshindwa kikazi, na Pilato atawaadhibu vikali. Baadhi waliamua kwenda kwa wakuu wa makuhani na kuwaelezea matukio hayo. Wakuu walikata shauri kuwanyamazisha kwa kuwapa rushwa ya fedha nyingi, wakawafundisha kusema uongo kwamba wanafunzi walikuja na kuiiba maiti. Kumbe! waliwekwa ili hilo lisitokee sasa wapaswa kusema uongo wa hilo kutokea. Wakuu waliosema "yule mjanja asije awadanganye watu" kumbe! wao wenyewe watadanganya watu!! Mbona wasiwafuatie wanafunzi na kuipata maiti? kupata maiti itakomesha uvumi wote!!!

v. **Yesu yu hai na kupewa mamlaka kuu na kutoa Agizo Kuu:** 28:16-20:
Mathayo aliifikisha Injili katika upeo wa Yesu kuonekana Mshindi mkuu, mtawala wa yote mbinguni na duniani, wa kuabudiwa sawa na Baba na Roho Mtakatifu na kuwekwa pamoja nao, akiupokea utiifu wa wafuasi sawa na hao. Umoja wao waonekana katika lugha ya "jina la" si majina ya.

k.16-17. Walipokutana naye huko Galilaya walimsujudia ila wengine walikosa uhakika.

k.18 Yesu alishuhudia kwamba "amepewa mamlaka yote .. " Kwa sababu hiyo aweza kuwatuma kotekote, kama Baba alivyomtuma, hao nao watumwa. Wafanye nini? Wawafanye watu wa mahali pote kuwa wafuasi wake: wawatie kwenye ufuasi huo kwa kuwabatiza: halafu kuwafundisha kushika maagizo yake, yaani waishi maisha ya Kikristo; ya maadili yake si sheria za kale bali yale ambayo tumeyakuta katika Injili hiyo.

k.20: Alifunga na ahadi njema ya kusema atakuwa nao sikuzote timizo la jina Imanueli 1:23. Pia 18:20; maana hawataweza kutimiza Utume wao pasipo Yeye kuwa pamoja nao. Mathayo alianza Huduma ya Yesu kwa kumwonyesha yuko Galilaya akileta Habari Njema na mwangu mkuu 4:12-16 na kuwaita wanafunzi; ndipo akaifunga na Yesu kuwa huko Galilaya akiwatuma wanafunzi kwenda kuhubiri habari zake ulimwenguni mwote.

*MASWALI:*

*Kwa nini neno la Ufufuo ni muhimu sana? Je linakutia moyo kwa njia gani? Uhakika wake waonyeshwa katika matukio gani?*

*Wengi siku hizi wasema si vema kuhubiri Injili kwa watu wa imani nyingine na dini nyingine? Dini zote ni sawa n.k. Ni kiburi kudai dini ya Kikristo ni bora? Utawajibuje? Upekee wa Kristo na wa dini ya Kikristo ni katika nini? Nani alituamuru kwenda ulimwenguni mwote na kufanya watu kuwa wanafunzi? na alidai kuwa na nini alipotuamuru? Je! hii ndiyo sababu kuu na ya kutosha kufanya uinjilisti?*

*Kwa kuchunguza Injili ya Mathayo ni msaada gani mkubwa ambao umepata kwa mambo yake, na hasa kumhusu Yesu na huduma yake na kufikiri juu ya huduma yako?*